KISWAHILI

Kwa shule za Rwanda

# KITABU CHA MWANAFUNZI

KIDATO CHA 5

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda
Haki zote zimehifadhiwa.
Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda.
Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# DIBAJI

Mwanafunzi mpendwa**,**

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa Kitabu cha Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha tano, michepuo mingine, katika ngazi ya juu ya sekondari.

Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri maisha yake na kumpa fursa ya kujipatia ajira au kuandaa miradi mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii anamoishi.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza kuhusu umuhimu wa kufungamanisha shughuli za ujifunzaji na ufundishaji pamoja na zana na mitaala ili kufanikisha mchakato mzima wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale yanayofundishwa na uwezo waupatao wanafunzi. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Hivyo basi, kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza unaokuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti ya kibinafsi na yale utakayofanya katika makundi kwa msaada wa walimu ambao huwajibika kufanikisha ufundishaji. Aidha, utapata stadi muhimu zitakazokuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha mbalimbali ya maisha halisi ili uweze kuonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Mwelekeo uliozingatiwa katika kitabu hiki unatofautiana na ule uliotiliwa maanani katika mfumo wa zamani ambapo mchakato wa kujifunza ulifanywa kwa kutilia mkazo upataji wa maarifa kutoka kwa mkufunzi ambaye pia alifikiriwa kumzidi mwanafunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi. Kwa hiyo, dhana huanzishwa aghalabu kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na kupata maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya ujifunzaji hujihusisha na shughuli mbalimbali zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri kuhusu yale anayoyafanya, kuonyesha uzoefu wake halisi na maarifa aliyo nayo katika mchakato huo wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, utakuwa na majukumu yafuatayo ili uweze kutumia kitabu hiki kwa ufanisi:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi au mazoezi yanayolenga kwenye mada;
- Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kupitia mawasilisho, mijadala, kazi za makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama vile michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, mitandao na hata nje ya shule;

- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa /mtandaoni, wataalamu na kuwasilisha matokeo ya utafiti;
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi ulizopewa kupitia maelezo na majadiliano kila unapoongea hadharani;
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi yako ya ujifunzaji.

Mwishowe, ningependa kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki na kutoa mchango wao kwa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioongoza mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu kutoka shule tofauti kwa kuendeleza na kufanikisha kazi hii. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. Irénée NDAYAMBAJE**

**Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Elimu Rwanda**

**SHUKRANI**

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki, jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziwaendee viongozi wa shule mbalimbali walioruhusu walimu wao kufanya kazi na Bodi ya Elimu Rwanda katika mradi wa ukamilishaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu ambao juhudi zao na uandikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, shukrani ziwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

# YALIYOMO


**DIBAJI**..........iii
**SHUKRANI**..........v
**UTANGULIZI**..........1

**SURA YA 1: NADHARIA NA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI** .......... **3**

SOMO LA 1: FASIHI YA KISWAHILI NI NINI? .......... 3
SOMO LA 2: SUALA LA UDHAMINI WA KAZI ZA SANAA ZA FASIHI SIMULIZI 14
SOMO LA 3: TANZU NA VIPERA VYA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI .......... 21
SOMO LA 4: NYIMBO ZA KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI.......... 33
SOMO LA 5: METHALI ZA KISWAHILI.......... 44
SOMO LA 6: NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI.......... 53
SOMO LA 7: VITENDAWILI VYA KISWAHILI .......... 64
SOMO LA 8: USHAIRI WA KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI .......... 75
SOMO LA 9: KUAINISHA SENTENSI ZA KISWAHILI.......... 83

**SURA YA 2: FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI** ........ **95**

SOMO LA 10: UHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI NA VIPENGELE VYAKE ..... 95
SOMO LA 11: KUHAKIKI HADITHI ZA KISWAHILI .......... 102
SOMO LA 12: KUHAKIKI METHALI ZA KISWAHILI .......... 116
SOMO LA 13: KUHAKIKI VITENDAWILI VYA KISWAHILI.......... 124
SOMO LA 14: KUHAKIKI NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI .......... 132
SOMO LA 15: KUHAKIKI NYIMBO ZA KISWAHILI.......... 138
SOMO LA 16: KUHAKIKI MASHAIRI SIMULIZI YA KISWAHILI.......... 149
SOMO LA 17: KUTOA MAONI BINAFSI JUU YA KAZI YA FASIHI SIMULIZI.... 158
SOMO LA 18: KUTOA UWASILISHAJI KUHUSU KAZI ZA FASIHI SIMULIZI.... 164
SOMO LA 19: TUELEWE MUUNDO WA SENTENSI ZA KISWAHILI .......... 172

**SURA YA 3: UTUNGAJI WA BARUA RASMI, SIMU NA MATANGAZO** .......... **179**

SOMO LA 20: UTUNGAJI WA BARUA RASMI AU YA KIKAZI .......... 179
SOMO LA 21: UTUNGAJI WA SIMU .......... 186
SOMO LA 22: UTUNGAJI WA MATANGAZO .......... 192
SOMO LA 23: KUPAMBANUA SENTENSI ZA KISWAHILI .......... 198

**SURA YA 4: UFAHAMU NA UFUPISHO** .......... **206**

SOMO LA 24: UFAHAMU WA HABARI .......... 206
SOMO LA 25: UFUPISHO WA HABARI .......... 214

SOMO LA 26: MUHTASARI WA MATUMIZI YA NYAKATI KUU ZA KISWAHILI . 220
**FAHARASA AU ORODHA YA MSAMIATI ULIOTUMIWA................................. 225**
**MAREJEO.................................................................................................. 230**

# UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hayo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi nchini Rwanda na hata katika jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa kidato cha tano, michepuo mingine, katika ngazi ya juu ya sekondari nchini Rwanda.

Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki imegawanywa katika masomo. Masomo haya yamegusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu
- Matumizi ya msamiati wa msingi
- Sarufi
- Kusikiliza na kuzungumza
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwa sababu Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo, utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu ujinsia na elimu jumuishi.

Ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya kazi zilizotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki. Kazi nyingi zilizopendekezwa zitamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa muda mrefu. Vilevile, kazi za mijadala ya kibinafsi na ya makundi zote zitasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha.

Kazi za makundi zilizopendekezwa zitamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi akumbuke kwamba kitabu hiki kinafuata vitabu vingine vya Kiswahili ambavyo viliandaliwa kwa wanafunzi wa vidato vingine nchini Rwanda. Kwa hiyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa awali wa kutosha ambao utamwezesha kuelewa mada zilizotolewa katika kitabu hiki kwa kuhakikisha kwamba amepata uwezo wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za maisha.

# SURA YA 1: NADHARIA NA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI KATIKA KISWAHILI


## SOMO LA 1: FASIHI YA KISWAHILI NI NINI?

**Kazi ya 1:**

Jiunge na mwenzako na kutazama picha ya hapa chini. Toeni **maoni** yenu kuhusu picha hiyo.

**Kazi ya 2:**

Elezeni **maana** ya jambo linalozungumziwa.




**Kazi ya 3:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusisheni** na picha hiyo.

***Dhana ya fasihi na fasihi ya Kiswahili***

Somo hili si geni kwa mwanafunzi kwani ni mada iliyoshughulikiwa katika Kitabu cha Mwanafunzi, kidato cha nne. Hatuwezi kusema kuwa tulisoma mengi katika muktadha huu kwa sababu tulitoa maelezo bila kuingia kwa undani. Mara hii, ndipo tunatarajia kufasili kwa kina fasihi ya Kiswahili.

### 1. Nadharia ya fasihi na dhana yake

Fasihi, kama dhana, ilielezwa na wataalamu wengi kwa kuegemea nadharia na mitazamo mbalimbali. Ieleweke kuwa nadharia ni taratibu, kanuni na misingi inayomwongoza mtafiti au mtaalamu. Nadharia husaidia katika kulielezea vema jambo fulani kwa mtazamo imara zaidi kuliko mtazamo mwingine.

Nadharia kuhusu kueleza chanzo, ukuaji na ueneaji wa fasihi simulizi ni nyingi.

Katika muktadha wa nadharia hizi, mitazamo mbalimbali iliendelea kumiminika:

- Wengine waliitazama fasihi kama mwavuli wa mtu, jamii, utu, maisha, hadhi na taadhima;
- Wengine waliitazama kama kioo na mwonzi wa maisha ya mtu na jamii;
- Wengine walisema kuwa ni kazi ya sanaa inayotumia lugha ili kuwasilisha ujumbe au fikra za fanani;
- Wengine walipata kutaja sihiri kuwa ni chanzo kimojawapo cha dhana ya fasihi ilhali sihiri ni sehemu ya mila na desturi za jamii nyingi duniani;
- Wengine wa kimagharibi walisisitizia kwamba fasihi humaanisha maandishi na matokeo yake , mtazamo ambao unaipuuza fasihi simulizi na kadhalika.

Watu hawa wote tusiwabishie kwani waliendeleza utafiti kuhusu dhana hii. Isitoshe, ubishi si kiwango chanya cha usomi.

Tukizingatia mitazamo hii na mingine ambayo haikutajwa, kinachoonekana ni kuwa fasihi:

a. inagusa ufasaha wa lugha;
b. chanzo chake kisitafutwe nje ya watu wa jamii husika;
c. ni kongwe ndani ya kila jamii ya watu na kila jamii ina fasihi yake inayoelezwa kwa lugha yake.

Maana inayopewa dhana ya fasihi huchukuana na mambo mbalimbali kama vile:

- matumizi ya dhana yenyewe;
- watu wanaohusika yaani jamii ya watu;
- mahali dhana hiyo inamotokea;
- kipindi au wakati husika.

Hivyo basi, tukiziangalia fasili zote na kuzifafanua ipasavyo, tunaweza kusema kuwa fasihi:

a. ni hazina ya kazi za kubuni za sanaa inayotumia lugha yaani maneno kama njia ya kuwasilisha mambo yake;

b. inatumia lugha mahususi, yenye mvuto na mguso wa kusisimua. Fasihi hutawaliwa na kaida na masharti ya kisanaa, ni kusema kuwa maneno hupangwa kisanaa);
c. inaweza kutumia lugha kwa njia ya masimulizi na kuitwa “fasihi simulizi”. Inapotumia lugha kwa njia ya maandishi huitwa “fasihi andishi”. Hizi ndizo nyanja kuu za fasihi;
d. inaundwa na kazi za sanaa zinazowasilisha ujumbe fulani kwa hadhira inayokusudiwa. Ni kusema kuwa fasihi hulenga hadhira fulani ambayo huiathiri. Ujumbe huo hutokana na hisia za binadamu katika maisha yake ya kila siku;
e. inahusu maisha ya jamii husika lakini si kwa kutoa picha ya moja kwa moja kama historia.

Kwa machache, fasihi ni sanaa ya lugha inayoshughulikia masuala mbalimbali yanayomhusu binadamu kama vile:

- matatizo yake;
- ndoto zake;
- matumaini yake;
- migogoro yake na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake.

**2. Dhima ya fasihi**

Kila fasihi ina umuhimu wake kwa jamii ya watu husika. Jambo hili linatokana na hali ile ya fasihi kujishughulisha na ubinadamu na mazingira yake ya kila siku. Umuhimu huo unaweza kujitokeza katika nyanja mbalimbali kama vile:

a. kiuchumi;
b. kisiasa;
c. kijamii;
d. Na kiutamaduni;

Fasihi inaweza:

- Kuburudisha, kufurahisha na kuchangamsha jamii: Kupitia tanzu mbalimbali kama vile hadithi, mashairi, nyimbo na vitendawili, fasihi huwa na kusudi la kufurahisha, kutumbuiza na kusisimua hadhira.
- Kuelimisha jamii: Fasihi hutumika kama wenzo wa kufundisha wanajamii kuhusu vipengele mbalimbali vya maisha. Hapa tunaweza kutaja:
  - kuishi kwa amani na kuendeleza jamii;
  - kujikomboa kifikra na kiuchumi;
  - ubaya wa ufisadi;
  - kufichua uozo wa jamii;
  - kumkomboa mnyonge kutoka dhuluma na kadhalika.
- Kuionya jamii na kuipa mwelekeo: Fasihi inasaidia katika kuhakikisha kama wanajamii wana maadili yanayotakiwa na jamii husika. Hivyo, wanajamii wanapewa mwongozo kuhusu jinsi ya kufuata mwelekeo unaokubalika

katika jamii. Mwelekeo mzuri ni kama ule unaowahimiza wanajamii kushughulikia:

- usawa wa kijinsia;
- kuepukana na mabaya kama vile mauaji ya kimbari;
- kutilia mkazo elimu isiyo na ubaguzi na kadhalika.

- Kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii: Wanajamii hufahamishwa kifasihi historia yao, chimbuko lao, jadi zao. Kwa hiyo, wao huweza kujielewa vizuri na kujitambua.
- Kuunganisha jamii na vizazi: Mila, tamaduni na itikadi husika za vizazi hurithishwa kwa vizazi vingine kwa kupitia kazi za fasihi. Kizazi huweza kujinasibisha na maisha ya kizazi kilichotangulia kunapokuwa na uwiano wa amali, mwelekeo na maadili.
- Kukuza na kuendeleza kipawa cha lugha: Fasihi hutumia lugha kufikisha ujumbe wake kwa jamii. Lugha hiyo ni ya kisanaa zaidi na yenye mvuto kwa wasikilizaji au wasomaji wanaohitaji kuwa na utajiri mkubwa huo wa lugha. Mtu anaposikiliza au kusoma kazi ya fasihi anapata ujuzi wa lugha unaotokana na vipengele imara mbalimbali vya fasihi. Kwa hiyo, fasihi inajitokeza kama chombo cha kukuza lugha.
- Kukuza uwezo wa kufikiri: Kazi nyingi za fasihi kama vile vitendawili, nahau, hadithi,...huichochea hadhira kufikiri sana ili kupata suluhisho. Katika kuweza kufikiri, ndipo inatuimarisha kuwa na ujasiri wa kujiamini na uwezo wa kugundua dharau au kedi inayotuhusu. Kwa mfano, inasemekana kuwa SENGO, mwanafasihi Mtanzania mmoja, aliulizwa na mtu mwenzie mmoja akiwa Ulaya “Je, ni kweli kwamba Afrika kuna manyani weusi wengi?” Alipoligundua lililokuwa linamaanishwa, ndipo alijibu, “Ni kweli, kama walivyo manyani weupe wengi huku Ulaya!” Ujuzi mkubwa alionao katika lugha kutokana na fasihi ulimwezesha kujitetea ipaswavyo na kutokosa sifa zake za kimsingi na utu wake.

### 3. Fasihi ya Kiswahili

Siyo jambo rahisi kueleza kuhusu fasihi ya Kiswahili. Licha ya kuwa Kiswahili kilianzia Pwani ya Afrika Mashariki, historia ya eneo hilo imefanya kuongezeka kwa idadi ya Waswahili kutoka pande mbalimbali za dunia. Aidha, maendeleo ya Kiswahili pia yalisababisha Kiswahili kuvuka mipaka ya eneo la awali la watumiaji wa Kiswahili. Hivyo, tunapoongelea Fasihi ya Kiswahili, ni muhimu kutilia maanani namna ambavyo jamii ya Waswahili ilivyo mchanganyiko. Hivyo, tunaweza kuiangalia fasihi ya Kiswahili kwa kujiegemeza katika jamii mahususi ya Waswahili wa eneo fulani kama vile Pemba, Unguja, Mombasa, Tanga, Waswahili wa bara, na pia tunaweza kujiegemeza katika jamii pana ya Waswahili kwa kuzingatia mawanda ya kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki na maeneo mengine.

Jamii hii pana ya Waswahili ina mambo yanayofanana. Hata fasihi yake, msingi wake ni kutoka katika jamii mahususi za Waswahili au katika jamii zilizoshirikiana kwa muda mrefu na Waswahili. Hivyo basi, fasihi ya Kiswahili ni ile iliyoandaliwa na mswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili na ikiakisi utamaduni wa Waswahili kama jamii mahususi au jamii pana ya Waswahili.

Kwa kuwa mtunzi wa Fasihi ni zao la jamii yake hatuwezi kumtenga Mswahili na jamii yake ya Kiswahili na hivyo hata kazi yake lazima itakuwa inawahusu Waswahili wenzake. Hivyo, Fasihi ya Kiswahili ya Waswahili lazima iwe inawazungumzia Waswahili. Hata iwapo inawazungumzia watu wa jamii nyingine lakini mtunzi ni Mswahili basi hiyo itakuwa ni Fasihi ya Kiswahili ya watu hao waliotungiwa.

**4. Fasihi kwa Kiswahili**

Kazi za sanaa za fasihi ya Kinyarwanda au ya Kirundi au ya Kiingereza zikiandikwa kwa Kiswahili haziwezi kuitwa kazi za fasihi ya Kiswahili. Hili linatokana na kuwa ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima:

a. izungumzie utamaduni wa Waswahili;
b. na itungwe katika Kiswahili.

Wajamaika walioko Uingereza kwa miaka na karne nyingi hawajakubalika kuwa ni Waingereza. Hivi ndivyo zilivyo kazi za kifasihi zilizotafsiriwa katika Kiswahili. Kazi za fasihi ya Kinyarwanda au ya Kiingereza zinahusu utamaduni wa Wanyarwanda au Waingereza ilhali zimetafsiriwa katika Kiswahili. Kazi hizi zote za kifasihi zisizo za Waswahili zinaingia katika “fasihi kwa Kiswahili”.

## A. Maswali ya Ufahamu

**Kazi ya 4:**

**Soma** kifungu cha habari hiki **zaidi ya** mara moja kisha ujibu maswali yafuatayo :

1. Nadharia ni nini?
2. Unakubali kuwa sihiri ni chanzo cha fasihi? Eleza kinaganaga.
3. Je, ni upi umuhimu wa fasihi katika jamii?
4. “Fasihi simulizi ya Kiswahili haikuwepo kabla ya majilio ya wageni sehemu za pwani ya Bahari ya Hindi”. Eleza kinagaubaga.
5. “Siku za leo, hatuwezi kuwapata watu wanaotunga kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili”. Unafikiri nini kuhusu kauli hii? Eleza vizuri.
6. Eleza kidogo nadharia za ubadilikaji taratibu, msambao, nadharia ya kisosholojia, nadharia ya utaifa na nadharia hulutishi.
7. “Fasihi kwa Kiswahili” ni nini?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Sikiliza** jinsi wenzako wanavyokisoma kifungu cha habari hicho.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

**Soma** kwa sauti na ufasaha kifungu cha habari hicho.

**Kazi ya 7:**

**Soma** sentensi mbalimbali zifuatazo na **kuchagua** sehemu ya pili ambayo inaweza kukamilisha ipaswavyo ile ya kwanza kwa kila sentensi:

| | |
|---|---|
| 1. Fasihi, kama dhana, ilielezwa na wataalamu wengi kwa kuegemea | zikiandikwa kwa Kiswahili huitwa kazi za fasihi kwa Kiswahili. |
| 2. Nadharia ya kiutandawazi imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni | na kuchangamsha jamii. |
| 3. inaundwa na kazi za sanaa zinazowasilisha ujumbe | nadharia na mitazamo mbalimbali. |
| 4. Fasihi inaweza kuburudisha, kufurahisha | tofauti na vile vinavyopendelewa na Wakongo. |
| 5. Waswahili walikuwa na eneo lao, jadi zao, vyakula vyao | ubadilikaji taratibu, msambao na nadharia ya kisosholojia. |
| 6. Kazi za sanaa za fasihi ya Kinyarwanda au ya Kirundi au ya Kiingereza | fulani kwa hadhira inayokusudiwa. |

**Kazi ya 7:**

Simama mbele ya darasa na **kukamilisha** sentensi zifuatazo **mwanzoni, katikati au mwishoni** kama zilivyotumiwa katika habari:

1. ..............................................miaka na karne nyingi hawajakubalika kuwa ni Waingereza.
2. Fasihi ya Kiswahili inaundwa na nyanja kuu mbili yaani................na fasihi andishi ambayo ni changa.
3. Nadharia husaidia katika kulielezea vyema jambo fulani kwa mtazamo imara...........................

**Kazi ya 9:**

Tazama picha ifuatayo. **Sema** ni utanzu gani wa fasihi simulizi inaouwakilisha:




## d. Msamiati

**Kazi ya 10:**

Shirikiana na mwenzako mtumie Kamusi ya Kiswahili Sanifu ili kuweza kuelewa **maana** ya maneno yafuatayo:

**Chanya**
**Utandawazi**
**Kuhuluti (sha)**
**Hadhi**
**Ufisadi**
**Taadhima**
**Jadi**
**Kedi**

**Kazi ya 11:**

**Tunga** sentensi kwa kutumia maneno ya **hapo juu**. (Sentensi moja kwa kila neno)

**Kazi ya 12:**

Maneno yafuatayo yameendelezwa vibaya. Simama mbele ya darasa na **kuyaendeleza vizuri**. (Mfano: rampi--------mpira).

1. Adharina;
2. Zamotam;
3. Shiubi;
4. Pawaki.

**Kazi ya 13:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia **neno sahihi** kati ya haya: [**umuhimu; ufukara; ubishi; ufasaha; inashughulikia; kiutandawazi; nyenzo; husika**]

1. Nadharia ya ........................ ni mojawapo kati ya nadharia zinazohusu kueleza chanzo, ukuaji na ueneaji wa fasihi simulizi.
2. Serikali ya Rwanda imeanza kuhamasisha hadhira ..................... kuhusu amani na maendeleo ya kudumu.
3. ................................wa lugha huwasaidia viongozi mbalimbali kuaminiwa na raia kuhusu mikakati iliyochukuliwa na serikali zao.
4. ....................... unaendelea kupigwa marufuku nchini Rwanda kutokana na sera thabiti za serikali.

**Kazi ya 14:**

Andika sentensi zifuatazo kwa neno lililotumiwa katika kifungu cha habari na lenye **maana sawa** na lile lililochapwa kwa italiki na kupigiwa mstari:

1. Fasihi ni ***ya zamani sana*** ndani ya kila jamii ya watu.
2. Kazi zote za fasihi ya Kirundi ***zilizotolewa*** katika Kiswahili si za fasihi ya Kiswahili.
3. Uamuzi wa serikali yetu wa kutilia mkazo lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari unatokana na ***kiwango na uzito*** wake barani Afrika.

**Kazi ya 15:**

Katika jozi, changanueni maneno haya kutokana na **maana zake** na kuyaandika katika makundi yake halisi

Kirundi
Mwanafunzi
Ndoto
Kiroboto
Kimashomvi
Mwanafasihi
Kiingereza
Mnyonge
Ulimwengu
Kimanyema




## E. Kuzungumza

**Kazi ya 16:**

Jiunge na mwenzako na kujaribu **kuiga matamshi sahihi** ya maneno mbalimbali na kiimbo kinachofaa.

**Kazi ya 17:**

Simama mbele ya wenzako na **kuwaambia** yale ambayo umeyasoma katika kifungu cha habari chetu.

**Kazi ya 18:**

"Fasihi ya Kiswahili inatumia lugha ya Kiswahili ili kuupeleka ujumbe kwa hadhira husika". Ujumbe huu unaweza kuhusu elimu isiyo na ubaguzi. Waambie wenzako ujumbe mwingine unaoweza kutolewa.

**Kazi ya 19:**

Kwa njia ya mazungumzo, tazama mfano huu na **kisha kamilisha** sentensi zifuatazo kwa jibu sahihi:

| | |
|---|---|
| **Fasihi inajitokeza kama** | **chombo cha kukuza lugha** |
| | ........................................................ |
| | ........................................................ |
| | ........................................................ |

**Kazi ya 20:**

**Tazama** picha hii. Kuna uhusiano gani kati ya fasihi simulizi ya Kiswahili na maandishi yaonekanayo kwenye picha hiyo?







## F. Cheka uongeze siku za kuishi

**Kazi ya 21:**

Masai alipeleka redio yake kwa fundi ili itengenezwe. Ilipofunguliwa walitoka mende wengi sana. Masai alipoona hivyo, akamwambia fundi ''Kamata hao watangazaji waendelee na kazi yao!" Waambie wenzako kichekesho kingine cha Kiswahili unachokijua.

## G. Kuandika

**Kazi ya 22:**

Katika jozi, andikeni sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| Lugha | ni | mfumo | wa | sauti | nasibu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**Kazi ya 23:**

Andika jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| Ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima............................................... |
| Ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima............................................... |

**Kazi ya 24:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** neno lililoandikwa kwa italiki (mfano mmoja ulitolewa):

| Fasihi | hutumia | lugha | kufikisha | ujumbe | wake | kwa | *jamii* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Fasihi | hutumia | lugha | kufikisha | ujumbe | wake | kwa | ........... |

**Kazi ya 25:**

Katika kundi la wanafunzi watatu, **someni** matini ifuatayo na kuchunguza kama ni ya **kifasihi** au la. **Andikeni** sababu zinazowafanya kuwa na mtazamo huo na **kuzisomea** wenzenu.

[***Historia ya Shujaa Fumo Liyongo***]

Fumo Liyongo ni shujaa kama alivyoelezwa na Muhamadi Kijunwa mwaka 1913 BK. Japo kuna utata kuhusu tarehe aliyozaliwa Liyongo lakini tarehe inayoelekea kukubaliwa zaidi ni ile ya karne ya 13–14 BK. Baadhi ya vitabu vinamtaja mtawala wa eneo la Ozi aitwaye Fumo Liyongo aliyeishi wakati wa utawala wa Fumomari (Fumo Omari), mtawala wa ki-Nabhany wa dola ya Pate. Fumomari alitawala miaka ya 740 – 795 Hijriya (Miaka ya Kiislamu), sawa na 1340–1393. Liyongo huyo alipigana na Fumomari (Mulokozi 1999).

Vyanzo vinaonyesha kuwa Liyongo aliishi pwani ya Kaskazini mwa Kenya kwenye maeneo ya Pate na Ozi. Mama yake aliitwa Samoa Mwana. Liyongo alikuwa kiongozi katika jamii yake, japo hakuna uhakika kama alikuwa mfalme. Alikuwa shujaa, manju wa ngoma na malenga, na mwindaji hodari.

Kwa upande wa dini, hakuna uhakika kama alikuwa Mkristo au Mwislamu japo nyimbo zake zinaonesha kuwa huenda alikuwa mfuasi wa dini ya Jadi ya Waswahili. Liyongo alikuwa akiwinda na kufanya biashara sehemu za bara karibu na Pate. Aliweka makazi yake Ozi, na alifia na kuzikwa Kipini, mahali paitwapo Uungwana wa Mashaha (Mulokozi na Sengo 1995:52-53).

Liyongo ni shujaa aliyependwa na watu kwa kuwa aliwapigania na kuwasaidia. Kwa mfano, aliwasaidia Waggala kupata mbegu bora, aliishi porini na Watwa na kushirikiana nao vizuri, ushirikiano uliomsaidia kumnusuru na njama za mfalme za kutaka kumuua. Kutokana na uhusiano mzuri aliokuwa nao na jamii yake, Mfalme alimwonea wivu kwa kuogopa kuwa angeweza kumpokonya madaraka (ufalme). Alifanya njama za kumuua. Njama hizo hazikufanikiwa na ilimbidi mfalme amtumie mwanawe Liyongo ili amsaliti baba yake kwa kuahidiwa kuozwa binti mfalme, kupewa uwaziri na mali nyingi. Mtoto wa Liyongo alimuuliza babaye siri ya nguvu zake. Alipoambiwa kuwa ni kuchomwa sindano ya shaba kitovuni, alikubali kumchoma baba yake hatimaye Liyongo akafariki dunia. Mwanawe naye alikufa kutokana na uovu wake. Baada ya shujaa Liyongo kufa watu walisikitika, waliomboleza na wengine walionekana kukata tamaa kwa kuwa shujaa huyu alikuwa ni mtetezi wa watu katika jamii.

Taswira ya kifo cha shujaa Liyongo inaweza kujitokeza kwa namna tatu (3): Kwanza, kifo cha shujaa Liyongo kwa mfalme ni mafanikio kwa kuwa ana uhakika wa kuendelea kutawala. Hili linatokana na kuwa na hofu kuwa Fumo Liyongo angemnyang'anya ufalme kwa vile alivyokuwa na mshikamano na watu. Pili, kifo cha Liyongo kwa mwanawe ni adhabu kwani baada ya shujaa huyu kufa mwanawe naye alikufa kutokana na maradhi yasiyopona pamoja na kuchukiwa na jamii yote kwa ujumla. Tatu, kifo cha Liyongo kwa jamii yake ni sawa na kupoteza kitu chenye thamani kwa vile Liyongo alikuwa na mshikamano na jamii yake. Baada ya kifo chake watu waliomboleza na walionekana kukosa matumaini.

Kwa upande wa fasihi, kifo cha shujaa Liyongo kimejengwa katika dhana ya usaliti unaosababishwa na tamaa ya madaraka (Ufalme) na tamaa ya mali (Mtoto wa Liyongo). Mfalme (sultani) wa Pate alifanya fitina za kumuua Liyongo akiogopa kupokonywa ufalme. Mwanawe Liyongo naye alikubali kumsaliti baba yake kwa matarajio ya kuozwa mke (binti wa mfalme), kupewa mali na uwaziri pia. Dhana ya usaliti imejitokeza sana katika kazi za kifasihi na inaonekana kuwa ni silaha ya kumwangusha shujaa. Kwa upande mwingine dhana hii ina sura mbili yaani faida (anayenufaika baada ya usaliti) na hasara (anayeathirika baada ya usaliti).

Kifo cha shujaa pamoja na usaliti vinatupatia vinyume vya dhambi na mapatilizi. Ingawa mtoto wa Liongo alimsaliti babaye ili apewe zawadi nono hakutimiziwa ahadi hizo. Alinyanyaswa na hatimaye alikufa kama alivyokufa baba yake. Hii inaashiria kuwa katika mapigano kati ya wema na uovu, siku zote wema hushinda. Kwa hiyo hata sultani hakuwa na maisha marefu.

Historia imelishuhudia hili kwa kuwa muda si mrefu utawala wa kisultani ulivamiwa na ukoloni. Hata ukoloni huo nao leo hii haupo. Maisha ya milele ni maisha ya kutenda wema na haki.


## SOMO LA 2: SUALA LA UDHAMINI WA KAZI ZA SANAA ZA FASIHI SIMULIZI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kuitazama picha ya hapa chini. **Mnaona nini** kwenye picha hiyo?

**Kazi ya 2:**

Kwa maoni yenu, wanazungumzia **nini**?




**Kazi ya 3:**

Katika jozi, baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **mkihusishe** na picha hii.

Fasihi simulizi ni hazina kubwa ya kazi za sanaa zilizoumbwa kwa njia ya masimulizi. Fasihi hii huhitaji utafiti ili kukusanya data hizo na kuzifanyia uchambuzi ndio unaowawezesha wanafasihi kuhakikisha kuwa kazi fulani niya kifasihi au la.

Utafiti huo au ukusanyaji wa data na habari zinazohusu fasihi hauwezi kutekelezwa bila msaada wa kifedha yaani udhamini. Udhamini huu unamwezesha mtafiti kukidhi mahitaji fulani yanayohusu kazi hiyo ngumu ya ukusanyaji wa data.

### 1. Umuhimu wa utafiti katika fasihi simulizi

Jambo lolote la kisayansi linadai utafiti. Ukusanyaji wa data na habari zinazohusu fasihi simulizi au utafiti katika fasihi simulizi nao unafuata kanuni hiyo. Kuna mambo manne yanayolengwa na utafiti huo ambayo ni:

a. Kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa. Suala hilo ni kama vile:
   - mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu;
   - mafunzo kuhusu amani na maendeleo;
   - mafunzo kuhusu mauaji ya kuangamiza na kadhalika;

b. Kuongeza hazina ya maarifa katika uwanja unaohusika;

c. Kupima hali, fikra, mitazamo, na matarajio ya jamii ya watafitiwa;

d. Kuchangia katika kujenga na kuendeleza fani za fasihi simulizi na fani nyinginezo.

### 2. Pande zinazohusika katika utafiti

Katika utafiti wowote wa fasihi simulizi, zipo pande tofauti. Ni lazima pande hizo zisaidiane ili utafiti ulifikie lengo lake. Pande hizo ni:

- Mtafitiwa: Ni upande wa mtu au watu wanaochunguzwa. Ndiye anayemiliki data zinazotakiwa na walio katika mazingira maalum ya kijamii na kijiografia. Mazingira haya ndiyo mandhari ya fasihi simulizi husika. Wajibu wake ni:
  - kutoa taarifa;
  - kujenga uhusiano na mtafiti;
  - kuchagua taarifa za kumpa mtafiti;
- Mtafiti: Ndiye mtaalamu ambaye, pamoja na wasaidizi wake, anashughulikia ukusanyaji wa data na habari zozote zinazotakiwa katika uwanja huo. Baada ya kuzipata data hizo, mtafiti huzilinganisha, huzichambua, hizifasili, huzitathmini, na kuzijumuisha. Kazi hizi zinamsaidia ili kupata matokeo kamili ya utafiti wake;
- Mdhamini: Ndiye anayetoa fedha za kugharamia utafiti. Pesa hizo ndizo zinazomsaidia mtafiti katika kufikia shabaha yake. Mdhamini ndiye anayeweka malengo ya kiujumla ya utafiti na kupokea matokeo yake.

### 3. Uhuru wa mtafiti katika fasihi simulizi

Ingekuwa vizuri mtafiti awe na uhuru katika kazi yake. Walakini, ukweli ni kwamba uhuru na hiari aliyo nayo ni ile tu anayopewa na mdhamini wake. Mdhamini ndiye anayeainisha nyanja za kufanyia utafiti, aula za utafiti na watafiti wenyewe. Ndiye anayetoa fedha na nyenzo za utafiti na kupokea matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, mtafiti analazimishwa kuwa karagosi wa mdhamini.

Mdhamini naye huwa mara nyingi mwakilishi wa watu wengine wenye mamlaka juu yake au serikali. Ni kusema kuwa, mtafiti atajikuta akifanya utafiti ili kuendeleza na kutekeleza malengo na masilahi ya wengine. Watu wengine hao ni kama vile serikali au wale wenye mamlaka juu ya mdhamini. Malengo hayo yanaweza kuwa ya kiitikadi, kisiasa au kiuchumi. Kama matokeo ya utafiti hayaoani na matakwa au itikadi zao, yanaweza kuzuiwa na watu hao yasijulikane kwa raia. Jambo hili linadhihirisha kuwa mtafiti, kwa kujua au bila kujua, ni mwakilishi wa kiitikadi wa upande huo.

### 4. Athari za udhamini katika fasihi simulizi

Tumeona kuwa mdhamini ndiye mwenye fedha zinazotumiwa katika utafiti. Kwa hiyo, kazi ya mtafiti na matokeo yake huathiriwa sana na fikra na malengo ya mdhamini au upande anaouwakilisha. Katika muktadha huu, tunaona kwamba:

a. Kwa kawaida, mambo yanayochunguzwa ni yale tu yanayotakiwa, yanayohitajiwa au yanayokubaliwa na mdhamini. Kwa mfano, mtu anayepinga mauaji ya kimbari yaliyotokea nchini Rwanda hatapendelea udhamini wa kazi za kifasihi katika uwanja huo.
b. Mapana ya utafiti kidata, kijiografia na kimaudhui huamuliwa na mdhamini na hutegemea mahitaji yake na kiasi cha pesa anachotoa. Ni kusema kuwa, akiwa na uwezo mkubwa wa kifedha au mahitaji ya kushughulikia jambo fulani, anaweza kupanua kabisa uwanja wa utafiti kwa mtafiti wake.
c. Mara nyingi, fasiri na ufafanuzi rasmi wa data hubidi ulingane na mtazamo wa kiitikadi wa mdhamini. Ni sharti mambo yalingane na imani yake.
d. Mara nyingi, matokeo ya utafiti ni mali ya mdhamini. Ni kusema kuwa hutumiwa naye ili kuendeleza masilahi na malengo yake. Si lazima masilahi na malengo hayo yalingane na yale ya mtafiti au ya jamii inayotafitiwa. Wakati mwingine, matokeo hayo yanaweza hata kutumiwa kwa kuikandamiza au kuiangamiza jamii hiyo.

Kama hitimisho, tunaweza kusema kuwa ingekuwa vizuri mtafiti awe jasiri katika kazi yake ili lengo lake lifikiwe. Ingekuwa lazima atumie fursa yoyote kwa kutetea ukweli wa kisayansi dhidi ya uongo wa baadhi ya wadhamini.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 4:**

Jiunge na mwenzako na kujibu maswali yafuatayo:

1. Ni upi umuhimu wa udhamini kwa mtafiti ?
2. Ni ipi shabaha ya utafiti katika fasihi simulizi ?
3. « kazi ya utafiti hudai ushirikiano wa watu mbalimbali ». Eleza vizuri kwa kutoa mifano.
4. Ni mambo gani ambayo upande wa watafitiwa unalazimishwa kutimiza ili kitendo cha utafiti kiweze kufaulu ?
5. "Uhuru na hiari mtafiti aliyo nayo ni ile tu anayopewa na mdhamini wake". Eleza jahara.
6. Namna gani matokeo ya utafiti katika fasihi simulizi huathiriwa na udhamini ?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako au mwalimu anavyoisoma matini hiyo na kutilia mkazo matamshi yake bora.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

**Soma** tena kifungu cha habari kimoyomoyo na kujaribu **kumwiga** mwenzako au mwalimu kwa sauti.

**Kazi ya 7:**

Katika jozi, tazameni picha ifuatayo. **Husisheni** picha hiyo na uhusiano wa kikazi uliopo kati ya mtafiti na mdhamini wake.



**Kazi ya 8:**

**Soma** kwa sauti sentensi zifuatazo na **kuzikamilisha** kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Baada ya kuzipata data hizo, mtafiti huzilinganisha, huzichambua, .......................... |
| 2. Ingekuwa lazima atumie fursa yoyote kwa ..................... dhidi ya uongo wa baadhi ya wadhamini |

**Kazi ya 9:**

Soma kwa sauti maneno yafuatayo kwa kuzingatia matamshi bora:

1. Udhamini;
2. Athari;
3. Kukidhi;
4. Maalum;
5. Kiitikadi

## D. Msamiati

**Kazi ya 10:**

Shirikiana na mwenzako na kujadiliana juu ya maana ya maneno yafuatayo au mtumie **Kamusi** ya Kiswahili Sanifu.

**Data**
**Aula**
**Wenzo (nyenzo)**
**Itikadi**
**jasiri**

**Kazi ya 11:**

Shirikiana na mwenzako na **kutunga** sentensi zinazohusu **mazingira na maendeleo ya kudumu** kwa kutumia maneno ya hapo juu:

**Kazi ya 12:**

Kamilisha sentensi zifuatazo ***zilizotumiwa*** katika kifungu cha habari cha hapo juu

1. Mapana ya utafiti kidata, ....................................huamuliwa na mdhamini na hutegemea mahitaji yake na kiasi cha pesa anachotoa.
2. Mara nyingi, matokeo ya utafiti ni ........................ya mdhamini.
3. Mtafiti analazimishwa kuwa .................... wa mdhamini.

**Kazi ya 13:**

Katika jozi, **jazeni pengo** kwa kutumia silabi inayofaa ili kulipata neno sahihi la Kiswahili lililotumiwa katika kifungu cha habari cha hapo juu:

1. U---mini;
2. ---ta;
3. ---ala;
4. Ku---ramia;
5. Ma---lahi

**Kazi ya 14:**

Katika pea, **changanueni** maneno haya kufuatana na maana zake na kuyaandika katika makundi yake halisi

Data
Mdhamini
Matokeo
Bakteria
Masilahi
Mtafiti
Kijasumu
Mkariri
Maendeleo
Muflisi
Mtafitiwa
Mkongwe

**1**

**Watu wanaochangia katika kuendeleza utafiti**

**2**

**Mengine**

**Kazi ya 15:**

Katika jozi hiyo, andikeni sentensi zifuatazo kwa kutumia neno moja tu lililotumiwa katika kifungu cha habari na lenye **maana sawa** na lile lililopigwa chapa kwa italiki na kupigiwa mstari:

1. Utunzi wa kazi za fasihi simulizi kuhusu malezi bora hufuata ***kaida*** hizo.
2. Mtafiti anapaswa kuwa ***shujaa*** katika kazi yake ili asije akaathiriwa na mdhamini wake.

**Kazi ya 16:**

Katika pea, **elezeni** kauli zifuatazo:

1. “Udhamini si udhahili“.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 17:**

**Simama mbele** ya darasa uwaambie wanafunzi wenzako yale ambayo umeyasoma.

**Kazi ya 18:**

**Kwa njia ya mazungumzo**, kamilisha sentensi ifuatayo kwa kutumia sehemu nyingine ambayo **inapatikana** katika kifungu cha habari (Mfano umetolewa hapa chini):

| | |
|---|---|
| **Kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa** | **kama vile mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu** |
| Kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa | kama vile............................................................. ....... |

**Kazi ya 19:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza kwa usahihi pengo** linalopatikana katika sentensi ya pili ili iwe ya Kiswahili sanifu. Fuata **muundo** wa sentensi ya kwanza.

| Jambo | lolote | la | kisayansi | linadai | utafiti |
|---|---|---|---|---|---|
| Jambo | lolote | la | kidini | linadai | |

**Kazi ya 20:**

"Ingekuwa vizuri mtafiti awe na uhuru katika kazi yake". Kwa njia ya mazungumzo, wanafunzi wote watoe **maoni** yao kuhusu uhuru wa mtafiti katika kazi yake na umuhimu wake.

## F. Cheka uongeze siku za kuishi

**Kazi ya 21:**

"Mpaka sasa sijaelewa ni shetani gani aliyewadanganya nyinyi mliojifunza mambo ya hesabu! Mkitaka kujua kama kuna tofauti kati ya 1X3 na 3X1 nendeni hospitali mpewe dawa iliyoandikwa 1X3 na badala yake muifanye 3X1. Ndipo mtakapojua kwamba pikipiki inaweza kwenda kwa kasi!" Sasa, **waambie** wenzako kichekesho kingine unachojua.

## G. Utafiti

**Kazi ya 22:**

Shirikiana na wanafunzi watatu na kufanya **utafiti** kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu mbalimbali kuhusu mambo yanayotawala ukusanyaji wa data katika utafiti, vifaa vya utafiti na njia kuu za utafiti. Wasilisheni matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

## H. Kuandika

**Kazi ya 23:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| Si | lazima | masilahi | hayo | yalingane | na | yale | ya | mtafiti |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |

**Kazi ya 24:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** sehemu iliyoandikwa kwa italiki kwa kuzingatia mawazo yanayopatikana katika kifungu cha habari cha hapo juu (mfano mmoja ulitolewa):

| **Wajibu** | **wa** | **mtafitiwa** | **ni** | ***Kutoa taarifa*** |
|---|---|---|---|---|
| Wajibu | wa | mtafitiwa | ni | ........................ |
| Wajibu | wa | mtafitiwa | ni | ........................ |

**Kazi ya 25:**

Katika jozi, jadilianeni kuhusu mada ifuatayo: **"Faida na athari ya udhamini katika kazi za fasihi"** kisha andikeni mawazo makuu:

| **Mada** | **Mawazo makuu** |
|---|---|
| **Faida na athari ya udhamini katika kazi za fasihi** | 1. |
| | 2. |
| | 3........... |


## SOMO LA 3: TANZU NA VIPERA VYA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako mtazame picha zifuatazo. Nini **kinaonekana** kwenye picha hizo?

**Kazi ya 2:**

Kwa maoni yenu, ni nini **maana** ya kauli inayoonekana kwenye picha ya kwanza?






**Kazi ya 3:**

Shirikiana na wenzako watatu na **kutofautisha** picha hizo mbili kutokana na tanzu za fasihi simulizi zinazoziwakilisha. Mmoja kati yenu awasomee wengine matokeo ya kazi hiyo.

**Kazi ya 4:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusishe** na picha hizi kwa njia ya mazungumzo.

***Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili***

Kigezo muhimu cha kuainisha fasihi ni namna msanii anavyoupitisha ujumbe wake yaani masimulizi ya mdomo au maandishi. Mintarafu jinsi hii, tuna aina au nyanja kuu mbili za fasihi. Aina hizo ni fasihi simulizi inayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine kwa njia ya masimulizi ya mdomo na fasihi andishi inayotumia maandishi. Katika habari hii tutashughulikia fasihi simulizi ya Kiswahili tu ambayo ni ya awali. Tutatilia mkazo tanzu zake na vipera vya tanzu hizo.

**1. Sifa bainifu za fasihi simulizi ya Kiswahili**

Fasihi simulizi ya Kiswahili kama fasihi simulizi nyingine ina sifa zake. Sifa hizo ni tofauti na zile za fasihi andishi ya Kiswahili. Fasihi simulizi ya Kiswahili:

a. Husambazwa kikalima. Ni kusema kuwa mwanzo wake ni masimulizi na huwasilishwa na kusambazwa kupitia mdomo na vitendo. Utendaji huu ndio unaoifanya iwe hai;
b. Huwa na hadhira mahususi iliyo hai. Hadhira inashiriki moja kwa moja na kuathiri kazi nzima;
c. Huwasilishwa kwa wakati na mahali maalumu kama vile jioni baada ya kazi, katika sherehe na kadhalika;
d. Huwa na mwanzo na mwisho maalumu. Muundo wake ni rahisi kufuatika;
e. Ni mali ya jamii kwani mtunzi hajulikani;
f. Hubadilika kulingana na wakati hasa inapowasilishwa kupitia ufaraguzi. Fanani anaweza kufahamu mawazo ya hadhira yake papo hapo na kuubadilisha uwasilishi wake. Kwa mfano, kwenye sherehe ya harusi, mtu anaweza kutongoa shairi lake na kuingiza mafunzo kuhusu uzalishaji mali au mila na desturi na kuzalisha kwa kiwango;
g. Huwa na wahusika wengi tofauti yaani wahusika wa aina mbalimbali. Msimulizi ndiye mhusika wa kati;
h. Huwa na tanzu nyingi zenye vipera vingi;
i. Hutungwa kila wakati na baadhi yake huzuka papo hapo;
j. Hutumia sauti, mdomo na ishara za mwili. Kwa hiyo, si lazima fanani au hadhira wajue kusoma. Kiungo muhimu katika mapokezi ni masikio;
k. Huhusu visa vya kubuni na vya kihistoria na huhifadhiwa akilini mwa wanajamii;

l. Huwa na uzuri unaotegemea ubingwa wa fanani;
m. Ni kongwe kwani ilianza tu lugha ilipoanza.

Jambo linalobabaisha leo ni upungufu wa idadi ya watu wanaoendelea kujivunia ubunifu wa kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili. Tumeisha jua umuhimu wake katika kuelimisha watu kuhusu mambo mbalimbali kama vile mazingira na maendeleo ya kudumu na mengineyo. Tufanye nini ili suala hili lipatiwe suluhisho?

**2. Sababu za kupungua kwa kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili**

Vizazi vilivyotutangulia vilitajirisha sana fasihi simulizi ya Kiswahili. Vilitunga kazi nyingi sana za sanaa ya lugha kiasi kwamba leo ndizo tunazotumia na kuzifanyia uchambuzi. Waswahili wachache ndio wanaojishughulisha na ubunifu katika fasihi hiyo. Uhaba huu wa kazi hizo unasababishwa na mambo makuu matatu ambayo ni:

- Uvumbuzi wa maandishi: Katika enzi za kale, fasihi simulizi ndiyo iliyokuwa sanaa ya pekee ya lugha. Kupitia fasihi hii, vizazi viliweza kurithi kazi mbalimbali za vizazi vingine. Walakini, wanajamii walizipoteza kazi nyingi kutokana na njia hiyo ya masimulizi. Uvumbuzi wa maandishi ndio uliorahisisha kuhifadhi mila na tamaduni zao. Vilevile, kazi mbalimbali za fasihi simulizi zilihifadhiwa.
- Mfumo mpya wa elimu na maendeleo: Awali, watoto walikuwa wakijumuika kwenye moto nyakati za jioni ili kusimuliwa hadithi au vitendawili. Siku hizi, wanajumuika kwenye kumbi na madarasa yanayoangaziwa kwa kutumia umeme. Wao wametekwa na vifaa vipya kama vile redio, runinga, vitabu na kadhalika. Mfumo huu mpya wa elimu hutilia pia mkazo masomo mengine huku fasihi simulizi ikipuuzwa. Elimu ya vitabu ndiyo inayoshughulikiwa mno kuliko ile ya mapokeo.
- Mwingiliano na mgusano wa jamii mbalimbali: Kule kuingiliana kwa jamii mbalimbali ulimwenguni kulipunguza uhalisia wa fasihi simulizi ya Kiswahili. Hasara za mwingiliano huo ni kama vile kutoweza kujieleza kwa lugha moja, kutoweza kujigamba mbele ya hadhira na kadhalika. Kumeibuka jamii ya Waswahili yenye utamaduni mseto na lugha iliyopunguziwa nguvu zake.

**3. Jambo la kuzingatia ili fasihi simulizi ya Kiswahili iendelee kuwepo**

Ni lazima fasihi simulizi ya Kiswahili ilindwe ipaswavyo ili iendelee kuwepo. Mambo manne ndiyo yanayoweza kupendekezwa:

a. Wanajamii wanalazimishwa kusisitizia utafiti wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi hiyo;
b. Ni vizuri jamii husika iunde mikakati thabiti ya kufundisha fasihi hiyo shuleni;
c. Ni lazima jamii husika ihimize uhifadhi wa kazi za sanaa za fasihi hiyo;

d. Ni lazima lugha ya Kiswahili itumiwe kwa ufasaha ili kupambana na lugha za kikoloni. Kwa hiyo, wanajamii wanatakiwa kutopuuza fasihi simulizi ya Kiswahili.

**4. Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake**

Kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni nyingi. Tukiegemea muundo wake, kazi hizo hujigawa katika makundi makuu manne ambayo ni:

a. Kundi la masimulizi. Masimulizi haya hutumia lugha ya nathari na mtiririko wake huwa mwepesi. Kazi zinazopatikana katika kundi hili huwa zile ambazo husimuliwa hadhira. Katika kundi hili, ndimo tunaupata utanzu wa hadithi. Urefu wa hadithi hutofautiana kutoka kitanzu au kipera kimoja hadi kingine.
b. Kundi la semi. Linaundwa na mafungu ya maneno au tungo fupi zinazotumiwa ili kuleta maana nyingine badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika. Matamko hayo mafupi ya Kiswahili yanapatikana katika tanzu kama vile vitendawili, mafumbo, methali na nahau na misemo.
c. Kundi la ushairi. Kazi za kundi hili, ni zile zinazosisitizia utumiaji wa lugha teule ya mkato na mnato. Sentensi huundwa kwa njia inayoweza kuleta kiimbo kinachopendeza wakati wa kuzitamka. Hapa tunapata utanzu wa nyimbo na utanzu wa ushairi simulizi.
d. Kundi la mazungumzo. Mazungumzo haya ni maongezi au maelezo ya mdomo juu ya jambo fulani katika lugha ya kawaida. Walakini, kila mazungumzo si kazi ya fasihi. Ili mazungumzo yaitwe kazi ya fasihi, ni lazima yawe na usanii wa aina fulani. Katika kundi hili, ndimo tunazipata tanzu za hotuba simulizi, soga na malumbano ya watani.

Baadhi ya tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili huwa na vipera vyake yaani aina zake. Kwa mfano, hadithi simulizi zinaweza kuwa ngano, hekaya au hurafa. Nyimbo zinaweza kuwa za vita, za maombolezo, za kazi na kadhalika. Mashairi ya kimapokeo yanaweza kuwa ya simango, ya uzinduzi, ya waadhi na kadhalika. Hivi ndivyo vipera vya tanzu hizo. Mengi kuhusu vipera hivi yatashughulikiwa katika masomo yatakayofuata hili.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 5:**
Soma kifungu cha habari kilichotolewa hapo juu na kuyajibu maswali yafuatayo:

1. Zitaje sifa bainifu tano za fasihi simulizi ya Kiswahili.
2. “Jambo linalobabaisha leo ni upungufu wa idadi ya watu wanaoendelea kujivunia ubunifu wa kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili”. Je, ni kipi chanzo cha jambo hili?
3. Namna gani mfumo wa elimu mpya na maendeleo huchangia katika kupunguka kwa idadi ya kazi za fasihi simulizi?
4. Tunalazimishwa kufanya nini ili kazi za fasihi simulizi ya Kiswahili ziendelee kutungwa?
5. Taja na kueleza vipera vya utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili unaoingia katika kundi la masimulizi.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 6:**

**Sikiliza** kwa makini yale anayoyasoma mwanafunzi mwenzako.

## C. Kusoma

**Kazi ya 7:**

Soma matini mara **nyingine** kwa sauti ili kuifahamu vizuri.

**Kazi ya 8:**

Tazama picha ifuatayo. Unaona **nini**? Kuna hadithi nyingi za Waswahili au Wanyarwanda zinazohusu wahusika hawa. Katika jozi, tafuteni hadithi moja husika na kuisomea wenzenu.




**Kazi ya 9:**

Soma sentensi zifuatazo na kuzikamilisha kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

1. Kigezo muhimu cha kuainisha fasihi ni namna msanii anavyoupitisha ujumbe wake yaani masimulizi .........................................................

2. ..............................huhusu visa vya kubuni na vya kihistoria na huhifadhiwa akilini mwa wanajamii.

## D. Msamiati

**Kazi ya 10:**

Shirikiana na mwenzako na kutafuta katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu **maana** ya maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari:

**Kigezo**
**Kalima**
**Kiada**
**Ufaraguzi**
**Fanani**

**Kazi ya 11:**

Katika jozi, **tungeni sentensi** kwa kutumia maneno ya hapo juu.

**Kazi ya 12:**

Tunga sentensi zinazohusu **"kutunza na kulinda mazingira na maendeleo ya kudumu"** kwa kutumia maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari cha hapo juu:

1.Mfumo.....................................................................
2.Jamii………………………………………………………

Mfano: Serikali yetu imeanzisha mfumo thabiti wa kulinda mazingira yetu.

**Kazi ya 13:**

Katika jozi, jazeni pengo kwa kutumia silabi inayofaa ili kulipata neno sahihi la Kiswahili lililotumiwa katika kifungu cha habari cha hapo juu:

1. Ufara---zi;
2. U---mbuzi;
3. Mi---rafu;
4. Ha---ra

**Kazi ya 14:**

Shirikiana na mwenzako mzikamilishe ipaswavyo sentensi zifuatazo kwa kutumia **maneno ya kifungu cha habari** hicho:

1. Ni lazima serikali yetu iunde..................thabiti ya kufundisha fasihi simulizi shuleni.
2. Uvumbuzi wa maandishi ni mojawapo kati ya mambo yanayosababisha..................wa kazi za fasihi simulizi..
3. Serikali ya Rwanda imepiga hatua kubwa katika kuendeleza................... isiyo na ubaguzi.

**Kazi ya 15:**

Katika jozi, **changanueni** tanzu na vipera vifuatavyo kutokana na makundi mawili ya hapa chini:

Maombolezo
Tamthilia
Ngano
Hekaya
Riwaya
Hurafa
Tanzia

| 1 | 2 |
|---|---|
| **Fasihi Simulizi ya Kiswahili** | **Fasihi Andishi ya Kiswahili** |

**Kazi ya 16:**

Jiunge na wenzako wawili, mjadili **mfumo wa elimu isiyo na ubaguzi** nchini Rwanda. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 17:**

Waambie wenzako **yaliyomo** katika kifungu cha habari ambacho kimesomwa.

**Kazi ya 18:**

Kwa njia ya mazungumzo, **simulia wengine hadithi** uliyoisikia nyumbani au mahali pengine.

**Kazi ya 19:**

Kwa njia ya mazungumzo, waambie wenzako **umuhimu** wa chombo kifuatacho katika kulitatua tatizo la uhaba wa kazi za fasihi simulizi?



**Kazi ya 20:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza ipaswavyo** sentensi zifuatazo kwa kutumia mambo yanayopatikana katika kifungu cha habari ambacho kimesomwa:

| | |
|---|---|
| **Uhaba wa kazi za fasihi simulizi ulisababishwa na** | **1. uvumbuzi wa maandishi** |
| | .2......................................................... |
| | 3......................................................... |

**Kazi ya 21:**

Katika jozi, someni kimoyomoyo habari ifuatayo. Kwa maoni yenu, habari hii ni ya kifasihi? Elezeni kinagaubaga:

***Kupogoka kwa uchumi***

Uchumi wa nchi unapoharibika tunasema kwamba umepogoka. Katika hali hii, matatizo huwa mengi katika nchi na bei za bidhaa hupanda au bidhaa huadimika katika maduka na masoko.

Fedha ya nchi ambayo uchumi wake umepogoka hushuka thamani kwa sababu uwezo wake wa kununua vitu huwa mdogo. Watu huwa hawaihitaji katika mabadilishano. Huikimbilia fedha yenye nguvu.

Viwanda katika uchumi uliopogoka hufanya kazi kwa shida sana. Mara kwa mara huwa na matatizo ya vipuli na malighafi. Matatizo haya hutokea zaidi kwa sababu nchi huweza kukosa fedha za kigeni ambazo zinahitajika ili kuagiza bidhaa iwapo nchi yenyewe haizitengenezi.

Mashamba kwa upande wake hukosa pembejeo na vifaa vya kulimia kama matrekta, plau na majembe. Matokeo yake ni uzalishaji hafifu wa mazao ya chakula na ya biashara.

Hali ya usafiri na mawasiliano huwa mbaya pia. Magari, magari moshi, meli, ndege na vyombo vingine huweza kukosa vipuli na mafuta na kulala. Vyombo hivi visipofanya kazi maana yake ni kwamba mali inayozalishwa viwandani na mashambani haiwezi kusafirishwa. Hivyo, huweza kutokea mlundikano wa bidhaa na pasipokuwa na bahari na ghala za kutosha za kuhifadhia, bidhaa huweza kuharibika.

Kupogoka kwa uchumi huathiri pia huduma muhimu kama vile huduma za afya, elimu, posta na kadhalika. Hospitali na zahanati huweza kukosa dawa na vifaa vya tiba. Shule huweza kukosa vitabu, madaftari, chaki, madawati na vifaa vingine muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Wakati mwingine, hata upanuzi wa majengo huwa shida idadi ya wanafunzi inapoongezeka.

Hali ya kupogoka kwa uchumi huathiri moja kwa moja maadili ya jamii. Jamii imara huweza ikaingiliwa na rushwa na magendo. Watu katika hali hiyo hujaribu kupigana na maisha magumu yanayosababishwa na hali mbaya ya uchumi kwa kutumia njia zisizo halali kujiongezea kipato. Majambazi na wezi wa kawaida huongezeka. Mara kwa mara hutokea vitendo vya uuaji, unyang'anyi na wizi.

Imani miongoni mwa watu hutoweka. Ndugu huwa hawaaminiani. Maisha hujaa uhasama. Utendaji wa kazi kwa ujumla huzorota. Ari ya kazi hushuka. Hali ya uchumi inapofikia hatua hii, maendeleo ya nchi hudidimia kabisa.

Ni lazima serikali inayohusika ichukue hatua za haraka na zenye busara ili kuiokoa nchi katika mashaka na maangamizi.

**Kazi ya 22:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Katika Kinyarwanda, fasihi simulizi ni | ........................................................................ |
| 2. ..................................................... | ni mhusika aliyependelewa sana na Wanyarwanda na Waswahili katika hadithi zao na ambaye huwakilisha tabia ya werevu na ujanja |
| 3. Hadithi simulizi za Waswahili huwa na mwisho ufuatao: | ........................................................................ |

## G. Utafiti

**Kazi ya 23:**

Shirikiana na wanafunzi watatu na kufanya **utafiti** kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu mbalimbali kuhusu tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake. Wasilisheni matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu. Kitabu cha NKWERA, F.V.M., ***"Sarufi na fasihi: Sekondari na vyuo"***, kinaweza kurahisisha kazi yenu.

**Kazi ya 24:**

**Andikeni** na **kusomea** wenzenu maelezo mafupi kuhusu kila utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake.

## H. Mchezo

**Kazi ya 25:**

Katika jozi, tafuteni kwenye jedwali hili maneno matano ya Kiswahili mnayoyajua **yaliyotumiwa** katika kifungu cha habari cha "***Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili***":

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| K | I | Z | A | Z | I |
| I | G | I | W | U | S |
| S | D | N | A | W | H |
| W | K | A | L | F | A |
| A | P | W | I | E | R |
| H | R | E | P | O | A |
| I | E | Z | U | G | U |
| L | O | A | R | R | O |
| I | H | T | H | Y | L |
| N | M | I | P | T | V |

## I. Kuandika

**Kazi ya 26:**

Andika **mawazo makuu** yanayopatikana katika habari yetu ya hapo juu yaani "***Kupogoka kwa uchumi***". Usisahau kuwasomea wenzako matokeo ya kazi yako.

**Kazi ya 27:**

Andika **katika umoja** majina yafuatayo yaliyotumiwa katika habari yetu ya hapo juu yaani "Kupogoka kwa uchumi". Usisahau kuwasomea wenzako matokeo ya kazi yako.

| **Neno** | **Umoja** |
|---|---|
| Majambazi | ..................................... |
| Wezi | ..................................... |
| Maghala | .................................... |

**Kazi ya 28:**

Unda **neno kamili** lililotumiwa katika kifungu cha habari chetu kwa kujaza silabi katika mapengo:

1. Ru---nga hii mpya itatumiwa katika kuwahamasisha wafanyakazi kuhusu kuzalisha mali kwa kiwango.
2. Mwanangu, hizi ndizo ha --- raza kutumia dawa za kulevya.
3. Mwanafunzi wa kidato cha tano analazimishwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa u---saha.

**Kazi ya 29:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja ulitolewa):

| **Kundi la** | ***kwanza*** | **la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni** | ***masimulizi*** |
|---|---|---|---|
| Kundi la | | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | |
| Kundi la | | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | |
| Kundi la | | la kazi za sanaa za fasihi simulizi ya Kiswahili ni | |

**Kazi ya 30:**

Katika kundi la wanafunzi watatu, andikeni katika madaftari yenu tofauti ya kifasihi iliyoko kati ya kifungu cha habari "***Kupogoka kwa uchumi***" na habari ifuatayo:

***Jongoo na chura***

Hapo zamani palitokea Jongoo na Chura ambao walikuwa marafiki wakubwa sana. Kila wakati walikuwa wanatembeleana.

Siku moja, Chura alimwuliza Jongoo, "Rafiki yangu huwa unafanya nini na ngozi yako? Mbona inang'ara sana! Tazama ngozi yangu, siyo laini. Ningependa iwe kama yako. Hebu nidokezee kidogo".

Jongoo alifurahi kuambiwa kwamba alikuwa na ngozi nyororo. Alianza kumpa rafiki yake ushauri kama ifuatavyo, "rafiki yangu Chura, ngozi hii nyororo unayoiona ni kazi kubwa tena ngumu ambayo mke wangu amekuwa akifanya kwa muda wa miaka mingi. Kila asubuhi huweka kikaango motoni kisha hujaza mafuta...". Kabla hajaendelea na kumaliza, Chura alimkata kauli rafiki yake kwa kusema, " Basi! Basi! Nimeisha elewa. Huna haja ya kunielezea zaidi. Yote haya nitayatenda na utaona nitakavyonawiri".

Jongoo alijaribu kumshawishi amsikilize lakini Chura alisisitiza kwamba kwa utangulizi ule amekwisha elewa kila kitu. Marafiki wale waliagana. Alipofika nyumbani Chura, alimwita mkewe na kumwambia, "Mke wangu! Leo rafiki yangu Jongoo amenieleza jinsi ya kuifanya ngozi yangu iwe nyororo na ya kung'ara kama yake. Sasa hivi ninataka uweke chungu jikoni. Hakikisha jiko lina moto mkali sana".

Mke alifanya kama alivyoelezwa. Chura aliendelea kutoa maagizo, "Ninataka utie mafuta ya kukaangia mboga mengi sana. Yakiisha chemka unieleze mara moja". Mkewe alitekeleza maagizo ya mara kwa mara na kumpa taarifa kwamba

mafuta yalikwisha kuchemka. Chura aliiingia jikoni akamwambia mkewe, “sasa nitumbukize katika mafuta maana ninataka niibabue ngozi hii ya juu ili ibaki nyororo iliyopo chini yake”. Mkewe alipigwa na bumbuazi na kumjibu, “Mume wangu, mbona unaniambia nifanye kitu cha hatari! Ukitumbukizwa katika mafuta haya utapona? Haiwezekani hata kidogo! Balaa hilo!”

Chura alisisitizia kwa ukali kutumbukizwa katika mafuta. Alisema, “Mimi nilikuwa nikikuambia siku zote kwamba ngozi hii inanitia aibu na leo nimepata njia ya kuiondoa, na wewe unapinga! Ukitaka kukaa nyumbani kwangu sharti utimize ninayokuambia kufanya ama sivyo nitakufukuza!”

Mkewe Chura kusikia hivyo, alimnyanyua mumewe na kumtumbukiza katika kikaango. Chura alilia, “Yooooo! Yooooo! Nigeuze upande mwingine!” Mkewe alipomgeuza tu mlipuko mkubwa ulisikika. Chura alipasuka vipande. Utumbo ulitoka katika kikaango na kuanguka chini. Huu ndio ulikuwa mwisho wa mzee Chura. Mauti ya kujitakia yalimfikia.

Mkewe alipoona yaliyokuwa yametokea, alikimbia mara moja na kuwaita majirani. Majirani walikuja kushuhudia msiba. Mjane aliwaelezea jinsi alivyoshurutishwa kumtumbukiza marehemu katika mafuta. Majirani waliamua kwamba mkwe hakuwa na hatia bali marehemu Chura alisababisha kifo chake mwenyewe kwa ujinga wake.

Huu ndio mwisho wa hadithi!

**Kazi ya 31:**

Matini hii “***Jongoo na chura***” ni kazi ya fasihi gani? Ni **utanzu** gani na **kipera** gani? Mwaelezee wenzenu.

**Kazi ya 32:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| **Tumeisha** | **jua** | **umuhimu** | **wa** | **fasihi** | **simulizi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

Mfano:
Tumeisha elewa ubingwa wa msanii mweusi.


# SOMO LA 4: NYIMBO ZA KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kutaja kila kitu ambacho **mnaona** kwenye picha ya hapa chini.

**Kazi ya 2:**

Picha hii **inahusu** utanzu gani wa fasihi simulizi ya Kiswahili? Eleza vizuri.




*Bendi ya wanamuziki*

**Kazi ya 3:**
Soma kifungu cha habari na kukihusisha na picha hiyo.

***Nyimbo katika fasihi simulizi ya Kiswahili***

### 1. Fasili na sifa za nyimbo

Nyimbo ni mojawapo kati ya tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili. Kipengele hiki huundwa na maneno yanayochaguliwa na kupangwa vizuri na kutamkwa kwa sauti ya muziki. Lugha ya mnato huingizwa ili kuvutia hadhira. Nyimbo huwa na sifa zake yaani:

a. Kutumia kiimbo au sauti maalumu na mdundo unaosisimua.
b. Kuweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi. Wakati mwingine, huweza kuimbwa kwa kupokezana.
c. Kuweza kuambatana na utumiaji wa ala za mziki. Mwimbaji ana uhuru wake wa kutumia zana za muziki anazotaka au kutumia sauti yake tu.
d. Kutumia lugha teule, lugha ya mkato. Lugha hii ndiyo inayovuta msikilizaji ili aweze kupenda kazi hizo za sanaa ya lugha.
e. Kutungwa katika mishororo na beti na kurudiarudia au kukariri maneno ili kusisitizia ujumbe. Nyimbo nyingi huwa na kiitikio.

### 2. Umuhimu wa nyimbo

Jamii mbalimbali za kiafrika hupenda sana nyimbo ambazo ni chanzo cha ushairi. Huimba katika shughuli mbalimbali na mahali tofauti. Ndiyo sababu watu wanasema kuwa "Afrika ni Afrika iimbayo". Jambo hili linatokana na umuhimu wa nyimbo. Ni ukweli kuwa nyimbo, kama ishara mojawapo kwamba jamii ina uhai, huwa na umuhimu wa:

- Kuburudisha yaani kumfanya mtu astarehe kwa muziki. Mtu anaposikia wimbo anafurahi moyoni na kujisikia katika hali ya kutokuweko na usumbufu.
- Kuelimisha, kufunza, kuonya na kuelekeza wanajamii kuhusu mambo mbalimbali yanayowagusa kama vile:

  - Vitendo vya kupigana, kuuana na chuki vilivyoanza kujitokeza ulimwenguni kuzungukia masuala ya kidini;
  - Mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi yaani zeruzeru au albino. Nyimbo za Kiswahili zilitungwa kupinga ukatili huu;
  - Zama za ufukara na ujinga;
  - Janga la ugonjwa wa UKIMWI na madhara yake;
  - Ukosefu wa amani na maendeleo ya kudumu;
  - Ukosefu wa usawa wa jinsia miongoni mwa watu;
  - Kushiriki kwa vyama vingi vya kisiasa na kadhalika.

Mwimbaji anaweza kutunga nyimbo zake kwa kuwafanya wanajamii wafahamu masuala hayo na kuwapa suluhisho.

- Kuliwaza mtu. Wakati wa majonzi, nyimbo hutumiwa kwa kumbembeleza mtu na kumfanya asimame wima.
- Kutia moyo watu wakati wa kufanya kazi ngumu kama vile kilimo, kuvuta kitu kizito, uvuvi, ujengaji nyumba na kadhalika.
- Kusifia kitu au mtu katika jamii.
- Kuunganisha jamii kwa kuwakumbusha watu wake uhusiano na undugu wa kimsingi miongoni mwao, kuvumiliana na kupendana.
- Kudumisha na kuhifadhi tamaduni za jamii.
- Kukuza ubingwa na sanaa katika jamii.

### 3. Aina au vipera vya nyimbo

Katika tamasha na shughuli nyingi, nyimbo hutumiwa kwa makusudi mbalimbali kama tulivyosema hapo juu. Kutokana na shughuli na sherehe hizo, nyimbo huweza kuwa:

a. Nyimbo za watoto: Ni zile zinazoimbwa na watoto katika michezo yao. Mara nyingi, huimbwa kwa kujibizana.

b. Nyimbo za kubembeleza: Mama au mlezi au mtu mwingine humwimbia mtoto mchanga nyimbo hizi kwa makusudi ya kumwongoa na kumlaza. Mwimbaji ana uhuru wa kuongeza maneno fulani na mishororo mingine.
c. Nyimbo za kazi: Huimbwa wakati wa kufanya kazi ili watu wasichoke. Kazi hizo ni kama vile kilimo, kutwanga, kusuka, uvuvi, useremala, uashi na kadhalika. Nyimbo hizi huwatia moyo wafanyakazi. Kwa hivyo, wao huweza kutimiza kazi zao na kuendeleza uchumi wa jamii au nchi yao. Nyimbo za hodiya na wawe huingia katika kundi hili;
d. Nyimbo za kisiasa: Ni nyimbo za kuwasifu viongozi wa kisiasa, kuunga mkono mfumo wa utawala fulani na kuonyesha uzalendo kwa kusifia taifa au nchi;
e. Nyimbo za sherehe: Huimbwa katika sherehe mbalimbali kama vile harusi, mavuno, maulidi, kutahiriwa au jando, unyago na kadhalika. Nyimbo za harusi huimbiwa bwana na bibi harusi kwa kuwapa heko kwa kufunga ndoa na mawaidha ya kutunza familia. Zile za jando au tohara huonyesha ushujaa wa vijana wanaotahiriwa ambao wamekuwa watu wazima.
f. Nyimbo za maombolezo: Huimbwa wakati wa huzuni au simanzi, msiba, njaa,... ili kuwapa matumaini waombolezaji;
g. Nyimbo za kutumbuiza au tumbuizo: Taarabu ni mojawapo kati ya nyimbo hizo. Huimbwa kwa kufurahisha au kutoa burudani kwa watu tu. Taarabu ni muziki wa mahadhi unaotumia ala za mchanganyiko wa kiarabu, kihindi na kizungu. Nyimbo hizi zinaweza kuwa na onyo fulani au la.
h. Nyimbo za kashifa: Huimbwa kwa kuwakashifu watu wasio na adabu, wachawi, watoto vikojozi na wengineo. Nyimbo hizi zinalenga kuwakashifu, kurekebisha mwenendo wao katika jamii na kuwakumbusha kwamba ni mwiko kutenda jambo hilo;
i. Nyimbo za dini: Kasida ni mojawapo kati ya nyimbo hizo. Huimbwa kwa kumsifu Muumba au kuomba na kutoa mafunzo yanayohusu dini;
j. Nyimbo za mapenzi: Huimbwa na mtu kwa kumsifia mpenzi wake hasa kwa tabia zake, urembo wake, mwenendo wake na kadhalika.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 4:**

Soma kimoyomoyo kifungu cha habari “**Nyimbo katika fasihi simulizi ya Kiswahili**” kisha ujibu maswali yafuatayo:

1. Zitaje sifa za nyimbo.
2. “Afrika ni Afrika iimbayo”. Eleza kinagaubaga.
3. Kwa nini ni lazima Wanyarwanda wahamasishwe kuhusu ugonjwa wa UKIMWI?
4. Kwa maoni yako, ni upi umuhimu wa mfumo wa kisiasa wa vyama vingi?

## b. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Sikiliza** anayoyasoma mwenzako na kuzingatia mawazo muhimu.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

Rudia matini ile uisome **mara** nyingine.

**Kazi ya 7:**

Soma **kwa sauti** majina ya zana za muziki zinazoonekana kwenye picha ifuatayo:




**Kazi ya 8:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

1. Jamii mbalimbali za kiafrika hupenda sana nyimbo ambazo ni .................... cha ushairi.
2. Mtu anaposikia wimbo anafurahi moyoni na kujisikia katika hali ya kutokuweko na .........
3. Nyimbo za harusi huimbiwa bwana na bibi harusi kwa kuwapa ...................... ndoa na mawaidha ya kutunza familia.

**Kazi ya 9:**

**Soma kwa sauti** nyimbo mbili zifuatazo. Waelezee wenzako **tofauti** iliyopo kati ya nyimbo hizo ukizingatia vipera vya nyimbo.

1. **Yaweke yako machozi**

   Howa, howa kibibie,
   U wangu kibibi silie,
   Ukaniliza na mie,
   Yaweke yako machozi!

   Machozi yako yaweke,
   Nikifa unililie,
   Watu wakufikirie,
   Ewe mwana wa ulizi!

   Mwana wa ulizi wewe,
   U wangu silie,
   Nikifa unililie,
   Yaweke yako machozi!

2. **Wimbo uliotafsiriwa kutoka kabila la Wanyasa - Tanzania**

   Kilimo aine aine!
   Haya!
   Na ardhi ikubali!
   Haya!
   Na uwele uneemeke!
   Haya!

**Kazi ya 10:**

Shirikiana na mwenzako na **kujaza jedwali** lifuatalo kwa kutumia maneno ya Kiswahili **yanayopatikana** katika kifungu cha habari (mfano umetolewa):

| Neno au kundi la maneno | Maelezo |
|---|---|
| *Nyimbo za maombolezo* | ***huimbwa wakati wa huzuni au simanzi, msiba, njaa,... ili kuwapa matumaini waombolezaji*** |
| .......................................... | ni muziki wa mahadhi unaotumia ala za mchanganyiko wa kiarabu, kihindi na kizungu |
| .......................................... | huundwa na maneno yanayochaguliwa na kupangwa vizuri na kutamkwa kwa sauti ya muziki |

## D. Msamiati

**Kazi ya 11:**

Katika jozi, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na kuchunguza **maana** ya maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari "***Nyimbo katika fasihi simulizi ya Kiswahili***":

Kiitikio
Kustarehe
Zeruzeru
Kuliwaza
Nana
Labeka

**Kazi ya 12:**

**Tunga** sentensi moja kwa kila neno kati ya hayo ambayo umejua maana yake.

**Kazi ya 13:**

**Soma** wimbo ufuatao na **kuuelewa msamiati** uliotumiwa. Hiki ni kipera gani?

**Wimbo kutoka Pemba**

Tulifyeke lino gugu, tulifyeke!
Kwa mundu tulifyeke, tulifyeke!
Kwa pamoja tulifyekeeeee!
Kwa nguvu tulifyekeeeee!

Tulikache lino situ, tulikache!
Kwa mashoka tulikache, tulikache!
Pamoja tulikacheeeee!
Kwa nguvu tulikacheeeee!

Tulishome lino jani, tulishome!
Kwa mioto tulishome, tulishome!
Pamoja tulishomeeeee!
Kwa nguvu tulishomeeeee!

Tulitimbuge hili dongo, tulitimbuge!
Kwa majembe tulitimbuge, tulitimbuge!
Pamoja tulitimbugeeeee!
Kwa nguvu tulitimbugeeeee!

Tulipandile lino shamba, tulipandile!
Kwa nyafaka tulipandile, tulipandile!
Pamoja tulipandileeeee!
Kwa nguvu tulipandileeeee!

Tulivune lino zao, tulivune!
Kwa mapato tulivune, tulivune!
Pamoja tulivuneeeee!
Kwa nguvu tulivuneeeee!

(**Tanbihi:** Maneno ya Kiswahili na lahaja zake yalichanganywa. Kwa mfano,


- Tulikache=tulikate / Tulishome=tulichome / Tulitimbuge=tulitimue / Tulipandile=tulipandie / Nyafaka=nafaka)

**Kazi ya 14:**

Kuna **tofauti** gani kati ya “kupanda mmea” na “kupandikiza mmea”?

**Kazi ya 15:**

Jiunge na mwenzako na kujadiliana juu ya majina ya **ala za muziki** zifuatazo. Mwaambie wenzenu jinsi wanavyotumia zana hizi.






**Kazi ya 16:**

**Yapange** majina haya kwenye vikundi vyake.

Kilimo
Uashi
Mavuno
Uvuvi
Harusi
Maulidi
Unyago
Jando

| 1 | 2 |
| --- | --- |
| Sherehe | Kazi |

**Kazi ya 17:**

Pamoja na mwenzako, **mzikamilishe** sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayopatikana katika kifungu cha habari cha hapo juu:

1. ................................ni mojawapo kati ya nyimbo hizo.
2. Wakati wa majonzi, nyimbo hutumiwa kwa ...................... na kumfanya asimame wima.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 18:**

Waambie **kwa sauti** wanafunzi wenzako yale ambayo umeyasoma katika kifungu cha habari "**Nyimbo katika fasihi simulizi ya Kiswahili**".

**Kazi ya 19:**

Kwa sauti nyororo, **waimbie** wenzako wimbo wa Kiswahili unaoujua. Baada ya kuimba, waaambie **mahali pazuri** nchini Rwanda ambapo Bwana na Bibi Harusi wanaweza kwenda kupumzikia wakati wa fungate.

**Kazi ya 20:**

Simama mbele ya darasa ueleze **linalozungumziwa** katika beti za nyimbo mbili za sherehe (harusi) zifuatazo:

**1 Mapokezi ya harusini**

Bibi harusi ndoo Kaole,
Kaole mgeni kaingia,
Mgeni mwezi kongo,
Aya eei mgeni kaingia!

Hongera mwanangu ee,
Hongera nami nihongere mwana eei,
Mama uchungu mwana uchungu,
Eei,
Nyamala mwanangu silie oyee,
Tumbo la uvyele linauma mno eei,
Linauma mno hoyee!

Sema yu wapi mamake harusi aje hapa,
Tuhangaike naye!
Na ndugu yake harusi aje hapa,
Tuhangaike naye!
Na rafiki yake harusi aje hapa,
Tuhangaike naye!
Aje amfunze mwari,
Asije kufedheheka,
Amwitikie mumewe kwa kila anachotaka.

**2 Bibi songa nywele**

Bibi songa nywele, shanuo la nini?
Kitwa chaniuma dawa yake nini?
Ponda tangawizi upake nyusoni,
Mahaba sindano, yachoma maini!

(**Tanbihi:** Maneno ya Kiswahili cha zamani na lahaja zake yalichanganywa. Kwa mfano,

- Ndoo=njoo / Nyamala=nyamaza / Kitwa=kichwa / Uvyele=uzazi / Mvyele=Baba au mama wa fulani au mzazi)

**Kazi ya 21:**

"Nyimbo hizi zinalenga kuwakashifu, kurekebisha mwenendo wao katika jamii na kuwakumbusha kwamba **ni mwiko** kutenda jambo hilo". Simama mbele ya wenzako uunde, kwa njia ya mazungumzo, sentensi zinazoanza na "Ni mwiko..." Zingatia **muundo** huo.
**Mfano:** Ni mwiko kushona nguo unayovaa kwani kunaleta ufukara.

| | |
|---|---|
| **Ni mwiko** | **Kitendo** |
| | ........................................................... |
| | ........................................................... |

**Kazi ya 22:**

Kwa njia ya mazungumzo, tumia neno jingine lenye **maana sawa** na lile lililoandikwa kwa italiki na kupigiwa mstari chini.

| | |
|---|---|
| 1. Kuelimisha, kufunza, kuonya na kuelekeza wanajamii kuhusu mambo mbalimbali yanayowagusa kama vile ***zama*** za ufukara na ujinga |
| 2. Nyimbo huwa na umuhimu wa kukuza ***ubingwa*** na sanaa katika jamii |

**Kazi ya 23:**

"*Nyimbo za kashifa huimbwa kwa kuwakashifu watu wasio na adabu, wachawi, watoto vikojozi na wengineo*". Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Nyimbo za kashifa huimbwa kwa kuwakashifu | watu wasio na ...................., wachawi, watoto vikojozi na wengineo |
| 2. Nyimbo za kashifa huimbwa kwa kuwakashifu | watu wasio na adabu, ...................., watoto vikojozi na wengineo |

## F. Utafiti

**Kazi ya 24:**

Shirikiana na mwenzako mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au kwa watangazaji wa redio fulani **nyimbo mbalimbali za Kiswahili** na kuzichanganua kutokana na vipera vyake. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

## G. Cheka uongeze siku za kuishi

**Kazi ya 25:**

"Kulikuwa na msiba wa mtoto wa Mwanabunge. Ulipofika muda wa kuongea kwa niaba ya familia, Mwanabunge alijisahau na kusema "Wananchi oyee!" Wote walipigwa na bumbuazi na kukaa kimya!" Waambie wenzako kichekesho kingine **cha Kiswahili** unachokijua.

## H. Kuandika

**Kazi ya 26:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| Nyimbo | huwa | na | sifa | zake |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**Kazi ya 27:**

Maneno haya yameendelezwa vibaya. **Panga silabi vizuri** na kuandika katika daftari lako neno sahihi lililotumiwa katika kifungu cha habari chetu.

1. Dasika;
2. Arakibu;
3. Arabuta;
4. Diyaho.

**Kazi ya 28:**

**Andika** jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Lugha ya .................................. huingizwa ili kuvutia hadhira |
| 2. Lugha hii ndiyo inayovuta msikilizaji ili aweze kupenda kazi hizo za ............................ |
| 3. Wakati mwingine, huweza kuimbwa kwa .......................................... |

**Kazi ya 29:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B na kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Ni nyimbo za kuwasifu viongozi wa kisiasa, kuunga mkono mfumo wa utawala fulani | kwa makusudi ya kumwongoa na kumlaza |
| 2. Nyimbo hutia moyo watu wakati wa kufanya kazi ngumu kama vile kilimo, | na kuonyesha uzalendo kwa kusifia taifa au nchi |
| 3. Mama au mlezi au mtu mwingine humwimbia mtoto mchanga nyimbo hizi | kuvuta kitu kizito, uvuvi, ujengaji nyumba na kadhalika |

**Kazi ya 30:**

Katika jozi, **tungeni** wimbo wenye beti tano unaohusu “Mapigano ya serikali dhidi ya vitimbakwiri au vitimbakwira”.

# **SOMO LA 5**: METHALI ZA KISWAHILI


**Kazi ya 1:**

**Tazama** picha zifuatayo. Unaona **nini**?

**Kazi ya 2:**

Picha hizi zinahusu utanzu gani wa fasihi simulizi ya Kiswahili? Eleza vizuri.




**Kazi ya 3:**

Soma kifungu cha habari kifuatacho na **kukihusisha** na picha hiyo.

***Methali hutajirisha lugha***

Methali ni mojawapo kati ya semi za Kiswahili. Semi hizi hutumiwa na kila mtu katika maisha yake ya kila siku.

**1. Fasili ya methali**

Methali ni sanaa ya kale inayodaiwa kuwa ilianza kutokana na ushairi na hatimaye kujitokeza kama utanzu wa kipekee. Semi hizi za kimapokeo hutambuliwa haraka kutokana na:

a. lugha yake;
b. yaliyomo;
c. muundo mahususi unaokumbukika upesi.

Ni semi zenye maana kamili, busara au mafundisho na maonyo yanayotolewa kwa njia ya mafumbo. Methali hutumiwa kila wakati katika mazungumzo ya kawaida ya wanajamii na hunata akilini kwa urahisi kuliko kauli nyingine. Mnato huo ndio unaozifanya methali zitajirishe lugha kwani humwezesha msemaji kuonyesha hekima yake na kipaji chake cha lugha.

## 2. Utamu wa methali katika mazungumzo

Utamu wa methali katika mazungumzo hutokana na lugha nyepesi inayopenya moja kwa moja katika mioyo ya wasikilizaji. Lugha hiyo huwa ya mifano yenye picha ndani yake na maneno machache hupangwa vizuri kwa njia ya kuvutia na kushawishi akili. Kwa mfano, zipo methali zinazotutahadharisha katika janga la UKIMWI au tabia mbaya ya punyeto: “Tamaa mbele mauti nyuma”, “Asiyeangalia huishia ningalijua!”. Ni kusema kuwa tamaa inatangulia msiba: Unapojikita sana katika anasa za dunia na kuwa na tabia ya kupenda kuzini, hii ni tamaa. Kinyume chake ni kupata majanga ya magonjwa ya zinaa na mwishoni kujuta na kuangamiza mwenye tamaa hiyo yaani kifo. Katika methali hiyo, maneno yanayotumiwa yana fumbo. Ni lazima mtu ajue linalozungumziwa ili aweze kulifumbua.

## 3. Dhima au umuhimu wa methali katika jamii

Methali ni semi muhimu kwa binadamu kwani ni njia ya mkato ya:

- Kuelimisha wanajamii: Methali kama utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili zilichangia, zinachangia na zitachangia kwa kiasi kikubwa katika kuelimisha wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayoikabili jamii yao. Masuala hayo yanaweza kuwa ya kiuchumi, kisiasa, kitabia, kiafya na kadhalika. Kwa mfano, methali huweza kutumiwa kwa kunasihi wanajamii kuhusu janga la UKIMWI. Unapomwambia mtu “kama hujui kufa, chungulia kaburi” unamshauri kuiangalia mifano kwa watu waliokumbana na janga hilo la hatari linaloangamiza maelfu na maelfu ya watu duniani na kutahadhari au kuwa macho. Vilevile, unaweza kumwonya mtu ukimwambia, “Kidole kimoja hakivunji chawa”. Hapa unataka ashirikiane na wengine kwani “umoja ni nguvu”.
- Kuonya wanajamii: Zipo methali nyingi zinazotumiwa kwa kuipa jamii maadili bora. Kwa mfano, mtu ambaye hakuweza kurekebisha mwenendo wake na tabia yake mbaya unaweza kumwonya kwa kupitia methali kama vile “asiyesikia la mkuu huvunjika guu” au “asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu”.
- Kukosoa jamii na kurekebisha mwenendo wake: Jamii yoyote ile huundwa na watu tofauti kitabia, kielimu, kimwenendo na kadhalika. Hii ndiyo sababu ya kuwepo kwa watu wanaoouunga mkono usawa wa kijinsia na wengine wanaoupinga, watu wepesi katika kushika maneno na wengine ambao wanasitasita, watu wanaopendelea kuzaa watoto wengi na wengine wanaotii mpango wa serikali wa kuboresha uzazi na kadhalika. Methali ni mojawapo kati ya kauli zinazoweza kutumiwa kwa kuikosoa jamii hiyo na kuwafanya wanajamii warekebishe mwenendo wao. Kwa mfano, kuhusu jambo la kuboresha uzazi unaweza kuwaambia watu wanaotaka kuzaa watoto wengi, “asiyeangalia huishia ningalijua”. Hapa unawakosoa ili wawe na uangalifu wabadilishe msimamo wao, na ufukara na matatizo mengine yatokanayo na jambo hilo yasije yakawaingilia bila kujua.

- Kuhamasisha wanajamii na kuwatia moyo: Mtu anawahamasisha wanajamii wasikumbane na janga fulani. Wanapokuelewa vizuri na kufuata mawaidha yako, unawatia moyo. Ili watu waweze kuepukana na shida zinazotokana na mawazo ya kiutamaduni ya wanajamii katika kuboresha uzazi, unaweza kutumia methali kama hii “aliye kando haangukiwi na mti”. Ni kusema kuwa mtu aliyeweza kuboresha uzazi, familia yake haitakumbana na njaa kwa sababu uwezo wake wa kifedha utamwezesha kukidhi mahitaji yote.

**4. Kuelewa maana ya methali na kuitafsiri**

Kuelewa maana ya methali ni kujua wakati ambapo au shughuli ambamo inatumiwa. Kutafsiri methali ni kueleza maana yake kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Kuelewa maana ya methali hutokana na ujuzi mtu alio nao katika lugha husika.

Kazi ya kutafsiri methali si rahisi kama inavyodhaniwa na watu ambao hawajapevuka katika mambo ya lugha. Watu hawa hufikiri kuwa ni kazi inayofanywa neno kwa neno yaani “tafsiri sisisi”. Ukweli ni kwamba ni jambo la kumakinikia. Kwa mfano, mtu akisema “mtaka cha uvunguni, sharti ainame”. Kauli hii hutumiwa kwa kumhamasisha mtu afanye kazi ili apate faida. Kwa kuitafsiri neno kwa neno katika Kinyarwanda [ushaka ikiri munsi y’ameza, agomba kunama], inapoteza utamu wake. Ni lazima kutafuta methali ya Kinyarwanda yenye maana sawa na ile ili utamu wake ubakie. Methali ya Kinyarwanda yenye maana sawa na ile ni “ushaka inka aryama nka zo”.

**5. Mifano ya methali**

Katika fasihi ya Kiswahili, uwanja wa methali ni mpana sana kiasi kwamba hakuna mtu anayeweza kuzijua methali zote za Kiswahili.

Hii ifuatayo ni mifano ya methali hizo na maana yake:

a. “**Dawa haitolewi bure**”: Dunia si dunia ya vitu vya bure. Inafaa mtu afanye kazi, atoe gharama.
b. “**Chovya chovya humaliza buyu la asali**”: Tunapotenga kitu kwa manufaa ya baadaye (akiba) na kuanza kukimega kidogo kidogo, mwisho tutashtuka tumekimaliza.
c. “**Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo**”: Tusibabaishwe na mabaya yaliyofanyika kwani ni mambo yaliyopita. Tumakinikie yale yatakayofanyika katika siku zijazo na kufanya kulihali ili yawe mema kwetu.
d. “**Mke kipo**fu huangazia nyumba”: Ingawa mtu anaweza kuwa na ulemavu au upungufu fulani wa kimaumbile, ana sifa nyingine ambazo zinakosekana kwa watu wengine.
**e.** **“Ngoja ngoja huumiza matumbo”**: Kusubiri muda mrefu kunasumbua mtu. Ni lazima afanye kazi moja kwa moja ndipo atafaidika.
**f.** **“Nguo za kuazima hazisitiri matako”:** Usiwategemee wengine katika kukidhi mahitaji yako. Jitahidi wewe mwenyewe utafanikiwa.

g. **“Adabu ni dhahabu”**: Ni vizuri kuwa na adabu kwani adabu ni tabia ya staha au kitu cha thamani.
h. **“Jina zuri hukohoa”**: Jina zuri ni tabia nzuri. Ni kusema kuwa mtu mwenye tabia njema hujulikana katika jamii yake.
i. **“Bidii huzaa matunda”**: Ni vizuri watu wafanye kazi kwa bidii kwani uvivu ni adui wa maendeleo.
j. **“Iwapo nia, pana njia”:** Unapotaka kukidhi haja yako kuu maishani, ni lazima ujipe moyo na usikate tamaa.

**6. Matumizi ya methali katika habari**

Linalowezekana leo lisingoje kesho

Hapo zamani za kale palikuwa na mzee mmoja aliyejulikana kama Kagabo “Kimezeo”. Kagabo alisifika sana kwa uwezo wake wa kutumia methali. Kila siku kutoka asubuhi hadi jioni alikuwa akitumia methali nyingi sana.

Watu walikuwa wakimwita maktaba ya kabila. Wengi walimsifu na kusema kwamba wakati sisi tunatafuta methali, methali za mzee Kagabo zimo kinywani tu. Mzee Kagabo alizoea kusema methali ni “kimezeo” cha maneno makavu. Jina lake la kupanga likawa Kagabo Kimezeo. Kila wakati alipozungumza na mkewe, watoto, marafiki na wengine, alitoa maneno makavu makavu. Watu walimshangilia sana Kimezeo.

Siku moja mkewe alichelewa kuamka asubuhi. Kimezeo alimwamsha na kumwonya asizoee tabia hiyo mbaya ya kuchelewa. Alisema, “Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako”. Halafu, aliendelea kusema, “Mke wangu, ‘ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu’. Ukiyakumbuka maneno haya, bila shaka tutafanikiwa kwani ‘linalowezekana leo lisingoje kesho’. Hili ni onyo mke wangu”.

Basi mkewe alichukua jembe na kumpa Kagabo panga lake. Hapo ndipo alipomsihi mkewe afanye haraka ili wafike mapema shambani. Kagabo alimwambia mkewe, “Wakati una mabawa” na kuendelea kusema, “Wakati titi la nyati hukamuliwa kwa mashaka”. Mkewe akamjibu, “Haraka haraka haina baraka”. Kagabo Kimezeo alimkomesha kwa kumwambia, “Ngoja ngoja huumiza matumbo”. Ndipo waliamua kufanya haraka na kufika shambani.

Walipofika shambani, walianza kufanya kazi kwa bidii. Saa kama sita hivi baada ya jua kuchomoza yaani wakati jua lilikuwa utosini, ndipo mzee Kimezeo alimwambia mkewe, “Sasa ninakubaliana na wahenga kwamba “mchumia juani hulia kuvulini”. Unasikia?” Mkewe alimjibu, “sasa umeanza ‘vimezeo’ vyako!” Kagabo akamjibu, “Vimezeo ni bora! Kumbuka kwamba ‘maneno mengi hayavunji mfupa’, ila yanapoteza wakati. Waswahili hawakutambua kuwa ‘wakati una mabawa’. Je, unakubaliana nami?” Waliendelea kulima huku jua kali likichoma migongo yao. Hawakujali jua hilo na hawakukubaliana na kauli ya mvivu asemaye, “Kesho kesho nitafanya”. Kagabo alimhimiza mkewe

kazi wamalize ngwe waliyokuwa wameanza na kusema, “Linalowezekana leo lisingoje kesho!”

Jioni, jua lilididimia kuelekea Ziwa Kivu. Kagabo Kimezeo alimwasa mkewe warudi nyumbani na kusema, “Wahenga walinena ‘Mwoga hukimbilia wanawe’. Tusifurahie kulima hadi usiku kwani watoto nao wanahitaji huduma zetu”. Walipofika nyumbani, mkewe akisaidiana na mumewe walitayarisha chakula kitamu na watoto wakakifurahia sana. Ndipo Kagabo mfurahifu alisema, “Kitamu hutokea kwa mwenye nguvu”. Mkewe alifurahi sana kutokana na ustadi wa mumewe wa kutumia methali na kumuuliza, “Mwandani, tangu asubuhi mapema mpaka jioni unatumia methali ngapi?” Kagabo alimjibu, “Elfu na moja!”

## A. Maswali ya Ufahamu

**Kazi ya 4:**

Soma kifungu cha habari cha hapo juu zaidi ya mara moja kisha ujibu maswali yafuatayo:

1. Je, ni ipi asili ya utamu wa methali?
2. Je, ni ipi dhima ya methali katika jamii?
3. “Kazi ya kutafsiri methali huwa ngumu”. Eleza kinaganaga kauli hii.
4. Toa maoni yako kuhusu kauli ifuatayo: “Wanafasihi wengi wanajua methali zote za Kiswahili”.
5. Taja methali zote zilizotumiwa katika hadithi “Linalowezekana leo lisingoje kesho.”

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako anavyokisoma kifungu cha habari hiki na kuandika mawazo makuu kwenye karatasi.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

Soma kifungu cha habari hiki zaidi ya **mara** moja.

**Kazi ya 7:**

**Husisha** picha ifuatayo na yaliyomo katika kifungu cha habari ambacho umesoma. Waambie wenzako mambo ambayo umeyaona.



**Kazi ya 8:**

**Soma kwa sauti** sentensi zifuatazo na kuzikamilisha kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Waliendelea kulima huku jua kali ............................................. yao |
| 2. Kazi ya kutafsiri methali si rahisi kama inavyodhaniwa na watu ambao ................. katika mambo ya lugha |
| 3. Usiwategemee wengine katika ....................................... yako |

## D. Msamiati

**Kazi ya 9:**

Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya **maana** ya maneno yafuatayo:

Kunata
Kupenya
Anasa
Kuganga
Maktaba

**Kazi ya 10:**

Tunga wewe mwenyewe sentensi zinazohusu **amani na maendeleo** kwa kutumia maneno matano ya hapo juu.

**Kazi ya 11:**

**Zipange** kauli hizi katika vikundi vyake vifuatavyo:

| Kauli | Kikundi cha methali | Kikundi cha nyimbo |
|---|---|---|
| - Baada ya dhiki faraja;<br>- Ada ya mja hunena muungwana ni kitendo;<br>- Mama nipe radhi;<br>- Chanda chema huvishwa pete;<br>- Sega langu la asali;<br>- Lala salama;<br>- Jogoo la shamba haliwiki mjini. | | |

**Kazi ya 12:**

Katika jozi, **jazeni pengo** kwa kutumia silabi inayofaa ili kulipata neno sahihi la Kiswahili lililotumiwa katika kifungu cha habari cha hapo juu:

1. Walikumbana na ma---nga ya magonjwa ya zinaa.
2. Kidole kimoja hakivunji ----wa.
3. Kusubiri muda mrefu kuna---mbua mtu.
4. Ilikuwa saa tano baada ya jua ku---moza.

**Kazi ya 13:**

Katika pea, **chagueni** jibu bora na sahihi.

1. Methali ni...................kama nahau. (semi; vitendawili)
2. Hizo unazoona ni..................za vitabu. (kababu; rafu)
3. Mume wake amempa...............la noti. (bunda; bandia)
4. Amenunua................wa ndizi. (Mkundu; mkungu)

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 14:**

Simama mbele ya darasa **uwaambie** wanafunzi wengine kwa maneno machache yale ambayo umeyasoma katika kifungu cha habari chetu.

**Kazi ya 15:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza jedwali lifuatalo kwa kutumia **methali** inayofaa kwa kila hali:

| Hali | Methali |
|---|---|
| 1. Tabia ya kuombaomba vitu humfanya mwombaji kuwa mnyonge au duni | ........................................ ............... |
| 2. Mkubwa wao akiondoka, walio chini yake hujiona kuwa huru na hufanya mambo wapendavyo | ........................................ ............... |
| 3. Usiporekebisha kosa dogo tangu mwanzo, hatimaye utapata hasara kubwa | ........................................ ............... |

**Kazi ya 16:**

Kwa njia ya mazungumzo, waelezee wenzako jinsi **utakavyofanya** ili uweze kupevuka katika methali kama KIMEZEO.

**Kazi ya 17:**

Katika pea na kwa njia ya mazungumzo, **mhusishe** methali za Kiswahili zifuatazo na zile za Kinyarwanda zenye maana sawa.

1. Chema chajiuza kibaya chajitembeza:........................
2. Bandubandu humaliza gogo:.......................................................................
3. La kuvunda halina ubani:...........................
4. Umleavyo mtoto ndivyo akuavyo:.................................
5. Paka akiondoka, panyahutawala:.............................

**Kazi ya 18:**

"Wakati titi la nyati hukamuliwa kwa mashaka". Kwa njia ya mazungumzo, taja vitu hivi kwa jina moja [Mfano: Nyati, punda, pundamilia, tembo, simba ni "**wanyama**"]

1. UKIMWI, homa, mafua, upele na kifaduro
2. Kilemba, suruali, kanzu na fulana
3. Kiroboto, chawa, nyigu, nyuki na panzi

## F. Utafiti

**Kazi ya 19:**

Shirikiana na mwenzako mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au kwa majirani zenu **methali mbalimbali za Kiswahili** na matumizi (mazingira) yake. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

## G. Mchezo

**Kazi ya 20:**

Shirikiana na mwenzako na kujaza kwenye jedwali hili herufi **zilizoachwa**:

| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** | K | I | S | W | A | H | I | L | I |
| **B** | | | | | | O | | | |
| **C** | | | | | | N | | | |
| **D** | | | | | | G | | | |
| **E** | P | | | | | E | | | |
| **F** | E | | | | | R | | | |
| **G** | O | R | O | D | H | A | | | |

## H. Cheka uongeze siku za kuishi

**Kazi ya 21:**

Karake mshaufu alienda kwa babu yake kuchukua dawa. Baada ya kupewa kikombe akasimama pembeni kwa muda mrefu bila kunywa dawa. Babu akamwuliza; "Mbona hunywi?" Karake akajibu, "Ninasubiri mrija, Babu!" Waambie wenzako kichekesho kingine **cha Kiswahili** unachokijua.

## I. Kuandika

**Kazi ya 22:**

**Andika** sentensi mbili zinazofuata **muundo** huu:


| Ni | kusema | kuwa | tamaa | inatangulia | msiba |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**Kazi ya 23:**

1. Andika methali ambamo **majina** ya vitu hivi yalitumiwa.


Mvua inanyesha.

....................


Jua kali.

........................

.................



... ................



.................

..............................................................

**Kazi ya 24:**

Andika jedwali hili katika daftari lako na **kujaza** sentensi zifuatazo jinsi **unavyotaka** lakini zitofautiane na zile zipatikanazo katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Wengi walimsifu na kusema kwamba wakati sisi tunatafuta methali,.............................. |
| 2. Tusibabaishwe na mabaya yaliyofanyika kwani............................................................ |
| 3. Ingawa mtu anaweza kuwa na ulemavu au upungufu fulani wa kimaumbile,................. |

**Kazi ya 25:**


Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** sehemu iliyoandikwa kwa italiki kwa kuzingatia ujumbe unaopatikana katika kifungu cha habari cha hapo juu (mfano mmoja ulitolewa):

| | |
|---|---|
| **Methali ni semi muhimu kwa binadamu kwani ni njia ya mkato ya** | ***kuelimisha wanajamii*** |
| | .............................. |
| | .............................. |
| | .............................. |

## SOMO LA 6: NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Kwa ushirikiano na mwenzako, tazameni picha ifuatayo. Nini **kinaonekana** kwenye picha hiyo?




**Kazi ya 2:**

Shirikiana na wenzako wawili na **kutofautisha** misemo na nahau kimaana.

**Kazi ya 3:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusishe** na picha hiyo kwa njia ya mazungumzo.

*Tupevuke katika lugha*

Nahau na misemo ni mojawapo kati ya semi za fasihi simulizi ya Kiswahili. Kauli hizi hutumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili katika mazungumzo yao ya kila siku. Walakini, uwezo wao wa kutumia nahau na misemo hutokana na ujuzi wa kila mtu katika matumizi ya lugha.

**1. Maana ya nahau na misemo**

Nahau na misemo ni semi fupi zinazotumia maneno ya kawaida lakini maana yake huwa fiche. Ni kusema kuwa maana yake kamili ni tofauti na maana ya asili. Picha ambazo zinatumiwa ndizo zinazozifanya semi hizi zisieleweke moja kwa moja. Kwa mfano, unaposema "Fulani amegonga mwamba katika shughuli zake za kibiashara" humaanishi kuwa "amepiga jiwe kubwa kwa mkono au mguu au kwa kifaa chochote". Unataka kusema kwamba "Fulani hakufanikiwa au hakuweza kuendelea katika shughuli zake za kibiashara".

**2. Tofauti kati ya nahau na misemo**

Nahau na misemo ni semi tofauti. Wanafasihi husema kuwa "nahau" ni semi zinazodai kitenzi maalumu ndani yake ili ziwe na maana ilhali "misemo" ni semi zisizokuwa na au zisizohitaji vitenzi. Maana kamili ya "misemo" haihitaji kitenzi ili kueleweka ingawa inaweza kutumiwa pamoja na vitenzi. Kwa mfano, "kupigwa kalamu", "kumwaga unga", "kugonga mwamba" ni nahau lakini "lila na fila", "mdomo na pua", hii ni misemo. Walakini, kutokana na tofauti hiyo ndogo, wanafasihi wengi hupendelea kutumia maneno hayo mawili pamoja yaani "nahau na misemo".

**3. Umuhimu wa nahau na misemo**

Hakuna jambo linalotumiwa katika fasihi lisilo muhimu. Vilevile, nahau na misemo huwa na umuhimu ufuatao:

a. Kupamba lugha: Matumizi ya nahau na misemo huletea lugha utamu wa hali ya juu. Kwa mfano, mwenzako anaweza kuwa na "tabia ya uchoyo". Haya ni maneno ya kawaida ambayo hutumiwa mahali kote na maana yake hueleweka kwa upesi. Kuna namna ya kutumia maneno mengine ya kawaida lakini yanayoiongezea tungo utamu kutokana na maana yake fiche. Unaweza kusema kuwa "fulani ni mkono wa birika". Vilevile, kama "fulani amekufa", unaweza kusema kuwa "amerudisha namba" au "ameaga dunia" au "amekata kamba". Hii ndiyo sababu matumizi haya huchukuliwa kama pambo la lugha.
b. Kupunguza ukali wa maneno: Siku za leo, mataifa yote yanapigana na janga la ugonjwa wa kuambukiza wa UKIMWI ambalo linaendelea kuangamiza watu wengi sana. UKIMWI si kama tetekuwanga au kifaduro kwani hauna dawa. Kwa hiyo, ni lazima wale wenye kiini au virusi vya ugonjwa huo watunzwe vizuri kama vile:

- kupatiwa dawa zinazowasaidia katika maisha yao na ambazo wanahitaji;
- kutofanyiwa ubaguzi wowote na kutotengwa na watu wengine;
- kutotumia kauli zinazoweza kuwafanya wadharauliwe na kadhalika.

Kuhusu kauli hizi, badala ya kusema kuwa "fulani aliweza kuvumilia" ingawa yuko katika hali mbaya ya kiafya kutokana na kuugua ugonjwa wa UKIMWI, unaweza kusema kuwa "fulani anajikaza kisabuni". Kama "amekufa", unaweza kutumia tamko la "kuaga dunia". Hii ni nahau na inaeleweka kuwa inapunguza ukali wa maneno ya kwanza.

c. Kuhifadhi lugha kama amali ya jamii: Nahau na misemo huundwa kutokana na vituu au vifaa vipya vinavyotumiwa na jamii. Mswahili alipoiona "darubini" na kuelewa jinsi inavyotumiwa, ndipo aliunda nahau mpya ambayo ni "kupiga darubini". Maana yake ni "kufanya uchunguzi". Ni kusema kuwa nahau hii inasaidia katika kuhifadhi dhana mpya ya Kiswahili. Hii ni namna ya kuhifadhi amali ya lugha ya jamii.

**4. Mifano ya nahau na misemo**

Soma mifano ya nahau na misemo ifuatayo ili kuelewa zaidi utamu wa lugha iliyotumiwa ndani yake:

- "Babu yangu **amekula chumvi nyingi**": Ni kusema kuwa "Babu yangu ameishi miaka mingi";
- "Kaka yake **amemwaga unga**": Inamaanisha kwamba "Kaka yake amefukuzwa kazini";
- "Fulani **ana ulimi wa upanga**": Ni kusema kuwa "Fulani ana maneno makali";
- "Aliyedhaniwa kuwa ni rafiki yake **alimpa nyama ya ulimi** tu": Inamaanisha kuwa "Aliyedhaniwa kuwa ni rafiki yake alimdanganya kwa maneno matamu";
- "Mwishoni mwa wiki, wafanyakazi wawili watapewa **kiinua mgongo**": Wao "watapewa malipo ya pongezi";
- "Wenye roho mbaya **wataona cha mtema kuni**": Ni kusema kwamba "Wenye roho mbaya watapata mateso mengi";
- "Kesho ndipo **tutapiga mali shoka**": Ni kusema kuwa "Kesho ndipo tutagawana mali yetu";
- "Wanyarwanda **wasivunjike moyo** katika harakati zao za amani na maendeleo ya nchi yao": Ni kusema "Wanyarwanda wasikate tamaa katika harakati zao za amani na maendeleo ya nchi yao".

**5. Matumizi ya nahau na misemo katika habari**

***Tamaa mbele mauti nyuma***

Siku hiyo, sote tulikuwa nyumbani. Jua liliaga miti na nuru ya mchana ikafifia. Anga ikavaa joho jeusi tititi kama kizimwili. Giza totoro likazagaa na kushamiri kote. Usiku ukashika hatamu na kutamalaki. Mimi na umbu zangu tulijipweteka

pwete makochini. Baadhi yao walisikika wakitia chumvi porojo zangu kuhusu nia ya kakangu ya kujipatia jiko huku mama na mnuna wangu wakituandalia chakula.

Muda mrefu haukupita kabla ya meza kujaa mapochopocho kochokocho na harufu nzuri kusikika kote sebuleni. Mara mchuano kati ya magego na mlo ukaanza. Mara kunyofoa minofu nyofu nyofu, mara kutafuna chapati sikwambii kugwengwenya mifupa!

Punde si punde, mambo yakatokea vuu. Kama ajali, tuligutushwa na kishindo kikuu kilichotisha kama Izraili. Sote tulituama na kuachama, tukabaki tumemaka. Nilinyanyuka na kusimama dede huku nikitetemeka tetete kama kifaranga aliyenyeshewa na mvua ya gharika katika msimu wa kipupwe. Nao wasiwasi wa mwasi ukanivaa kama libasi lakini nilipiga moyo konde. Kwa wayowayo na jakamoyo nilikwenda nyatunyatu na kutupa jicho. Kwetu na mahali penyewe palikuwa pua na mdomo. Viwiliwili vya watu wengi wenye kurunzi vilionekana vikikimbia mkikimkiki kuelekea barabarani.
Kumbe ni kweli, mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo! Mara maneno tepetepe na mipayuko kama ya wehu ikatamalaki na kuhinikiza hewani. “Leta mitungi! Ondoka nichote! Hiki ni chanzo cha amani na maendeleo ya kijiji chetu! Umaskini kwaheri! Ondoa ushamba, bwege wewe! Kila mtu anataka kuchota mafuta, usilete ubaradhuli!”  Ndizo sauti zilizowakosesha watu usingizi.

Fumbo hufumbiwa mjinga mwerevu akatambua! Papo hapo, niling’amua kuwa vya bwerere vilikuwa vimepatikana. Nilighairi kubaki nyuma kama koti la mzee na kuamua kuwa wa mbele kama mfuko wa shati. Nani asiyejua kuwa aliye kando haangukiwi na mti? Nilinyakua mtungi na kufululiza kenyekenye hadi palipokuwa na umati wa watu. Nilipofika, watu walikuwa wakiangukiana. Wengine walifokeana ungedhani walikuwa na kamusi ya matusi vinywani. Wengi wao walikula mwande! Wengine walifanya kazi chapuchapu. Nami nilifanya kulihali lakini nikagonga mwamba.

Tukiwa katika pilikapilika za kuyateka mafuta ya bwerere, jamaa fulani njorinjori, mrefu kama mlingoti na mweusi tititi kama lami aliwasha sigara. Kwa kweli, lila na fila havitangamani! Kabla hajapuliza fundo la kwanza, mlipuko wa ajabu ulisikika. Lo! Lahaula! Moto mkubwa ulizuka zu kama mizuka na kuzidi kuenea! Kukurukakara za kujinusuru zilianza. Ikawa ni pata shika, nguo kuchanika na miguu niponye. Watu waligongana dafrau na kuangushana kama magari barasteni.

Kila mmoja alijaribu kuisalimisha aushi yake. Moto nao uliendelea kuwaka na kuchoma bila huruma. Maskini wanyonge waliteketea teketeke kiasi cha kutoweza kutambulika.

Watu takriban hamsini walikata kamba na wengine kugeuzwa vilema. Niliponea katika tundu la sindano!

Kuona hivyo, niliikumbuka kauli ya wahenga kuwa “tamaa mbele, mauti nyuma.” Maneno tamaa, pupa na papara niliyazika katika kaburi la sahau maadamu yanaweza kuwa chanzo cha balaa. Tangu siku hiyo, maisha yangu yalichukua mwelekeo mpya.

(www.swahilihub.com)

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 4:**

Soma habari kisha ujibu maswali yafuatayo:

1. Eleza waziwazi kichwa cha kifungu cha habari kile.
2. Kwa nini wanafasihi wengi hupendelea kusema “nahau na misemo” ingawa ni mambo mawili tofauti?
3. Namna gani nahau na misemo ni semi zinazopunguza ukali wa maneno? Eleza vizuri.
4. Taja nahau (na misemo) zote zilizotumika katika kifungu cha habari “Tamaa mbele mauti nyuma”. Ni zipi maana yake?
5. Taja methali zote zilizotumika katika atini “Tamaa mbele mauti nyuma”. Toa matumizi yake.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

Anapokisoma mwenzako kifungu cha habari hiki, **tega sikio** na kuandika kwenye karatasi mawazo makuu ambayo umeyazingatia kutoka matini.

## B. Kusoma

**Kazi ya 6:**

Soma matini hii **mara** nyingine.

**Kazi ya 7:**

Unaona **nini** kwenye picha hii? **Taja** nahau moja ya Kiswahili inayotokana na kitendo cha mwizi unachokiona kwenye picha:



**Kazi ya 8:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. Kwa .................................. nilikwenda nyatunyatu na kutupa jicho.
2. Nahau na misemo ni semi fupi zinazotumia maneno ya kawaida lakini maana yake .......
3. Nilighairi kubaki nyuma kama .................... na kuamua kuwa wa mbele kama mfuko wa shati.
4. Kama ajali, tuligutushwa na kishindo kikuu kilichotisha kama ....................

**Kazi ya 9:**

**Soma** tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na **kuzihusisha** na zile za kikundi cha B ili kupata sentensi sahihi:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Kabla hajapuliza fundo la kwanza, | kwani hauna dawa |
| 2. UKIMWI si kama tetekuwanga au kifaduro | ikatamalaki na kuhinikiza hewani |
| 3. Muda mrefu haukupita kabla ya meza kujaa mapochopocho kochokocho | mlipuko wa ajabu ulisikika |
| 4. Mara maneno tepetepe na mipayuko kama ya wehu | na harufu nzuri kusikika kote sebuleni |

## C. Msamiati

**Kazi ya 10:**

Katika jozi, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na **kuchunguza maana** ya maneno yafuatayo:


**Darubini**
**Majungu**
**Kuzagaa**
**Kushamiri**
**Umbu**
**Kochokocho**
**Kugwengwenya**
**Kutuama**
**Libasi**
**Jakamoyo**
**Ushamba**
**Bwege**
**Bwerere**
**Dafrau**

**Kazi ya 11:**

Katika pea hiyo, tungeni sentensi kwa **kila neno** kati ya hayo ya hapa juu.

**Kazi ya 12:**

Tazama picha zifuatazo na **kuzitaja** nahau zinazohusiana nazo na maana yake. Tumia kitenzi "kupiga":









**Kazi ya 13:**

Katika pea, tajeni **maana** ya nahau (au misemo) zifuatazo na **kuzitumia** katika sentensi (sentensi moja kwa kila nahau au msemo):

1. Kuchungulia kaburi;
2. Kutia utambi;
3. Kutoa lulu;
4. Kumwaga unga.

**Kazi ya 14:**

Katika jozi, **jazeni** jedwali lifuatalo kwa kutumia nahau zinazotokana na vitenzi ambavyo vimetolewa. Kumbukeni kutoa maana yake:

| **Kitenzi** | **Nahau** |
|---|---|
| 1. Kupiga | ...........................................(nahau saba) |
| 2. Kuchapa | ............................................(nahau tatu) |

**Kazi ya 16:**
"Giza **totoro** likazagaa na kushamiri kote". Neno "totoro" limetumiwa kama msisitizo. Tafuta maneno mengine yaliyotumiwa kama msisitizo katika matini "tamaa mbele mauti nyuma".

**Kazi ya 16:**

Katika jozi, **sisitizieni** kauli zifuatazo:

1. Hadija alimwomba dadake viatu lakini dadake alimwambia, "sikupi................".
2. Mvua ilimnyeshea na kurowa...........................................................................
3. Alishika buku lile na kulichana.........................................................................
4. Alipofika nyumbani alitulia...............................................................................
5. Fulani alifunga kamba na kulikaza......................................................................

**Kazi ya 17:**

"Anga ikavaa joho jeusi tititi **kama kizimwili**". Hii ni namna ya kulinganisha vitu. **Tafuta** katika kifungu cha habari "Tamaa mbele, mauti nyuma" kauli zote ambamo mbinu hii ya mlinganisho au tashbiha au mshabaha ilitumiwa.

**Kazi ya 18:**

Katika jozi, **kamilisheni** sentensi zifuatazo kwa kutumia neno linaloingiza mlingano au tashbiha au mshabaha:

1. Mganga anayeshughulikia mambo ya kuboresha uzazi ni mrefu kama.........................
2. Kiranja wa darasa letu ni mfupi kama.............................................................................
3. Dadake anayeugua UKIMWI amekonda na kuwa kama.........................................
4. Yeye anasema kama..........................................................................................................
5. Kiongozi anayeshughulikia mambo ya uzalishaji mali ana akili kama.............................

**Kazi ya 19:**

Panga kauli zifuatazo katika makundi yake haya:

Cheche huzaa moto
Alimpiga pambaja mwandani
Uchungu wa mwana aujuaye mzazi
Usimpe nyama ya ulimi
Kaza kamba ndugu!
Yote yang'aayo si dhahabu

| 1 | 2 |
|---|---|
| Nahau | Methali |

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 20:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako yale ambayo **umeyasoma**.

**Kazi ya 21:**

Kwa njia ya mazungumzo, **kamilisha** tungo zifuatazo ili kupata **nahau (au msemo)** inayofaa:

| Tungo ya kukamilisha | Neno la kukamilisha |
|---|---|
| 1. Badala ya kutumia neno "kuoa", yeye alisema kuwa "alijipatia..................." | ..................................... |
| 2. Kumezea..............kitu ni kukitamani sana | .................................... |
| 3. Anapoishi si mbali; ni pua na.............. | .................................... |

**Kazi ya 22:**

Kwa njia ya mazungumzo, **taja** nahau zako sita bila kurudilia zilizotajwa darasani.

**Kazi ya 23:**

Kwa njia ya mazungumzo, **kamilisha** ipaswavyo misemo ifuatayo:

1. Ndugu yake alimkaribisha..............................upande.
2. Mdogo wangu ni...............na njia yaani mtu asiyetulia mahali pamoja.
3. Kwa ................na sindano, waliweza kuboresha uzazi katika familia yao.

**Kazi ya 24:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari na kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

1. Tukiwa katika pilikapilika za kuyateka mafuta ya **bwerere**, jamaa fulani njorinjori, mrefu kama mlingoti na mweusi tititi kama lami aliwasha sigara
2. "Kaka yake **amemwaga unga**": Inamaanisha kwamba "Kaka yake **amefukuzwa kazi**"
3. Nami nilifanya **kulihali** lakini nikagonga mwamba

## F. Utafiti

**Kazi ya 25:**

Shirikiana na mwenzako mtafute kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au kwa majirani zenu **nahau mbalimbali za Kinyarwanda** na maana yake na kuzitafsiri katika Kiswahili. Msisahau kuwasomea wenzenu matokeo ya kazi yenu.

## G. Mchezo

**Kazi ya 26:**

Uliza **swali la kijinga** na kutoa jibu lake la kijinga.
Mfano: Umeisha piga mswaki? / Ndiyo! Ngumi tano na makofi mawili.
Lakini jana ulichapa maji! / Hapana! Nilikosa taipu yaani mashine ya kupigia chapa!

## H. Kuandika

**Kazi ya 27:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| Kwa | wayowayo | na | jakamoyo | nilikwenda | nyatunyatu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**Kazi ya 28:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja ulitolewa):

| *Kukurukakara* | *za* | *kujinusuru* | zilianza |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

**Kazi ya 29:**

**Andika** jedwali hili katika daftari lako na **kulijaza** kwa kutumia **nahau** ambamo jina la kitu kifuatacho lilitumiwa:

| Kitu | Nahau | Maana |
|---|---|---|
| | | |









**Kazi ya 30:**

Katika jozi, **tungeni** aya moja ambamo mtatumia nahau tano **tofauti** na zile mlizorudilia darasani.

# SOMO LA 7: VITENDAWILI VYA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Taja vitu mbalimbali **unavyoona** kwenye picha hii.




**Kazi ya 2:**

Soma hadithi ifuatayo na **kuihusisha** na picha hii kwa njia ya mazungumzo.

***Vitendawili hukuza uwezo wa kufikiria***

Kipera kingine cha fasihi simulizi ni vitendawili. Hiki ni kipengele cha semi fupi ambazo humfanya mtu afikiri sana kuhusu mazingira yake.

**1. Maana ya vitendawili**

Kitendawili ni tungo fupi ambayo huwa na swali wazi yaani swali linaloulizwa kwa kutumia lugha ya mafumbo. Mafumbo hayo ndiyo yanayoufanya utanzu huu uwe wa sanaa ya hali ya juu.

Majibu hutolewa kwa makusudi ya kupima ufahamu wa hadhira kuhusu mazingira yake. Kujibu kunahitaji ujuzi mkubwa kulingana na tamaduni za mazingira ya jamii husika. Mtu hujibu kiufundi kwa kuzingatia utaratibu wa kuvutia.

**2. Kutega na kutegua vitendawili**

Vitendawili huzingatia mfumo wa kutega (yaani kuuliza swali) na kutegua (au kujibu swali). Mtegaji na mteguaji hutii utaratibu ufuatao:

a. Mtegaji : Kitendawili!
b. Mteguaji : Tega!
c. Mtegaji : (Anatoa kitendawili chake yaani “kutega kitendawili”).
Mfano : Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona
d. Mteguaji : (Anatoa jibu yaani “kutegua kitendawili”).
Jibu : Nyota

Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.

**3. Umuhimu wa vitendawili**

Vitendawili ni kipengele cha fasihi simulizi ya Kiswahili ambacho ni muhimu katika jamii ya Waswahili. Vitendawili:

- **Huburudisha watu**: Hii ni namna ya kuwafanya watu wapumzike na kutulia. Kwa kawaida, jioni ni wakati mzuri wa kupumzika kwa watu mbalimbali baada ya kumaliza kazi za mchana. Wakati huu, ndipo vitendawili hutolewa. Walakini, siku hizi yapo masomo ya wanafunzi shuleni yanayohusu vitendawili. Kwa hiyo, wao hulazimishwa kutega na kutegua vitendawili kama zoezi linalolenga kuwaongezea ujuzi katika lugha. Ili watu waweze kuburudika ipaswavyo, vitendawili hutegwa kwa njia ya uchangamfu na ushindani.
- **Huunganisha jamii**: Kwa kawaida, vitendawili vinapotegwa na kuteguliwa, watu hukusanyika pamoja. Huko kuwaleta watu pamoja huwa chanzo cha kuwasiliana kati yao, kushirikiana, kuunga urafiki na kuwa na umoja. Wakubwa na watoto, wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, wote huweza kukusanyika pamoja bila ubaguzi ili kufaidika kutoka elimu hii isiyo na ubaguzi.
- **Huhamasisha watu kuhusu mazingira yao**: Vitendawili, kama mchezo wa ushindani, hulenga vitu vinavyopatikana katika jamii husika. Vitendawili vya jamii isiyojua “kompyuta na mtandao wa intaneti” haviwezi kuzungumzia kuhusu jambo hili kwani halijulikani katika mazingira yake. Kulenga vitu vinavyojulikana mahali hapo huwafanya wanajamii wote wavijue na wajue umuhimu wake kwao katika mvuvumko wa kiutandawazi. Kwa mfano, Wanyarwanda wengi wana mwamko wa kutumia kompyuta na intaneti. Kuunda vitendawili kuhusu jambo hili kutawafanya Wanyarwanda wa vitongojini walijue na kushughulikia matumizi yake. Namna hii ya kuwahamasisha kuhusu mazingira yao itawawezesha kushughulikia amani na maendeleo ya nchi yao.
- **Hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka**: Kutegua kitendawili huhitaji kukumbuka kitendawili ambacho kimetolewa, kufikiri kuhusu mazingira yake na kujaribu kupata jibu. Katika shughuli hii, mteguaji huwaza sana kuhusu mazingira hayo na kulinganisha majibu mbalimbali yanayoweza kutolewa. Hii ni namna moja ya kukuza uwezo wake wa kukumbuka na kufikiria.

- **Hukuza na kuhifadhi amali na tamaduni za jamii**: Siku za leo, vipo vitendawili vingi vilivyotungwa na watu wa vizazi vilivyotangulia. (Mfano: *Wanangu wote wanavaa vizibao, wasiovaa si wangu* / Jibu: *Kunguru wenye mabaka meupe*). Vilevile, vipo vitendawili vya kisasa vinavyoundwa kutokana na mazingira mapya ya jamii husika. (Mfano: *Nina watoto wanne lakini akiondoka mmoja wanaosalia hawafanyi kazi* / Jibu: *Magurudumu ya gari*). Hali hii hudhihirisha kuwa tamaduni za vizazi vya zamani zilitufikia kupitia vitendawili kwa sababu utanzu huu hupokezanwa kutoka kizazi hadi kizazi.
- **Vilitumika kwa muda mrefu kupitisha wakati na kuwafanya watoto wasilale mapema kabla ya chakula kuwa tayari**: Katika siku zilizopita, vitendawili vilitumiwa kama njia ya kuwafanya watoto wangojee na kuvumilia mpaka chakula kiwe tayari.

**4. Mifano ya vitendawili na majibu yake**

Hivi vifuatavyo ni baadhi ya vitendawili vya Kiswahili. Majibu yake yanapatikana mkabala na vitendawili hivyo.

| Namba | Kitendawili | Jibu |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba yangu ndogo ina madirisha mengi | Dema |
| 2 | Mama nieleke | Kitanda |
| 3 | Nyumba yangu haina milango | Yai |
| 4 | Kipo lakini sikioni | Kisogo |
| 5 | Parrrr! Mpaka Makka! | Utelezi |
| 6 | Pana visu vingi lakini mpini mmoja tu | Chane ya ndizi |
| 7 | Popoo mbili zavuka mto | Macho |
| 8 | Ini la ng’ombe huliwa hata na walio mbali | Kifo |
| 9 | Chatembea na hakijapata kupumzika hata nukta moja | Jua |
| 10 | Njoo hapa nije hapo | Kiraka |
| 11 | Anajenga ingawa hana mikono | Ndege |

**Tanbihi:** Kuna kipengele kingine cha fasihi simulizi kinachofanana kwa kiasi na vitendawili lakini chenye utaratibu wake wa kipekee. Kipengele hicho ni “**mafumbo**”. Mafumbo ni kauli zinazoeleza jambo kwa njia fiche yaani isiyo wazi. Msimulizi anatoa fumbo lake na kazi ya wasikilizaji ni kulifumbua.

Katika mchezo huu wa ushindani wa mafumbo, msimulizi anasema “Fumbo mfumbie mjinga”. Msikilizaji anajibu “Mwerevu hiling’amua” na kufumbua jambo linalozungumziwa. Mifano ya mafumbo na ufumbuzi wake:

a. Mimi na ndugu yangu tulinunua fahali mmoja kutoka sokoni. Baada ya mwaka mmoja alijifungua ndama wawili. Je, kila mtu alipata wangapi? / [Ufumbuzi: Fahali hajifungui].
b. Watu watatu walikuwa safarini. Walipofika karibu na mto, iliwabidi wote kuvuka kwenda ng'ambo lakini hawakuwa na mtumbwi wala daraja la kuvukia. Wakati wa kuvuka, mmoja aliyaona na kuyakanyaga maji. Mwingine aliyaona lakini hakuyakanyaga. Wa tatu hakuyaona wala kuyakanyaga lakini alivuka. Je, watu hao walikuwa nani? / [Ufumbuzi: Aliyeyaona na kuyakanyaga ni mama mjamzito. Aliyeyaona na kutoyakanyaga ni mtoto aliyebebwa mgongoni. Aliyekosa kuyaona na kuyakanyaga ni mtoto aliyekuwa tumboni mwa mama yake].
c. Ajali mbaya ya gari ilitokea kwenye mpaka wa Kenya na Uganda. Wengi kati yao walipoteza maisha yao. Je, majeruhi walizikwa wapi? / [Ufumbuzi: Majeruhi hawakuzikwa, walipelekwa hospitalini].

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari na **kujibu** maswali yafuatayo:

1. Namna gani vitendawili hukuza uwezo wa kufikiria na kukumbuka? Eleza waziwazi.
2. "Vitendawili hutegwa kwa njia ya uchangamfu na ushindani". Eleza kinagaubaga.
3. Je, ni ipi tofauti kati ya vitendawili na mafumbo kuhusu namna michezo hiyo inavyochezwa? Eleza waziwazi.
4. Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mambo huwaje?
5. Je, ni ipi dhima ya vitendawili katika jamii? Taja bila kueleza.
6. "Vitendawili ni kipengele cha masimulizi". Eleza vizuri.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Anapoisoma habari hii mwenzako, **tega sikio** na kuandika kwenye karatasi mawazo makuu ambayo umeyazingatia kutoka matini.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma matini hii **mara** nyingine ili kuielewa vizuri.

**Kazi ya 6:**

**Husisha** picha ifuatayo na kitendawili hiki "**Anajenga ingawa hana mikono**":



**Kazi ya 7:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. Siku za leo, vipo vitendawili vingi vilivyotungwa na ................................ vilivyotangulia.
2. Kitendawili ni tungo fupi ambayo huwa na .................... yaani swali linaloulizwa kwa kutumia lugha ya mafumbo.
3. Kujibu kunahitaji ujuzi mkubwa kulingana na tamaduni ............................. ......... husika.

**Kazi ya 8:**

**Soma kwa sauti na ufasaha** sentensi zifuatazo zilizotumiwa katika kifungu cha habari chetu:

1. Walipofika karibu na mto, iliwabidi wote kuvuka kwenda ng'ambo lakini hawakuwa na mtumbwi wala daraja la kuvukia.
2. Hali hii hudhihirisha kuwa tamaduni za vizazi vya zamani zilitufikia kupitia vitendawili kwa sababu utanzu huu hupokezanwa kutoka kizazi hadi kizazi.
3. Mafumbo hayo ndiyo yanayoufanya utanzu huu uwe wa sanaa ya hali ya juu.

## D. Msamiati

**Kazi ya 9:**

Katika pea, **tumieni** Kamusi ya Kiswahili Sanifu na **kuchunguza maana** za maneno yafuatayo:

**Kizibao**
**Dema**
**Chane**
**Popoo**

**Kazi ya 10:**

Katika pea hiyo, tungeni sentensi kwa **kila neno** kati ya hayo ya hapo juu.


**Kazi ya 11:**

Kwa kutumia maneno yafuatayo, tunga sentensi kamili zenye maana zinazohusu **ujasiriamali**:

Ubaguzi.......................................
Kutegua kitendawili...........................
Mjamzito.........................................
Kung'amua.....................................

**Kazi ya 12:**

Katika pea, tajeni vitendawili ambamo mna **majina** ya vitu vifuatavyo (**si** katika majibu yake):

1. 
   (kupiga mbizi).......................... .............

2. 
   (nyumba yangu)...................................

**Kazi ya 13:**

Katika jozi, **tegueni** vitendawili vifuatavyo kwa kutumia **picha** (choreni picha).

1. Nimesimika moja nikaezeka /..............................................................
2. Saa yangu kila siku hutembea, ikisimama haitengenezeki tena /....................
3. Mifugo ya babu imetafuna ukuta /.......................................................

**Kazi ya 14:**

Katika jozi, **someni** majina yafuatayo. Mnaona kuwa yameendelezwa **vibaya**. Sasa, **pangeni silabi vizuri** ili kulipata neno sahihi:

1. Opopo;
2. Gokiso;
3. Windateliki.

**Kazi ya 15:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa maneno **yaliyotumiwa** katika habari:

1. Wanyarwanda wengi wana mwamko wa kutumia mashine iitwayo................. na intaneti.
2. Kutegua kitendawili huhitaji kukumbuka kitendawili ambacho kimetolewa, kufikiri kuhusu .................................... yake na kujaribu kupata jibu.
3. Katika siku zilizopita, vitendawili vilitumiwa kama njia ya kuwafanya watoto wangojee na kuvumilia mpaka ................................. kiwe tayari.

**Kazi ya 16:**

Katika jozi, **changanueni** maneno haya kufuatana na **maana** zake na kuyaandika katika makundi yake halisi. Tumieni **alama** hii (X).

| Kauli | Methali | Kitendawili |
|---|---|---|
| 1. Huzitoa zikarudi | | |
| 2. Dunia hadaa na walimwengu shujaa | | |
| 3. Ninacho lakini sikitumii | | |
| 4. Mkufu wangu mrefu unatembea | | |

**Kazi ya 17:**

Jiunge na wenzako wawili na kujadili **dhima ya mafumbo** katika kufundisha lugha. Msisahau kuwasomea wanafunzi wengine matunda ya kazi yenu.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 18:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako yale ambayo **umeyasoma**.

**Kazi ya 19:**

Kwa njia ya mazungumzo, yataje **majina ya watu** wanaofanya **kitendo** kifuatacho:

| Kitendo | Jina |
|---|---|
| 1. Kutega kitendawili | |
| 2. Kutegua kitendawili | |

**Kazi ya 20:**

Kwa njia ya mazungumzo, soma vitendawili vifuatavyo na majibu yake yaliyotolewa kwa kutumia michoro:

1. Askari mlangoni / 

2. Mhuni wa ulimwengu / 
3. Mfalme katoa jicho jekundu / 
4. Mzungu anachungulia dirishani / 


**Kazi ya 21:**

Kwa njia ya mazungumzo, **tegua** vitendawili vifuatavyo:

1. Pana visu vingi lakini mpini mmoja tu /......................................................
2. Ng'ombe wangu huchungiwa mlimani /.......................................................
3. Mkufu wangu mrefu unatembea /................................................................
4. Hazikauki umande /...................................................................................

**Kazi ya 22:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Kuna kipengele kingine cha fasihi simulizi kinachofanana kwa kiasi na vitendawili lakini chenye | ............................................................... ...................... |
| 2. Hali hii hudhihirisha kuwa tamaduni za vizazi vya zamani zilitufikia kupitia vitendawili kwa sababu utanzu huu | ............................................................... ...................... |

| | |
|---|---|
| 3. Kwa kawaida, jioni ni wakati mzuri wa kupumzika kwa watu mbalimbali baada ya | ................................................................................... |

## F. Mchezo

**Kazi ya 23:**

Uliza **swali la kijinga** na kutoa jibu lake la kijinga.
Mfano: Hilo ni gazeti la leo? / hapana ni langu.
Umeamkaje? / Kwa kufungua macho na kushuka kitandani kwa miguu yangu miwili.

**Kazi ya 24:**

Shirikiana na mwenzako na kujaza jedwali lifuatalo kwa kutumia maneno yenye **maana** hizi:

| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | | | | | | | | |
| B | | | ■ | ■ | | ■ | ■ | |
| C | | | ■ | ■ | | ■ | | |
| D | | | | | | | | |
| E | | | ■ | ■ | | ■ | | |
| F | | | | | | | | ■ |
| G | | | ■ | ■ | ■ | ■ | | ■ |
| H | ■ | | | | | | | ■ |

**Upande wa kushoto-kulia:**

A/1: Sehemu nyembamba katika nyumba au baina ya nyumba na nyumba;
D/1: Aina ya andazi dogo la duara linalotengenezwa kwa nyama iliyosagwa kisha ikakaangwa;
F/1: Majira ya mvua nyingi za mfululizo katika ukanda karibu na ikweta;
H/2: Maandiko ya wafuasi wa Yesu Kristo yenye kueleza maisha, matendo na mafundisho yake.

**Upande wa juu-chini:**

1/A: Kazi ya kuhukumu au ya hakimu;
2/A: Chombo kirefu cha udongo au bati kinachotumiwa kuchemshia maji na chenye nafasi ya kutilia makaa chini;
5/A: Aina ya mtungi mkubwa wa kuwekea maji;
7/C: -enye udhaifu;
8/A: Mwanamke mzee sana au bikizee.

## G. Utafiti

**Kazi ya 25:**

Katika kundi la wanafunzi wanne, **tafuteni** kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au ulizeni majirani zenu vitendawili ishirini (20) vya Kiswahili na majibu yake.

## H. Tafsiri

**Kazi ya 26:**

**Tafsiri** katika Kiswahili vitendawili vya Kinyarwanda vifuatavyo:

1. Nshinze umwe ndasakara / Igihumyo (icyobo)
2. Mugongo mugari mpekera abana / Uburiri
3. Gitimba araguye n'ingabo ze / Igitoki n'amakoma
4. Karakurizaga karakurutaga wa duri we! / Akanyarirajisho

## I. Kuandika

**Kazi ya 27:**

Andika vitendawili ambavyo **majibu yake** ni haya yafuatayo (yanaonekana kwa kutumia **michoro au picha**):

1. 

2. 

3.  .............................................

**Kazi ya 28:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| **Mtu** | **hujibu** | **kiufundi** | **kwa** | **kuzingatia** | **utaratibu wa kuvutia** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

**Kazi ya 29:**

Andika sentensi hii katika daftari yako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja ulitolewa):

| **Vitendawili** | ***huburudisha*** | ***watu*** |
|---|---|---|
| Vitendawili | | |

**Kazi ya 30:**

Katika jozi, andikeni **aya moja** ambamo mnaelezea **ugumu wa kazi ya kutafsiri** vitendawili.

**Kazi ya 31:**

Tumia **mishale** kwa kuhusisha tungo katika kikundi cha A na tungo katika kikundi cha B ili kupata **sentensi yenye maana kamili**.

| **Kikundi cha A** | **Kikundi cha B** |
|---|---|
| 1. Walipofika karibu na mto, iliwabidi wote kuvuka kwenda ng'ambo | kutokana na mazingira mapya ya jamii husika |
| 2. Vilevile, vipo vitendawili vya kisasa vinavyoundwa | apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu |
| 3. Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huitisha | lakini hawakuwa na mtumbwi wala daraja la kuvukia |

# **SOMO LA 8**: USHAIRI WA KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI

**Kazi ya 1:**

Taja vitu mbalimbali **unavyoona** kwenye picha hii.






**Kazi ya 2:**

**Husisha** picha hii na kifungu cha habari cha hapo chini.

***Tujue ushairi simulizi wa Kiswahili***

Ushairi ni utanzu mkongwe sana katika fasihi ya Kiswahili. Utanzu huu unahusiana sana na nyimbo na una sanaa ya juu ya lugha.

**1. Maana ya shairi na ushairi**

Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo. Mtungo huo unaeleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha. Hufuata utaratibu wa urari na muwala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa shairi unaohusika. Muundo maalumu ndio unaoletea shairi utamu unaotakiwa.

Ushairi nao ni kazi au namna ya kutunga mashairi na kipengele chenyewe kinachoundwa na mashairi.

**2. Historia ya ushairi wa Kiswahili**

Ni vigumu kidogo kubashiri ni lini ushairi wa Kiswahili ulipoanza. Walakini, wanafasihi wengi wanaamini kuwa ushairi huo ni zao la jamii ya Waswahili lililokuwepo tangu karne ya pili Baada ya Kristo (BK). Mashairi yaliyokuwa yakitungwa enzi hizo hayakuwa na utaratibu wa vina, mizani na beti kama ilivyo katika mashairi ya kisasa. Mashairi ya siku hizo yalifanana sana na nyimbo kwani ndizo zilizokuwa chimbuko lake. Kutokana na kazi alizokuwa akifanya, binadamu alianza kutunga maneno na sauti za muziki zilizokuwa zikifuata mapigo ya zana za kazi. Wimbo wa kazi ukawa ndio utanzu wa fasihi wa mwanzo. Polepole, ushairi ulianzishwa kwa kuiga mapigo ya nyimbo.

Nyakati hizo, mashairi yalikuwa yakienezwa kisimulizi tu kwa sababu jamii ya Waswahili ilikuwa haijapata ustaarabu wa kusoma na kuandika. Mabadiliko mengi ya kimaudhui yalifanyika wakati wa majilio ya Waarabu sehemu za pwani ya Afrika ya Mashariki. Waarabu walikuja na hati yao ya Kiarabu na mashairi yao yenye beti, mizani, vina na maudhui ya kidini. Basi mashairi simulizi ya Waswahili yakafuata mtindo huo mpya. Ni kusema kuwa ushairi wao ulikua na kuendelea kadiri jamii ilivyokua na kuendelea.

### 3. Umuhimu wa ushairi simulizi wa Kiswahili

Ushairi simulizi wa Kiswahili kama utungo unaotumia lugha ya Kiswahili hueleza maisha ya Waswahili yaani wenyeji na watumiaji wa lugha hiyo. Wao walitumia mashairi katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile katika harusi, jando na unyago. Ushairi huo huwa na umuhimu wake kama vile:

a. **Kusaidia kurithisha maarifa kwa jamii, kuelimisha na kukosoa hadhira husika**: Kupitia ushairi huu, jamii inaweza kujifunza mambo mbalimbali kama vile:

- Kutoa nasaha njema na wasia;
- Kutahadharisha watu kuhusu ulimwengu na malimwengu;
- Namna ya kuepukana na magonjwa ya kuambukiza ambayo yanayaangamiza maisha ya watu kama vile UKIMWI;
- Umuhimu wa usawa wa jinsia;
- Umuhimu wa kutunza mazingira;
- Umuhimu wa kuwa na tabia au mwenendo mwema katika jamii na kadhalika.

Kwa mfano, katika ubeti ufuatao, mtunzi anarithisha jamii maarifa kwa kusisitizia jamii izingatie umuhimu wa elimu:

“Elimu ni kikata kiu,
Huondoa pia ukungu,
Pasipo njia pakawa,
Fanya kazi utayapata,
Kazi ni kinga ya heba,
Sasa umekuwa na uwe,
Huu usinga nakupa,
Na unyoya nakuchomekea nyweleni.”

**(Kezilahabi Euphraseus)**

b. **Kusaidia kuhamasisha jamii:** Tendo la kuhamasisha wanajamii hufanyika katika shughuli mbalimbali.

c. **Kusaidia kudumisha na kuendeleza utamaduni katika jamii:** Kupitia ushairi huu, wanajamii huhakikisha kuwa utamaduni wao unabaki hai. Kwa mfano, katika sherehe mbalimbali, mashairi hutongolewa kwa kusifu amali na tamaduni za jamii.

d. **Kuburudisha, kufurahisha, kuchekesha hadhira na kuliwaza mtu wakati wa majonzi:** Licha ya nyimbo na vitendawili, mashairi ni wenzo kuu wa burudani katika jamii. Jambo hili hutokana na uwezo wake wa kuathiri hisia za wasikilizaji na kuwaburudisha. Mashairi huweza pia kuliwaza mtu wakati wa majonzi.

e. **Kusaidia kukuza kipawa cha mtu katika sanaa ya lugha na ukwasi wa lugha na kuisarifu lugha:** Kwa kawaida, mashairi hutungwa kwa lugha nzito, lugha ya ishara na mafumbo inayoeleweka kwa wanajamii wanaohusika. Sifa hii huwa njia ya kuwasaidia Waswahili na watu wengine kukuza hisia za kujitambua kwao kama watu wa kundi moja lenye mtazamo na mwelekeo fulani.

**4. Aina za mashairi simulizi ya Kiswahili**

Mashairi simulizi ya Kiswahili hugawanyika katika makundi mbalimbali kutokana na jambo linalozungumziwa. Makundi hayo ni:

- **Mashairi ya simango:** Ni yale yenye kauli ya simbulio.
- **Mashairi ya kashifa:** Ni mashairi yanayotoa siri ya mtu au ya jamii hadharani kwa kumkosoa au kuikosoa.
- **Mashairi ya wasifu:** Humsifu mtu au jamii ili kumtukuza au kuitukuza.
- **Mashairi ya uzinduzi:** Humwamsha mtu atoke katika hali ya kupumbazwa au kuwa mtumwa na kupigania haki zake.
- **Mashairi ya waadhi:** Ni yale yanayotoa maudhui ya nasaha njema kwa kumwadibu mtu.
- **Mashairi ya mapenzi:** Ni yale yanayohusu kuteka penzi la mtu.
- **Mashairi ya kujigamba au majigambo:** Kujigamba ni kujisifu au kujinaki. Mtu hujisifu kutokana na matendo yake ili wengine wamwogope na wamheshimu kwa ujasiri wake.
- **Mashairi ya kuomboleza au maombolezo:** Ni yale yanayozungumzia msiba au wakati wa huzuni.

**5. Mfano wa shairi simulizi la Kiswahili**

(Hili ni shairi linaloingia katika kundi la majigambo):

"Mimi ni Shikwekwe mwana wa Amuli.
Ninaitwa Simbamkali wa Bwanamkali,
Ningurumapo waoga hukimbilia mwituni,
Ukali wangu washindana na pilipili!
Nishikapo adui zangu,
Hata wakibeba sime na mikuki,
Hujinyea na kuomba samahani hurumia!
Nimevikomboa vichaka vya Msumbiji,
Na Angola nimekomesha majangili
Mwana wa Amuli nawika!

Heshima ni yako mtemi!"

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari kimoyomoyo kisha ujibu maswali yafuatayo:

1. Je, ni ipi tofauti kati ya shairi na ushairi?
2. Mashairi ya Kiswahili ya mwanzoni (kabla ya karne ya pili BK) yalikuwaje kimuundo?
3. Ushairi wa Kiswahili ulianzishwa namna gani?
4. Wakati gani mabadiliko mengi ya kimaudhui yalifanyika katika ushairi wa Kiswahili?
5. Ushairi wa kiarabu ulikuwaje?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Anapokisoma kifungu cha habari mwenzako, **tega sikio** na kuandika kwenye karatasi mawazo makuu ambayo umeyazingatia.


## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma kifungu cha habari hiki **mara** nyingine ili kukielewa vizuri.

**Kazi ya 6:**

**Husisha** shairi la hapa juu linaloingia katika kundi la majigambo na picha ifuatayo:



**Kazi ya 7:**

**Kamilisha** sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. Kwa kawaida, mashairi hutungwa kwa lugha nzito, lugha ya ..................... inayoeleweka na wanajamii wanaohusika.
2. Wanafasihi wengi wanaamini kuwa ushairi huo ni zao la jamii ya Waswahili lililokuwepo ................................ Baada ya Kristo (BK).
3. Mtu hujisifu kutokana na matendo yake ili wengine wamwogope na wamheshimu kwa .....................wake.

**Kazi ya 8:**

**Soma** kwa sauti na ufasaha ubeti ufuatao wa shairi lililotungwana Kezilahabi Kichomi na **kulikariri** ipaswavyo. Ni **burudani** gani tunayoipata katika ubeti huo?:

“Mtoto wa tajiri akilia hupewa mkate,
Mtoto wa tajiri akilia hupewa picha ya kuchezea,
Akilia mtoto wa tajiri huletewa kigari akapanda,
Akiendelea kulia hupanda mgongo wa yaya,
Akikataa kunyamaza ulimwengu mzima hulaumiwa!”

## D. Msamiati

**Kazi ya 9:**

Katika pea, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na **kuchunguza maana** ya maneno yafuatayo:

Muwala
Ustaarabu
Sime

**Kazi ya 10:**

**Tunga** sentensi moja kwa **kila neno** kati ya hayo ya hapo juu.

**Kazi ya 11:**

**Kamilisha** sentensi zifuatazo kwa kutumia neno linalopatikana **katika kifungu** cha habari chetu:

1. Mashairi ya....................hutoa maonyo kuhusu nasaha njema.
2. Walinzi wa Mbuga ya Wanyama ya Akagera walilikimbiza kundi la ..................... kumi.

**Kazi ya 12:**

Katika jozi, wekeni maneno yafuatayo katika **vikundi vyake**:

| **Maneno** | **Kikundi cha shughuli za kijamii ambamo mashairi huweza kutungwa** | **Kikundi cha mambo mengine** |
|---|---|---|
| Jando<br>Wanafasihi<br>Mshairi<br>Unyago<br>Msiba<br>Uyoga<br>harusi | | |

**Kazi ya 13:**

Maneno haya **yameendelezwa** vibaya. Panga silabi hizi vizuri ili neno liwe **sahihi**.

1. Gonyau..............................................................
2. Ngimalija...........................................................
3. Kumiki...............................................................
4. Omwekele.........................................................

**Kazi ya 14:**

**Tunga** shairi lenye **beti tatu** kuhusu “elimu”. Ni lazima maneno haya yatumiwe katika shairi hilo [mwanadamu; ufunguo; elimu].

**Kazi ya 15:**

Jiunge na wenzako watatu, **jadilini istilahi** zinazotumiwa katika ushairi wa Kiswahili. Msisahau **kuwasomea** wanafunzi wengine matunda ya kazi yenu.

**Kazi ya 16:**

**Kamilisha** sentensi zifuatazo kufuatana na **jinsi zilivyo** katika kifungu cha habari chetu:

1. Mashairi huweza pia .......................... mtu wakati wa majonzi.
2. Tendo la ............................ wanajamii hufanyika katika shughuli mbalimbali.
3. Ushairi simulizi wa Kiswahili kama utungo unaotumia lugha ya Kiswahili hueleza maisha ya Waswahili yaani ........................................... wa lugha hiyo

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 17:**

Waambie wenzako yale ambayo **umeyasoma** katika kifungu cha habari chetu.

**Kazi ya 18:**

Kwa njia ya mazungumzo, jadili **dhima** ya ushairi wa Kiswahili kwa kutumia sentensi yenye **muundo** ufuatao:

| *Kusaidia* | *kuelimisha* | *hadhira* | **ni mojawapo kati ya dhima za ushairi wa Kiswahili** |
|---|---|---|---|
| ................ | ............. | ................ | ni mojawapo kati ya dhima za ushairi wa Kiswahili |
| ................ | ............. | ................ | ni mojawapo kati ya dhima za ushairi wa Kiswahili |

**Kazi ya 19:**

Shirikiana na mwenzako msome beti hizi mbili zilizotungwa na Benjamin Nashon Magawi na **kuwaelezea** wengine yale ambayo mmeyasoma na **msamiati** uliotumiwa.

Farakano za hewani, zenye kuzusha mikasa,
Wema ukiwa moyoni, kweli hutazitomasa,
Utaziacha njiani, ziende zinakopasa,
Ugomvi, usengenyi, adui za mtu mwema.

Ukarimu maishani, upole, utii hasa,
Mambo haya duniani, yazishinda hata pesa,
Wema kitu cha thamani, toka jana hadi sasa,
Mtu aliye na wema, anazo busara nyingi.

**Kazi ya 20:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Mashairi yaliyokuwa yakitungwa enzi hizo hayakuwa | ........................................................................ ....... |

| | |
|---|---|
| 2. .................................................. | hugawanyika katika makundi mbalimbali |
| 3. Muundo maalumu ndio unaoletea shairi | ........................................................................ ..... |

## F. Mdahalo

**Kazi ya 21:**

Jiunge na wenzako wawili na kujadili kwa njia ya mdahalo "**athari za ushairi simulizi wa Kinyarwanda katika maendeleo ya jamii ya Wanyarwanda**".

## G. Cheka uongeze siku za kuishi

**Kazi ya 22:**

Padre mmoja alipotea mjini Kigali akamuuliza kijana mmoja, "ninaomba unifahamishe wapi ilipo posta". Kijana akamfahamisha mpaka akafika posta kisha padre akamjibu, "Asante kwa kunionyesha njia! Na wewe njoo kanisani nikuonyeshe njia ya peponi". Kijana akaguna akamjibu, "Padre hutaweza ninakwambia! Imekushinda njia ya posta sembuse ya peponi!"

**Waambie** wenzako kichekesho kingine.

## H. Kuandika

**Kazi ya 23:**

**Tunga** shairi moja lenye beti tano kuhusu "**Maendeleo**". Jaribu **kulikariri** na **kulisimulia** wenzako darasani.

**Kazi ya 24:**

Andika sentensi mbili zinazofuata **muundo** huu:

| Ushairi | huo | ni | zao | la | jamii | ya | Waswahili |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | zao | | | | |
| | | | faida | | | | |

**Kazi ya 25:**

**Andika** ubeti huu katika daftari yako. **Badilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki na kupigiwa mstari chini na kutumia mengine yenye **maana sawa**. Ni kipi **kichwa** kinachoweza kutolewa?

"Mti unaponyauka,
Nyasi nazo ***<u>hunyauka</u>***.
Nchi kavu huwa uchi,
Nyika huwa kame.
Ukame ukamatanapo,
Viumbe ***<u>humakamaka</u>***.

Hulia bila ***fanaka***,
Maskini,
Kufa ***havina budi***.

**Kazi ya 26:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** neno lililoandikwa kwa italiki (mfano mmoja ulitolewa):

| **Mashairi** | **ya** | ***simango*** | **ni** | **mojawapo kati ya vipera vya ushairi wa Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| Mashairi | ya | | ni | mojawapo kati ya vipera vya ushairi wa Kiswahili |

**Kazi ya 27:**

Baada ya kusoma ubeti huu, uandike **wazo kuu** linalotolewa na mtunzi:

“Wanawake wa Afrika,
Wakati wenu umefika,
Unganeni,
Shikaneni,
Mjitoe utumwani,
Nguvu moja!”

## SOMO LA 9: Kuainisha sentensi za kiswahili

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kuitazama picha ya hapa chini, Toeni **maoni** yenu kuhusu picha hiyo.

**Kazi ya 2:**

Katika jozi hiyo, elezeni **maana** ya jambo wanalolizungumzia.



**Kazi ya 3:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusishe** na picha hiyo.

***Salamu kwa wachungaji ng'ombe***

**1. Mashamba kuvamiwa na mifugo**

Hapo zamani paliishi Mfalme na Kabeba, Mheshimiwa Panya. Siku moja ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba. Jambo hili lilitokana na kuwa katika enzi hizo, watu walikuwa hawajaunda mikakati thabiti ya kutunza vizuri mazingira kwa kuwachungia ng'ombe zizini. Wachungaji walijitahidi kuwatafuta ng'ombe hao lakini hawakuwaona. Wapita njia waliwapa habari kwamba ng'ombe hao walikuwa wameyavamia na kuyaharibu mashamba ya Kabeba. Kufuatana na jambo hilo, Mheshimiwa Panya alikuwa amewafungia nyumbani kwake. Alikuwa na nia ya kuwauza ili kuboresha kazi zake za uzalishajimali.

**2. Hofu kwa wachungaji**

Wachungaji waliposikia habari hiyo, waliamua kwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwa Kabeba. Walipofika huko, walimsalimu wakisema, "Heri kwenu enyi mnaoishi kuliko na ng'ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini". Panya akajibu, "Naam! Ni kweli kuwa ng'ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini lakini siyo bila sababu. Ng'ombe hawa wanatoka kwa Bucyanya. Mheshimiwa huyu ni:

a. Bwana Mwenda-mbio na Mwenda-pole-na-taratibu;
b. Bwana Mkubwa wa juu mbinguni ambaye anaweza kuwakata, bila kusita, vidole vyenu vidogo ambavyo vingetawanyika ardhini;
c. Bwana ambaye angewapakulia ugali ambao kila anayekula kufumba na kufumbua ungemnenepesha".

Wachungaji waliposikia hivyo, walighairi na kukimbia bila kuangalia nyuma.

**3. MFALME akawa na woga**

Kisa hiki cha ng'ombe hakikukawia kumfikia Mfalme. Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea. Alipofika huko, alimwamkia kama kawaida, "Heri kwenu enyi mnaoishi kuliko na ng'ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini". Mheshimiwa Panya akajibu, "Ng'ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini kwa sababu maalum. Ng'ombe hawa ni mali ya Bucyanya. Huyu ni:

- Mwenda-shoti na Mwenda-pole-na-taratibu;

- Bwana Mkubwa wa huko juu ambaye anaweza kukukata kidole chako kidogo na kukiangusha chini ardhini;
- Bwana ambaye hupika ugali ambao kila aulaye, kufumba na kufumbua, humnenepesha".

Mfalme kusikia hivyo, alikimbia bila kuangalia nyuma.

**4. Ujasiri wa MBWA**

Bwana Mbwa aliposikia yaliyotokea alimwambia Mheshimiwa Mfalme, "Ewe Mfalme wetu, endapo utaniahidi kunichinjia fahali mdogo kati ya ng'ombe hao waliochukuliwa. Mimi binafsi nitafanya jitihada ya kuwarudisha ng'ombe wako". Mfalme akakubali na Bwana Mbwa akaondoka mara moja na kwenda nyumbani kwa Kabeba. Alipofika huko, alimwamkia kama walivyokuwa wamefanya wengine, "Heri kwenu mnaoishi pamoja na ng'ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini". Bwana Panya akamjibu kama alivyokuwa amewajibu wengine. Lakini, badala ya Bwana Mbwa kuogopa na kwenda zake, akafanya hatua moja mbele. Panya kuona vile, aliruka na kuingia ndani ya nyumba yake.

Mbwa alimwamkia tena, "Heri kwenu mnaoishi pamoja na ng'ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe zizini". Panya alirudilia maneno yale ya kujigamba. Mbwa aliendelea kupiga hatua mbele. Panya naye aliruka na kuingia ndani ya nyumba. Mbwa alipomwamkia mara ya tatu, kimya kilitawala. Basi ndipo Mbwa aliichukua fimbo ya wachungaji na kuwarejesha ng'ombe katika maskani ya Mfalme. Naye Mfalme alimfanyia sikukuu Mbwa wake kwa kutimiza ahadi yake. Alimchinjia ndama dume.

Kuwa na mkuki siyo kuwa na nguvu.

Huu ndio mwisho wa hadithi!

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 4:**

Soma kifungu cha habari kilichotolewa hapo juu na kuyajibu maswali yafuatayo:

1. Habari hii ni ya aina gani? Eleza kinagaubaga.
2. Je, ni lipi jambo lililosababisha mawasiliano kati ya MFALME na MBWA wake?
3. Mheshimiwa Panya alifanya nini ili wachungaji na MFALME wasije wakawachukua ng'ombe wake?
4. Eleza waziwazi kauli hii „Kuwa na mkuki siyo kuwa na nguvu".

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Sikiliza** kwa makini yale anayoyasoma mwanafunzi mwenzako na kuyazingatia mawazo makuu.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

Soma matini mara **nyingine** ili kuifahamu vizuri.

**Kazi ya 7:**

**Husisha** picha hii na ujumbe uliotolewa katika kifungu cha habari chetu:






**Kazi ya 8:**

Soma sentensi zifuatazo na kuzikamilisha kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

1. Mfalme aliamua ..................................... kwa Mheshimiwa PANYA ili aulize yaliyotokea.
2. Heri kwenu mnaoishi pamoja na ng'ombe wanaojichunga na kujirudisha wenyewe .............
3. Wachungaji waliposikia hivyo, .......................... na kukimbia bila kuangalia nyuma
4. Ni kweli kuwa ng'ombe hawa wanajichunga na kujirudisha wenyewe zizini lakini ...............

**Kazi ya 9:**

Soma jedwali lifuatalo na **kulijaza** kwa kutaja jina moja la mfalme aliyetawala nchi husika:

| **Nchi aliyoitawala** | **Jina la mfalme unalolijua** |
|---|---|
| Rwanda | |
| Swazi | |

## D. Msamiati

**Kazi ya 10:**

Shirikiana na mwenzako na kutafuta katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu **maana** ya maneno yafuatayo yanayopatikana katika matini:

Zizi
Kwenda shoti
Fahali

**Kazi ya 11:**

Katika jozi hiyo, **mtunge sentensi** kwa kutumia maneno ya hapo juu ambayo mmejua maana yake.

**Kazi ya 12:**

Tunga sentensi zinazohusu **"kutunza na kulinda mazingira"** kwa kutumia maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari hicho:

1. Kuvamia...................................................
2. Kuharibu……………………………………
3. Taratibu……………………………………

**Kazi ya 13:**

Shirikiana na mwenzako na kuzikamilisha ipasavyo sentensi zifuatazo kwa kutumia **maneno ya kifungu cha habari**:

1. Mtu mwenye.............................hawezi kumwua nyoka.
2. Nchini Rwanda, ng'ombe huchungiwa.....................ili kutimiza ombi la serikali.
3. Nilipopata................ya faranga elfu hamsini, ndipo niliamua kumwajiri meneja wa kampuni.

**Kazi ya 14:**

"Bwana Mkubwa wa huko juu ambaye anaweza kukukata **kidole chako kidogo** na kukiangusha chini ardhini". Yataje **majina** ya vidole vitano vya mkono.

**Kazi ya 15:**

**Jaza** jedwali hili ipaswavyo kutokana na **maagizo** yaliyotolewa:

| Neno | Neno lenye maana sawa na lile | Kinyume cha neno lile |
|---|---|---|
| 1. Mbio<br>2. Kunenepa | | |

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 16:**

Waambie wenzako **yaliyomo** katika matini ile ambayo umeisoma.

**Kazi ya 17:**

Kwa njia ya mazungumzo, **ambatanisha** tungo za kikundi cha A na zile za kikundi cha B ili kupata sentensi **sahihi**:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Mimi binafsi nitafanya jitihada ya | akafanya hatua moja mbele |
| 2. Lakini, badala ya Bwana MBWA kuogopa na kwenda zake, | kuwarejesha ng'ombe katika maskani ya Mfalme |
| 3. Kufuatana na jambo hilo, Mheshimiwa Panya alikuwa | kuwarudisha ng'ombe wako |
| 4. Basi ndipo MBWA aliichukua fimbo ya wachungaji na | amewafungia nyumbani kwake |

**Kazi ya 18:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Mfalme kusikia hivyo | ................................................................... |
| 2. ............................................. | waliamua kwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwake |
| 3. MBWA alipomwamkia mara ya tatu, | ..................................................................... |

## F. Sarufi na matumizi ya lugha

**Kazi ya 19**:

Hii ni mifano ya sentensi tofauti zilizotumiwa katika kifungu cha habari chetu. Soma sentensi hizo **kwa makini** ukizingatia aina zake.

- Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba.
- Ng'ombe hawa ni mali ya Bucyana.
- Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea.

Linganisha mifano hiyo ya kwanza na sentensi hizi zifuatazo:

- Mimi ninaona ua.
- Kalisa amekanyaga mtoto.
- Mtoto anakuja hapa.

**Kazi ya 20**:

Sentensi mbili (Mimi ninaona ua / Kalisa amekanyaga mtoto) zinaweza kuwa na **maana mbili**. Eleza vizuri

**Kazi ya 21**:

Shirikiana na mwenzako na kutafuta kwenye intaneti au katika vitabu **aina za sentensi** za Kiswahili. Msisahau **kuwasomea** wenzenu matokeo ya kazi yenu.

**Kazi ya 22**:

Shirikiana na mwenzako na kuandika **herufi** zinazotumiwa katika **kufupisha aina za sentensi**. Msisahau **kuwasomea** wenzenu matokeo ya kazi yenu

**Kazi ya 23**:

"**Sentensi nyoofu**" na "**sentensi tata**" ni nini? Eleza na kutoa mifano.

**Kazi ya 24**:

Shirikiana na mwenzako na **kuainisha** sentensi zifuatazo kwa kutumia **vifupisho** vinavyotakiwa:

1. Ng'ombe wa Mfalme waliyavamia mashamba ya Kabeba.
2. Kalisa amekanyaga mtoto.
3. Panya aliruka na kuingia ndani ya nyumba yake.
4. Mfalme aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya ili aulize yaliyotokea.
5. Tulikuwepo alipoingia hospitalini.

**Kazi ya 25**:

Katika jozi hiyo na kwa kutumia **vifupisho** vinavyotakiwa, tajeni **aina za maneno** yanayoziunda sentensi zifuatazo:

1. Dada amemeza vidonge vingi sana.
2. Mwalimu anafundisha Kiswahili na wanafunzi wanaandika maelezo yake.

**Kazi ya 26**:

Katika jozi hiyo, **kamilisheni** sentensi hizi kwa **istilahi** inayotakiwa:

1. Sentensi isiyojitosheleza kimaana na kutegemea sentensi nyingine ili kuleta taarifa kamili huitwa sentensi..........................
2. Sentensi ambayo inajengwa na kitenzi kimoja na kujitosheleza kimaana huitwa sentensi...............................................
3. Sentensi ambazo huwa na virejeshi vyenye dhana za masharti ambayo yamejikita katika mofimu za -nge, -ngeli- na -ngali- huitwa sentensi.......................................

**Kazi ya 27:**

**Linganisha** majibu ambayo umetoa na maelezo ya hapa chini.

"**Sentensi**" au "**tungo**" ni kundi la maneno au neno lenye kuleta maana. Neno hujengwa na "**mofimu**" moja au zaidi.

Maneno yanaweza kuwa ya aina zifuatazo:

a. Nomino (N);
b. Kitenzi (T) kinachoweza kuwa "kitenzi kikuu" (T) au "kitenzi kisaidizi" (TS) au "kitenzi kishirikishi" (t)
c. Kivumishi (V);

d. Kiwakilishi (W);
e. Kielezi (E);
f. Kiunganishi (U);
g. Kihisishi (H)

**Kuna:**

- Sentensi zinazoundwa na neno moja: (Mfano: Kimbia!);
- Sentensi zinazoundwa na maneno zaidi ya neno moja: (Mfano: Mtoto wangu analia).

**Kishazi**: ni kifungu chochote cha maneno kuanzia neno moja na kuendelea ambacho hutoa ujumbe kamili. Aghalabu vishazi kadhaa hubebwa na kipashio kingine kikubwa ambacho ni sentensi.

**Mfano:** Mariya amemtoroka mume wake ***kwa sababu hana nyonda naye***

**Sehemu ya 1** **Sehemu ya 2**

Kwa kawaida, sentensi huwa na maana moja tu na wazi. Sentensi hiyo huitwa "**sentensi / tungo nyoofu**".

**Mfano:** Mama analima shamba

Lakini, sentensi inaweza kuwa na maana zaidi ya moja (maana zisizo wazi kabisa). Sentensi hii inaweza kueleweka hivi na vile na kila maana ikawa sahihi katika mazingira yake. Kutokana na utata huo, inaitwa "**sentensi / tungo tata**".

**Mifano:**

- [Hakuna maua!] Mfano huu unaweza kuwa na maana ya "maua" kama "sehemu ya mmea inayochanua" au "hakuna faida". Huo ndio utata unaojitokeza.
- [Ona paa!] Mfano huu unaweza kuwa na maana ya "paa" kama "sehemu ya juu inayofunika nyumba" au "mnyama wa porini anayefanana na mbuzi mdogo". Huo ndio utata unaojitokeza.

Sentensi huundwa na "**kiima**" na "**kiarifu**". "Kiima" ni kikundi cha nomino kinachofanya tendo linalopatikana katika kitenzi. "Kiarifu" ni sehemu ya sentensi inayotawaliwa na kitenzi kinachoambatana na shamirisho au chagizo na ambayo inatoa taarifa kamili.

Mfano: Ng'ombe wa Mfalme [*waliyavamia mashamba ya KABEBA*]

**KIIMA** **KIARIFU**

**Aina za sentensi**

Kuna:

1. **Sentensi / tungo sahili au huru (S)**: Ni ile ambayo inaundwa na kishazi huru kimoja tu kinachojitosheleza kwa maana. Sentensi hiyo inaweza kuwa na:

a. Kitenzi kikuu (T):

Mfano: Ruganzu na mkewe **wameboresha** uzazi (Wameboresha: T)

b. Kitenzi kikuu (T) na kitenzi kisaidizi (TS)

Mfano: Ruganzu na mkwe **walikuwa *wamekwenda*** Rubavu.
(Walikuwa: TS / Wamekwenda: T)

c. Kitenzi kishirikishi (t)

Mfano: Ruganzu na mkewe **ni** wapole.
Nyama ya ulimi **haina** mfupa.
Chakula **ki** tayari.
Wanafunzi **wamo** darasani.
(ni; haina; ki; wamo: t)

2. **Sentensi / tungo tegemezi (ST)**: ni ile ambayo inaundwa na kishazi ambacho hakijitoshelezi kwa maana. Kwa hiyo, ni lazima kishazi hicho kitegemee kishazi kingine (ambacho ni tungo sahili) ili sentensi iwe na maana kamili.

Mifano:

**MFALME aliamua kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Panya** *ili aulize yaliyotokea*
**S** (Sentensi sahili) **ST** (Sentensi tegemezi)

**Tulikuwepo** *alipomfukuza*
**S** **ST**

**Mtoto amepona** *kwa sababu alifuata maagizo ya daktari kuhusu matumizi ya dawa*
**S** **ST**

*Anayelia* **si mtoto wangu**
**ST** **S**

**TANBIHI:**

- Sentensi sahili nyingi zinapoambatana peke yake au zinapochanganywa na sentensi tegemezi, tunaweza kuwa na aina nyingine za sentensi ambazo ni:

3. **Sentensi ambatano**: Ni ile inayoundwa na sentensi sahili zaidi ya moja zinazotumiwa pamoja bila sentensi tegemezi. Sentensi sahili hizi huambatanishwa na kiunganishi (U) chenye dhana ya "**na**".

Mifano:

- **Baba analima shamba** *na* **mama anapanda mahindi**.
**S** **U** **S**

- **Wanafunzi wanaimba** *na* **kucheza**.
  **S** **U** **S**

**4. Sentensi changamano**: Ni ile inayoundwa na sentensi sahili moja au zaidi na sentensi tegemezi moja au zaidi. Sentensi sahili na sentensi tegemezi hutumiwa pamoja.

Mifano:

- **Hakushtuka** *aliposikia* **mtoto wake amekufa**.
  **S** **ST** **S**
- **Tulikuwepo** *alipomfukuza*
  **S** **ST**
- **Mtoto amepona** *kwa sababu alifuata maagizo ya daktari kuhusu matumizi ya dawa*
  **S** **ST**

- Kuna sentensi nyingine zinazoundwa na vishazi tegemezi (au tungo tegemezi) viwili ambamo virejeshi vyenye dhana za masharti [**–nge-**, **-ngeli-** na **-ngali-**] vinatumiwa ili ziweze kutoa taarifa kamili.

**5.** Huitwa **"Sentensi shurutia"**.

Mifano:

- Ni**nge**kuwa na pesa, ni**nge**nunua mbolea ili kurutubisha shamba langu na kupata mavuno mengi.
- Ni**singe**kuwa na pesa, ni**singe**nunua mbolea ili kurutubisha shamba langu na kupata mavuno mengi.
- Ni**ngali**jua, ni**ngali**chanjwa ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.
- Ni**singali**jua, ni**singali**chanjwa ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.
- Ni**ngeli**jua, ni**ngeli**chanjwa ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.
- Ni**singeli**jua, ni**singeli**chanjwa ili kujikinga na ugonjwa wa kifua kikuu.

## G. Kuandika

**Kazi ya 28:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| Hakushtuka | aliposikia | mtoto | wake | amekufa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | | | | |

**Kazi ya 29:**

"Alikuwa na nia ya kuwauza ili kuboresha kazi zake za uzalishajimali". **Husisha** kauli hiyo na ile inayosomeka kwenye picha ifuatayo:




**Kazi ya 30:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B na kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Wachungaji walijitahidi kuwatafuta ng'ombe hao | kama walivyokuwa wamefanya wengine |
| 2. Alipofika huko, alimwamkia | moja kwa moja hadi nyumbani kwa KABEBA |
| 3. Naye MFALME alimfanyia sikukuu MBWA wake | lakini hawakuwaona |
| 4. Wachungaji waliposikia habari hiyo, waliamua kwenda | kwa kutimiza ahadi yake |

**TATHMINI KUHUSU SURA YA KWANZA**

►Soma maswali yafuatayo na kutoa majibu:

1. Fasihi simulizi ni nini?
2. Eleza kidogo "nadharia ya msambao" katika fasihi.
3. Eleza athari ya mdhamini katika matokeo ya utafiti.
4. Tunga shairi la simango linaloundwa na beti tano. Kila ubeti uwe na mishororo mitano.

5. Toa maana ya semi fupi hizi:

- Kuponda raha;
- Kuona cha mtemakuni;
- Jogoo la shamba haliwiki mjini;
- Uchungu wa mwana aujuaye mzazi.

6. Tegua vitendawili hivi:

- Hazikauki umande;
- Mtoto ana ndevu mzazi hana.

►Ainisha sentensi zifuatazo:


1. Tungepata bomba za kutosha, tungekunywa maji safi.
2. Wanyarwanda walifurahi waliposikia serikali yao imeunda mikakati thabiti ya kutunza mazingira.
3. Viongozi wote ulimwenguni ni watumwa wa raia.
4. Wanafunzi hawa wakisoma kwa bidii watafaulu mtihani wa taifa.
5. Walioshindwa si wanafunzi wa shule yetu.
6. Walimu wetu wasingalikuwa na muda wa kutosha wasingaliweza kutusaidia katika kazi zetu.

# SURA YA 2: FANI NA MAUDHUI KATIKA FASIHI SIMULIZI

## SOMO LA 10: UHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI NA VIPENGELE VYAKE

**Kazi ya 1:**

**Shirikiana** na mwanafunzi mmoja na **kueleza kichwa** cha kitabu kinachoonekana kwenye picha ifuatayo:




**Kazi ya 2:**

Soma habari ifuatayo kisha **uihusishe** na picha hiyo.

***Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi***

Kuhakiki au kuchambua kazi ya fasihi ni jambo ambalo hutiliwa maanani na watu mbalimbali. Hao ni kama vile wanafunzi na walimu wao shuleni, vyuoni na katika taasisi ambapo somo la fasihi hushughulikiwa.

**1. Uhakiki ni nini?**

Uhakiki au uchambuzi ni dhana ambayo ilielezwa kwa njia tofauti na wataalamu mbalimbali Lengo la somo hili ni kueleza na kuchunguza kwa makini kazi ya fasihi. Tunapochunguza maelezo ya wataalamu hao kuhusu suala la uhakiki, tunaona kwamba kauli kuu zilizotolewa ni:

a. Kutathmini na kueleza;
b. Kuainisha;
c. Kutoa maoni.

Kwa kuzingatia maoni hayo, uhakiki unaweza kuchukuliwa kama kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na fikra za mchambuzi.

**2. Ukongwe wa uhakiki wa kazi za fasihi**

Kitendo cha kuhakiki kazi za fasihi si kipya ulimwenguni. kuwepo kwa uhakiki kulianza wakati binadamu alipokuwa na uwezo wa kuzungumza na kuadhiri maoni na maisha ya wengine. Yeyote yule anayelinganisha kazi za fasihi na tajiriba yake maishani au na kazi nyingine huwa ameanza kufanya uhakiki. Uhakiki huanza katika kitendo cha kujaribu kuielewa kazi ya fasihi na kujibu maswali kama vile kwa nini, nani na vipi.

Hivyo basi, uhakiki ulikuwepo hata wakati ambapo fasihi simulizi ilikuwa fasihi ya kipekee katika jamii ya wanadamu.

**3. Vigezo vinavyozingatiwa katika uhakiki**

Nadharia za uhakiki ni nyingi lakini hugawika katika makundi makuu matatu yafuatayo:

- Kundi linalosisitizia kinachosemwa yaani maudhui tu;
- Kundi linalosisitizia kinavyosemwa yaani fani tu;
- Kundi linalosisitizia nani anayesema, anasema nini, anamwambia nani na anatumia lugha gani. Ni kusema kuwa kundi hili la tatu linasisitizia mtunzi na hadhira yake. Misingi inayozingatiwa na nadharia hii ni kama vile:

- Nafsi ya mtunzi na msikilizaji au msomaji (hadhira) wake yaani dhamira ya mtunzi, itikadi yake, uteuzi wa maneno au lugha anayoitumia, jumuia au tabaka linalotungiwa fasihi au jamii inayolengwa na kazi ya mtunzi;
- Historia ya maisha ya mtunzi katika jamii, mazingira alimotungia na wakati;
- Nafasi ya mtunzi katika jamii;
- Wahusika wake;
- Historia ya jamii ya mtunzi;
- Ujumbe wake;
- Jinsi hadhira ilivyoupokea ujumbe huo.

Kwa ufupi, tunaweza kusema kuwa kundi hili la tatu linajishughulisha na vipengele muhimu viwili vya uhakiki wa kazi za fasihi ambavyo ni maudhui na fani. Maudhui hujumuisha vigezo kama vile kichwa cha habari, dhamira (kuu na ndogondogo), ujumbe, falsafa ya mtunzi, migogoro na muhtasari wa habari. Fani huundwa na wahusika, muundo, mtindo au matumizi ya lugha na mandhari. Kundi hili ndilo tutakalofuata katika uhakiki wetu.

Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na wajibu unaohitajika kutekelezwa na kazi fulani na utanzu unaohusika. Hata hivyo, vigezo hivyo vinategemea

nguzo mbili yaani maudhui na fani. Wakati uliopo ndio unaopendekezwa katika uhakiki.

**4. Umuhimu wa uhakiki wa kazi za fasihi**

Kuhakiki kazi za fasihi ni muhimu sana kwani:

a. **Hutuwezesha kuthibitisha iwapo kazi hiyo inatimiza kaida ipaswavyo na kumshauri mtunzi ili kutunga kazi bora zaidi:** Utunzi wa kazi ya fasihi si jambo la kubahatisha bali huongozwa na kaida maalum. Kaida hizo ndizo zinazomwongoza mhakiki.

b. **Hutuwezesha kuielewa, kuieleza na kuifaidi kazi ipaswavyo:** Mtu hawezi kuhakiki kazi ambayo yeye haifahamu au hana habari kuihusu. Ni lazima mhakiki aifahamu vizuri, ajue linalozungumziwa kama ni mafunzo kuhusu mwenendo na tabia njema, uzalishajimali, mazingira na maendeleo ya kudumu, mpango wa kuboresha uzazi na kadhalika. Jambo hili hutokana na kuwa mhakiki anapaswa:

- Kudondoa mambo muhimu kuhusu kazi hiyo ya fasihi;
- Kubainisha nadharia mbalimbali za fasihi;
- Kuzingatia maendeleo ya mada husika na mada nyingine mbalimbali za fasihi.

c. **Hutuwezesha kulinganisha kazi tofauti za fasihi:** Kulinganisha kazi za fasihi ndiko kunakotuwezesha kumtambua mtunzi bingwa au yule ambaye kazi yake ni legevu.

d. Hutuwezesha kuchambua na kufafanua mifumo na picha za kisanaa zinazotumika katika kazi za fasihi: Sisi tunaweza kuiga mifumo na picha hizo na kupevuka katika lugha.

e. Hutuwezesha kuchambua na kuweka hadharani maonyo yanayopatikana katika kazi za fasihi: Maonyo hayo tunaweza kuyatumia kwa kuwakosoa wanajamii wengine.

**5. Ubora wa uhakiki wa kazi ya fasihi**

Kama tathmini halisi kuhusu mbinu za kilugha zilizotumiwa katika kazi ya fasihi pamoja na maudhui yake, uhakiki unapaswa kuwa bora. Uhakiki hupangwa vizuri ili kuwa wa kimvuto na kimguso. Ubora huo hutegemea:

- **Ukomavu wa mhakiki:** Umri na elimu ni baadhi ya mambo ambayo huchangia sana katika kuboresha uhakiki wa kazi ya fasihi. Uhakiki unaofanywa na kijana wa kidato cha pili, shule za sekondari, ni tofauti kabisa na ule wa mwenzake wa kidato cha tano. Jambo hili linatokana na kiwango chao kuhusu umri na maarifa waliyonayo kuhusu elimu.
- **Uwezo wa mhakiki:** Uhakiki wa kazi ya fasihi hudai utafiti wa kutosha katika vitabu mbalimbali, kwenye mtandao wa intaneti na mahali pengi. Ukosefu wa uwezo hasa wa kifedha kwa mhakiki huwa kizuizi kikubwa kwa utekelezaji mzuri wa kazi hiyo.

- **Mwenendo wa jamii inayoshughulikiwa:** Ni lazima kuijua vizuri jamii ya mtunzi wa kazi ya fasihi kama ni jamii iliyotawaliwa na ubaguzi wa rangi au iliyokumbwa na janga la UKIMWI na kadhalika. Jambo hili litamwezesha mhakiki kujua kwa nini mtunzi alichagua kichwa fulani. Kama ni vigumu kujua historia na utamaduni wake, kazi ya mhakiki haitafaulu.

Kama suluhishi, tunaweza kusema kuwa uhakiki ni somo muhimu katika maisha ya mwanafunzi. Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha tano, fanya mazoezi mengi ili kupevuka katika kazi hiyo.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari kisha ujibu maswali yafuatayo:

1. Uhakiki ni nini?
2. Eleza kidogo ukongwe wa uhakiki wa kazi za fasihi.
3. Je, ni vipengele vipi vya uhakiki wa kazi za fasihi vinavyoshughulikiwa?
4. Taja vigezo vinavyozingatiwa katika kuhakiki kazi za fasihi.
5. Je, ni ipi dhima ya uhakiki wa kazi za fasihi katika maisha ya mwanafunzi? Eleza kinagaubaga.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Anapoisoma habari hii mwenzako, **tega sikio** na kuandika kwenye karatasi mawazo makuu ambayo umeyazingatia kutoka matini.


## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma kifungu cha habari hiki **mara** nyingine ukifuata alama za vituo zilizotumiwa.

**Kazi ya 6:**

"Uhakiki wa kazi za fasihi hutuwezesha kuchambua na kuweka hadharani maonyo yanayopatikana katika kazi za fasihi". Fuata kauli hii na **kuweka hadharani onyo** linalopatikana katika kauli iliyoandikwa kwenye picha ifuatayo:



**Kazi ya 7:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. Ni kusema kuwa uhakiki ni uchambuzi wa ndani kabisa wa jambo lililozingatiwa na ........... za mchambuzi.
2. Utunzi wa kazi ya fasihi si jambo la ................ bali huongozwa na kaida maalum.
3. Uhakiki wa kazi ya fasihi huhitaji utafiti wa kutosha katika vitabu mbalimbali, kwenye ....................... na mahali pengi.

**Kazi ya 8:**

Soma **kwa sauti na ufasaha** sentensi zifuatazo

1. Kwa kuzingatia maoni hayo, uhakiki unaweza kuchukuliwa kama kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalumu.

2. Kuwepo kwa uhakiki kulianza wakati binadamu alipokuwa na uwezo wa kuzungumza na kuadhiri maoni na maisha ya wengine.

## D. Msamiati

**Kazi ya 9:**

Katika pea, tumieni Kamusi ya Kiswahili Sanifu na **kuchunguza maana** ya maneno yafuatayo:

Ukongwe
Kutathmini
Tajiriba
Kuadhiri
Janga

**Kazi ya 10:**

Katika pea hiyo, tungeni sentensi kwa **kila neno** kati ya hayo ya hapo juu.

**Kazi ya 11:**

Kwa kutumia maneno yafuatayo, tunga sentensi kamili zenye maana zinazohusu **amani na maendeleo**:

Historia.........................
Kaida.............................
Hadhira.........................

. **Kazi ya 12:**

Maneno yafuatayo yameandikwa vibaya kwa kuchanganya silabi. **Yaendeleze vizuri** ili yawe sahihi.

1. Jibarita
2. Itakiayonalama
3. Gevizo

**Kazi ya 13:**

Katika jozi, **changanueni** maneno haya kufuatana na **maana yake** na kuyaandika katika vikundi vyake halisi:

Dhamira
Mshairi
Udongo
Mandhari
Wahusika
Chandarua
Mtindo
Migogoro

| 1 | 2 | 2 |
|---|---|---|
| **Fani** | **Maudhui** | **Mengine** |

**Kazi ya 14:**

Jiunge na wenzako wawili na **kueleza vizuri** kauli ifuatayo:
"Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na wajibu unaohitajika kutekelezwa na kazi fulani na utanzu unaohusika".

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 15:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako yale ambayo **umeyasoma** katika kifungu chetu cha habari.

**Kazi ya 16:**

Kwa njia ya mazungumzo, zitaje **nguzo za ubora wa uhakiki** kwa kutumia sentensi yenye **muundo** ufuatao:

| | |
|---|---|
| **Ubora wa uhakiki hutegemea** | ***mwenendo wa jamii husika*** |
| | |
| | |

**Kazi ya 17:**

Kwa njia ya mazungumzo, shirikiana na mwenzako na **kueleza** kauli hii:
"Maswali yanayojibiwa katika uhakiki ni nini, nani na vipi".

**Kazi ya 18:**

Kwa njia ya mazungumzo, kamilisha sentensi kwa jibu sahihi. Tumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari.

| | |
|---|---|
| 1. Ukosefu wa uwezo hasa wa kifedha kwa mhakiki huwa | ............................................... |
| 2. .................................................... | kazi ya mhakiki haitafaulu |
| 3. Uhakiki hupangwa vizuri ili kuwa | ................................................ |

## F. Mchezo

**Kazi ya 19:**

Katika jozi, tafuteni kwenye jedwali hili maneno matano ya Kiswahili mnayoyajua **yaliyotumiwa** katika kifungu cha habari chetu:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | K | O | M | A | V | U | P |
| H | S | Y | T | U | O | K | L |
| A | D | F | K | E | Y | I | M |
| K | F | D | U | J | T | M | M |
| I | G | G | P | T | M | W | K |
| K | U | B | Y | P | K | I | A |
| I | I | E | T | S | R | H | I |
| S | K | L | J | F | A | M | D |
| T | A | J | I | R | I | B | A |
| A | W | R | T | Y | I | P | O |

## G. Kuandika

**Kazi ya 20:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| **Uhakiki** | **unapaswa** | **kuwa** | **bora** |
|---|---|---|---|
| | | | |

**Kazi ya 21:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja umetolewa):

| | |
|---|---|
| **Kazi za fasihi simulizi zinazoweza kufanyiwa uhakiki ni kama** | ***hadithi*** |
| | |
| | |

**Kazi ya 22:**

**Andika** jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. | ............ ni baadhi ya mambo ambayo huchangia sana katika kuboresha uhakiki wa kazi ya fasihi. |
| 2. | .......................ndiko kunakotuwezesha kumtambua mtunzi bingwa au yule ambaye kazi yake ni legevu. |
| 3. | Vigezo vya uhakiki huainishwa kulingana na ..................na kazi fulani na utanzu unaohusika. |

**Kazi ya 23:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Lengo la somo hili ni kueleza na kuchunguza | kujibu maswali kama vile kwa nini, nani na vipi |
| 2. Uhakiki huanza katika kitendo cha kujaribu kuielewa kazi ya fasihi na | kwa makini kazi ya fasihi |
| 3. Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha tano, fanya mazoezi mengi | ili kupevuka katika kazi hiyo |

## SOMO LA 11: KUHAKIKI HADITHI ZA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Jiunge na mwenzako na kutazama picha ya hapa chini, kisha toeni **maoni** yenu kuhusu picha hiyo.



**Kazi ya 2:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusishe** na picha hiyo.

***NYAMBERE***

Hapo zamani za kale palikuwa mwanamke mmoja ambaye alizaa watoto wa kike wawili. Mtoto mmoja alikuwa mrembo sana wa sura lakini mwingine alikuwa mbaya sana na mwenye jicho moja bovu. Mshichana huyo mrembo alikuwa mnene na aliitwa Mariya. Yule mbaya wa sura alikuwa mwembamba na aliitwa Nyambere.

**1. Tabia hutofautiana**

Nyambere alikuwa na tabia nzuri sana ingawa alikuwa na sura mbaya. Alikuwa anampenda dada yake Mariya lakini Mariya, msichana mwenye kiburi na maringo sana na sura nzuri ya kupendeza, hakumpenda mdogo wake Nyambere. Kila mahali alipotaka kwenda alikuwa hataki kuandamana na ndugu yake Nyambere. Peke yake, alikwenda kwa:

a. Majirani;
b. Shangazi na wajomba zake;
c. Marafiki zake na kwengineko.

Hakuandamana na nduguye maana alifikiri angemtia aibu kwa ajili ya sura yake mbaya. Licha ya kiburi na majivuno, dondoo haikukosekana kwake. Angeishi enzi hizi, angeambukizwa magonjwa mengi ya zinaa kama vile Ukimwi.

**2. Msichana bila makini**

Siku moja, mwanamume mmoja mtanashati kutoka nchi ya mbali alikuja kumtaka uchumba Mariya maana alikuwa amesikia sifa za uzuri wake. Mwanamume huyu alikuwa si mwanamume hasa, bali zimwi lililokuwa limejigeuza na kuwa binadamu. Basi mwanamume huyu alipomwuliza Mariya kama angeweza kuolewa naye, alikubali bila kusita. Harusi kubwa ilifanyiwa nyumbani kwa wazazi wa Mariya.

Siku ya Mariya kuchukuliwa na mumewe ilipofika, Nyambere alimwambia mama yake, “Mama! Na mimi nitakwenda na dada yangu Mariya”. Dada yake aliposikia hivyo alikasirika sana akasema, “Sitaki kwenda na Nyambere. Yeye ni mbaya sana na atanitia aibu kwa wakwe zangu”. Mama yao alimbembeleza sana Mariya akasema, “Mariya! Usimchukie ndugu yako. Kumbuka kuwa mlizaliwa na mama na baba mmoja”. Kusikia hivyo, Mariya alikubali kwenda naye lakini shingo upande.

**3. Maria kuchukuliwa na mumewe**

Mariya na mume wake pamoja na Nyambere walianza safari yao kuelekea nchi ya mume wa Mariya. Mume wake alikuwa ameandamana na watu wengi sana kutoka nchi yake. Watu hao hawakuwa binadamu bali vichaka ambavyo

vilikuwa vimegeuzwa na zimwi hilo kuwa watu.
Walipokuwa njiani, watu hawa walianza kutoweka mmoja mmoja na kugeuka tena kuwa vichaka. Mariya alimwuliza mume wake, “Watu wako wameenda wapi?” Mume akajibu, “Wamerudi kwao msituni maana wanaishi msituni”. Basi waliendelea na safari yao mpaka wakafika nyumbani kwa zimwi yaani mumewe Mariya. Nyumba ya zimwi ilikuwa kubwa sana.

### 4. Mume mwenye maajabu

Ilipofika usiku, mume huyo alingojea mkewe alale fofofo ili kujigeuza kuwa zimwi. Alimchukua Mariya, akamkatakata vipande vipande na, ilipofika asubuhi, aliviunga vipande hivyo tena na kumtengeneza Mariya. Na yeye mwenyewe alijigeuza kuwa binadamu tena. Alimpatia Mariya chakula kitamu sana maana alikuwa anataka anenepe ili aweze kumla siku moja. Ilikuwa kama kuwekeza mali yako ili uweze kupata faida katika siku zijazo.

Mumewe alizidi kufanya maajabu yake wakati wa usiku. Kumbe Nyambere, msichana mwangalifu kuzidi kifani, alikuwa akiyaona yote siku zote. Siku moja, Nyambere alimwambia dadake, “Dada yangu mpendwa, umeolewa na zimwi”. MARIYA alikasirika sana akasema, “Acha ujinga wako! Mimi nitakufukuza nyumbani kwangu”.

Katika nchi ya mumewe kulikuwako na wanawake wengi ambao walikuwa wameletwa kutoka nchi za mbali na kuolewa huko. Wengi wao walikuwa wamegundua tabia na hali za wanaume wao kuwa hawakuwa watu halisi. Na walipowaona Mariya na Nyambere, waliwasikitikia sana na kuwapenda. Lakini wao hawakujua njia za kujiokoa. Sikitiko kubwa ni kuwa Mariya alipoelezewa habari hii, aliipuuza na kusema kwamba ni uvumi.

Mumewe Mariya alikuwa akienda kuwinda msituni kila siku. Msituni, baada ya kujigeuza na kuwa zimwi, alikuwa akifanya kazi ya kung’oa miti mikubwa. Siku moja Nyambere alimchukua Mariya msituni kumwonyesha maajabu ya mumewe. Mariya alipoona mumewe amegeuka kuwa zimwi, alishikwa na woga na kutetemeka ovyo. Ndipo aliyaamini maneno ya ndugu yake. Maajabu mengine aliyoyafanya ni kama:

- Kuning’inia kwenye paa;
- Kula mijusi kafiri ambayo haikupikwa;
- Kujigeuza kuwa kware na kadhalika.

Wakati huo, alishangazwa na kumwona mumewe akiing’oa miti mikubwa sana na kumwambia ndugu yake, “Nyambere, tutatoroka vipi?” Nyambere alimjibu, “Usiwe na woga nitatafuta njia ya kujiokoa”.

### 5. Kutoroka kwa Maria na nduguye

Wakati wa madhara makubwa, Mola huwanusuru wanawe. Basi Nyambere,

kwa kutumia vijiti na nguvu zake za kichawi za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo. Ndege hii iliitwa “Mangera”. “Mangera” ilipokuwa tayari wakati wa jioni, Mariya na Nyambere waliingia ndani na kupaa juu kuelekea nchi yao.

Punde si punde, mumewe Mariya alirudi nyumbani na kuita, “Mariya! Mariya eh! Fungua mlango”. Yeye hakusikia jibu lolote. Aliita mara ya pili, “Nyambere! Nyambere!” Ndipo aliosikia sauti nyororo, “Niko chumbani!” Alipoingia chumbani hakuona mtu. Kumbe ilikuwa sauti ya kasuku aliyekuwa akiyarudilia maneno ya Nyambere kabla ya kutoroka. Ndipo kasuku alimwambia, “Ni mimi kasuku!” Mumewe Mariya alijibu, “Acha we!”

Alipotoka nyumbani na kwenda nje, ndipo aliiona “Mangera” angani na kusikia Mariya na Nyambere wakiimba wimbo huu:

“Ndege yangu, kimbia, kimbia!
Nipeleke nyumbani, kimbia, kimbia!”

Mume naye alijigeuza kuwa zimwi na kuanza kupaa juu akiwafuata Mariya na nduguye. Nyambere alipoona zimwi linawakaribia, alikunya mavi halafu mlima mrefu sana karibu kugusa mbingu ulitokea. Zimwi lilipoanza kuupanda mlima, Nyambere alikojoa mkojo mkali na ikatokea bahari pana na yenye kina kirefu sana. Zimwi lilipojaribu kuogelea lilizama ndani ya bahari na kuaga dunia.
Mariya na Nyambere waliendelea na safari yao na kufika mahali walikozaliwa. Mariya alimwomba msamaha Nyambere kwa chuki aliyokuwa amemfanyia. Alimshukuru pia kwa kuweza kumwokoa katika hatari iliyokuwa imemkabili. Hapo ndipo Nyambere alifahamu methali isemayo kuwa “Damu nzito kuliko maji”.

Waliishi pamoja kwa muda mrefu, wakaolewa na bwana mmoja na kukaa kwa raha mstarehe mpaka mwisho wa maisha yao.

Huu ndio mwisho wa hadithi.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma hadithi ile kisha **uyajibu** maswali yafuatayo:

1. Je, ni aina ipi ya hadithi hii? Eleza.
2. “Mariya alikuwa msichana asiye na makini”. Eleza waziwazi.
3. Je, ni lipi lilikuwa chimbuko la watu walioambatana na mumewe Mariya katika safari yake kwenda kumchukua mchumba wake? Eleza.
4. Taja maajabu yaliyofanywa na mumewe Mariya.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako anavyoisoma habari hii na kuyazingatia mawazo makuu.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii **mara** nyingine ukifuata alama za uakifishaji zilizotumiwa.

**Kazi ya 6:**

Soma **kwa sauti na ufasaha** sentensi zifuatazo na kuzielewa vizuri:

1. Wakati wa madhara makubwa, Mola huwanusuru wanawe
2. Mtoto mmoja alikuwa mrembo sana wa sura lakini mwingine alikuwa mbaya sana na mwenye jicho moja bovu
3. Walipokuwa njiani, watu hawa walianza kutoweka mmoja mmoja na kugeuka tena kuwa vichaka

**Kazi ya 7:**

Wasomee wenzako **jambo** linalozungumziwa na kulieleza vizuri.



Fanyeni uhakiki wa hadithi .....

## D. Msamiati

**Kazi ya 8:**

Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya **maana** ya maneno yafuatayo:

Dondoo
Uchumba
Mkwe
Kichaka

**Kazi ya 9:**

Kila mmoja kati yenu **atunge** sentensi moja kwa kila neno kati ya haya manne ya hapa juu.

**Kazi ya 10:**

Kivumishi **"-embamba"** kinaweza kutumiwa mahali pengi. Eleza **maana** ya "-embamba" katika sentensi zifuatazo:

1. Fuata njia **nyembamba** ili kufika kwenye kituo cha kuboresha uzazi.
2. Mchanga **mwembamba** hutumiwa katika kujenga nyumba za kisasa.
3. Watoto wanapaswa kunywa uji **mwembamba** ili wasije wakakumbana na maumivu ya tumboni.
4. Nyakati za kisasa, watanashati wanapenda sana nguo **nyembamba**.

**Kazi ya 11:**

Kamilisha sentensi zifuatazo zilizotumiwa **katika kifungu chetu** cha habari:

1. Kumbe ilikuwa sauti ya.................aliyekuwa akiyarudilia maneno ya NYAMBERE kabla ya kutoroka.
2. Katika nchi ya mumewe kulikuwako na ............ wengi ambao walikuwa wameletwa kutoka nchi za mbali na kuolewa huko.
3. Mume naye alijigeuza kuwa zimwi na kuanza .............. akiwafuata MARIYA na nduguye.

**Kazi ya 12:**

Katika jozi, **jazeni** jedwali lifuatalo kwa kuyataja maajabu yaliyofanywa na mumewe Mariya na yale yaliyofanywa na Nyambere.

| Maajabu yaliyofanywa na mumewe MARIYA | Maajabu yaliyofanywa na NYAMBERE |
|---|---|
| | |

**Kazi ya 13:**

Simama mbele ya darasa ueleze methali hii kwa **kuihusisha** na ujumbe unaotolewa katika hadithi.
"Damu nzito kuliko maji"

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 14:**

Simama mbele ya darasa **uwaambie** wenzako yale ambayo umeyasoma katika hadithi yetu.

**Kazi ya 15:**

Kwa njia ya mazungumzo, taja **methali** moja ya Kiswahili inayotumia ndani yake neno "**zimwi**".

**Kazi ya 16:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo zinazopatikana katika habari kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. MARIYA na NYAMBERE waliendelea na safari yao | ................................................................... |
| 2. Kuning'inia kwenye paa | .................................................................. |
| 3. ........................................................... | na kufika mahali walikozaliwa |

## F. Utafiti

**Kazi ya 17:**

Katika kundi la wanafunzi watatu, tafuteni **hadithi simulizi mbili za Kinyarwanda** na **kuzitafsiri** katika Kiswahili. Mmoja kati yenu alisomee darasa matokeo ya kazi yenu.

## G. Kuandika

**Kazi ya 18:**

Jiunge na wenzako wawili na **kubuni hadithi** moja ya Kiswahili ambayo ni **ngano**. (Hadithi hizi zitabadilishanwa na makundi mengine ili kufanyiwa uhakiki katika kipengele cha "H. Uhakiki")

**Kazi ya 19:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu:

| Wakati | wa | madhara | makubwa | Mola | huwanusuru | wanawe |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |

**Kazi ya 20:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja ulitolewa):

| | |
|---|---|
| ***NYAMBERE*** | **yu miongoni mwa wahusika wakuu katika hadithi ya "Kasoroka"** |
| | |
| | |

**Kazi ya 21:**

**Andika** jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Mariya alipoona mumewe amegeuka kuwa zimwi, alishikwa na woga na ........... ovyo. |
| 2. Basi Nyambere, kwa kutumia vijiti na ..................... za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo. |
| 3. Basi mwanamume huyu alipomwuliza Mariya kama .......... naye, alikubali bila kusita. |

**Kazi ya 22:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Mariya alimwomba msamaha Nyambere | bali zimwi lililokuwa limejigeuza na kuwa binadamu |
| 2. "Mangera" ilipokuwa tayari wakati wa jioni, Mariya na Nyambere | waliingia ndani na kupaa juu kuelekea nchi yao |
| 3. Mwanamume huyu alikuwa si mwanamume hasa, | kwa chuki aliyokuwa amemfanyia |

### H. Uhakiki au uchambuzi wa hadithi ''*Nyambere*"

Katika kidato cha nne, tulijifunza jinsi uhakiki wa hadithi simulizi ya kiswahili unavyofanywa. Tuliona kuwa vipengele vinavyoshughulikiwa ni maudhui na fani. Ebu tujikumbushe na kufanyia uhakiki hadithi simulizi yetu "Nyambere".

► **Maudhui**

Vipengele vitakavyoshughulikiwa ni hivi vifuatavyo:

- **Kichwa cha hadithi:**

Kichwa cha hadithi hii ni"*Nyambere*". Mtunzi alihusisha kichwa na mhusika mmoja kati ya wahusika wakuu ambaye anaitwa Nyambere. Ni kusema kwamba Nyambere ndiye atakayetatua tatizo kubwa katika hadithi na kuwapa wasikilizaji au wasomaji funzo fulani.

- **Dhamira:**

Vipengele viwili vifuatavyo ndivyo vitakavyoshughulikiwa:

- **Dhamira kuu:** Katika hadithi hii, mawazo makuu ni haya yafuatayo:

  **«*<u>Jihadhari maishani kabla ya kupata uamuzi</u>*»**. Hadhari ni hali ya kuwa na makini au uangalifu. Mtu kutoka nchi ya mbali alipokuja kumtaka uchumba Mariya alikubaliwa moja kwa moja na Mariya. Msichana huyu hakuwa na makini na hakuwaza kuhusu matatizo ambayo angekabiliana nayo hapo mbeleni. Tatizo alilokumbana nalo lilikuwa kubwa yaani kuolewa na zimwi lililokuwa limejigeuza kuwa binadamu. Zimwi hilo lilimfanyia maajabu mengi na hata kupanga kumla.

  **«*<u>Damu nzito kuliko maji</u>*»**. Ni kusema kuwa ndugu ni ndugu hata kama wakigombana kwani mwishoni wanapatana. Hawatengani kamwe. Kumbukeni jinsi Mariya alivyokuwa akimchukia ndugu yake Nyambere na kutotaka kuandamana naye popote alipokuwa anakwenda. Walakini, Nyambere ndiye aliyemwelezea kuwa mumewe Mariya alikuwa zimwi na kumsaidia kutoroka na kurudi makwao. Mpende kila mtu hasa ndugu yako hata kama yeye hakupendi kwani siku moja ataelewa ukweli wa mapenzi yako.
- **Dhamira ndogondogo:** Mawazo madogomadogo ni kama vile:

  **. « <u>Kuwa na urembo siyo kuwa na moyo mkunjufu</u>» :** Watoto pacha, Mariya na Nyambere ni mfano mzuri kwetu. Mariya alikuwa mrembo wa sura lakini mwenye kiburi na majivuno. Nyambere alikuwa mbaya wa sura na mwenye jicho bovu lakini mwenye roho nzuri, mvumilivu na mnyenyekevu. Ni kusema kuwa unapotaka mchumba, jihadhari kwani umdhaniaye mrembo, zingatia huyo si mwenye tabia nzuri hasa.

  **. « <u>Uchawi unaweza kutumiwa na matokeo yake yakawa mazuri kama vile katika kuokoa maisha ya watu</u>» :** Maajabu ya zimwi yalikuwa mengi lakini lengo lake lilikuwa kuliwa kwa mkewe. Kumbukeni wakati lilipomkatakata vipande vipande na hatimaye kumgeuza kuwa binadamu au kule kumnenepesha ili kuwa kitoweo chake kizuri na kitamu. Mambo haya si mazuri na, kwa ujumla, matendo ya kichawi si mazuri. Walakini, Nyambere alipoona kuwa maisha ya nduguye yalikuwa hatarini, alitumia nguvu zake za kichawi na kutengeneza ndege ya maajabu ili kuweza kumtoroka zimwi. Kwa kawaida, uchawi si mzuri lakini yeye aliutumia katika mambo mazuri.

  **. « <u>Usimchukie mwenzako kwani anaweza kuwa muhimu kwako</u>» :** Mariya alimchukia sana Nyambere kiasi kwamba hakutaka kuandamana naye mahali kote alikokuwa anakwenda. Hakuijua hii dunia hadaa. Hakujua kuwa katika dunia hii, watu husaidiana. Alipochukuliwa na mumewe kwenda makwao hakutaka Nyambere aende naye kufuatana na chuki dhidi yake. Jambo la kushangaza ni kuwa yule aliyekuwa anamchukia sana ndiye aliyeyaokoa maisha yake wakati alipokuwa anakaribia kuliwa na zimwi.
  - **Ujumbe:**

Mtunzi anatuonya kuhusu jambo la kutokuwa na makini na kuwachukia wenzetu. Mariya hakuwa na uangalifu na alionyesha chuki dhidi ya ndugu

yake Nyambere lakini mwishoni Nyambere ndiye aliyenusuru maisha yake yaliyokuwa hatarini. Kuliwa na zimwi ndio uliokuwa mwisho wake. Ndiyo sababu msanii anasema kwamba « damu nzito kuliko maji ».

- **Falsafa:**

Msanii anampa msomaji au msikilizaji maadili bora kuhusu mwenendo wake maishani hasa mtu anayejisifu kuwa mrembo na mwenye tabia mbaya kama vile tabia ya kiburi, majivuno, dondoo na chuki.

- **Migogoro :**

Migogoro ni hali ya kutokubaiana kimawazo, kimatendo,…kati ya wahusika. Mgogoro unaojitokeza katika hadithi hii unahusiana na tabia ya Mariya. Msichana huyu anapinga na kuchukia sana ndugu yake Nyambere kutokana na sura yake mbaya. Mgogoro mwingine unajitokeza kati ya Nyambere na mumewe Mariya kufuatana na maajabu ya kizimwi anayoyatenda kila mara.

- **Muhtasari:**

Zamani za kale, mwanamke mmoja alizaa mapacha wa kike. Mmoja alikuwa mrembo sana lakini mwenye kiburi na majivuno na mwasherati. Jina lake lilikuwa Mariya. Ndugu yake aliyejulikana kwa jina la Nyambere, alikuwa mbaya wa sura na mwenye jicho bovu lakini mwenye tabia nzuri. Mariya hakumpenda ndugu yake kiasi kwamba hakutaka kuongozana naye mahali kokote alikokuwa anakwenda.

Siku moja, mwanamume mmoja mtanashati kutoka nchi ya mbali alikuja nyumbani kwao ili kumtaka uchumba Mariya. Msichana huyu mwenye maringo alikubali moja kwa moja bila kuwaza. Hakujua kwamba bwana huyo alikuwa zimwi lililokuwa limejigeuza kuwa binadamu. Ndoa ilifungiwa nyumbani kwa wazazi wa Mariya. Siku ya Mariya kuchukuliwa na mumewe, mama yake alimsihi aongozane na Nyambere. Mwanzoni alikataa katakata lakini, mwishoni, kufuatana na msisitizo wa mama yake alikubali. Mumewe alikuwa ameandamana na watu wengi sana.

Safari yao kuelekea nchi ya mbali ilikuwa nzuri lakini, walipokuwa njiani, watu hao walianza kutoweka mmoja mmoja. Jambo hili linatokana na kuwa walikuwa vichaka vilivyokuwa vimegeuzwa na zimwi kuwa watu. Walifika nyumbani kwa mumewe Mariya salama salimini.

Wakati wa usiku baada ya kusinzia, mumewe Mariya alijigeuza kuwa zimwi na kuanza matendo yake ya ajabu kama vile kumkatakata mkewe vipande vipande na kumgeuza kuwa binadamu na kadhalika. Lengo lake lilikuwa kumlisha vizuri mkewe ili aweze kuwa kitoweo chake baada ya kunenepa ipaswavyo. Maajabu hayo yaliendelea kufanywa kwa muda wa siku kadhaa. Nyambere alibahatika kuyaona maajabu yote. Kila wakati alipomwelezea ndugu yake maajabu hayo, Mariya alimtukana na hakukubali.

Siku moja Nyambere alimwomba ndugu yake waende msituni. Hapo ndipo walimwona mumewe Mariya akiing'oa miti mikubwa kwa mikono yake na kukubali kuwa alikuwa zimwi. Nyambere ndiye aliyetumia nguvu zake za kichawi na kutengeneza ndege ya vijiti ambayo waliitumia kwa kupaa juu na kulitoroka zimwi.

► **Fani**

Tutashughulikia vipengele vifuatavyo :

- **Wahusika:**

Hadithi yetu ni ngano. Ni kusema kwamba wahusika ni mchanganyiko wa wanyama, ndege, watu na vitu mbalimbali vinavyopewa uhai. Kuna:

**. « Wahusika wakuu» :** Hao ni:

***Mumewe Mariya*:** Ni zimwi lililojigeuza kuwa binadamu. Ni mtanashati anayetenda maajabu kutokana na nguvu zake za kizimwi. Maajabu hayo ni kama vile kumkata mkewe vipande vipande na kumgeuza kuwa mtu, kung'oa miti mikubwa sana kwa mikono yake, kuvigeuza vichaka kuwa watu na kadhalika.

***Mariya*:** Ni msichana mrembo sana mwenye kiburi na maringo. Yeye na ndugu yake Nyambere ni pacha. Msichana huyu hampendi ndugu yake Nyambere na ndiyo sababu hawezi kuongozana naye kokote anakokwenda. Hana uangalifu kwani macho yake yamefumbwa na kule kujisifu kwa urembo wake. Ukosefu wa hadhari ndio uliomfanya aolewe na zimwi lililokuwa limejigeuza kuwa binadamu kwani alikubali moja kwa moja kuolewa naye bila kuwauliza wazazi wake au watu wengine. Ulimfanya pia apuuze ukweli wa mambo aliyokuwa anaambiwa na Nyambere kuhusu maajabu ya zimwi yaani mumewe. Maajabu aliyoyatendewa na mumewe ni mengi. Baada ya kujua kuwa mumewe ni zimwi, ndipo aliungana na nduguye Nyambere.

***Nyambere*:** Ni msichana mbaya sana wa sura lakini mwenye tabia nzuri. Yeye na ndugu yake Mariya ni pacha. Msichana huyu anampenda sana ndugu yake Mariya ingawa yeye hampendi. Ndiyo sababu alikwenda kuishi naye kwa mumewe Mariya. Chuki ya nduguye dhidi yake haikumkatisha tamaa bali aliendelea kumwonyesha mapenzi na kumwonyesha ukweli wa maajabu ya mumewe.

**. « Wahusika wadogo» :** Wahusika hawa ni:
***Mama wa Nyambere na Mariya*:** Huyu ndiye mama mzazi wa Nyambere na MARIYA. Anapenda sana watoto wake. Kumsihi Mariya akubali kuongozana na nduguye Nyambere kunaonyesha kuwa nia yake ni kuwaona watoto wake wakiwa pamoja.

***Kasuku***: Ni ndege anayeweza kuiga kusema kama binadamu. Unachomwambia ndicho anachozingatia na kujaribi kuiga sauti yako. Baada ya Mariya na Nyambere kutoroka, kasuku aliyarudilia maneno ya Nyambere “Niko chumbani“.

**. « Wahusika wajenzi» :** Kuna:

***Watu waliokuwa wameambatana na mumewe Mariya***: Watu hawa si binadamu halisi bali ni vichaka vilivyokuwa vimegeuzwa na zimwi kuwa watu.

- **Muundo:**

Mpangilio wa kiufundi alioutumia msanii katika kuorodhesha matukio ni huu ufuatao:

**. Mwanzo :**

- Mariya, mrembo wa sura, na Nyambere, mbaya wa sura, kuzaliwa na mwanamke mmoja;
- Nyambere kuchukiwa na ndugu yake Mariya na Mariya kupendwa na ndugu yake Nyambere;
- Mariya kutotaka kuongozana na Nyambere kokote anakokwenda.

**. Upeo :**


- Mwanamume kutoka nchi ya mbali kuja kumtaka uchumba Mariya;
- Mariya kukubali moja kwa moja kuolewa naye bila uangalifu;
- Ndoa kufungiwa nyumbani kwa wazazi wa Mariya;
- Mariya kukubali kuongozana na Nyambere kwa shingo upande;
- Mariya kuchukuliwa na mumewe;
- Safari ya kurudi nyumbani kwa mumewe Mariya
- Kufika nyumbani kwa mume, Mariya na Nyambere;
- Mumewe Mariya kufanya maajabu;
- Mariya kupuuza ukweli wa mambo kuhusu maajabu yanayotendwa na mumewe;
- Nyambere na Mariya kwenda msituni na kupata ukweli kuhusu maajabu ya mumewe Mariya;
- Mariya na Nyambere kukubaliana kutoroka.

**. Mwisho :**

- Nyambere kutengeneza ndege kichawi kama chombo kitakachotumiwa ili kutoroka;
- Mariya na Nyambere kutoroka;
- Mumewe Mariya kurudi nyumbani na kukosa mkewe na ndugu yake;
- Kasuku kurudilia maneno ya Nyambere;

- Mumewe Mariya kwenda nje ya nyumba na kuona “Mangera“ angani yaani ndege waliyoitumia Mariya na Nyambere ili kutoroka;
- Mumewe Mariya kusikia wimbo wa Mariya na Nyambere;
- Mumewe Mariya kujigeuza zimwi na kuanza kupaa juu ili kufika kwenye ndege;
- Nyambere kunya na mlima mrefu sana karibu kugusa mbingu kutokea;
- Zimwi kuanza kupanda mlima;
- Nyambere kukojoa na bahari kutokea mara moja;
- Zimwi kujaribu kuogelea lakini likazama na kufa.

Matukio haya yote yakiandikwa kwenye mchoro huwa namna hii:




- **Mtindo:**

Mitindo aliyoitumia msanii katika kazi hii ya sanaa ni hii ifuatayo:

**. Lugha hai:**
Msanii anatumia lugha ya kila siku ambayo inaeleweka kwa kila mtu. Anawaeleza wahusika wake.

**. Majibizano:**
Majibizano yanapatikana katika aya ambamo mumewe MARIYA anamwita Nyambere na kasuku akamjibu, „Niko chumbani“. Hapa ndipo alianza kujibizana na kasuku.

**. Methali:**
Msanii alitumia pia methali (mfano: “Damu nzito kuliko maji“)

**. Nahau na misemo :** Hapa kuna mifano:
- Alikubali kwenda naye lakini shingo upande;
- Mume huyo alingojea mkewe **alale fofofo**.

. **Maneno ya msisitizo:** Hapa kuna mifano:

- Nyambere, msichana mwangalifu kuzidi kifani;
- Nyumba ya zimwi ilikuwa kubwa **sana**;

. **Tamathali za usemi:** Hizo ni kama vile:

- **Tashihisi au uhaishaji:** Hukipa uhai kitu kisicho na uhai

Ndipo kasuku alimwambia, «Ni mimi kasuku“

- **Balagha au mubalagha:** Matumizi ya lugha hutiwa chumvi ili kuongeza utamu na kuleta athari fulani.

Mlima mrefu sana **karibu kugusa mbingu**.

- **Mandhari:**

Katika hadithi hii, dhana ya mahali inajitokeza namna hii:

. **Mwanzo :**

Visa vinatokea **nyumbani kwa wazazi wa Mariya**

. **Upeo :**

Mahali ni **nyumbani kwa zimwi**.

. **Mwisho :**

Mambo yote yanatokea **nyumbani kwa zimwi**.

**Kazi ya 23:**

Jiunge na wenzako wawili na kuchagua hadithi simulizi moja ya Kiswahili. Baada ya kuisoma polepole na kuielewa, **muifanyie uhakiki** kwa kuzingatia mwongozo wa uchambuzi uliotolewa. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wanafunzi wengine.

**Kazi ya 24:**

**Someeni** wenzenu uhakiki mlioufanya ili waweze **kujibu maswali** mbalimbali kuhusu maoni yao binafsi juu ya utanzu huo.

**Kazi ya 25:**

Kundi lenu lililobuni ngano (hadithi) **libadilishane** na kundi jingine ili **kuifanyia uhakiki** na kuitolea **tathmini** darasani.

## **SOMO LA 12**: KUHAKIKI METHALI ZA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Tazama vizuri picha hii. **Nini** kilichoandikwa kwenye fulana hii?




**Kazi ya 2:**

Kwa maoni yako, ni **utanzu** gani wa sasihi simulizi ya Kiswahili?

**Kazi ya 3:**

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha **uhusishe** picha hii na yaliyomo katika habari.

***Vipengele muhimu vya uhakiki wa methali***

Methali hufanyiwa uhakiki kama tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiswahili. Uhakiki wa methali huzingatia vipengele vya maudhui na fani lakini kwa njia inayotofautiana na ile ya uhakiki wa hadithi.

**1. Uhakiki wa methali kimaudhui**

Methali, kama semi zenye busara, hutoa maadili mbalimbali katika maisha ya binadamu. Katika kueleza jambo kwa njia fulani, methali:

a. **Huwa na mazingira yake:** Kila methali huelezea uwanja fulani wa maisha ya mtu kama vile ukulima, amani na maendeleo, usawa wa jinsia, uzalishajimali, burudani, uimbaji na kadhalika. Hii ifuatayo ni mifano ya methali na mazingira yake:

| Methali | Mazingira |
|---|---|
| - Hasira za mkizi, furaha ya mvuvi | Uvuvi |
| - Uchungu wa mwana aujuaye mzazi | Familia |
| - Mchagua jembe si mkulima | Ukulima |

b. **Huwa na maana au funzo lake:** Ujumbe wa methali unapofafanuliwa kutokana na mazingira yake ndipo tunapata ufafanuzi wake na maana yenyewe ya methali. Ni kusema kuwa methali huwa na maana ya nje na maana ya ndani au maana yenyewe. Hebu tutoe mfano wa methali "Kidole kimoja hakivunji chawa". Chawa ni kidudu kinachokaa kwenye mwili wa binadamu hasa katika nywele na nguo chafu na hunyonya damu yake. Ufafanuzi wake au maana yake ya nje ni kuwa mtu hawezi kumwua chawa kwa kidole kimoja. Ni lazima ambanie katikati ya vidole viwili. Maana yake ya ndani ni kuwa "mtu mmoja hawezi kufanya kazi inayohitaji watu wengi". Umoja huu ndio unaoweza kuifikisha nchi yake kwenye maendeleo ya kudumu. Maana ya ndani ya methali ni kama funzo tunalolipata kutoka methali hiyo. Methali yetu hiyo inatufundisha kuwa "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu."

c. **Huwa na matumizi yake:** Hakuna methali isiyokuwa na matumizi yake. Kwa mfano, unapotaka kumwonya mtu ashirikiane na wengine katika kazi fulani ili jambo fulani liweze kufana na kutekelezwa, unaweza kutumia methali hii "Kidole kimoja kahivunji chawa". Matumizi yake ni kwamba watu wanapaswa kushirikiana ili kazi itekelezwe ipaswavyo.

d. **Baadhi ya methali huwa na maana sawa:** Kwa mfano, methali hii "Haraka haraka haina baraka" ina maana sawa na hii "Polepole ndio mwendo".

**2. Uhakiki wa methali kifani**

Methali hutungwa kwa umbo maalumu kutokana na ufundi wa msanii. Umbo hilo ndilo linaloifanya methali iwe na mvuto katika kuitamka. Methali hutambuliwa haraka kutokana na:

- **Muundo wake:** Kwa kawaida, methali:
  - Huwa na vipande viwili
    Mifano: "Mtaka cha uvunguni, sharti ainame"
    1 2
    "Sikio la kufa halisikii dawa"
    1 2
  - Huwa fupi au ndefu kidogo
    Mifano: "Hasira hasara" (Methali fupi)
    "Mapenzi ni kama kikohozi, hayafichiki" (Methali ndefu kidogo)

- Baadhi ya methali zinaweza kuwa na ukinzani yaani methali zinazojipinga kimaana.

Mifano: “Mavi ya kale hayanuki” ‡ “Mavi ya kale hayaachi kunuka”
“Fuata nyuki ufe mzingani” ‡ “Fuata nyuki ule asali”

- **Lugha yake:** Methali hutumia mbinu maalumu za lugha au za kishairi zinazochangia katika kukumbukika kwake. Utanzu huu:
    - Huweza kutumia tamathali za usemi:

Mifano:
“Ibilisi wa mtu ni mtu” (tamathali ya usemi iliyotumiwa ni takriri).
“Mapenzi ni kama kikohozi hayafichiki” (tashbihi ndiyo iliyotumiwa). Maana yake ni kuwa unapompenda mtu fulani wengine wataitambua hali hiyo ijapo unajaribu kufichaficha mapenzi yako.
“Sikio la kufa halisikii dawa” (Tashihisi ndiyo iliyotumiwa). Maana yake ni kuwa hakuna dawa inayoweza kutumiwa kwa kuzuia kifo. Kifo kikimwita mtu fulani, ni lazima aitikie mwito huo.

- Huwa na wakati: Kuna methali za kale zinazotumia lugha ya kale na methali za kisasa zinazotumia lugha ya kisasa.

Mifano:
“Mti mkuu ukingwa, wana wa nyuni huyumba” (lugha ya kale)
“Mti mkuu ukianguka, ndege huwa mashakani” (lugha ya kisasa)

### 3. Mifano ya uhakiki wa methali

Hii ifuatayo ni mifano ya methali ambazo tumezifanyia uhakiki:

**a. “Ibilisi wa mtu ni mtu”**

- Mazingira: Mtu au binadamu.
- Maana: Ibilisi ni shetani, kiumbe kinachodhaniwa kutendea mabaya binadamu. Methali inamaanisha kuwa si kiumbe mwingine anayeweza kukufanyia mabaya bali ni binadamu mwenzako.
- Matumizi: Methali hii inamkumbusha mtu yeyote kuwa macho au kuwa na uangalifu kuhusu binadamu mwenzake ili asije akamtendea mabaya.
- Muundo: Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Ibilisi wa mtu) na (ni mtu).
- Lugha iliyotumiwa: Ni methali inayotumia lugha ya kisasa. Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni takriri.

**b. “Fadhila za punda ni mashuzi”**

- Mazingira: Ufugaji.
- Maana: Fadhila ni wema au ukarimu. Shuzi ni upepo utokao kwenye tupu ya nyuma. Methali hii inamaanisha kuwa shukrani za mtu mjinga ni kumtukana yule aliyemtendea mema.
- Matumizi: Methali hii inatumiwa kwa kumkumbusha mtu kutoshtushwa na

maovu anayoweza kutendewa na yule aliyemfanyia hisani na kutokasirika kwani ujinga ndio chanzo cha yote.

- Muundo: Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (fadhila za punda) na (ni mashuzi).
- Lugha iliyotumiwa: Ni methali inayotumia lugha ya kisasa.

**c. "Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo"**

- Mazingira: Maradhi au ugonjwa.
- Maana: Uwele (ndwele) ni ugonjwa. Kuganga ni kufanyia mgonjwa matibabu au kutibu. Methali hii inamaanisha kuwa tusibabaike kutokana na mambo mabaya yaliyopita bali tuwaze na kujiandaa kuyakabili na kuyadhibiti yale yatakayokuja.
- Matumizi: Methali hii inatumiwa kwa kuwaonya watu wafanye kulihali ili kuboresha maisha yao ya mbeleni.
- Muundo: Methali hii ina vipande viwili ambavyo ni (Yaliyopita si ndwele) na (tugange yajayo).
- Lugha iliyotumiwa: Ni methali inayotumia lugha ya kale.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 4:**

**Soma** kifungu chote cha habari na **kujibu maswali** yafuatayo:

1. "Methali huwa na maana ya juu au nje na maana ya ndani au maana yenyewe." Eleza kinagaubaga.
2. "Methali huwa na mazingira yake". Eleza vizuri.
3. Kitu gani kinachozifanya methali zitambuliwe haraka?
4. Methali hizi huzungumzia uwanja au mazingira gani ya maisha?
    - Mpanda farasi wawili hupasuka msamba;
    - Mchovya asali hachovyi mara moja;
    - Mbuzi wa maskini hazai mapacha.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Tega sikio** wakati mwenzako anakisoma kifungu cha habari na kuelewa vizuri yanayozungumziwa.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

Soma kifungu cha habari hiki **kwa makini**.

**Kazi ya 7:**

Soma kwa **sauti na ufasaha** kauli zifuatazo na kuchagua **jibu sahihi** kutokana na picha ya hapa chini:

1. Kauli ile “Ukipata shukuru, ukikosa usikufuru” ni nahau;
2. Kauli ile “Ukipata shukuru, ukikosa usikufuru” ni methali;
3. Kauli ile “Ukipata shukuru, ukikosa usikufuru” ni hurafa;
4. Hakuna jibu sahihi.




**Kazi ya 8:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. ........................unapofafanuliwa kutokana na mazingira yake ndipo tunapata ufafanuzi wake na maana yenyewe ya methali.
2. Methali hutumia mbinu maalumu za lugha au za ........................ zinazochangia katika kukumbukika kwake.
3. Methali yetu hiyo inatufundisha kuwa “Umoja ni nguvu na ........................ ni udhaifu.”

## D. Msamiati

**Kazi ya 9:**

Shirikiana na mwenzako na kutumia kamusi ili kutafuta **maana** ya maneno yafuatayo:

**Mkizi**
**Utengano**
**Udhaifu**
**Ukinzani**
**Ndwele**
**Kuganga**

**Kazi ya 10:**

Katika pea, tumieni maneno hayo kwa **kujaza nafasi** zilizoachwa wazi katika kifungu cha habari kifuatacho:

- Dunia ni mti mkavu wenye maajabu mengi. Linaloshangaza ni kuwa watu wake wengi hawapendi kushirikiana na wenzao. Wao husahau kwamba hawana budi kuutupilia mbali.....................ili waishi katika utengemano. Hawajui kwamba hali hii ni................ kabisa! Unapowahamasisha kuhusu jambo hilo, wao hupinga na kuruka kama .............. baharini. Ni kweli kuwa ..................... huo ni kizuizi cha maendeleo yao binafsi na ya nchi zao. Kuepukana na jambo hili kunawezekana kwani dawa ya kuponya .................. huo haijakosekana. Ni lazima kila mtu arekebishe mwenendo wake na kufanya bidii ili ............... yajayo.

**Kazi ya 11:**

Katika jozi, **tajeni** methali ambamo yalitumiwa **majina** ya vitu vifuataui,,dvyo:

1.  ....................................................

2. 
Mvua inanyesha. ..................................................

3.  ....................................................



4. ......................................................

**Kazi ya 12:**

**Jaza** methali zifuatazo ili ziwe kamili:

1.Angurumapo ..............., mchezaji nani;
Usitukane ................ na uzazi ungalipo;
Mwezi na .................., giza na mwizi;
Mtaka yote kwa .............. hukosa yote.
-

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 13:**

Waelezee wanafunzi wengine yale ambayo **umeyasoma** katika kifungu cha habari cha hapo juu.

**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza** jedwali lifuatalo kwa kutumia sehemu za methali zinazotakiwa:

| **Shukrani** | **za** | **punda** | **ni** | **mashuzi** |
|---|---|---|---|---|
| Fadhila | za | punda | ni | ................ |
| Fadhila | za | ....... | ni | moto |

**Kazi ya 15:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza** sentensi zifuatazo jinsi **zilivyo** katika kifungu cha habari:

1. Methali hii inatumiwa kwa kuwaonya watu wafanye kulihali ili .... yao ya mbeleni
2. Kuna methali za kale zinazotumia .... na methali za kisasa zinazotumia lugha ya kisasa
3. Methali, kama semi zenye busara, hutoa ...... katika maisha ya binadamu

## F. Cheka uongeze siku za kuishi

**Kazi ya 16:**

Mke mmoja alimpa mme wake redio aende nayo chooni ili asiudhike kwa vile huwa anakaa muda mrefu chooni. Basi alipotoka akamuuliza, ‘’Ehe! Mume wangu ulifurahi?”
Mume akajibu, “Aa! Wajinga hawa! Wameniwekea wimbo wa taifa na nimejisaidia huku nikisimama.” Waambie wenzako kichekesho kingine **cha Kiswahili** unachokijua.

## G. Uhakiki

**Kazi ya 17:**

Fanya **uhakiki** wa methali zifuatazo:

1. Cheche huzaa moto;
2. Chururu si ndo ndo ndo;
3. Maskini na mwanawe, tajiri na mali yake;

## H. Utafiti

**Kazi ya 18:**

Jiunge na wanafunzi wawili kisha **mtafute** kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu methali mbalimbali na kuzifanyia **uhakiki**. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

**Kazi ya 19:**

Baada ya kusomewa matokeo ya kazi hiyo, wanafunzi wengine **watoe maoni yao binafsi** juu ya kazi hiyo na kujibu maswali mbalimbali.

## I. Kuandika

**Kazi ya 20:**

Andika methali mbili zinazofuata **muundo** huu yaani sentensi ambayo kiima chake ni neno linalorudiliwa:

| Chovya chovya | humaliza buyu la asali |
|---|---|
| ......................... | .................................... |
| ........................... | .................................. |

**Kazi ya 21:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja umetolewa):

| **Methali hutambuliwa haraka kutokana na** | ***muundo wake*** |
|---|---|
| Methali hutambuliwa haraka kutokana na | |

**Kazi ya 22:**


**Andika** jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Ibilisi ni shetani, kiumbe ............................ kutendea mabaya binadamu. |
| 2. Methali hutungwa kwa umbo maalumu kutokana na ..................... wa msanii. |
| 3. Uhakiki wa methali huzingatia vipengele vya maudhi na fani lakini ................ na ile ya uhakiki wa hadithi. |

## SOMO LA 13: KUHAKIKI VITENDAWILI VYA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Tegua kitendawili **unachokisoma** kwenye picha hii.




**Kazi ya 2:**

Soma habari ifuatayo na **kuihusisha** na picha hii kwa njia ya mazungumzo.

*Vipengele muhimu vya uhakiki wa vitendawili*

Vitendawili ni utanzu wa fasihi simulizi unaoweza kufanyiwa uhakiki. Kama kawaida, vipengele muhimu vya uhakiki wa kazi za kifasihi ni maudhui na fani. Walakini, uhakiki wa vitendawili huwa tofauti kidogo na ule unaofanyiwa habari mbalimbali zinazoingia katika kundi la masimulizi kama hadithi.

**1. Uhakiki wa vitendawili kimaudhui**

Vitendawili huwa na fumbo lililofumbwa na msanii na ambalo linapaswa kufumbuliwa. Fumbo hilo hurejelea vitu vinavyopatikana katika mazingira ya mwanadamu na vinavyojulikana sana kama vile:

a. Vyombo vya jikoni;
b. Matunda mbalimbali;
c. Aina za nguo;
d. Magonjwa (kama vile UKIMWI, maradhi yanayoathiri maisha ya watu wengi);
e. Mimea;
f. Mashine na mitambo mbalimbali (kama vile magari ambayo ni muhimu ili nchi iweze kuwa na amani na maendeleo ya kudumu);
g. Sehemu za mwili na kadhalika.

Haya ndiyo mazingira ya vitendawili. Vitu hivyo vyote ndivyo vinavyochaguliwa kama majibu maalumu ya vitendawili.

Mifano:

| **Kitendawili** | **Jibu** |
|---|---|
| - Kifuko changu kiko mbali ningekupa | Mwezi |
| - Shikeni mzee anaanguka na ndevu zake | Mgomba na mkungu unapokatwa na kuanguka |
| - Mtemi amelala ndani ya nyumba yake na ndevu zake zinapepea nje | Hindi na nyuzinyuzi zake |
| - Mkufu wangu mrefu unatembea | Siafu |

**2. Uhakiki wa vitendawili kifani**

Vitendawili kama fumbo la kuvutia la kisanii huwa na muundo wake, lugha yake na wakati wake.

- **Muundo wake:** Kwa kawaida, vitendawili:

  - Hupitishwa baina ya pande mbili: upande unaotega kitendawili na upande unaokitegua.
  - Huwa na muundo maalumu wa kuendelezwa yaani utangulizi, swali (au jaribio) na jibu.

Mtegaji : Kitendawili!
Mteguaji : Tega!
Mtegaji : (Anatoa kitendawili chake yaani "kutega kitendawili").
Mfano: Nimeanika mpunga wangu juani lakini kulipopambazuka sikuuona
Mteguaji : (Anatoa jibu yaani "kutegua kitendawili").
Jibu : Nyota

Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji huomba apewe mji / zawadi na kisha atoe jibu. Anapopewa anachotaka ndipo anakubali kutoa jibu.

  - Huwa na vipande viwili: Swali (au kitendawili chenyewe) na jibu
    Mifano: "Kila niendapo ananifuata" / [Kivuli]

- **Lugha yake:** Vitendawili hutumia mbinu mbalimbali za lugha (au tamathali za usemi) ili fumbo lake liweze kuwa tamu. Mara nyingi, mbinu hizo ni sitiari, tashihisi, takriri na tanakali za sauti.

Mifano:

- "Drrrrrrrrrh mpaka ng'ambo" / [Buibui]": Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni tanakali za sauti.
- "Nyumba yangu haina mlango" / [Yai]: Mbinu ya lugha iliyotumiwa ni sitiari.

Urefu wa kitendawili, muundo wake na mbinu za lugha zinazotumiwa ndiyo mambo yanayotuwezesha kuainisha vitendawili. Kwa hiyo, kuna:

- **Vitendawili sahili:** Ni vitendawili vifupi vyenye muundo mwepesi kueleweka.
- Mfano: Hazikauki umande / [Pua za mbwa]

- **Vitendawili mkufu:** Huwa na vipande vinavyofuatana. Kila kipande huwa na uhusiano na kipande kilichotangulia.

Mfano: Nikisimama anasimama, nikiketi anaketi, nikiondoka anaondoka / [Kivuli changu]

- **Vitendawili vya tanakali za sauti:** Ni vile ambavyo vinatumia tanakali za sauti.

Mfano: Drrrrrrrrrh mpaka ngambo / [Buibui]

- **Vitendawili sambamba:** Huwa na maelezo marefu (kama hadithi fupi) halafu jibu lake huwa ni refu pia (kama mafumbo).

**3. Mifano ya uhakiki wa vitendawili**

Hii ifuatayo ni mifano ya vitendawili ambavyo vimefanyiwa uhakiki:

**a. "Nyumba yangu haina mlango" / [Yai]**

- Kitendawili chenyewe: [Nyumba yangu haina mlango]
- Jibu: [Yai]
- Mazingira: Jengo
- Lugha iliyotumiwa: sitiari
- Aina yake: Kitendawili sahili

**b. "Parrrrr mpaka Maka" / [Utelezi]**

- Kitendawili chenyewe: [Parrrr! Mpaka Maka]
- Jibu: [Utelezi]
- Mazingira: Hija / Ibada ya Waislamu
- Lugha iliyotumiwa: Tanakali za sauti
- Aina yake: Kitendawili cha tanakali za sauti

**c. "Mgeni wangu anapoingia humkaribisha vizuri sana lakini anapoondoka sipendi kumwangalia" / [Chakula na kinyesi]**

- Kitendawili chenyewe: [Mgeni wangu anapoingia humkaribisha vizuri sana lakini anapoondoka sipendi kumwangalia]
- Jibu: [Chakula na kinyesi]
- Mazingira: Mgeni
- Lugha iliyotumiwa: sitiari
- Aina yake: Kitendawili mkufu

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

**Soma** kifungu chote cha habari na **kujibu maswali** yafuatayo:

1. Taja vitu vitatu vinavyorejelewa na fumbo la vitendawili.
2. Muundo wa vitendawili ukoje?
3. Zitaje na kuzieleza mbinu mbili za lugha zinazoweza kutumiwa katika vitendawili.
4. Tegua vitendawili hivi:
   - Mchicha mzuri umechumwa na watu wa nje;
   - Anajipiga kisha analia;

- Nimpigapo mwanangu watu hucheza.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi wenzako **wanavyokisoma** kifungu kile cha habari kile na kuelewa vizuri yanayozungumziwa.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma kwa **sauti na makini** kifungu hiki cha habari.

**Kazi ya 6:**

Soma kwa **sauti na ufasaha** vitendawili vifuatavyo na kuchagua kimoja ambacho **jibu lake sahihi** ni picha ya hapa chini:

1. Chapanda mti bila mguu;
2. Anajipiga kisha analia;
3. Konokono kaacha alama;
4. Hakuna jibu sahihi.



**Kazi ya 7:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. Vitendawili hutumia mbinu mbalimbali za lugha (au .......................) ili fumbo lake liweze kuwa tamu.
2. Walakini, .....................huwa tofauti kidogo na ule unaofanyiwa habari mbalimbali zinazoingia katika kundi la masimulizi kama hadithi.
3. Vitendawili ni ...............................unaoweza kufanyiwa uhakiki.

## D. Msamiati

**Kazi ya 8:**

Katika jozi, tumieni kamusi na kutafuta **maana** ya maneno yafuatayo:

**Mkungu wa ndizi**
**Mtemi**
**Buibui**

**Kazi ya 9:**

**Tunga** sentensi moja kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

**Kazi ya 10:**

Katika jozi, **tajeni** vitendawili ambavyo **majibu** yake ni picha zifuatazo:

1.  ........................................................

2.  ............................................

**Kazi ya 11:**

**Jaza** vitendawili vifuatavyo ili viwe kamili kisha utoe majibu yake:

1. Yeye anasuka ................. lakini hulala chini / (..........);
2. Saa yangu kila siku ......................, ikisimama haitengenezeki tena / (.............).

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

Waelezee wanafunzi wengine yale ambayo **umeyasoma** katika kifungu cha habari cha hapo juu.

**Kazi ya 13:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza** jedwali lifuatalo kwa kutumia sehemu za vitendawili zinazotakiwa:

| | | |
|---|---|---|
| ............. | kaacha | alama |
| Hazikauki | ............................ | |
| ................ | bila | mguu |

**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza** sentensi zifuatazo jinsi **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Nikisimama anasimama, ............................, nikiondoka anaondoka |
| 2. Vitendawili kama ................. la kisanii huwa na muundo wake, lugha yake na wakati wake |

**F. Cheka uongeze siku za kuishi**

**Kazi ya 15:**

Kahaba mmoja alikwenda kumtembelea mteja wake wa kawaida. Alipofika kwa mteja aliingia chumbani na kwa mapenzi akamwambia, “ Mpenzi, ninaomba faranga elfu kumi na tano nilipie teksi niliyokuja nayo”. Mteja aliingiza mkono mfukoni kutoa pesa, ghafla akashtuka na kusema, “Mwenyemali, unasema umekuja na teksi? Mbona unavaa kofia ya pikipiki!” Waambie wenzako kichekesho kingine **cha Kiswahili** unachokijua.

## G. Uhakiki

**Kazi ya 16:**

Fanya **uhakiki** wa vitendawili vifuatavyo:

1. Mifugo ya babu imetafuna ukuta / Panya;
2. Ng’ombe wangu huchungiwa mlimani / Chawa;

**H. Utafiti**

**Kazi ya 17:**

Jiunge na wanafunzi wawili kisha **mtafute** kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu vitendawili mbalimbali na kuvifanyia **uhakiki**. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

**Kazi ya 18:**

Baada ya kuwasomea matokeo ya kazi hiyo, wanafunzi wengine **watoe maoni yao binafsi** juu ya kazi hiyo na kujibu maswali mbalimbali.

## I. Kuandika

**Kazi ya 19:**

Andika kitendawili kingine kinachofuata **muundo** huu yaani mwanzo kuwa sauti inayorudiarudia:

| Drrrrrrrrrrrrr | mpaka ng'ambo |
|---|---|
| ........................ | .................................... |

**Kazi ya 20:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja umetolewa):

| ***Vitendawili vya tanakali za sauti*** | **ni vile ambavyo vinatumia tanakali za sauti** |
|---|---|
| ........................... | vitendawili vifupi vyenye muundo mwepesi kueleweka |
| ........................... | Huwa na vipande vinavyofuatana. Kila kipande huwa na uhusiano na kipande kilichotangulia |

**Kazi ya 21:**

**Andika** jedwali hili katika daftari yako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. ..............anapoingia humkaribisha vizuri sana lakini anapoondoka sipendi kumwangalia. |
| 2. Mteguaji akishindwa kutegua kitendawili, mtegaji ............. mji / zawadi na kisha atoe jibu. |
| 3. Vitendawili huwa na ........................ na msanii na ambalo linapaswa kufumbuliwa. |

**Kazi ya 22:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.


| **Kikundi cha A** | **Kikundi cha B** |
|---|---|
| 1. Urefu wa kitendawili, muundo wake na mbinu za lugha zinazotumiwa | lakini kulipopambazuka sikuuona |
| 2. Nimeanika mpunga wangu juani | mazingira ya mwanadamu na vinavyojulikana sana |
| 3. Fumbo hilo hurejelea vitu vinavyopatikana katika | ndiyo mambo yanayotuwezesha kuainisha vitendawili |

# **SOMO LA 14**: KUHAKIKI NAHAU NA MISEMO YA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

**Tazama** picha hizi mbili. Unaona **nini**?




**Kazi ya 2:**

Soma habari ifuatayo na **kuihusisha** na picha hizi kwa njia ya mazungumzo.

***Vipengele muhimu vya uhakiki wa nahau na misemo***

Nahau na misemo ni semi fupi za Kiswahili zinazoweza kufanyiwa uhakiki kifani na kimaudhui. Uhakiki wake ni kama ule unaofanyiwa vitendawili lakini kuna tofauti ndogo sana inayojitokeza.

**1. Uhakiki wa nahau na misemo kimaudhui**

Nahau na misemo ni semi fupi zinazoingia katika kundi moja na methali na vitendawili. Semi hizo zote hurejelea vitu vinavyopatikana katika mazingira ya mwanadamu na vinavyojulikana sana au hali mbalimbali kama vile:

a. Vyombo au vitu vya jikoni (birika, jiko, chumvi...);
b. Sehemu za mwili wa binadamu (kidole, mdomo, maini, shingo,...);
c. Mitambo mbalimbali (jeki, bomu, darubini na mingineyo inayoweza kuboresha maisha na mazingira ya binadamu na kuyafikia maendeleo ya kudumu);
d. Hali (kifo, kiu, mapenzi, elimu isiyo na ubaguzi,...) na kadhalika.

Mazingira hayo ya mwanadamu ndiyo mazingira ya nahau na misemo. Vitu hivyo vyote ndivyo vinavyotumiwa ili kuleta maana nyingine badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika.Mifano:

| Nahau na misemo | Maana yake |
|---|---|
| - Kuaga dunia | Kufa |
| - Kupata jiko | Kuoa |
| - Shingo upande | Bila kupenda |
| - Kupiga mali shoka | Kugawana mali |

**2. Uhakiki wa nahau na misemo kifani**

Nahau na misemo ni semi zenye muundo wake na lugha yake.

- **Muundo wake:** Nahau huwa na kitenzi chake halisi (au maalumu) kinachotumiwa na kisichobadilika ilhali misemo haina kitenzi maalumu kwani huweza kutumiwa bila kitenzi au pamoja na kitenzi chochote anachokipendelea msemaji.

Mifano ya nahau:

- [Kupigwa kalamu=Kufukuzwa kazini] / John amepigwa kalamu kutokana na ulevi wake na kuchelewa kazi.
- [Kumezea mate=Kutamani sana] / Jihadhari mwanangu! Usimezee mate mali ya wengine ili usije ukakufuru.

Mifano ya misemo:

[Shingo upande=Bila kupenda]
/ Fulani alikubali kuambatana naye shingo upande (Kitenzi ni “Kukubali”)
/ Fulani alimpokea mgeni huyo shingo upande (Kitenzi ni “Kupokea”)
[Kiguu na njia=Mtu asiyetulia mahali pamoja] /
/ Ni kweli kwamba rafiki yake ni kiguu na njia. (Kitenzi ni “Kuwa”)
/ Maishani mwangu, siwezi kuambatana na kiguu na njia. (Kitenzi ni “kuambatana”).

- **Lugha yake:** Nahau na misemo ni semi zinazoweza kutumia mbinu mbalimbali za lugha (au tamathali za usemi) kama vile sitiari, kupunguza ukali wa maneno na kadhalika.

Mifano:

- “Kuwa na mrija=Kuwanyonya wenzako” / Tamathali ya usemi iliyotumiwa ni kupunguza ukali wa maneno.
- “Kukua kisabuni=Kukonda sana” / Mbinu ya lugha iliyotumiwa ni kupunguza ukali wa maneno.

### 3. Mifano ya uhakiki wa nahau na misemo

Hii ifuatayo ni mifano ya nahau na misemo ambayo imefanyiwa uhakiki:

**a. "Kuona cha mtema kuni"**

- Nahau yenyewe: [Kuona cha mtema kuni]
- Maana yake: [Kupata shida au kujuta]
- Mazingira: Mfanyakazi / mtu anayefanya kazi ya kukata kuni
- Lugha iliyotumiwa: kupunguza ukali wa maneno

**b. "Kuwa pete na kidole"**

- Msemo wenyewe: [Kuwa pete na kidole]
- Maana yake: [Kuwa marafiki sana]
- Mazingira: Sehemu ya mwili wa binadamu na pambo
- Lugha iliyotumiwa: sitiari

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

**Soma** kimoyomoyo kifungu hiki cha habari na **kujibu maswali** yafuatayo:

1. Taja nahau mbili zinazorejelea vitu vinaavyopatikana katika mazingira ya mitambo mbalimbali. Usisahau kutoa maana yake.
2. Vitaje vipengele vinavyozingatiwa katika uhakiki wa nahau na misemo kifani.
3. Toa maana ya nahau na misemo hii:
   - Kugonga mwamba;
   - Kuwa na damu ya kunguni;
   - Kuchapa maneno;
   - Kulea mtoto kwa hali na mali;
   - Mtu mwenye domo kaya.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi wenzako **wanavyokisoma** kifungu hiki cha habari k na kuelewa vizuri yanayozungumziwa.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma **kwa sauti, ufasaha na makini** kifungu hiki cha habari.

**Kazi ya 6:**

Soma kwa **sauti na ufasaha** kauli zifuatazo na kuchagua **jibu sahihi** kutokana na picha ya hapa chini:

1. Kauli ile "Mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika" ni nahau;
2. Kauli ile "Mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika" ni methali;

3. Kauli ile “Mapenzi ni kikohozi hayawezi kufichika” ni msemo;
4. Hakuna jibu sahihi.




**Kazi ya 7:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika habari:

1. Nahau huwa na kitenzi chake halisi (au maalumu) kinachotumiwa na kisichobadilika ilhali ................ kwani huweza kutumiwa bila kitenzi au pamoja na kitenzi chochote anachokipendelea msemaji.
2. Fulani alikubali kuambatana naye ................ upande.

## C. Msamiati

**Kazi ya 8:**

Shirikiana na mwenzako na kutumia kamusi ili kutafuta **maana** ya maneno yafuatayo:

1. **Mrija**
2. **Kukonda**
3. **Mtema kuni**

**Kazi ya 9:**

**Tunga** sentensi moja kwa kila neno lililopo hapo juu.

**Kazi ya 10:**

Maneno haya yameendelezwa vibaya. Panga silabi zake vizuri ili kuyapata maneno sahihi:

1. Uhana;
2. Kabiri.

**Kazi ya 11:**

Katika jozi, **tajeni** nahau au misemo ambamo yalitumiwa **majina** ya vitu vifuatavyo. Msisahau kutoa maana yake:

1.  .........................................................

2.  ..............................................................

**Kazi ya 12:**

**Kamilisha** sentensi hizi kwa kutumia nahau au misemo inayofaa:

1. Kalisa ..................... Yohana katika mapenzi yake na Nyiramana. Kwa hiyo alimchafulia mambo.
2. Kazi ile ya kuinua mitambo ........................ Ni kusema kuwa ilikuwa kazi ngumu ya kuchosha.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 13:**

Waelezee wanafunzi wenzako yale ambayo **umeyasoma** katika kifungu cha habari cha hapo juu.

**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, **jaza** jedwali lifuatalo kwa kutumia nahau au misemo inayotakiwa. (Mfano mmoja umetolewa):

| ***Kubugia mchanga*** | **ni kuanguka** |
|---|---|
| ................................. | ............................. |
| ................................. | ............................. |

**Kazi ya 15:**

Kwa njia ya mazungumzo, **kamilisha** sentensi zifuatazo jinsi **zilivyo** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Mazingira hayo ya mwanadamu ndiyo .......................... nahau na misemo |
| 2. John amepigwa ........................... kutokana na ulevi wake na kuchelewa kazi |

## F. Uhakiki

**Kazi ya 16:**

Fanya **uhakiki** wa nahau na misemo ifuatayo:

1. Kupiga umaridadi;
2. Amekula chumvi nyingi;
3. Kumwaga unga.

## G. Utafiti

**Kazi ya 17:**

Jiunge na wanafunzi wawili kisha **mtafute** kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu nahau na misemo mbalimbali na kuifanyia **uhakiki**. Msisahau kuwasilisha matokeo ya kazi yenu kwa wenzenu.

**Kazi ya 18:**

Baada ya kusomewa matokeo ya kazi hiyo, wanafunzi wengine **watoe maoni yao binafsi** juu ya kazi hiyo na kujibu maswali mbalimbali.

## H. Kuandika

**Kazi ya 19:**

Tunga sentensi sahihi kwa kutumia nahau au misemo ifuatayo:

1. Kuvunja ungo;
2. Kupiga mtu vijembe.

**Kazi ya 20:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki (mfano mmoja umetolewa):

| **Unapomwona mtu akianguka , unaweza kusema kuwa** | ***amebugia mchanga*** |
|---|---|
| ........................................................................................ | ............................. |
| ........................................................................................ | ............................. |

**Kazi ya 21:**


Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Vitu hivyo vyote ndivyo vinavyotumiwa ili kuleta maana nyingine | na kiguu na njia |
| 2. Nahau na misemo ni semi zinazoweza kutumia mbinu | badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika |
| 3. Maishani mwangu, siwezi kuambatana | mbalimbali za lugha (au tamathali za usemi) |

## **SOMO LA 15**: KUHAKIKI NYIMBO ZA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kutazama picha ya hapa chini. **je**,**mnaona nini**?









**Kazi ya 2:**

Katika kundi hilo, baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **mkihusishe** na picha hiyo.

***Tujue kuhakiki nyimbo***

Nyimbo ni utanzu mwingine wa fasihi simulizi ya Kiswahili. Utanzu huu unaweza kuzungumzia mambo mbalimbali kama vile:

a. Mapenzi;
b. Umoja na maridhiano;
c. Amani na maendeleo ya nchi;
d. Uongozi bora (kama vile “Gira inka Munyarwanda” yaani “ng’ombe kwa Mnyarwanda,...);
e. Na mengineyo.

Nyimbo huweza kufanyiwa uhakiki ili kuweza kueleweka vizuri zaidi

**1. Vipengele vinavyozingatiwa katika kuhakiki nyimbo**

Kuhusu kipengele cha maudhui, mambo ya kushughulikiwa ni haya yafuatayo:

- Maisha ya mtunzi (iwapo yanajulikana);
- Kichwa cha wimbo;
- Aina ya wimbo;
- Dhamira;
- Ujumbe;
- Falsafa;
- Muhtasari (kwa njia ya nathari).

Kuhusu uhakiki wa nyimbo kifani, mhakiki analazimika kushughulikia mambo yafuatayo:

a. Wahusika;
b. Mtindo: Ni lazima kuonyesha iwapo wimbo ni wa zamani au wa kisasa na mbinu mbalimbali za lugha zilizotumiwa kama vile tamathali za usemi na kadhalika.
c. Muundo au umbo la wimbo: Ikiwa wimbo ulitungwa kwa njia ya kishairi, mambo yatakayotiliwa mkazo ni haya yafuatayo:

- Idadi ya beti;
- Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti;
- Idadi ya vipande vya mstari;
- Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari;
- Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake;
- Bahari ama mstari wa mwisho. Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa "kibwagizo" au "kiitikio." Kama hakuna mstari wa mwisho unaorudiarudia, basi mstari huo utaitwa "kimalizio" au "kituo."

d. Uhuru wa mshairi: Mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika kazi yake. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lake liwe na umbo fulani. Kwa hiyo, msanii anaweza kutumia njia mbalimbali kama vile:

- "Inkisari" yaani kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo (Mfano: "Usifanya makelele, melipa mengi mapesa" badala ya "nimelipa");
- "Mazda" yaani kuongeza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo (Mfano: "Mato johari (i)yalo-umbiwa mwake usoni" badala ya "yalo-" peke yake);
- "Tabdila" yaani kubadilisha silabi ya mwisho ili kuwe na urari wa vina katika kipande bila kuathiri mizani (Mfano: "Jihadhari na dunia" huwa "Jihadhari na duniya");
- "Kuboronga sarufi" yaani kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi (Mfano: "Mviringo ndimu zalowamda" badala ya "Ndimu mviringo zalowanda");

- “Tohozi” yaani kuswahilisha maneno kutoka lugha nyingine ili litamkike kwa Kiswahili (Mfano: “Tutatumia intaneti” badala ya “Tutatumia internet”). Intaneti ni mtandao wa tarakilishi.

**2. Mfano wa wimbo wa Kiswahili**

Kasha langu (taarabu)

Kasha langu la zamani, kasha lisilo t’umbuu, (X2)
Kitasa ndani kwa ndani, na ufunguo ni huu,
Alofungua n’nani, amelivunda maguu. (X2)

[Kipokeo]

*Aa na njiwa rero, aa na njiwa rero,*
*Sipiki chungu hamnyima mkwe,*
*Sendi Manga na njiwa rero,*
*Sipiki chungu hamnyima mkwe,*
*Sendi Manga na njiwa rero.*

Kasha muundo wa kale, si muundo wa kisasa, (X2)
Ni kazi ya watu wale, si Banyani wa Mombasa
Usifanye makelele, melipa mengi mapesa.

Mafundi wote wa kale, kwa hivi sasa hakuna, (X2)
Na walobaki wafile, kabisa hutawaona,
Ilobaki ni pulele, na kazi sijaiona.

Kasha langu la mkafuu, madhubuti sawasawa, (X2)
Lenye harufu ya fuu, kila ukilifungua,
Lanukia karafuu, na waridi isotiwa.

Kifuwa cha kasha hilo, zabibu tosa na tini, (X2)
Mviringo ndimu zalo,-wanda mwake kifuwani,
Mato johari (i)yalo,-umbiwa mwake usoni.

(**ABD-AL-RAHIM SA’ID MUHAMMAD BASALIM**)

**Tanbihi:** Kuna maneno ya Kiswahili cha zamani na ya lahaja zake za Kimvita na Kimrima yaliyotumiwa.

- Kuvunda=Kuvunja
- Rero=Leo (Katika Kimrima)
- Manga=Arabia
- Banyani=Wahindi (jina lililokuwa likitumiwa na wakazi wa pwani ya Afrika ya Mashariki)
- Wafile=Walikufa
- Pulele=Kitu chenye thamani ndogo sana (Katika Kimvita)
- Zalowanda=Zilizowanda [=ambazo ziliwanda]
- Mato=Macho

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari ile kisha **uyajibu** maswali yafuatayo:

1. Je, ni lipi wazo kuu katika habari hii?
2. Zitaje sifa mbalimbali zinazopewa kasha lile.
3. "Mviringo ndimu, zalowanda mwake kifuwani". Eleza waziwazi.
4. Ni zipi sehemu za kasha anazozisifu msemaji?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako anavyoisoma habari hii.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii zaidi ya **mara** moja.

**Kazi ya 6:**

**Husisha** picha hii na ujumbe uliotolewa katika habari yetu.



## D. Msamiati

**Kazi ya 7:**

Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya **maana** ya maneno yafuatayo:

**Kasha**
**Tumbuu**
**Kitasa**
**Mkafuu**
**Kuwanda**

**Kazi ya 8:**

Kila mmoja kati yenu atunge sentensi zenye msingi katika **mapenzi** kwa kutumia maneno matano ya hapa juu.

**Kazi ya 9:**

**Yapange** kwenye vikundi vyake maneno haya yaliyotumiwa katika kifungu chetu cha habari.

Ufunguo
tumbuu
Kasha
Waridi
Zabibu
Tini
Fuu
Ndimu

**1**
**Mimea au matunda**

**2**
**Vyombo**

**Kazi ya 10:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayopatikana **katika kifungu chetu cha habari**:

1. Embe .................. ni lile ambalo lingali gumu lakini linalokaribia kuiva.
2. .............. ni kifaa mfano wa kisanduku kidogo chenye komeo ndani ambacho kinatumiwa kwa kufungia kama vile mlango au sanduku.
3. Ndege huyo mkubwa kuliko tetere na mwenye rangi ya kijivu, weupe usiokoza na ambaye hula nafaka anaitwa.........................

**Kazi ya 11:**

“Lanukia karafuu, na waridi isotiwa”. Tazama picha ifuatayo na kusema viungo hivi hutumiwa wapi.


Haradali nyeupe


Haradali nyeusi


Karafuu


Jira


Zafarani


Uwatu

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

Simama mbele ya darasa **uwaambie** wenzako yale ambayo umeyasoma katika habari.

**Kazi ya 13:**

Kwa njia ya mazungumzo, waambie wenzako wingi wa majina yafuatayo:

1. Kasha;
2. Waridi;
3. Njiwa.

**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, panga vizuri silabi za maneno haya ili yawe sahihi:

1. Fumuka;
2. Ndawaku.

**Kazi ya 15:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata muundo huu wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo kwa **kubadilisha** neno lililoandikwa kwa italiki:

| Kasha muundo wa | kale | si muundo wa | kisasa |
|---|---|---|---|
| Kasha muundo wa | zamani | si muundo wa | ............... |

## F. Uchambuzi au uhakiki wa wimbo ”*Kasha langu*“

Kama tulivyosema, uchambuzi au uhakiki wa kazi ya fasihi hushughulikia vipengele viwili vinavyokamilishana yaani maudhui na fani. Katika uchambuzi huu, nasi tutafuata mtindo huo.► **<u>Maudhui</u>**

Katika kipengele hiki, tutashughulikia mambo yafuatayo:

- **Mtunzi:**

Watunzi wengi wa nyimbo za Kiswahili za zamani kama “Kasha langu“ hawajulikani. Walakini, iliwezekana kufanya utafiti na kugundua mtunzi wa “Kasha langu“ ambaye ni ABD-AL-RAHIM SA’ID MUHAMMAD BASALIM.

Mtunzi huyu alizaliwa T’akaungu mnamo mwaka wa 1920. Ni mtoto wa HADRAMI (baba yake) na mwanamke mmoja Mswahili. Alipokuwa kijana, alihamia Kisauni (Mombasa ya kaskazini) na kuanza kuuza manukato katika mitaa ya Mombasa kwa kutumia kapu lake. Biashara hiyo ya mitaani ilimsaidia katika kujulikana sana kwa akina mama wa kisiwani.







Jambo jingine lililomfanya ajulikane kote kijijini ni nyimbo zake za mapenzi alizokuwa akitungia na kuimbia Bwana na Bibi harusi katika sherehe ya kufunga ndoa. Aliaga dunia mnamo mwaka wa 1978 na kuacha mtoto mmoja wa kiume na mtoto mmoja wa kike.

- **Kichwa cha wimbo:**

Wimbo "Kasha langu" uliotungwa na ABD-AL-RAHIM SA'ID MUHAMMAD BASALIM ulijulikana kote katika mitaa ya Mombasa, Unguja na visiwa vingine, Arabia na kwengineko. Kujulikana huko hakukusababishwa na utamu wa maneno yaliyotumiwa bali ni kutokana na muziki wenyewe na kutegemeana kwa maneno.

"Kasha" ni sanduku kubwa la karatasi ngumu linalotumiwa kuwekea nguo, bidhaa au vitu vya thamani. Katika wimbo huu, mtunzi anatumia neno hilo kwa kumaanisha "Mke" yaani "Mke wangu." Ikumbukwe kuwa ni wakati wa sherehe ya kufunga ndoa.

Baadaye, waimbaji mbalimbali walirudia wimbo huu na kuongeza maneno mengine lakini chimbuko lake ni lile lile yaani jamii ya Waswahili. Inasemekana kuwa kipokeo cha wimbo "Kasha langu'' hakikutungwa na mtunzi mwenyewe lakini hatuna uhakika kuhusu jambo hili. ATHMANI ABDULLAH KAJUNGU ndiye mwimbaji aliyerudia sana wimbo huo "Kasha langu" kiasi kwamba alipachikwa jina la "ATHMANI KASHA."

- **Aina ya wimbo:**

Wimbo huu (taarabu hii) ni wa sherehe, hasa sherehe ya kufunga ndoa (harusi).

- **Dhamira:**

- Katika wimbo huu, wazo kuu ni:

***"Urembo wa Bibi harusi"***: Beti zote za wimbo zinasisitizia urembo wa Bibi harusi: "Kasha muundo wa kale'' yaani Bibi harisi mwenye adabu kama

wanawali wa zamani; “ukilifungua lanukia karafuu” ni kusema kuwa anatoa harufu nzuri; “mviringo ndimu zalowanda mwake kifuani” yaani matiti yake ambayo ni kama ndimu; “kifua cha kasha hilo, zabibu tosa na tini“ ni kusema kuwa ana kifua kizuri sana na mengineyo.

- **Ujumbe:**

Baada ya kuusoma wimbo, tunaona kuwa msanii **« anamsifu mwandani wake yaani Bibi harusi »** kwa urembo wake na tabia yake njema. Si mwanamwali kama wengine na ndiyo sababu posa ilikuwa ya thamani yaani « pesa nyingi ».

- **Falsafa:**

Mtunzi anamtaka msikilizaji ashangilie urembo na uzuri wa mke wake.

- **Muhtasari:**

Bwana harusi anasifu « kasha lake » yaani Bibi harusi. Anasema kuwa hatakwenda Arabia, anataka kuchangia na mkwewe.Yeye ndiye anao ufunguo wa kasha hilo. Ndiye aliyevuta hisia za msichana huyo hakuna mwingine. Kwake, Bibi harusi ni mfano wa wasichana wenye tabia nzuri wa zamani, si kama hawa wa kisasa. Watu waliofundisha wengine maadili bora waliaga dunia. Waliobaki hawana thamani. Bibi harusi alifunzwa na mabingwa hao ambao hawawezi kupatikana.

Bibi harusi ana afya nzuri na anatoa harufu nzuri. Ana kifua kizuri, matiti yanayopendeza na ambayo ni mviringo kama ndimu. Pia, ana macho mazuri sana.

► **<u>Fani</u>**

Vipengele vinavyoshughulikiwa katika fani ni hivi vifuatavyo :

- **Wahusika:**

**. « Wahusika»** ni hawa wafuatao:

***<u>Bwana harusi</u>*****:** Ndiye anayemsifu Bibi harusi. Anaanzia kwa tabia yake nzuri na kuendelea na sehemu nyingine za mwili wake kama kifua na macho. Lakini hakusahau kujisifu yeye mwenyewe na kusema kuwa yeye mwenyewe ndiye aliyevuta hisia za msichana huyo «alofungua n’nani, amelivunda maguu», hakuna mwingine. Na aliweza kuliteka penzi lake « kitasa ndani kwa ndani na ufunguo ni huu » na hana tatizo kwani ni tajiri “melipa mengi pesa“.

***<u>Bibi harusi</u>*****:** Ni msichana mrembo kwa maoni ya Bwana harusi mwenye tabia nzuri. Ni mfano wa wasichana wa zamani wapole na watiifu. Urembo wake unastahili sifa za mwanamume

- **Muundo:**

Wimbo huu unafanana sana na shairi. Muundo wake unajitokeza namna hii:

- **Kipokeo**: Ni sehemu inayoimbwa kila mara mwishoni mwa kila ubeti;
- **Idadi ya beti**: Wimbo una beti tano.
- **Mistari (mishororo) kwa ubeti**: kila ubeti unaundwa na mistari mitatu (3). Mstari wa kwanza na mstari wa tatu inaimbwa mara mbili.
- **Vipande vya mstari**: Kila mstari una vipande viwili.
- **Mizani**: Kila nusu-mstari una mizani nane (8) isipokuwa katika kipokeo.
- **Vina**: kuna vina vya kati na vina vya mwisho lakini inatokana na ubeti.

| Ubeti | Kina cha kati | Kina cha mwisho |
|---|---|---|
| Ubeti wa 1 | -ni | -uu |
| Kipokeo | -ro<br>-ngu<br>-nga | -ro<br>-kwe |
| Ubeti wa 2 | -le | -sa |
| Ubeti wa 3 | -le | -na |
| Ubeti wa 4 | -fuu | -wa |
| Ubeti wa 5 | -lo | -ni |

- **Mtindo:**

Mitindo aliyoitumia msanii katika kazi hii ya sanaa ni hii ifuatayo:

- **Kiswahili cha zamani**: Mtunzi alitumia maneno na mtindo wa Kiswahili wa zamani kama vile “kuvunda“ badala ya “kuvunja“, “mato“ badala ya “macho“ na kadhalika.

- **Kutumia maneno ya lahaja za Kiswahili**: Mtunzi alitumia pia maneno kutoka lahaja za Kiswahili ambazo ni Kimrima “rero“ na Kimvita “pulele“.

- **Mbinu za lugha au tamathali za usemi**: tamathali za usemi alizozitumia ni kama vile:

  * **Sitiari**: Mfano: “Ndimu zalowanda mwake kifuani“ kumaanisha “matiti“, “kasha langu“ kumaanisha “mke wangu“.

- **Uhuru wa mtunzi**: Mtunzi hakufungwa na kanuni za kisarufi za lugha. Ndiyo sababu alitumia:

- **Inkisari**: Ni kupunguza idadi ya silabi katika neno ili urari wa mizani upatikane. Mfano: “Usifanya makelele, **me**lipa mengi mapesa” badala ya “**nime**lipa.”
- **Mazda**: Ni kuongeza idadi ya silabi katika neno ili urari wa mizani upatikane. Mfano: “Mato johari **(i)**yalo-umbiwa mwake usoni“ badala ya “yalo-“ peke yake.
- **Kuboronga sarufi**: Ni kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa mizani na mdundo wa kishairi. Mfano: “**Mviringo** ndimu zalowamda“ badala ya “Ndimu mviringo zalowanda.”

## G. Utafiti na uhakiki

**Kazi ya 16:**

Katika kundi la wanafunzi watatu, tafuteni **nyimbo mbalimbali za Kiswahili** zinazoweza kuambatanishwa na **mada ya mapenzi** iliyogusiwa katika habari yetu. Baada ya kuziandika, mmoja kati yenu azisomee darasa kisha **mzifanyie uhakiki** kwa kuzingatia mwongozo wa uchambuzi uliotolewa. Baadaye, **muwasomee** wenzenu uhakiki mlioufanya ili waweze **kujibu maswali** mbalimbali kuhusu maoni yao binafsi juu ya utanzu huo

## H. Kuandika na kuhakiki

**Kazi ya 17:**

Katika jozi, **fanyeni uhakiki** wa wimbo ufuatao. Mtakapomaliza, mmoja kati yenu **awasomee** wenzenu matokeo ya kazi yenu.

**Chozi la damu**

[Watoto wa nyumba zote njooni tuungane,
Tuwalilie wazazi chozi la damu,
Tupaaze sauti zetu za majonzi na kwikwi,
Kwa wachache wenye huruma watatusikia,
Haki ya malezi bora tumenyang’anywa,
Urithi wa maadili tumevunjiwa,
Oh dunia dunia, dunia unatutesa,
Oh dunia dunia, tumekukosea nini?
Oh dunia dunia, mbona hupendi watoto,
Oh dunia dunia, sikia kilio chetu]

1
Oh dada zetu na mama zetu, tunajua mnajipenda,
Ingawaje tungetamani, na sisi mtufikirie,
Mavazi mnayovaa leo, yanatufundisha nini?
Mnafikiria nini kwa kizazi mnachokilea?
Msije mkashang’aza dunia siku zinazokuja,
Viwanda vyote vya nguo vitakapofungwa!

2
Oh kila siku tunapolala, baba zetu hamjarudi,
Asubuhi tukiamka, baba zetu mmeondoka,
Usiku tukibahatika, kushtuka usiku wa giza,
Tunachokishuhudia ni mama anapigwa makofi,
Na vitisho vya talaka, matusi na harufu ya pombe,
Darasa gani mnatupa watoto wenu?

3
Oh tukirudi toka shuleni, madaftari hamkagui,
Eti kwa kuwa tumechoka, burudani mwatuwekea,
Video mnazowasha, picha za vita na mauaji,
Au mikanda iliyorekodiwa, Sodoma na Gomora,
Hamkumbuki ya kuwa, mnayafuta ya darasani,
Urithi gani mnatupa wazazi wetu?

4
Oh kwenye chakula cha usiku, siku zote baba hayupo,
Kusali sala za pamoja, kwenye nyumba yetu ni mwiko,
Amechelewa kutoka kwa mama mdogo yule wa siri,
Au giza likizidi, hatarudi mpaka asubuhi,
Na mama akisha jua, mbio kwa "anko" wa usiseme,
Familia moja, baba na mama watano.

5
Oh kwa sababu ya mambo haya, ndugu zetu wanaumia,
Wapo wanaorandaranda mitaani bila makazi,
Wengi wamelazimika kuajiriwa bado wadogo,
Hawana tena nafasi ya kusoma wapate elimu,
Na wengi wanajiuza miili yao ili waishi,
Mbona dunia umetugeuka watoto!

**(Bernard Mukasa)**

**Kazi ya 18:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** maneno yaliyoandikwa kwa italiki:

| ***Mafundi*** | **wote wa kale** | **kwa hivi sasa** | ***hakuna*** |
|---|---|---|---|
| | | | |

**Kazi ya 19:**

Shirikiana na wenzako wawili na kubuni wimbo kuhusu "**Uongozi bora**". Kundi lenu **libadilishane** wimbo huo na kundi jingine ili **kuufanyia uhakiki** na kuutolea **tathmini** darasani.

## **SOMO LA 16**: KUHAKIKI MASHAIRI SIMULIZI YA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kutazama picha ya hapa chini. **Je,mnaona nini**?



Jizatiti na mashairi ya Kiswahili

Mathias E. Munyampala

**Kazi ya 2:**

Katika kundi lako, baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusisheni** na picha hiyo.

***Vipengele muhimu vya uhakiki wa mashairi simulizi ya Kiswahili***

Mashairi simulizi ya Kiswahili kama tanzu nyingi za fasihi huweza kufanyiwa uhakiki. Kama kawaida, uhakiki huo huzingatia vipengele vya maudhui na fani.

**1. Uhakiki wa mashairi simulizi kimaudhui**

Kuhakiki shairi kimaudhui ni kulichambua na kuweka wazi mawazo na mafunzo yote anayoyazungumzia mtunzi pamoja na mtazamo wake juu ya mawazo hayo. Ili kazi hiyo ifanyike vizuri, ni lazima kulisoma shairi na kulielewa vizuri. Vipengele vinavyoshughulikiwa ni hivi vifuatavyo:

a. Maisha ya mtunzi (iwapo yanajulikana): Ni vigumu kuwajua watunzi wa mashairi simulizi ya Kiswahili kwani ni utanzu mkongwe sana. Ila, mshairi fulani anapojulikana, ni vizuri kuzungumzia kuhusu maisha yake.
b. Kichwa cha shairi: Ni kutaja kichwa chake.
c. Aina (au kipera) ya shairi: Shairi simulizi linaweza kuwa la simango, la mapenzi, la waadhi na kadhalika.

d. Dhamira au wazo kuu: Mashairi yanaweza kuwa na dhamira za kisiasa (uongozi bora, kuhamasisha watu kuhusu kuboresha uzazi...), kiuchumi (mafunzo kuhusu kuwekeza mali na kutegemea benki ili kuboresha maisha ya mtu,...), kijamii (mapenzi, dini,...), kiutamaduni (ndoa,...) na kadhalika.
e. Ujumbe au fundisho au maadili au onyo: Ni yale mambo ambayo mtunzi angependa hadhira ijifunze ili kuweza kufanikisha misimamo iliyojengwa na msanii huyo.
f. Falsafa au msimamo wa mshairi au mtazamo wa mshairi: Ni imani ya mshairi. Kutokana na dhamira za kazi yake. Kwa mfano, mshairi anapopambanisha wema na ubaya katika kazi yake, falsafa inaweza kuwa "wema hushinda ubaya". Si lazima kila wakati mshairi akubalike na wanajamii wote.
g. Muhtasari (kwa nathari): Ni kifungu cha habari kwa njia ya nathari kinachorudia yaliyomo katika shairi husika.

## 2. Uhakiki wa mashairi simulizi kifani

Kuhakiki shairi kifani ni kulichambua kwa kina na kuziweka wazi mbinu za kisanaa alizozitumia mshairi katika kutunga kazi yake. Vipengele muhimu vinavyoshughulikiwa ni hivi vifuatavyo:

- Wahusika: Ikiwa shairi limehusisha wahusika, ni vizuri pia mhakiki awabainishe.
- Mtindo: Ni lazima kuonyesha iwapo shairi ni la kimapokeo au la kisasa na mbinu mbalimbali za lugha zilizotumiwa kama vile tamathali za usemi na kadhalika.
- Muundo au umbo la shairi: Mambo yatakayozungumziwa hapa ni:

  - Idadi ya beti;
  - Idadi ya mistari (au mishororo) kwa kila ubeti;
  - Idadi ya vipande vya mstari;
  - Idadi ya mizani kwa kila ubeti au nusu-mstari;
  - Aina za vina (vya kati na vya mwisho) na mpangilio au urari wake;
  - Bahari ama mstari wa mwisho. Iwapo mstari wa mwisho unaorudiarudia kwa kila ubeti unaitwa "kibwagizo" au "kiitikio". Kama hakuna mstari wa mwisho unaorudiarudia, basi mstari huo utaitwa "kimalizio" au "kituo".

- Uhuru wa mshairi: Mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika kazi yake. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lake liwe na umbo fulani. Kwa hiyo, msanii anaweza kutumia njia mbalimbali kama vile:

  - "Inkisari" yaani kupunguza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo (Mfano: "Ugonjwa wenyewe, nimeuita dereva" kuwa "Ugonjwa wenyewe, meita dereva");

- "Mazda" yaani kuongeza idadi ya silabi katika neno ili kusawazisha idadi ya mizani katika mshororo (Mfano: "Hiyo ndiyo desturi yao" kuwa "Hiyo ndiyo de**si**turi yao");

- "Tabdila" yaani kubadilisha silabi ya mwisho ili kuwe na urari wa vina katika kipande bila kuathiri mizani (Mfano: "Jihadhari na dunia" huwa "Jihadhari na duniya");
- "Kuboronga sarufi" yaani kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi (Mfano: Siku hiyo ikifika" kuwa "Ikifika hiyo siku");
- "Tohozi" yaani kuswahilisha maneno kutoka lugha nyingine ili litamkike kwa Kiswahili (Mfano: "Tutatumia intaneti" badala ya "Tutatumia internet"). Intaneti ni mtandao wa tarakilishi.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

**Soma** kifungu kile cha habari kisha **uyajibu** maswali yafuatayo:

1. Taja mambo mbalimbali yanayoshughulikiwa katika kulichambua shairi kimaudhui.
2. Je, ni mambo yapi yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa umbo la shairi?
3. Je, ni yapi mambo yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa umbo la shairi?
4. Je, ni upi umuhimu wa "kuboronga sarufi"?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako anavyoisoma habari hii.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii zaidi ya **mara** moja ili kuielewa vizuri.

**Kazi ya 6:**

**Husisha** picha hii ya ukurasa wa kwanza wa kitabu cha SENKORO na ujumbe uliotolewa katika kifungu cha habari chetu.



## D. Msamiati

**Kazi ya 7:**

Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya **maana** ya maneno yafuatayo:

**Kuwekeza**
**Ubeti**
**Mshororo**
**Kina**
**Kuboronga**

**Kazi ya 8:**

Kila mmoja kati yenu atunge sentensi zenye msingi katika **kuwekeza mali na kutegemea benki** kwa kutumia maneno hapa juu.

**Kazi ya 9:**

**Panga** maneno au vifungu vya maneno hivi katika vipengele husika vya uchambuzi wa habari:

Vina
Dhamira
Mishororo
Ujumbe wa mtunzi
Muhtasari wa shairi
Idadi ya beti

**1**
**Fani**

**2**
**Maudhui**

**Kazi ya 10:**

Kamilisha sentensi zifuatazo **kama zilivyotumiwa** katika kifungu chetu cha habari:

1. Kuhakiki shairi kimaudhui ni kulichambua na kuweka wazi mawazo na mafunzo yote anayoyazungumzia mtunzi pamoja na ................................ya mawazo hayo.
2. Ni vigumu kuwajua watunzi wa mashairi simulizi ya Kiswahili kwani ni ............ sana.
3. Mshairi hafungwi na ............. katika kazi yake. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lake liwe na umbo fulani.

**Kazi ya 11:**

Unda neno kamili kwa kujaza silabi katika mapengo haya:

1. Ku.......ronga sarufi ni njia moja msanii anayoitumia ili kuifanya sentensi yake iwe tamu.
2. Ni vigumu kuwajua wa..........nzi wa mashairi ya fasihi simulizi.
3. “Titi la mama li ta........” ni mojawapo kati ya mashairi ya kimapokeo.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

Simama mbele ya darasa **uwaambie** wenzako, kwa maneno machache, yale ambayo umeyasoma katika kifungu chetu cha habari.

**Kazi ya 13:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata muundo wa sentensi hii na kujaza jedwali lifuatalo kwa kuzingatia **istilahi zinazotumiwa** katika kuhakiki shairi:

| | |
|---|---|
| **Kibwagizo** | **ni mstari wa mwisho unaojirudiarudia kwa kila ubeti** |
| ................................... | huitwa ubeti |
| Mshororo ni | ......................................................................... |
| | huitwa vina vya kati |

**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza sentensi zifuatazo zinazopatikana katika habari kwa kutumia maneno yako **mwenyewe** ambayo **hayakutumiwa** katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| 1. Falsafa au msimamo wa mshairi au mtazamo wa mshairi | .................................................... |
| 2. mshairi anapopambanisha wema na ubaya katika kazi yake, falsafa inaweza kuwa | ................................................... |

## F. Uchambuzi au uhakiki

**Kazi ya 15:**

Katika jozi, **fanyeni uhakiki** wa habari hii. Mtakapomaliza, mmoja kati yenu **awasomee** wenzenu matokeo ya kazi yenu.

Ujana

1

Ewe ulo na busara, fikiri bibi na bwana,
Fikiri lilo tohara, na lile lilo dhamana,
Pia fikiri izara, wewe nayo kukutana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

2

Ujana ni jambo bora, ameumba Rabana,
Tena umetia fora, ulitendalo hufana,
Basi usiwe mkora, akiba aweke sana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

3
Kuweka jambo dharura, jihimu kuweka mwana,
Siyo pato kulipura, kwa usiku na mchana,
Ukitoweka ujura, elewa umekubana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

4
Hebu zituze fikira, ushike ninayonena,
Akiba kwako sitamu, ukiijaza shehena,
Na pia huwa kafara, na shida isije tena,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

5
Ufanyapo biashara, ewe kijana kazana,
Ujihimu kila mara, na akiba kushikana,
Uzee ukikudara, uwe umetulizana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

6
Kwa kweli si masihara, mwanadamu hutatana,
Kukosa kitu ni dhara, jina hutojulikana,
Au uitwe fukara, mzee mja wa lana,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

7
Ujana hukuzingira, ukangiwa na fitina,
Ukafikwa na majira, uzee ukawa jina,
Basi na wako ujira, wa kazi weka hazina,
Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho.

**(Said Kizee)**

Hebu tuchambue shairi hili kwa kuzingatia vipengele muhimu vya uhakiki vifuatavyo:

► **Maudhui**

Katika kipengele hiki, tutashughulikia mambo yafuatayo:

- **Maisha ya mshairi:** Hayajulikani
- **Kichwa cha shairi:** Ni “Ujana“.
- **Aina ya shairi:** Hili ni shairi la waadhi
- **Dhamira:**

- **Dhamira kuu:** Katika shairi hili, wazo kuu ni:

***"Kutodanganywa na ujana na kukumbuka kuweka fedha akiba"***. Mshairi anawakumbusha mabibi na mabwana kutosahau kuweka akiba pesa zao. Ikiwa wanadanganywa na ujana na kusahau kuweka akiba pesa zao, uzee wao utakuwa matata.

- **Ujumbe:** Kuweka akiba pesa zako ili kuishi vizuri.

- **Falsafa:** Maisha tulivu ya uzeeni hutegemea juhudi zinazofanywa ujanani.

- **Muhtasari:**

  Mabibi na mabwana, fikirini kuhusu jambo zuri na jambo baya linaloweza kuwaletea aibu. Mwenyezi Mungu aliufanya ujana uwe wakati mzuri wa kutenda kila jambo. Lolote unalolifanya ujanani hufana kabisa. Lakini, jihadharini ili msije mkadanganywa na ujana huo !
  Kumbukeni kuweka akiba pesa zenu lakini kwa njia isiyo ya wizi, bali kwa njia iliyo halali. Ni muhimu sana kuweka akiba pesa na kuzichunga vizuri. Akiba si pato kwani « chovya chovya humaliza buyu la asali ». Msiwe wajinga. Amkeni mapema na kwenda kazini mngali vijana. Mkizipata pesa nyingi, kumbukeni kumtolea sadaka Mwenyezi Mungu ili kuepukana na shida.

  Kijana, ikiwa wewe ni mfanyabiashara, amka mapema ufanye kazi kwa bidii ili kuishi maisha ya utulivu uzeeni mwako. Ninayokuambia si mzaha. Ukipata hasara, wengine hawatakuheshimu. Watakuita fukara, mkosefu wa radhi za Mwenyezi Mungu.

  Ujana ukikudanganya na kuleta fitina, matatizo yatakuwa mengi na itakuwa vigumu kwako kuuona uzee wako.

Weka akiba mshahara wako, usidanganywe na ujana.

► **<u>Fani</u>**

Vipengele vinavyoshughulikiwa katika fani ni hivi vifuatavyo :

- **Wahusika:**

  Shairi hili halihusishi wahusika.

- **Muundo:**

Muundo wake unajitokeza namna hii:

- **Idadi ya beti**: Shairi hili lina beti saba (7).

- **Mistari (mishororo) kwa ubeti**: kila ubeti unaundwa na mistari minne (4).
- **Vipande vya mstari**: Kila mstari una vipande viwili.
- **Mizani**: Kila nusu-mstari una mizani nane (8).
- **Vina**: Kuna vina vya kati na vina vya mwisho.

| Ubeti | Kina cha kati | Kina cha mwisho |
|---|---|---|
| Beti zote | -ra | -na |
| Kibwagizo | -na | -sho |

- **Kibwagizo**: ni "Sihadawe na ujana, na ujana una mwisho". (kibwagizo ni mstari wa mwisho unaojirudiarudia mwishoni mwa kila ubeti).
- **Mtindo:**

Hii ni mitindo mbalimbali ambayo ilitumiwa na msanii:

- **Ushairi wa kimapokeo**: Mtunzi alitumia beti, mizani, vina vya kati na vya mwisho..

- **Mbinu za lugha au tamathali za usemi**: tamathali za usemi alizozitumia ni kama vile:

* **Sitiari**: Mfano: "ukiijaza shehena", kumaanisha "ukijaza mfuko au akaunti".
* **Tashihisi au uhaishaji**: Mfano: "Uzee ukikudara", kumaanisha "ukizeeka"

- **Uhuru wa mtunzi**: Mtunzi hakufungwa na kanuni za kisarufi za lugha. Ndiyo sababu alitumia:
- **Inkisari**: Ni kupunguza idadi ya silabi katika neno ili urari wa mizani upatikane. Mifano: "Ewe u**lo** na busara" badala ya "Ewe u**lio** na busara." "Akiba kwako **sitara**" badala ya " Akiba kwako **si sitara**", "Uka**ngiwa** na fitina" badala ya "Uka**ingiwa** na fitina".
- **Kuboronga sarufi**: Ni kupangua mpangilio wa maneno ili kuleta urari wa mizani na mdundo wa kishairi. Mifano: "Wewe **nayo** kukutana" badala ya " Wewe kukutana **nayo**", : "Ukitoweka **ujura**" badala ya " **Ujura** ukitoweka.

## G. Utafiti na uhakiki

**Kazi ya 16:**

Shirikiana na wenzako wawili na kutafuta kwenye mtandao wa intaneti au katika vitabu au kwa majirani zenu shairi moja la Kiswahili linalohusu "**Wema.**" Baada ya kuandika na kusoma polepole shairi hilo, **mlifanyie uhakiki** kwa kuzingatia mwongozo wa uchambuzi uliotolewa.

**Kazi ya 17:**

**Wasomeeni** wenzenu uhakiki mlioufanya ili waweze **kujibu maswali** mbalimbali kuhusu maoni yao binafsi juu ya utanzu huo.

**Kazi ya 18:**

Katika kundi la wanafunzi watatu, tafuteni **mashairi mbalimbali ya Kiswahili** yanazoweza kuambatanishwa na **mazingira ya nasaha njema**. Baada ya kuyaandika, mmoja kati yenu ayasomee darasa.

## H. Kuandika

**Kazi ya 19:**

Andika sentensi hii katika daftari lako na **kubadilisha** neno lililoandikwa kwa italiki:

| | |
|---|---|
| **Iwapo mstari wa mwisho unaojirudiarudia mwishoni mwa kila ubeti unaitwa** | ***kibwagizo*** |
| Iwapo mstari wa mwisho haukurudiwa mwishoni mwa kila ubeti unaitwa | ............... |

**Kazi ya 20:**

Shirikiana na wenzako wawili na kubuni shairi kuhusu "**Umoja na maridhiano nchini Rwanda.**" Kundi lenu **libadilishane** shairi hilo na kundi jingine ili **kulifanyia uhakiki** na kulitolea **tathmini** darasani.

**Kazi ya 21:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. "Kuboronga sarufi" ni kupangua mpangilio wa maneno ili | akubalike na wanajamii wote |
| 2. Si lazima kila wakati mshairi | mbinu mbalimbali za lugha zilizotumiwa kama vile tamathali za usemi na kadhalika |
| 3. Ni lazima kuonyesha iwapo shairi ni la kimapokeo au la kisasa na | kuleta urari wa vina au mdundo wa ushairi |


**Kazi ya 22:**

Shirikiana na wenzako wawili na kutunga shairi kuhusu "**Umoja na maridhiano**". Kundi lenu **libadilishane** shairi hilo na kundi jingine ili **kulifanyia uhakiki** na kulitolea **tathmini** darasani.

# **SOMO LA 17**: KUTOA MAONI BINAFSI JUU YA KAZI YA FASIHI SIMULIZI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kutazama picha ya hapa chini. **Je,mnaona nini**?




**Kazi ya 2:**

Katika kundi lako, baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusisheni** na picha hiyo.

***Taratibu za utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi***

Maishani mwake, binadamu huhitaji kujieleza mbele ya wenzake na kueleza yale ambayo amesikia au amesoma kuhusu kazi ya fasihi. Anaweza kukubaliana na mtunzi au kumpinga kutokana na mawazo aliyoweka hadharani katika kazi yake. Kitendo hicho cha kutoa msimamo wake au maneno yanayoonyesha fikra zake juu ya kazi ya fasihi fulani ndicho kinachoitwa “utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi hiyo.” Hili ndilo suala litakalozungumziwa katika kifungu cha habari hiki, lakini litahusishwa na kazi za fasihi simulizi tu.

**1. Umuhimu wa utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi**

Kila mtu ana uwezo wa kutoa maoni yake binafsi kuhusu kazi yoyote ya fasihi simulizi. Wengine huifanya kazi hii na kufanikiwa, wengine huifanya ovyoovyo na kufeli. Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi ni zoezi ambalo linadai ujuzi na uzoefu wa kiwango fulani katika taaluma ya elimu. Baadhi ya watu huweza kujisifu kuwa wana uwezo huo lakini si kweli kwa sababu watu wote hawana ujuzi na uzoefu sawa wa kielimu.

Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi ni zoezi muhimu katika maisha ya mwanadamu. Umuhimu wake hutokana na:

a. Kumwezesha mtu kumudu na kuboresha stadi za mazungumzo na kujieleza hadharani bila woga wala wasiwasi: Kuna watu ambao huwa na hofu au kutetemeka ovyo wanapoambiwa kutoa maoni yao mbele ya umati au hadharani. Zoezi hili la utoaji wa maoni binafsi ndilo jibu la tatizo hilo.
b. Kumfanya mtu aongeze ujuzi wake wa kihistoria kuhusu utanzu na kipera fulani cha fasihi simulizi: Zoezi hili la utoaji wa maoni binafsi hutarajiwa kufanyika mtu angali shuleni. Jambo hili linatokana na kuwa ni zoezi linalochukua muda mrefu ili kujitetea ipaswavyo. Hata wakongwe wanapaswa kulifanya wanapojieleza hadharani. Watoto, watu wazima na hata wakongwe wanapaswa kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu fasihi simulizi yao yaani tanzu na vipera vyake, kazi mbalimbali za kifasihi zilizotungwa, maisha ya watunzi wa kazi hizo na kadhalika.
c. Kumfanya mtu azingatie ipaswavyo mbinu za kushawishi wengine ili waunge mkono msimamo wake: Utoaji wa maoni binafsi ni kama nguzo ya mawasiliano baina ya watu. Mwenzako akitangaza au kuweka hadharani nia yake au mawazo yake, huwezi kukaa kimya kama mtu ambaye hajui kitu. Ni lazima na wewe utoe msimamo wako juu ya nia yake na maelezo ya kutosha ili mawasiliano kati yenu yafanyike na kumshawishi akubaliane na wewe. Kufaulu kwako kutategemea ujuzi na uzoefu ulio nao katika kuwashawishi watu ili kuunga mkono nia zako.
d. Kumfanya mtu aongeze uwezo wake wa kufafanua suala na kutatua tatizo haraka bila kukawia: Kufafanua suala si kazi rahisi, ni kazi ambayo inahitaji makini. Unapokuwa na ujuzi wa kutosha katika kutoa maoni binafsi hadharani ndipo unaweza kujitetea ipaswavyo.
e. Kumfanya mtu awe na adabu na uvumilivu katika kuyasikia maoni ya wengine na kutoa msimamo wake: Si vizuri kutupilia mbali maoni ya mtu wakati hajamaliza kutoa nia yake. Ni lazima kwanza kumsikiliza kwa makini na kufafanua anayoyasema. Msimamo wako unatolewa baadaye.
f. Kumwezesha mtu hasa hasa mwanafunzi kuelewa maswali katika mtihani na kuyajibu ipaswavyo: Anapohitimu masomo yake, mwanafunzi anatahiniwa ili kufaulu na kupewa cheti chake. Zoezi hili huamsha na kuimarisha kipaji chake cha kuelewa swali yaani kulisoma, kulifafanua, kuelewa maana yake na kutoa jibu sahihi.

**2. Mbinu zinazotumiwa katika utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi**

Kufaulu au kutofaulu katika utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi hutegemea mbinu mbalimbali zinazofuatiliwa na mtu anayefanya kazi hiyo. Mbinu hizo ni hizi zifuatazo:

- Kuelewa suala: Suala ni jambo linalotakiwa kujadiliwa na kukatiwa shauri. Suala linaweza kuwa uamuzi wa serikali wa kuwahudumia maskini hohehahe kwa kuwapa ng’ombe, elimu kwa wote, haki ya wanawake kuwa warithi na kadhalika. Ni lazima kuelewa suala ili kuweza kutoa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi. Kuelewa suala ni:

- Kuelewa kwanza maana ya maneno yaliyotumiwa;
- Kujua na kuelewa wakati na mahali husika yaani wakati gani jambo hilo lilitokea au lilifanyika na mahali lilipofanyiwa;
- Kujua maana ya viunganishi.

- Kusoma kazi ya fasihi na kuandika mambo yatakayojadiliwa: Ni kusema kuwa jinsi mtu anavyosoma ndivyo anavyoandika mawazo makuu yaliyozungumziwa katika kazi ya fasihi na sentensi ambazo zitarudiliwa katika kunukuu mambo muhimu.
- Kutayarisha mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi: Mpangilio huu utategemea suala husika. Ni lazima kuonyesha mambo mengine unayoyajua ambayo yatakusaidia katika kueleza suala na kutoa maoni binafsi juu ya kazi hiyo.
- Kueleza kazi ya fasihi husika: Mambo ambayo yanazingatiwa hapa ni:

  - Kutoa maelezo kuhusu maisha ya mtunzi (yanapojulikana);
  - Kueleza chimbuko au asili ya kazi ya fasihi;
  - Kuzitoa dhamira (kuu);
  - Kutoa suala husika;
  - Kutaja muhtasari wa mpangilio wa utoaji wa maoni binafsi.

- Kufafanua au kuchambua kazi ya fasihi husika: Kipengele hiki kinahusu maoni ya mtunzi wa kazi ya fasihi hiyo. Ni kusema kuwa msimamo wa mtunzi ndio utakaozungumziwa tu. Uchambuzi huu utazingatia mambo kama vile:

  - Kuzungumzia mawazo (dhamira) yanayozungumziwa katika kila aya: Mawazo hayo huelezwa kufuatana na jinsi mtunzi anavyoyaona mambo na msamiati aliotumia;
  - Sentensi chache za kunukuu ni muhimu;
  - Kuepukana na maelezo yasiyo na umuhimu.

- Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi: Kipengele hiki kinahusu maoni ya mtu ambaye ameichambua kazi ya fasihi husika yaani mchambuzi. Hapa ndipo mchambuzi ana uhuru wa:

  - Kusema kwamba msimamo wa mtunzi haukubaliwi na watu wote na kwamba kuna misimamo mingine;
  - Kupinga maoni ya mtunzi na kutoa maelezo yanayotetea upinzani huo;
  - Kukamilisha maoni ya mtunzi.

- Kukata shauri kuhusu suala: Hapa mchambuzi anatakiwa:

  - Kutoa muhtasari wa mambo yaliyosemwa katika kazi hii;
  - Kuzungumzia kidogo faida ya kazi hii ya utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi ambayo ameifanya

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma matini ile na **kujibu** maswali haya:

1. Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi ni nini? Eleza kinaganaga.
2. Je, ni upi umuhimu wa utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi? Eleza vizuri.
3. Zitaje mbinu zinazofuatiliwa katika kutoa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi.
4. Katika kipengele chenyewe cha utoaji wa maoni binafsi, mchambuzi anaruhusiwa kufanya nini?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako au mwalimu anavyoisoma habari hii na kuandika mawazo makuu kwenye karatasi.


## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii zaidi ya **mara** moja.

**Kazi ya 6:**

**Husisha** picha hii na **yaliyomo** katika kifungu chetu cha habari.



## D. Msamiati

**Kazi ya 7:**

Shirikiana na mwanafunzi mmoja na kutumia kamusi ili kujua **maana** ya maneno yafuatayo ambayo yanapatikana katika habari:

Ovyoovyo
Kufeli
Hohehahe

**Kazi ya 8:**

Katika pea hiyo, tungeni **kifungu cha habari** ambamo mtayatumia maneno ya hapo juu.

**Kazi ya 9:**

Katika pea hiyo, **pangeni vizuri** silabi za maneno yafuatayo ili maneno hayo yawe sahihi.

1. Likufe
2. Alasu

**Kazi ya 10:**

Jaza jedwali hili kwa **kutaja** mambo yanayozingatiwa katika **vipengele vyenyewe** vya mbinu zinazotumiwa katika utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi.

**1**
**Kueleza kazi ya fasihi husika**

**2**
**Kufafanua kazi ya fasihi husika**

**Kazi ya 11:**

**Kamilisha** sentensi hizi ukizingatia **jinsi zilivyotumiwa** katika kifungu chetu cha habari:

1. Kila mtu ana ............ wa kutoa maoni yake binafsi kuhusu kazi yoyote ya fasihi simulizi.
2. Si vizuri kutupilia mbali maoni ya mtu wakati hajamaliza .......................... yake.
3. Ni lazima kuonyesha mambo mengine unayoyajua ambayo yatakusaidia katika kueleza ................ na kutoa maoni binafsi juu ya kazi hiyo

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako yale ambayo **umeyasoma**.

**Kazi ya 13:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza jedwali kwa **kubadilisha** sehemu ya sentensi iliyoandikwa kwa italiki. Tumia tungo zinazopatikana katika matini:

| **Hapa ndipo mchambuzi ana uhuru wa** | ***kukamilisha maoni ya mtunzi*** |
|---|---|
| | ................................................ |
| | ............................................... |

## F. Utafiti

**Kazi ya 14:**

Katika jozi, **tafuteni** katika vitabu au kwenye intaneti kazi yoyote ya fasihi simulizi. Baada ya kuisoma, **jibuni** maswali kuhusu maoni yenu binafsi juu ya kazi hiyo. Kumbukeni **kulisomea** darasa matokeo ya kazi yenu.

## G. Kuandika

**Kazi ya 15:**

Soma sentensi hii. **Jaza** jedwali hili kwa kutumia maneno yako mwenyewe badala ya yale yaliyotumiwa. Fuata **muundo** uliotolewa

| **Hata** | **wakongwe** | **wanapaswa** | **kulifanya** | **wanapojieleza** | **hadharani** |
|---|---|---|---|---|---|
| Hata | .................. | wanapaswa | .............. | wanapoingia | ................ |
| Hata | .................. | ................. | kunyamaza | ...................... | kumbini |

**Kazi ya 16:**

**Andika** jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama **zilivyo** katika kifungu cha habari:

1. Ni lazima na wewe utoe msimamo wako juu ya .................. na maelezo ya kutosha ili mawasiliano kati yenu yafanyike na kumshawishi akubaliane na wewe.
2. Anapohitimu masomo yake, mwanafunzi .............. ili kufaulu na kupewa cheti chake.
3. Kuna watu ambao huwa na hofu au .................... wanapoambiwa kutoa maoni yao mbele ya ................ au hadharani.

**Kazi ya 17:**


Kwa njia ya **maandishi**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Kufafanua suala ni kazi isiyo rahisi, | ujuzi na uzoefu wa kiwango fulani katika taaluma ya elimu |
| 2. Utoaji wa maoni binafsi juu ya kazi za fasihi simulizi ni zoezi ambalo linahitaji | nguzo ya mawasiliano baina ya watu |
| 3. Utoaji wa maoni binafsi ni kama | kazi ambayo linahitaji makini |

## SOMO LA 18: KUTOA UWASILISHAJI KUHUSU KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

**Kazi ya 1:**

Tazama picha ya hapa chini. **Je,unaona nini**?



**Kazi ya 2:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **ukihusishe** na picha hiyo.

***Tujue kuwasilisha kazi za fasihi simulizi***

Maishani mwetu, tunaweza kutakiwa kuwasilisha kwa hadhira matokeo ya kazi tuliyoifanya au kazi ya wengine. Kazi hiyo inaweza kuwa na lengo fulani kama vile kuwahamasisha watu ili kuiunga mkono serikali yao, kuwashawishi kununua bidhaa za kweli yaani zisizo za bandia, kuwafundisha kuhusu amani na maendeleo ya nchi na kadhalika. Utoaji wa uwasilishaji kuhusu kazi hiyo hautakuwa rahisi kwa watu wote kwa kiwango kimoja. Ili tuweze kuwa na uwezo unaotakiwa katika kutekeleza jambo hilo, tungependa kutoa mwongozo wake katika kifungu cha habari hiki. Lakini, utoaji huo wa uwasilishaji utahusishwa na kazi za fasihi simulizi tu.

**1. Maana na umuhimu wa utoaji wa uwasilishaji kuhusu kazi ya fasihi simulizi**

"**Utoaji wa uwasilishaji**" au "**utoaji wa mhadhara**" ni utoaji wa maelezo mbele ya watu kwa ajili ya kufundisha. Mtu anayetoa mhadhara huitwa "**mhadhiri**".

Utoaji wa uwasilishaji ni zoezi muhimu sana katika maisha ya binadamu hasa mwanafunzi. Jambo hili linatokana na kuwa utoaji wa uwasilishaji:

a. Hukuza utu wa mtu: Ni kusema kuwa mhadhiri anatakiwa kuwa na tabia nzuri mbele ya hadhira yake ili nia zake zisije zikapuuzwa na hadhira hiyo. Kwa hiyo, itakuwa lazima kwake awe na tabia zinazolingana na hadhi ya watu wanaoiunda hadhira yake. Kwa mfano, katika mhadhara utakaotolewa na Mkuu wa Wilaya kwa wabunge, mhadhiri atazingatia cheo cha hadhira yake na kuchunguza mwenendo unaokwenda sambamba na cheo chao. Darasani, mwanafunzi anayetoa mhadhara kwa wenzake anapaswa kuiheshimu hadhira yake ili kuweza kuishawishi kukubali maoni yake.
b. Humfanya mhadhiri azingatie na kumiliki stadi za kuzungumza hadharani na kushawishi hadhira yake: Utoaji wa uwasilishaji humwezesha mhadhiri kuzungumza mbele ya wengine na kuepukana na makosa mbalimbali yanayoweza kufanywa wakati wa kuongea na watu wengine.
c. Humwongezea ujuzi mhadhiri: Jambo hili linatokana na kazi na utafiti anaoufanya mhadhiri katika kutayarisha mhadhara wake. Ili mhadhara wake ufaulu, mhadhiri analazimika kwenda maktabani kufanya utafiti katika vitabu au kwenye intaneti na mengineyo. Katika utafiti huo, anaelewa mambo mengi mapya ambayo hakuyajua.
d. Humfanya mhadhiri aheshimiwe na hadhira kutokana na ujuzi wake wa kiwango cha juu alioutoa hadharani: Mhadhiri akifaulu katika utoaji wa uwasilishaji, hadhira itamwona kama msomi mwenye ujuzi mkubwa na kumheshimu vilevile.
e. Huweza kumfanya mhadhiri ajiongezee mali: Jambo hili linatokana na muda fulani. Kuna mihadhara michache ambayo inawawezesha wahadhiri kuwa na mapato fulani. Mihadhara hiyo ni kama ile inayolenga kuwafundisha wanafunzi wa vyuo vikuu au wafanyakazi wa makampuni au taasisi mbalimbali na kadhalika.

**2. Mbinu zinazozingatiwa ili kufaulu katika utoaji wa uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi**

Kufaulu katika utoaji wa uwasilishaji ndiyo shabaha ya mhadhiri yeyote. Ili lengo hilo lifikiwe, kuna mbinu zinazoweza kuzingatiwa. Mbinu hizo ni kama vile:

- Kutilia mkazo maandalizi ya utoaji wa uwasilishaji: Ni lazima kujiandaa ipaswavyo ili kuweza kuvutia hadhira. Kujiandaa huko ni:
    - kufanya utafiti wa kutosha ili kuyapata maelezo yatakayozitetea hoja zako;
    - kuzingatia sehemu za kazi yako na yaliyomo ndani yake;
    - kujiweka katika hali ya utulivu na kujiamini;
    - kuwaza kuhusu namna ya utangulizi unaovuta hisia za hadhira.

- Kuwa tayari wakati wa kutoa mhadhara: Ingekuwa vizuri kujiandaa ipaswavyo na kuwa tayari kuhusu mhadhara siku mbili kabla ya utoaji wa uwasilishaji. Ni kusema kuwa ni lazima kazi yako iwe tayari siku mbili kabla ya mhadhara na uwe umeizingatia vya kutosha. Kumbuka kuwa unapaswa kuweka 90% ya kazi yako kichwani mwako kwani kufaulu kwako katika mhadhara hakutategemea zaidi maandishi yako. Isitoshe, fika mapema mahali patakapofanyiwa mhadhara.

- Kuonyesha mwenendo wa kisomi: Ni lazima ujue kwamba unakuja kuifundisha hadhira yako. Kwa hiyo, ni lazima mwenendo wako uonyeshe kwamba wewe ni msomi mwenye ujuzi wa kiwango cha juu. Kwa hiyo, unapaswa kufanya hivi:
    - Kuelewa na kumudu vizuri wazo kuu la kazi yako: Inafaa kuzungumzia mambo ambayo unayafahamu na kuyajua vizuri ili uweze kutoa maelezo ya kutosha juu yake.
    - Kuwaza vizuri kabla ya kusema: Mbinu hii inakusaidia katika kuepukana na matumizi ya maneno yasiyo na maana au ukosefu wa jambo la kusema. Unapouliza swali gumu, usiwe na wasiwasi. Waza kwanza kuhusu jibu kisha ujibu ipaswavyo.
    - Kukuza msamiati wako: Mhadhara wako utavuta hisia za watu kutokana na maneno unayoyatumia hasa maneno yaliyo na maana sawa na yale magumu ambayo yalitumiwa katika kazi ya fasihi husika. Kwa hiyo, unalazimika kusoma vitabu vingi tena mara nyingi na kufanya mazoezi mengi ya kuzungumza na wengine.
    - Kutumia maneno na sentensi kamili na sahihi.
    - Kutii kanuni za sarufi: Epuka maneno yanayovunja kanuni za sarufi au yanayotumiwa na wahuni na watoto wa mtaani yaani lugha chafu.
    - Kutumia maneno yanayoonyesha heshima: Ni lazima uionyeshe hadhira yako kwamba unaiheshimu. Hii ni namna moja ya kuvutia hisia zake.
    - Kuonyesha kuwa unafahamu na kumudu vizuri yale unayoyasema.
    - Kuzungumza bila kutazama sana maandishi.
    - Kuwa na maoni mazuri juu ya hadhira.

- Kuvaa vizuri.
- Kuchunga mwenendo wako mbele ya hadhira: Mwenendo huu ni mojawapo kati ya mambo yanayoifanya hadhira ikubali mawazo yako. Inafaa kuvaa vizuri, kusimama wima,...

- Kuzingatia na kumudu stadi za kuzungumza: Mhadhiri hulazimika :

    - Kutumia maneno machache lakini yanayoeleza vizuri mawazo yake: Ni lazima kuepuka kutumia maneno mengi ya mjazo kwani huwachanganya watu na kutoelewa vizuri linalozungumziwa.
    - Kutositasita katika mazungumzo: Ikiwa mhadhiri anatafutatafuta neno kichwani mwake, ingekuwa vizuri kunyamaza kidogo na kuendelea na mazungumzo yake. Mbinu hii huifanya hadhira ione kwamba anafikiri kuhusu anayoyasema na kumheshimu kama msomi.
    - Kusema polepole: Hii ni mbinu inayowafanya watu wazingatie vizuri yanayosemwa. Kumbuka kuwa kuongea haraka haraka huufanya usemi usiwe dhahiri.
    - Kutumia ishara za mikono: Mbinu hii humwezesha mhadhiri kutosahau na kueleza vizuri anayoyasema.
    - Kutochezacheza na vitu mbalimbali: Kuna watu wanaopenda sana kuchezacheza na simu au kalamu zao. Jambo hili huwaudhi watu wanaoiunda hadhira yao. Ingekuwa vizuri kuzima simu yako ya mkononi wakati wa kutoa mhadhara.

- Kuchambua kazi na kuingia katika undani wake: Kuhusu jambo hili, mhadhiri anatakiwa:

    - Kukuza au kuongeza ujuzi alio nao kuhusu kazi ya fasihi simulizi husika: Ni sharti mhadhiri afafanue vizuri kazi ya fasihi simulizi husika na kusoma kazi nyingine au kuyajua mambo mbalimbali ya kiulimwengu ili kukuza ujuzi wake.
    - Kuijua athari ya kazi ya fasihi simulizi husika kwa hadhira yake: Kuna kazi za fasihi simulizi zinazoweza kuwa na athari mbaya kwa hadhira. Kwa mfano, kama kazi ya fasihi simulizi inahusu kupuuza usawa wa jinsia au mauaji ya kimbari, ni vizuri mhadhiri ajue kwanza mbinu atakazotumia ili hadhira yake ibakie katika hali nzuri. Mhadhiri anapaswa kujua hilo kabla ya kutoa mhadhara wake.

- Kutoa mhadhara ipaswavyo kwa kuzingatia sehemu mbalimbali zinazotakiwa.

**3. Mpangilio wa kitendo cha kutoa uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi**

Kila mhadhara hutakiwa kutolewa kwa njia nzuri ili kufana sana. Kwa hiyo, ni lazima kufuata mpangilio huu:

a. Utangulizi: Ni sehemu ya kwanza ya mhadhara. Mhadhiri hutakiwa:

- Kuanzisha jambo au hadithi au msemo mwingine unaoweza

kuifanya hadhira itoe maoni yanayoelekeza kwenye mada itakayozungumziwa;
- Kutaja mada ya kazi yake;
- Kukumbusha mambo inayoyafahamu hadhira kuhusu mada yenyewe;
- Kutaja shabaha ya kazi yake;
- Kutaja mawazo makuu yanayopatikana katika kazi yake na jinsi mhadhara unavyotarajiwa kuendelezwa.

b. Upeo: Mambo ya kuzingatia ni haya yafuatayo:

- Urefu wa mhadhara: urefu wa sehemu hii hutokana na muda wa mhadhara (kuanzishwa na kufungwa kwake);
- Kujihadhari ili kutoenda mbali na mada husika;
- Ujuzi wa hadhira: Si vizuri kutegemea ujuzi wa hadhira;
- Kutumia sentensi fupi;
- Kueleza istilahi muhimu na maneno magumu yatakayotumiwa katika mhadhara;
- Kunukuu ni muhimu.

c. Mkaguo: Hii ni sehemu ya mwisho ya mhadhara. Mhadhiri hutakiwa:

- Kutumia mkagua unaosisimua hadhira;
- Kutoa muhtasari wa yale ambayo yamezungumziwa katika mhadhara;
- Kukumbusha kidogo wazo lake kuu;
- Kuipa hadhira fursa ya kuuliza maswali na kuyajibu;
- Kutoa shukrani kwa hadhira kwa kuhudhuria mhadhara.

Ewe mwanafunzi, fanya mazoezi mengi ili kupevuka katika mambo ya utoaji wa mhadhara.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma matini ile na **kujibu** maswali haya:

1. "Utoaji wa uwasilishaji" ni nini?
2. Je, ni upi umuhimu wa utoaji wa uwasilishaji kwa ujumla?
3. Nyinyi wanafunzi, mnatakiwa kufuata taratibu gani ili kuweza kufaulu katika kutoa mhadhara?
4. "Mhadhara huwa na sehemu muhimu ambazo huzingatiwa katika utayarishaji wake". Eleza kinagaubaga.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako au mwalimu anavyoisoma habari hii na kuandika mawazo makuu kwenye karatasi.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii zaidi ya **mara** moja.

**Kazi ya 6:**

Tazama picha hii. Watu hawa wanazungumzia kuhusu **nini**? Toa **maana** ya jambo linalozungumziwa.




## C. Msamiati

**Kazi ya 7:**

Shirikiana na mwanafunzi mmoja na kutumia kamusi ili kujua **maana** ya maneno yafuatayo ambayo yanapatikana katika habari:

**Stadi**
**Msimu**
**Taasisi**
**Mapato**

**Kazi ya 8:**

Katika jozi hiyo, mtunge **sentensi moja kwa kila neno** kwa kuyatumia maneno ya hapo juu.


**Kazi ya 9:**

Katika jozi hiyo, **pangeni vizuri** silabi za maneno yafuatayo ili maneno hayo yawe sahihi.

1. Livuutu
2. Dhamiraha

**Kazi ya 10:**

Jaza jedwali hili kwa **kutaja** mambo yanayozingatiwa katika **vipengele** vya mbinu zinazotumiwa katika utoaji wa mhadhara juu ya kazi ya fasihi simulizi.




**Kazi ya 11:**

**Kamilisha** sentensi hizi ukizingatia **jinsi zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari chetu:

1. Darasani, mwanafunzi anayetoa mhadhara kwa wenzake anapaswa kuiheshimu hadhira yake ili kuweza kuwashawishi .......................... zake.
2. Mhadhiri ...............katika utoaji wa uwasilishaji, hadhira itamwona kama msomi mwenye ujuzi mkubwa na kumheshimu vilevile.
3. Epuka maneno yanayovunja kanuni za sarufi au yanayotumiwa na ...........na watoto wa mtaani yaani lugha chafu.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

Simama mbele ya darasa uwaelezee wenzako yale ambayo **umeyasoma**.

**Kazi ya 13:**

Kwa njia ya mazungumzo, jaza jedwali kwa **kubadilisha** sehemu ya sentensi iliyoandikwa kwa italiki. Tumia tungo zinazopatikana katika matini:

| | *kutaja mada ya kazi yake* |
|---|---|
| **Katika utangulizi wa mhadhara, mhadhiri hutakiwa** | ........................................... |
| | ............................................ |
| | ............................................ |

## F. Utafiti

**Kazi ya 14:**

Katika jozi, **tafuteni** katika vitabu au kwenye intaneti hadithi yoyote ya fasihi simulizi ya Kiswahili. Baada ya kuisoma, **tayarisheni mhadhara** juu ya kazi hiyo na kuwasilisha kazi yenu kwa wenzenu.

## G. Kuandika

**Kazi ya 15:**

Soma sentensi hii. **Jaza** jedwali hili kwa kutumia maneno yaliyotumiwa katika kifungu cha habari. Fuata **muundo** uliotolewa.

| Utoaji | wa | mhadhara | huongeza | ujuzi | wa | mhadhiri |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Utoaji | wa | mhadhara | .......... | utu | wa | mhadhiri |
| Utoaji | wa | mhadhara | .......... | mali | ..... | mhadhiri |

**Kazi ya 16:**

Andika jedwali hili katika daftari lako na kujaza sentensi zifuatazo kama zilivyo katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Ni lazima ............. wako uonyeshe kwamba wewe ni msomi mwenye ujuzi wa kiwango cha juu. |
| 2. Mbinu hii inakusaidia katika kuepukana na matumizi ya maneno yasiyo na maana au .................. la kusema. |
| 3. Kuna kazi za fasihi simulizi zinazoweza kuwa na .....................kwa hadhira. |

**Kazi ya 17:**

Kwa njia ya **maandishi**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B ili kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Mhadhara wako utavuta hisia za watu kutokana na maneno unayoyatumia hasa maneno yenye | matokeo ya kazi tuliyoifanya au kazi ya wengine |
| 2. Kumbuka kuwa unapaswa kuweka 90% ya kazi yako kichwani mwako kwani | maana sawa na yale magumu ambayo yalitumiwa katika kazi ya fasihi husika |
| 3. Maishani mwetu, tunaweza kutakiwa kuwasilisha kwa hadhira | kufaulu kwako katika mhadhara hakutategemea zaidi maandishi yako |

## SOMO LA 19: TUELEWE MUUNDO WA SENTENSI ZA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kuitazama picha ya hapa chini. Toeni **maoni** yenu kuhusu picha hiyo.




**Kazi ya 2:**

Baada ya kukisoma kifungu cha habari cha hapa chini, **kihusishe** na picha iliyo hapo juu.

***Viwanda vyetu***

Nchi nyingi za kiafrika zinakitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yake. Hata hivyo, imethibitika kwamba ili nchi zipate kuendelea, ni lazima viwanda vitiliwe mkazo.

**1. Viwanda na kilimo hukamilishana**

Mchangamano wa kilimo na viwanda huweza kuleta maendeleo ya haraka ya uchumi wa nchi kwani ni vitu ambavyo hukamilishana. Kilimo huhitaji:

a. Zana za kazi kama vile majembe, matrekta na kadhalika;
b. Pembejeo kama vile mbolea ya chumvi chumvi ambayo hurutubisha shamba na kustawisha mimea;
c. Dawa za kuua wadudu waharibifu kwa afya njema ya mimea.

Vitu vyote hivi ni matokeo ya kazi za viwanda. Viwanda navyo kwa upande mwingine huhitaji malighafi kama vile kahawa, pamba, mkonge, tumbaku na kadhalika. Mazao haya hutokana na kilimo.

**2. Matatizo katika viwanda**

Katika uzalishaji, ingekuwa rahisi zaidi kama sekta hizi mbili zingekamilishana. Ndiyo maana nchi nyingi za kiafrika hazikuridhika kuegemea kwenye kilimo. Mara baada ya uhuru wake, zilijitoma katika kuanzisha na kuendeleza viwanda kama vile:

- Viwanda vya nguo;
- Viwanda vya sigara (ingawa sigara huharibu afya ya mtu);
- Viwanda vya chakula na kadhalika.

Badala ya kuuza malighafi katika nchi za Ulaya na Marekani, bidhaa zilitengenezewa nyumbani ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi ambao wengi wao walikuwa wakulima.

Licha ya mafanikio mengi ambayo viwanda hivi viliyapata, kumekuwa na matatizo mengi ya kimsingi. Tatizo kubwa kwa viwanda vingi ni lile la kukosa vipuli na kubadilika kwa miundo ya mitambo. Mitambo ya viwanda vingi barani Afrika iliagizwa kutoka Ulaya, Marekani au sehemu nyingine zenye viwanda-mama. Hivi sasa, nchi zinazouza vipuli zimeathiriwa na matatizo ya kiuchumi na, kwa hiyo, bei yake imepanda. Kubadilika kwa miundo ya mitambo husababisha pia kutotumika kwa viwanda. Ingawa juhudi zinafanywa na baadhi ya nchi ili kujitengenezea vipuli, bado matokeo yake hayajatosheleza mahitaji yote.

Tatizo la pili ni kukosa wataalamu. Mara nyingi imelazimu kupata wataalamu wa kuendesha viwanda kutoka nchi zilizoendelea. Wataalamu hao wamezigharimu serikali au mashirika yanayoendesha viwanda kiasi kikubwa cha fedha. Aghalabu ni watu wanaokuja kwa mkataba wa miaka michache na kuondoka. Labda tatizo hili litapunguzwa kwa kuwaandaa wataalamu wananchi katika nchi zenye teknolojia sadifu ya juu.

Ingawa nchi nyingi hulisha viwanda vyake kwa malighafi ambayo imezalishwa humo humo nchini, kuna aina nyingine ya malighafi ambayo huagizwa kutoka nchi za ng'ambo. Nchi zinapokuwa katika matatizo ya kifedha, hushindwa kuagiza malighafi hizo na husababisha viwanda kufungwa.

Matatizo haya pamoja na mengine mengi yamevifanya viwanda mbalimbali vijikute katika matatizo makubwa.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma kifungu cha habari cha hapo juu na kuyajibu maswali yafuatayo:

1. "Nchi nyingi za kiafrika zinakitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yake". Eleza kinagaubaga.
2. Kwa nini ni vizuri katika nchi kuwa na sekta ya kilimo na sekta ya viwanda? Eleza kwa kina.
3. Ni matatizo gani yanayovikabili viwanda vingi barani Afrika?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** kwa makini yale anayoyasoma mwanafunzi mwenzako na kisha zingatia mawazo makuu.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma kifungu cha habari "Viwanda Barani Afrika" na kutilia maanani alama za uakifishaji.

**Kazi ya 6:**

**Unaona** nini kwenye picha hizi? **Linganisha** unachokiona kwenye picha ya kwanza na kile kionekanacho kwenye picha ya pili kutokana na umuhimu wake kwenye soko la kimataifa.





**Kazi ya 7:**

Soma sentensi zifuatazo na kuzikamilisha kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

1. Mara nyingi imelazimu kupata .............. wa kuendesha viwanda kutoka nchi zilizoendelea.

| | |
|---|---|
| 2. Tatizo kubwa kwa viwanda vingi ni lile la kukosa ............ na kubadilika kwa miundo ya mitambo | |
| 3. Nchi zinapokuwa katika matatizo ya kifedha, hushindwa kuagiza ............. hizo na husababisha viwanda kufungwa | |

**Kazi ya 8:**

Soma jedwali lifuatalo na **kulijaza** kwa kutaja jina la viwanda kinachoendeleza kazi zake nchini Rwanda kutokana na bidhaa inayohusika. (Mfano: (BRALIRWA)

| Bidhaa | Kiwanda |
|---|---|
| Sharubati | |
| Pombe | |
| Saruji | |
| Nguo | |

## D. Msamiati

**Kazi ya 9:**

Katika jozi, **tafuteni** katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu **maana** ya maneno haya yaliyotumiwa katika kifungu cha habari:

1. Kutoma
2. Pembejeo
3. Malighafi

**Kazi ya 10:**

Katika jozi hiyo, **tungeni sentensi** kwa kutumia maneno ya hapo juu ambayo mmejua maana yake.

**Kazi ya 11:**

Tunga sentensi zinazohusu **"kuboresha afya"** kwa kutumia maneno yafuatayo kama yanavyopatikana katika kifungu hicho cha habari:

1. Dawa........................................................
2. Sigara…………………………………………

**Kazi ya 12:**

Shirikiana na mwenzako na kuzikamilisha ipasavyo sentensi zifuatazo kwa kutumia **maneno kama yalivyotumiwa katika kifungu cha habari**:

1. Wataalamu hao wamezigharimu serikali au .................. yanayoendesha viwanda kiasi kikubwa cha fedha.

2. Nchini Rwanda, mbolea ya samadi huchanganywa na ile ya ..................... ili kurutubisha mashamba.
3. Badala ya kuuza malighafi katika nchi za Ulaya na Marekani, ................ zilitengenezewa nyumbani ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi ambao wengi wao walikuwa wakulima.

**Kazi ya 13:**

Taja vitu hivi kwa **jina moja** (mfano mmoja umetolewa):
]Mfano: Ng'ombe, mbuzi, kondoo, farasi ni "**mifugo**"]

1. Jembe, trekta, panga, mkokoteni ni……………………….
2. BRALIRWA, BMC, UTEXRWA, TOLIRWA ni…………..

**Kazi ya 14:**

"Kufaulu" na "kuharibu" ni maneno yaliyotumiwa katika kifungu cha habari chetu. **Jaza** jedwali hili ipaswavyo kutokana na **maagizo** yaliyotolewa.

| Neno | Neno lenye maana sawa na lile | Kinyume cha neno lile |
|---|---|---|
| 1. Kufaulu<br>2. Kuharibu | | |

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 15:**

Waelezee wenzako **yaliyomo** katika kifungu kile cha habari ambacho umekisoma.

**Kazi ya 16:**

Kwa njia ya mazungumzo, **ambatanisha** tungo za kikundi cha A na zile za kikundi cha B ili kupata sentensi **sahihi**:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Ingawa nchi nyingi hulisha viwanda vyake kwa malighafi ambayo imezalishwa humo humo nchini, | na, kwa hiyo, bei yake imepanda |
| 2. Hivi sasa, nchi zinazouza vipuli zimeathiriwa na matatizo ya kiuchumi | kama vile kahawa, pamba, mkonge, tumbaku na kadhalika |
| 3. Viwanda navyo kwa upande mwingine huhitaji malighafi | kutoka Ulaya, Marekani au sehemu nyingine zenye viwanda-mama |
| 4. Mitambo ya viwanda vingi barani Afrika iliagizwa | kuna aina nyingine ya malighafi ambayo huagizwa kutoka nchi za ng'ambo |

## F. Sarufi na matumizi ya lugha

**Kazi ya 17:**

Soma sentensi zifuatazo:

1. Viwanda huhitaji malighafi na vipuli.
2. Nchi nyingi za kiafrika zinakitazama kilimo kama uti wa mgongo wa maendeleo yake.

Ni yapi maoni yako kuhusu **muundo** wa sentensi hizo?

**Kazi ya 18**:

Katika jozi, onyesheni **aina za maneno** yanayoziunda sentensi hizo (tumieni **vifupisho** kama vile N, T, W,...).

**Kazi ya 19**:

Shirikiana na mwenzako na **kuonyesha muundo** wa sentensi zifuatazo:

1. Serikali ya Rwanda iliunda mikakati thabiti ya kuboresha uzazi.
2. Umoja wa wananchi ni nguzo muhimu ya amani na maendeleo.
3. Nchi yake huagiza malighafi kutoka Rwanda.

**Kazi ya 20**:

Katika jozi hiyo, **kamilisheni** sentensi hizi kwa **istilahi** inayotakiwa:

1. .................. ni neno au fungu la maneno katika sentensi ambalo hutangulia kitenzi. Aghalabu huonyesha mtenda.
2. ....................... ni sehemu inayoundwa na kitenzi, shamirisho na chagizo.
3. ................ ni sehemu ya sentensi inayowakilisha kitu kilichofanyiwa jambo yaani mtendwa au mtendewa katika sentensi.

**Kazi ya 21:**

**Linganisha** majibu ambayo umetoa na maelezo ya hapa chini.

## G. Kuandika

**Kazi ya 22:**

Andika sentensi tatu zinazofuata **muundo** huu.

| ***Majembe, matrekta,...*** | **ni** | **zana** | **za** | **kilimo** |
|---|---|---|---|---|
| .................................... | ni | zana | za | vita |
| .................................... | ni | zana | za | usafirishaji |

**Kazi ya 23:**

Kwa njia ya **maandishi**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B na kupata sentensi zenye maana kamili.

| **Kikundi cha A** | **Kikundi cha B** |
|---|---|
| 1. Katika uzalishaji, ingekuwa rahisi zaidi kama | mbalimbali vijikute katika matatizo makubwa |
| 2. Hata hivyo, imethibitika kwamba ili nchi zipate kuendelea, | sekta hizi mbili zingekamilishana |
| 3. Matatizo haya pamoja na mengine mengi yamevifanya viwanda | katika nchi zenye teknolojia sadifu ya juu |
| 4. Labda tatizo hili litapunguzwa kwa kuwaandaa wataalamu wananchi | ni lazima viwanda vitiliwe mkazo |

## TATHMINI KUHUSU SURA YA PILI

►**Jibu** maswali haya:

1. "Uhakiki wa kazi za fasihi si jambo la hivi karibuni." Fafanua kauli hii.
2. Kwa nini mwanafunzi huhitaji kufanya mazoezi kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi?
3. Katika jozi, chagueni hadithi simulizi moja ya Kiswahili, na baada ya kuisoma na kuielewa, ifanyieni uhakiki.
4. Tafuta methali mbili za Kiswahili ambazo hazikushughulikiwa darasani na kuzifanyia uhakiki.
5. Tafuta vitendawili viwili ambavyo havikushughulikiwa darasani na kuvifanyia uhakiki.
6. Toa maana ya nahau hizi:

- Kumwaga unga;
- Kugonga mwamba.

7. Vipengele gani hushughulikiwa katika kuhakiki shairi?
8. Zitaje mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika kutoa maoni binafsi juu ya kazi ya fasihi simulizi.
9. Shirikiana na mwenzako na kutunga sentensi tatu zinazohusu "amali za tamaduni na kuzalisha kwa kiwango," kisha onyesheni muundo wa sentensi hizo.

# SURA YA 3: UTUNGAJI WA BARUA RASMI, SIMU NA MATANGAZO

## SOMO LA 20: UTUNGAJI WA BARUA RASMI AU YA KIKAZI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kusema **kile** kinachoonekana kwenye picha hii.




**Kazi ya 2:**

Soma kifungu cha habari kinachofuata kisha **kihusishe** na picha hapo juu.

***Barua rasmi au ya kikazi***

(Katika kifungu cha habari cha hapa chini, mwalimu anajibu maswali ya wanafunzi wake kuhusu barua rasmi na utungaji wake)

**1. Barua ni nini?**

**Katikiro:**
Mwalimu, mwanafunzi anapohitimu masomo yake huhitaji kuandika barua ili kuomba kazi. Barua hizo ni sawa na hizi tunazowaandikia marafiki zetu?

**Mwalimu:**

Katikiro, kabla ya kutaka kuijua tofauti iliyoko kati ya barua hizo, hebu kwanza tufasiri neno “barua”. Barua au waraka ni maandishi kwa mtindo wa kinathari yanayopelekwa kwa mtu kutoka mtu mwingine kwa madhumuni ya:

a. Kuarifu kwa haraka;
b. kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa,...;
c. kuagiza bidhaa na kadhalika.

Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo. Ndiyo sababu watu husema kuwa “Waraka ni nusu ya kuonana”. Barua pia ni kumbukumbu ya kudumu kwani inadokeza tabia, elimu na nidhamu ya mwandishi.

**2. Barua hutofautiana**

**Sumaya:**

Asante sana mwalimu, lakini umesahau kujibu swali la Katikiro. Ameuliza ikiwa barua tunazoziandika kwa madhumuni ya kuomba kazi ni sawa na zile tunazowaandikia marafiki zetu.

**Mwalimu:**

Sijasahau swali hilo mtoto wangu. Ni kweli kwamba barua hutofautiana kutokana na lengo lake. Kuna aina tofauti za barua, k.v:

- Barua ya kirafiki: Ni ile unayoandikia rafiki yako au mzazi wako ambamo unaweza kuandika mambo mbalimbali kama vile porojo, kifo cha mwenzako aliyeangamizwa na ugonjwa mkali wa UKIMWI, watu waliokutukana na kadhalika. Mwandishi huwa anajulikana kwa wale anaowaandikia.
- Barua ya mwaliko: Ni ile ya kumwalika mtu katika sherehe yako ya kufunga ndoa au ya kuadhimisha sikukuu yako ya kuzaliwa, kwenye michezo au midahalo na kadhalika.
- Barua rasmi au ya kikazi au ya kiofisi na ya gazetini: Ni barua inayoandikiwa viongozi ili kuomba kazi, kutoa ripoti, kuagiza bidhaa, katika shughuli za kiserikali au kichama au kidini na kadhalika.

**Kamali:**

Samahani mwalimu, tuseme kuwa mimi ni mwanafunzi. Ninamwandikia mwalimu barua ya kisiri ili kumjulisha kuwa mwenzangu hupinga sana umoja na maridhiano baina ya Wanyarwanda na kuleta matata baina ya wanafunzi. Barua hii haitakuwa ya kirafiki kwa kuwa mwalimu si kiongozi!

**Mwalimu:**

Hapana mwanangu! Mwalimu ni kiongozi wako darasani. Kwa hiyo, ni lazima barua yako iwe ya kikazi. Mbona Mariam ananyoosha kidole! Kuna nini mwanangu?

### 3. Utaratibu au muundo wa barua rasmi

**Mariam:**

Asante sana Mwalimu! Katika vidato vilivyotangulia hiki cha tano, tulijifunza namna ya kuandika barua ya kikazi na barua ya mwaliko. Lakini, mambo yakoje kuhusu barua hii ya kikazi?

**Mwalimu:**

Vizuri mwanangu! Kuhusu utaratibu unaofuatiliwa katika kutunga barua rasmi, mambo ambayo huzingatiwa ni haya yafuatayo:

a. Kumbukumbu namba (ikiwa unayo): Upande wa kushoto, sehemu ya juu;
b. Anwani ya mwandishi na tarehe: Chini kidogo, upande wa kulia;
c. Anwani ya mwandikiwa: Chini kidogo, upande wa kushoto;
d. (Kupitia kwa na anwani ya mwenye kusaini na kutia muhuri): Chini kidogo, upande wa kushoto. Sehemu hii inatumiwa kwa nadra kwa madhumuni fulani;
e. Salaam: Chini kidogo, upande wa kushoto. (Hapa salaam ni neno "Bwana" / "Bibi");
f. Yahusu / Kuhusu / Yah. / Kuh.: Chini ya salaam kuelekea katikati. Huu ni mtajo wa kichwa cha habari;
g. Mwanzo au utangulizi: Katika aya moja. (Mara nyingi, tunaandika "Kichwa cha habari cha hapo juu chahusuka").
h. Ujumbe: Katika aya mbili au tatu (chache);
i. Mwisho au hitimisho: katika aya moja.
j. Saini ya mwandishi na jina lake: Chini kidogo, upande wa kushoto. Kuambatanisha barua na saini ndiko kunakoifanya ichukuliwe kama shahidi wa nafsi. Kwa hiyo, unapoandika barua yoyote, iandike kwa makini na tahadhari;
k. (Nakala kwa): Chini kidogo unawaandika maafisa mbalimbali watakaotolewa nakala na anwani yao.

Hebu niweke mchoro ubaoni ili kila mwanafunzi aufahamu na kuuelewa vizuri.

**Wanafunzi wote:**

Ndiyo. Asante sana Mwalimu! Asante sana Mwalimu!

**Utaratibu wa barua rasmi kwenye mchoro**

Kumbukumbu namba

Anwani ya mwandishi na tarehe
Sanduku la Posta

Anwani ya mwandikiwa

K/K (kupitia kwa) na anwani
ya kiongozi anayesaini

Salaam,

<u>Kichwa</u>

Mwanzo.

Ujumbe wa barua
(katika aya mbalimbali)

(katika aya mbalimbali)

(katika aya mbalimbali)

Mwisho

(Saini)

(Jina la mwandishi)

Nakala kwa:
-........
-........

## A. Maswali ya Ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari na **kujibu** maswali yafuatayo:

1. Barua ni nini?

2. Zitaje sababu tatu zinazoweza kumlazimisha mtu kuandika barua rasmi.
3. “Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo”. Eleza vizuri.
4. “Barua ni nusu ya kuonana”. Eleza kinagaubaga.
5. Kwa maoni yako, barua huandikwa kwa mtindo gani?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

**Sikiliza** yale mwenzako anayoyasoma na kuandika mawazo makuu.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma matini hii **mara** nyingine ili kuielewa zaidi.

**Kazi ya 6:**

**Husisha** picha ifuatayo na yaliyomo katika kifungu cha habari.



**Kazi ya 7:**

Soma sentensi zifuatazo na kuzikamilisha kama **zilivyotumiwa** katika habari:

| |
|---|
| 1. Mwanafunzi ........................ yake huhitaji kuandika barua ili kuomba kazi |
| 2. Barua ni risala au ................ anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo |

## D. Msamiati

**Kazi ya 8:**

Shirikiana na mwenzako na kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu ili kujua **maana** ya maneno yafuatayo:

**Risala**
**Kuadhimisha**
**Nadra**
**Saini**
Nakala

**Kazi ya 9:**

Kila mmoja atunge sentensi zinazohusu **Sikukuu ya Mashujaa nchini Rwanda** kwa kutumia maneno ya hapo juu.

**Kazi ya 10:**

Jaza jedwali lifuatalo kwa kutaja **sehemu tatu za barua rasmi** zinazopatikana chini ya "ujumbe":

| | |
|---|---|
| **Ujumbe** | **Sehemu** |
| | ............................ |
| | .......................... |
| | ............................ |

**Kazi ya 11:**

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia **maneno yako mwenyewe** ambayo hayakutumiwa katika kifungu cha habari:

| |
|---|
| 1. Samahani mwalimu, tuseme kuwa mimi ni ............................................. |
| 2. Barua hii haitakuwa ya kirafiki kwa kuwa .............................. si kiongozi! |
| 3. Sehemu hii inatumiwa .......................... kwa madhumuni fulani. |

**Kazi ya 12:**

Jadili na mwenzako mkitoa maelezo ya **kutosha** kuhusu sehemu kuu za barua ya kikazi.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 13:**

Waambie wenzako **sehemu kuu** zinazozingatiwa katika utungaji wa barua rasmi.

**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata **muundo huu** wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo kwa kuzingatia **sifa za barua** zilizotajwa katika kifungu cha habari

| | |
|---|---|
| **Barua ni** | **nusu ya kuonana** |
| | .......................... |
| | .......................... |
| | .......................... |

## F. Mfano wa barua rasmi

Huu ni mfano wa barua rasmi:

Kijiji cha Sovu,
Kata ya Hema,
Tarafa ya Tiro,
Wilaya ya Gasabo,
Namba ya Simu: 0788521355.
S.L.P 25 Kigali
KIGALI
25/03/2016

KUMB:
GA/103/03/2016

Mkuu wa Wilaya ya Gasabo
SLP 48 Kigali
KIGALI

Mkuu wa Wilaya,

**YAH: Ombi la kazi**

Kichwa cha hapo juu chahusika.

Kutokana na tangazo lenu la redioni la tarehe 20/03/2016, ninapata fursa hii kutuma maombi yangu kwenu kutaka kuwekwa kwenye orodha ya watu watakaotahiniwa ili kupewa kazi ya Ualimu katika Shule ya Msingi ya Runoni.

Mimi ni msichana, Mnyarwanda. Nina umri wa miaka ishirini. Nilihitimu masomo yangu mwaka jana katika Shule ya Sekondari ya Cyanika, Mchepuo wa Ualimu. Niliweza kufuzu mtihani wa taifa na kupata alama 42 .

Ni matumaini yangu kuwa ombi langu litafikiriwa .

Asante.

Wako mtiifu,

(Saini)

UMULISA Shadia

**Kazi ya 15:**

"Umefuzu katika mtihani wa kitaifa, elimu ya sekondari, mchepuo wa Sheria. Mwandikie Waziri wa Sheria ukimwomba kazi ya kuwa msajili wa mahakama ya Rutsiro". **Iga muundo** wa hapo juu.

## G. Kuandika

**Kazi ya 16:**

Soma sentensi ya hapa chini. **Jaza** jedwali hili kwa kutumia maneno mengine ya aina moja na yale yanayobadilishwa lakini usiende mbali na **muundo** wa sentensi unaotakiwa:

| **Si** | **kusahau** | **mtoto** | **wangu** |
|---|---|---|---|
| Si | ................ | ............ | yangu |
| Si | ................ | ............ | zangu |
| Si | ................ | kaka | ........... |

**Kazi ya 17:**

Katika jozi, mwanafunzi mmoja atunge barua rasmi kuhusu "Kufunga shule" kisha mwenzake atoe jibu kulingana na ombi husika.

**Kazi ya 18:**

Umepata habari kwamba rafiki yako alifanya ajali ya barabara na kulazwa katika Hospitali kuu ya CHUK. **Mwandikie barua** ya kumpa pole na kumtakia kupona haraka.

# SOMO LA 21: UTUNGAJI WA SIMU

**Kazi ya 1:**

Unaona **nini** kwenye picha hii.



**Kazi ya 2:**

Waambie wenzako umuhimu wa **vitu** hivi maishani mwako.

**Kazi ya 3:**

Soma kwanza habari ifuatayo, kisha **uihusishe** na picha hii.

***Simu***

Hapa na pale tunaweza kuwasikia watu wakisema, “simu yangu imeibiwa”, “amenitumia simu”, “hii ni simu ya mkono” na mambo mengine. Wote wanatumia neno “simu”. Kwa kweli, simu ni nini?

**1. Maana ya simu**

Simu ni chombo kinachotumia umeme na kuwawezesha watu wawili kuwasiliana. Chombo hicho hupelekea na kupokelea mawimbi ya sauti baina ya mtu na mtu papo kwa papo. Simu ina nambari na mkono wa kusikilizia na kusemea. Awali, simu ilihitaji iunganishwe na nyaya, lakini leo hii kuna siwaya au simu bila waya.

Isitoshe, simu inaweza kuwa ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia chombo hicho au kwa kutumia mtambo mwingine (kama vile faksi, teleksi,...) na kuandikwa baadaye.

**2. Aina za simu**

Kuainisha simu kunategemea mambo mawili ambayo ni “simu kama chombo” na “simu kama ujumbe”.

Tunapotilia mkazo “simu kama chombo”, aina za simu zinazojitokeza ni hizi zifuatazo:

a. Simu inayounganishwa na nyaya na yenye nambari na mkono wa kisikilizia na kusemea: Hii ndiyo simu asilia iliyotumiwa kwa miaka hadha wa kadha.
b. Simu bila waya, yenye nambari na mkono wa kisikilizia na kusemea: Ni kama hiyo ya kwanza lakini haitumii nyaya. Aina hii huingia katika kundi la simu ziitwazo “nyayatupu” au “siwaya” au “simu bila waya”.
c. Simu ya mkononi: Ni simu ndogo sana iliyoenea sana tangu mwisho wa karne ya ishirini (20). Inayofanya kazi kwa mfumo wa kielektroniki na kupata mawasiliano kwa njia ya mawimbi. Simu hii ndiyo inayotumiwa na watu wengi nchini Rwanda kwani mtu anaweza kwenda nayo popote anapotaka.

Tunapozungumzia kuhusu “simu kama ujumbe”, tunazipata aina za simu zifuatazo:

- Simu ya mdomo yaani simu au ujumbe wa kuzungumza na mtu mwingine.

- Simu ya upepo yaani habari inayosafirisha mawimbi ya sauti hewani kutoka mahali hadi mahali fulani bila ya kutumia nyuzi.
- Simu ya maneno au simu ya kuandika au barua ya simu au telegramu: ambayo ni ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia mitambo mingine (kama vile faksi, teleksi,...) na kuandikwa baadaye.

**3. Sifa za simu ya maneno**

Simu ya maneno (inayoitwa pia "**telegramu**") ina sifa zake ambazo ni:

a. Kuwa fupi sana: Mtu hana fursa ya kueleza mengi au kuzungumza moja kwa moja na yule anayempelekea taarifa;
b. Kwenda haraka zaidi kuliko barua za kawaida: Kwa kusafirishwa na mitambo mbalimbali, simu ya maneno humfikia mtu baada ya muda mfupi sana (sekunde chache sana);
c. Kuwa na maneno machache: hili linatokana na kuwa mtunzi hulipa fedha kwa kila neno na kituo kinachoandikwa;
d. Kuandikwa kwa kutumia herufi kubwa.

**4. Muundo wa simu ya maneno**

Simu ya maneno au "**telegramu**") hutungwa kwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

- Anwani kamili ya mtu yule anayempelekea simu;
- Taarifa fupi na wazi. Ni lazima kutozidi idadi ya maneno inayokubaliwa kwani maneno yanayozidi hutozwa pesa zaidi;
- Anwani ya mtuma simu au mwandikaji;

Kumbukeni kwamba malipo taslimu yanayotolewa pale pale posta.

**5. Ujumbe wa simu ya maneno**

Taarifa inayompelekewa mtu inatokana na jambo ambalo mtuma simu anataka lizungumziwe. Kwa hiyo, taarifa inaweza kuhusu kutuma pesa kwa mtu, utekelezaji wa mikakati ya serikali kuhusu usawa wa jinsia au uzalishaji mali na kadhalika.

**6. Mfano wa simu ya maneno**

Ufuataо ni mfano wa simu ya maneno:

KALISA JOHN SLP 40 KIGALI

TUMA PESA KWANGU LEO KWA SIMU YA MKONO NINA SHIDA

KAMALI PETER

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 4:**

Soma hadithi na kujibu maswali haya:

1. Simu ni nini?
2. Kwa nini simu ya maneno huwa fupi sana?
3. Zitaje sifa za simu ya maneno unazojua.
4. "Simu ni mjumbe mwepesi sana". Eleza vizuri.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 5:**

**Sikiliza** jinsi mwenzako au mwalimu anavyoisoma habari hii na kuandika mawazo makuu kwenye karatasi.

## C. Kusoma

**Kazi ya 6:**

Soma habari hii zaidi ya **mara** mojaili kuielewa zaidi.

**Kazi ya 7:**

**Husisha** picha hii na **ujumbe wa kifungu cha habari chetu**.




## D. Msamiati

**Kazi ya 8:**

Shirikiana na mwanafunzi mmoja na kutumia kamusi ili kujua **maana** ya maneno yafuatayo ambayo yanapatikana katika habari:

Waya
Umeme
Wimbi

**Kazi ya 9:**

Katika pea hiyo, mtunge **aya moja** kuhusu **mawasiliano** na ambamo mtayatumia maneno ya hapo juu.

**Kazi ya 10:**

Jaza jedwali lifuatalo ukizingatia yale ambayo umeyasoma katika habari ile. Jedwali linaitwa "**Simu ya kuandika**".

**1**
**Sehemu zake**

**2**
**Mitambo inayotumiwa ili kutuma ujumbe**

**Kazi ya 11:**

**Kamilisha** sentensi zifuatazo zilizotumiwa katika kifungu chetu cha habari:

1. Simu ni chombo kinachotumia .............. na kuwawezesha watu wawili kuwasiliana.
2. Kwa kusafirishwa na .............. mbalimbali, simu ya maneno humfikia mtu baada ya muda mfupi sana (sekunde chache sana).
3. Awali, simu ilihitaji iunganishwe na .................., lakini leo hii kuna siwaya au simu bila waya.

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako yale ambayo **umeyasoma**.

**Kazi ya 13:**

**Mnara huu** una **uhusiano gani** na simu ya maneno?



**Kazi ya 14:**

Kwa njia ya mazungumzo, **fuata muundo** huu wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo:

| | |
|---|---|
| **Simu inaweza kuwa ujumbe au habari zinazopokelewa kwa kutumia mtambo mwingine kama vile** | **faksi** |
| | |

## F. Kuandika

**Kazi ya 15:**

Fuata **muundo huu** wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo kwa kuzingatia **sifa za simu ya maneno** zilizotajwa katika kifungu cha habari:

| | |
|---|---|
| **Simu ya maneno** | **huwa fupi sana** |
| | .......................... |
| | .......................... |
| | .......................... |

**Kazi ya 16:**

Katika jozi, mwanafunzi mmoja ampelekee mwenzake **ujumbe wa simu** kwa niaba ya kiongozi wake na mwingine atoe jibu.

**Kazi ya 17:**

**Mtungie simu ya maneno** ndugu yako anayeishi mjini Kigali ili kumwarifu aje kukupokea kwenye Uwanja wa Ndege wa Kanombe kesho asubuhi saa mbili.

# SOMO LA 22: UTUNGAJI WA MATANGAZO

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako **mtazame** vizuri picha hii. Mnaona **nini** kwenye picha hiyo?




**Kazi ya 2:**

Someni kifungu cha habari kifuatacho kisha mkihusishe na picha hii.

***Ni rahisi kutunga matangazo***

Matangazo si kitu kipya kwetu. Tunazoea kusikia matangazo yakitolewa na kupitishwa kwenye redio na runinga, makanisani, darasani na kwengineko. Matangazo hayo hutungwa namna gani na yanalenga nini?

**1. Maana na lengo la matangazo**

Tangazo au "ilani" ni maandishi ambayo yanatoa na kusambaza habari juu ya jambo fulani. Jambo hilo linaweza kuhusu:

a. Kifo cha mtu;
b. Mkutano (kwa mfano, kuhusu kuwekeza pesa na kuwasiliana na benki ili kukuza mtaji);
c. Mkataba wa amani;
d. Alama za barabara ambazo zimebadilika;
e. Wizi;
f. Kazi na mengineyo.

Ni kusema kuwa matangazo huainishwa kufuatana na shughuli au jambo linalozungumziwa. Kwa hiyo, tutakuwa na matangazo ya serikali, matangazo ya biashara, matangazo ya kazi, matangazo ya kifo na kadhalika.

Matangazo huweza kuwa na lengo la kutoa taarifa, kuonya na kushawishi lakini lengo hilo lina uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa. Kwa mfano,

tangazo la kifo hutoa taarifa, tangazo la kujihadhari na UKIMWI au kuepukana na kuvuta sigara huonya lakini tangazo la biashara hushawishi wateja.

**2. Sifa za matangazo**

Ili tangazo liweze kufikia lengo linalokusudiwa, ni lazima sifa zake au mbinu zinazotumiwa zizingatiwe vizuri. Sifa au mbinu hizo ni kama vile:

- Kuandikwa kwa muhtasari: Matangazo hutumia maneno machache ili kutomchosha mlengwa. Kwa hiyo, ni lazima kuyachagua maneno yenye nguvu ya kumshawishi mlengwa kwa muda mfupi.
- Kutumia lugha rasmi: Lugha rasmi ndiyo inayoeleweka kwa watu wote.
- Kueleza saa, siku na tarehe za matukio yanayohusika.
- Kutoa maagizo ya matukio mbalimbali yaani mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu matukio hayo.
- Kutoa sifa za vitu au mtu (kwa mfano mwizi aliyetoroka).
- Kutumia lugha ya mvuto au ya kisanii: Maneno ya kisanii katika matangazo hasa ya biashara huwa mepesi kukumbukwa na huwa yanaeleweka kirahisi. Kwa mfano, tumia kauli “nunua viatu **vya ukweli**”, “mwone mganga **bingwa Afrika ya Mashariki**” na kadhalika.
- Kuambatanisha matangazo na picha: Matangazo mengi ya biashara huwa yanaambatana na picha. Lengo la picha hizi ni kujaribu kumshawishi mteja aamini kuwa bidhaa ile ni bora na hivyo ni muhimu kuinunua.
- Kutumia watu maarufu: Matangazo mengi ya biashara huwatumia watu maarufu ili kuwashawishi walengwa. Kwa mfano, kama ni tangazo kuhusu bidhaa fulani, unaweza kutumia mchezaji maarufu ili iweze kununuliwa.

**3. Mambo ya kuzingatia katika utungaji wa matangazo**

Kuandika matangazo kunahitaji ujuzi fulani na kuzingatia mambo yafuatayo:

a. Kuandika kichwa cha tangazo;
b. Kutaja mtu au shirika linalotangaza;
c. Kutaja watu ambao wanalengwa;
d. Kuonyesha kiini (au wazo kuu) cha tangazo: Ni ujumbe unaokusudiwa kufikishwa kwa walengwa;
e. Kuandika masharti ya tangazo;
f. Kuonyesha anwani ya mtoa tangazo;
g. Kujulisha jina, wadhifa na njia za mawasiliano (namba ya simu, faksi, tovuti, barua pepe) za mtu yule anayewasilisha tangazo.

**4. Kielelezo cha tangazo**

# TANGAZO

**Waziri wa Afya anawakumbusha watu wote wanaotumia madawa ya kulevya hasa hasa vijana kwamba hii ni namna ya kuweka maisha yao hatarini na njia ya kuambukizwa magonjwa mbalimbali ukiwemo UKIMWI.**

Madawa hayo ya kulevya ni kama vile:

- Bangili;
- Kokaini;
- bangi
- na mengine mengi.

Anawakumbusha pia kwamba atakayekamatwa akitumia madawa hayo atapelekwa kwenye kituo cha polisi na kufikishwa mahakamani ili aweze kuhukumiwa ipaswavyo.

Boresha afya yako kwa kujitenga na madawa ya kulevya!

Kigali, tarehe 20/03/2016

Waziri wa Afya
BUTORANO Robert

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari ifuatayo na **kujibu** maswali haya:

1. Tangazo ni nini?
2. "Lengo la matangazo huwa na uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa". Eleza kinagaubaga na kutoa mifano.
3. Kwa nini matangazo huandikwa kwa muhtasari?
4. Kwa nini katika matangazo ya biashara, lugha ya mvuto hutumiwa?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Sikiliza jinsi mwenzako anavyoisoma habari hii na kuandika mawazo makuu.

## B. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii kwa kuheshimu alama za uakifishaji.

**Kazi ya 6:**

Tazama picha hii. Ikiwa kijijini kwenu ulimwona mtu kama huyu, eleza **umuhimu wake** kwa wanakijiji.




## C. Msamiati

**Kazi ya 7:**

Jiunge na mwanafunzi mwingine nakutafuta **maana** za maneno yafuatayo:

1. **Mkataba**
2. **Tukio**
3. **Mtaji**
4. **Maarufu**
5. **Wadhifa**

**Kazi ya 8:**

T**unga sentensi fupi** kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

**Kazi ya 9:**

Tunga sentensi zinazohusu **maridhiano** kwa kutumia maneno yafuatayo yanayopatikana katika kifungu cha habari:

1. Kusambaza.........................................................................................
2. Kuwasiliana.......................................................................................
3. Kuepukana.........................................................................................

**Kazi ya 10:**

Jaza jedwali lifuatalo ukizingatia yale ambayo umeyasoma katika habari ile. Jedwali linaitwa "**Matangazo ya Kiswahili**".

| 1<br>Lengo la matangazo | 2<br>Mambo ya kuzingatiwa katika utungaji wa matangazo |
|---|---|
| | |

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 11:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako kwa maneno machache mambo **muhimu uliyoyasoma katika kifungu cha habari.**

**Kazi ya 12:**

Tazama picha hii. Soma tangazo hili na **kujadiliana** na wengine kwa njia ya mazungumzo kuhusu ukweli wa ujumbe uliotolewa.




**Kazi ya 13:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata **muundo** huu wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo:

| | |
|---|---|
| **Matangazo ni maandishi yanayoweza kutoa habari juu ya** | **mkutano** |
| | ................................ |
| | ................................ |
| | ................................ |

**Kazi ya 14:**

Kamilisha sentensi kama zilivyotumiwa katika kifungu cha habari:

1. Matangazo mengi ya biashara huwatumia watu .................... ili kuwashawishi walengwa
2. Maneno ya kisanii katika matangazo hasa ya biashara huwa mepesi .................... na huwa yanaeleweka kirahisi

## F. Kuandika

**Kazi ya 15:**

Kama Waziri wa Usafirishaji, Nishati na Maji, andika tangazo linalowafunza wapita njia jinsi ya kutumia taa za barabarani na alama za barabarani zinazoitwa kivukomilia.



*Taa za barabarani*



*Kivukomilia*

**Kazi ya 16:**

Kwa njia ya **mishale**, husisha tungo zilizotolewa katika kikundi cha A na zile zinazopatikana katika kikundi cha B na kupata sentensi zenye maana kamili.

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Tunazoea kusikia matangazo yakitolewa na kupitishwa | ili kutomchosha mlengwa |
| 2. Matangazo mengi ya biashara huwa | kwenye redio na runinga, makanisani, darasani na kwengineko |
| 3. Matangazo hutumia maneno machache | lina uhusiano wa karibu na jambo linalozungumziwa |
| 4. Matangazo huweza kuwa na lengo la kutoa taarifa, kuonya na kushawishi lakini lengo hilo | yanaambatana na picha |

**Kazi ya 17:**

Katika jozi, **tayarisheni tangazo** linalowahamasisha vijana kuhudhuria **mkutano wa dharura** unaotarajiwa kufanyika kesho kutwa, tarehe 12/04/2016 katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Giti. Mada itakayozungumziwa ni **“Dawa Za kulevya”**


**Kazi ya 18:**

Wewe na mwenzako, kama viongozi katika kampuni ya BRALIRWA, **mtayarishe tangazo** kwa niaba ya Meneja Mkuu ili kuwataka wateja wakipende sana na kukitumia kinywaji cha "Sprite".

## SOMO LA 23: KUPAMBANUA SENTENSI ZA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Unaona **nini** kwenye picha ifuatayo?




UCHANGANUZI WA SENTENSI YA KISWAHILI

**Kazi ya 2:**

Soma maelezo yafuatayo kisha **yahusishe** na picha ya hapo juu.

***Utungulizi***

Uchanganuzi au upambanuzi wa sentensi si somo geni katika maisha ya mwanafunzi. Ni zoezi linalofanywa katika kujifunza lugha mbalimbali. Zoezi hilo humwezesha mwanafunzi kuchanganua vipashio vyote vinavyoiunda sentensi kuanzia kwa neno.

**1. Hatua za uchanganuzi wa sentensi**

Uchanganuzi wa sentensi haufanyiki kiholela. Ni kusema kuwa kuna hatua zinazofuatiliwa ili kazi hiyo iweze kufaulu. Hatua hizo ni kama vile:

a. Kutaja aina ya sentensi husika. Sentensi inaweza kuwa:

- Sentensi sahili (Mfano: Umoja na maridhiano huwezesha Wanyarwanda kuishi katika amani);

- Sentensi changamano (Aliposikia amewasili, alifoka kwa hasira);
- Sentensi ambatano (Mfano: Watu mbalimbali wanamwamini daktari lakini yeye hajavumbua dawa ya UKIMWI);
- Sentensi shurutia (Dada angekuwa na pesa, mdogo wake asingekosa matibabu).

b. Kutaja sehemu zake kuu. Sehemu hizo ni kama vile:

- Kiima;
- Kiarifu.

Ni lazima kutaja pia sehemu kuu za kiima na kiarifu ambazo ni:

- Kundi la nomino;
- Kundi la kitenzi.

c. Kutaja sehemu zote za maneno yaliyotumika katika sentensi husika.

**2. Njia za uchanganuzi au upambanuzi wa sentensi**

Kazi yoyote ya kisomi inafanyika kwa kufuata taratibu fulani. Hivyo ndivyo uchanganuzi wa sentensi ulivyo. Njia ambazo zinaweza kutumiwa katika uchanganuzi wa sentensi ni kama vile:

- Njia ya maneno: Tunatumia aina za maneno peke yake.
- Njia ya mishale au mistari: hutumia mishale au mistari katika kuichanganua sentensi;
- Njia ya visanduku au ya jedwali: hutumia visanduku ama jedwali katika kuichanganua sentensi;
- Njia ya matawi: Hutumia mchoro wa matawi katika kuichanganua sentensi.

Wewe mwanafunzi wa kidato cha tano, fanya bidii ili kupevuka katika uchanganuzi wa sentensi. Mazoezi mengi ndiyo yatakayokusaidia.

### A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma kifungu hiki kisha uyajibu maswali yafuatayo:

1. Uchanganuzi au upambanuzi wa sentensi ni nini?
2. Unalazimishwa kufanya nini ili kufanya uchanganuzi wa sentensi ipaswavyo?
3. Ni zipi namna mbalimbali za kuipambanua sentensi ya Kiswahili?
4. Katika kuchanganua sentensi, ni zipi sehemu kuu za kiarifu?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Katika jozi, **Sikiliza** jinsi mwenzako anavyoeleza matumizi ya aina za sentensi.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma maelezo kuhusu aina za sentensi kisha utoe mifano.

## D. Msamiati

**Kazi ya 6:**

Kwa kutumia kamusi, jadiliana na mwenzako juu ya **maana** ya maneno yafuatayo:

**Kiholela**
**Kuchanganua**
**Kupambanua**

**Kazi ya 7:**

Jaza jedwali lifuatalo ukizingatia yale ambayo umeyasoma katika habari ile. Jedwali linaitwa "**Uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili**".

**1**
**Aina za sentensi**

**2**
**Njia za uchanganuzi wa sentensi**

**Kazi ya 8:**

Tazama picha hii. **Tunga** sentensi mbili kuhusu picha na kuzifanyia uchanganuzi:



## E. Kuzungumza

**Kazi ya 9:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata **muundo** huu wa sentensi na kujaza jedwali lifuatalo kwa kutumia maneno yako mwenyewe ambayo **hayakutumiwa** katika habari.

| Dada | angekuwa | na | pesa, | mdogo wake asingekosa matibabu |
|---|---|---|---|---|
| ........... | angekuwa | na | kalamu, | ......................................................... |
| Bibi | ................... | | bumbuazi, | mume............................................... |

## F. Kuandika

**Kazi ya 10:**

Andika sentensi mbili zinazofuata **muundo** huu. Maneno yanayoonekana kwenye jedwali ni lazima yatumike.

| Aliposikia | amewasili | alifoka kwa hasira |
|---|---|---|
| .............. | amekufa | ......................... |
| Aliposikia | ................ | ......................... |

## G. Sarufi na matumizi ya lugha

**Kazi ya 11:**

Soma mifano ya sentensi ifuatayo:

1. UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.
2. Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni.

**Taja aina** za sentensi hizo.

**Kazi ya 12:**

Katika jozi, **changanueni** sentensi hizo kwa njia ya **visanduku au jedwali**.

**Kazi ya 13:**

Katika jozi, **changanueni** sentensi hizo kwa njia ya **mishale au mistari**.

**Kazi ya 14:**

Katika jozi, **changanueni** sentensi hizo kwa njia ya **matawi**.

**Kazi ya 15:**

**Linganisha** majibu ambayo umetoa na maelezo ya hapa chini.

Katika "uchanganuzi au uchambuzi wa sentensi", aina za maneno, vikundi vya maneno na aina za sentensi zifuatazo hutumiwa:

► Aina za maneno:

a. Nomino (N);
b. Kitenzi (T) kinachoweza kuwa "kitenzi kikuu" (T) au "kitenzi kisaidizi" (TS) au "kitenzi kishirikishi" (t)
c. Kivumishi (V);
d. Kiwakilishi (W);
e. Kielezi (E);
f. Kiunganishi (U);
g. Kihisishi (H)

► Vikundi vya maneno:

1. Kikundi cha nomino (KN);
2. Kikundi cha kitenzi (KT);
3. Kikundi cha kivumishi (KV);
4. Kikundi cha kielezi (KE).

► Aina za sentensi

a. Sentensi sahili (SS);
b. Sentensi tegemezi (ST);
c. Sentensi changamano (SCH);
d. Sentensi ambatano (SA);
e. Sentensi shurutia (SSH).

Hebu tutoe mifano ya uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili kwa njia mbalimbali.

1. Uchanganuzi kwa njia ya maneno

| UKIMWI | huo | unaangamiza | watu | wengi. |
|---|---|---|---|---|
| N | V | T | N | V |

| Wanafunzi | wote | wameshinda | mtihani | lakini | Sifa | hataki | kwenda | shuleni. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | V | T | N | U | N | Ts | T | E |

2. Uchanganuzi kwa njia ya visanduku

UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.

| SS | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| N | V | T | KN | |
| | | | N | V |
| UKIMWI | huo | unaangamiza | watu | wengi |

Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni

| SA | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | | U | S2 | | | |
| KN | | KT | | | KN | KT | | |
| N | V | T | N | | N | Ts | T | E |
| wanafunzi | wote | wameshinda | mtihani | lakini | Sifa | hataki | kwenda | shuleni |

3. Uchanganuzi kwanjia ya mishale


- UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.

- SS → KN + KT
- KN → N+V
- N → UKIMWI
- V → huo
- KT → T+KN
- T → unaangamiza
- KN → N+V
- N → watu
- V → wengi
- Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni.


- SA → S1 + S2
- S1 → KN+KT
- KN → N+V
- N → Wanafunzi
- V → wote
- KT → T+N
- T → wameshinda
- N → mtihani

□ U → lakini
□ S2 → KN+KT
□ KN → N
□ N → Sifa
□ KT → Ts+T+E
□ Ts → hataki
□ T → kwenda
□ E → shuleni

□ UKIMWI huo unaangamiza watu wengi.




Wanafunzi wote wameshinda mtihani lakini Sifa hataki kwenda shuleni.



## TATHMINI KUHUSU SURA YA TATU

Soma maswali yafuatayo na **kutoa** majibu:


1. Mwandikie barua Mkuu wa Polisi ili kumwomba kutatua tatizo ulilo nalo la ukosefu wa vitambulisho vyako.
2. Tuma simu ya maneno kwa mwenzako ili kumwomba auzishe nyumba yako.
3. Tunga tangazo la biashara na kulisomea wenzako.

# SURA YA 4: UFAHAMU NA UFUPISHO

## SOMO LA 24: UFAHAMU

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako na kueleza yanayoendelea kwenye picha hii.




**Kazi ya 2:**

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha kihusishe na picha ya hapo juu.

***Mbinu zinazofuatiliwa katika ufahamu wa habari***

Somo la ufahamu wa habari si geni kwa mwanafunzi wa shule ya sekondari kidato cha tano kwani lilidokezewa katika kidato cha nne. Hebu tujikumbushe mambo muhimu yanayohusu ufahamu wa habari.

**1. Maana na umuhimu wa ufahamu wa habari**

Ufahamu ni neno ambalo linatokana na kitenzi "kufahamu". Kitendo cha kujua, kutambua na kuelewa ndicho kinachoitwa "kufahamu". Kwa mfano, unapoisoma au kusimuliwa habari kuhusu mila na desturi na kuzalisha kwa kiwango au uzalishaji mali na kuweza kujibu maswali husika, ni kusema kuwa umeifahamu. Ufahamu ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi. Kwa hiyo, somo la ufahamu linampa msomaji au msikilizaji mbinu za uelewaji na kumjaribu kama anaelewa alichokisoma au alichokisikia.

**2. Aina na mbinu za ufahamu**

Kuna aina mbili kuu za ufahamu ambazo ni ufahamu wa kusoma na ufahamu wa kusikiliza. Aina hizo hutofautiana kutokana na jinsi kitendo kinavyofanyika kama ni kusoma au kusikiliza.

Ufahamu wa habari wa kusoma ni ule mtu anaoupata kama njia ya kusoma habari, majarida, magazeti na makala mbalimbali. Katika ufahamu wa habari wa kusoma, msomaji anatakiwa:

a. **Kubaini mawazo makuu**: Msomaji anapoisoma habari fulani au kitabu ni lazima kujua jambo linalozungumziwa. Kama habari inahusu mazingira na maendeleo ya kudumu, ni lazima ujue kuwa linalozungumziwa ni hilo. Anapowaza kuhusu jambo hili inakuwa rahisi kwake kuielewa habari husika.
b. **Kutilia mkazo alama za vituo**: Kuelewa na kuzingatia matumizi ya alama za vituo kutamwezesha kuelewa vizuri ujumbe wa habari. Kutoelewa matumizi ya alama za vituo kunaweza kumfanya msomaji apotoshe maana ya habari ya mwanzo.
c. **Kubaini maana ya maneno na misemo tofauti**: Kuna habari ambazo zinatumia maneno kwa njia ya kisanaa. Kwa hiyo, msomaji anatakiwa kubaini maana ya maneno hayo ili kuelewa vema maana ya maneno aliyoyatumia mwandishi.
d. **Kumakinikia kila kipengele anachokisoma**: Anapokuwa na makini kuhusu kipengele anachokisoma, ndipo msomaji anaelewa vizuri jambo analolisoma.

Ufahamu wa habari wa kisikiliza hufanyika kwa njia ya kusikiliza habari fulani. Mtu anaweza kusikiliza kwa kusimuliwa na kusomewa na mtu mwingine au kutoka redioni au habari iliyorekodiwa. Katika ufahamu wa habari wa kusikiliza, msikilizaji hana budi:

- Kuwa na makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji ili asikie vizuri kinachosemwa;
- Kuzingatia vidokezo vya maana ili kujua iwapo msemaji anafafanua au anaongeza jambo jipya;
- Kuandika baadhi ya mambo muhimu ili yamsaidie katika kukumbuka hapo baadaye;
- Kumakinikia ishara mbalimbali za mwili (kama vile kunyosha mkono, kutingisha kichwa, kupepesa macho na kadhalika).

Habari itakayofanyiwa ufahamu itatolewa katika kipengele cha “Kujizatiti na ufahamu wa habari”.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma habari na **kujibu** maswali yafuatayo:

1. Ufahamu wa habari ni nini?
2. Mwanafunzi wa kidato cha tano anatakiwa kufanya nini ili kufahamu habari anapoisoma?
3. Mwanafunzi huyo atafanya nini ili kufahamu habari anapoisimuliwa?
4. Eleza umuhimu wa kubaini maana ya maneno na misemo tofauti katika kuisoma habari ili kuifahamu zaidi.

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Sikiliza jinsi mwenzako au mwalimu anavyosoma habari hii huku ukiandika mawazo makuu kwenye karatasi.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

Soma habari hii mara mbili kwa kuheshimu matumizi ya alama za uakifishaji zilizotumiwa.

## D. Msamiati

**Kazi ya 6:**

Eleza maana ya maneno yafuatayo:

1. Kupotosha
2. Kubaini
3. Kurekodi
4. Kupepesa

**Kazi ya 7:**

Katika jozi, mtunge **sentensi moja** kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

**Kazi ya 8:**

Jaza jedwali lifuatalo ukizingatia yale ambayo umeyasoma katika habari ile. Jedwali linaitwa "**Ufahamu wa habari**".




**Kazi ya 9:**

**Kamilisha** sentensi zifuatazo ili zilete maana kamili.

| |
|---|
| 1. Anapokuwa na .................. kuhusu kipengele anachokisoma, ndipo msomaji anaelewa vizuri jambo analolisoma. |
| 2. Ufahamu wa ........................ unapatikana katika njia ya kusoma habari, majarida, magazeti na makala mbalimbali. |
| 3. Ufahamu ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo .............. ili kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupotosha maana yake ya msingi. |

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 10:**

Simama mbele ya darasa uwaambie wenzako yale ambayo **umeyasoma**.

**Kazi ya 11:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata muundo huu wa sentensi na kutoa maelezo kuhusu **ufahamu wa habari wa kusoma**:

| | |
|---|---|
| **Katika ufahamu wa habari wa kusikiliza,** | **msomaji anatakiwa kumakinikia ishara za mwili** |
| | ......................................................................... |
| | ......................................................................... |
| | ......................................................................... |

**Kazi ya 12:**

Soma **kwa sauti** kifungu chochote cha habari unachotaka kisha usimame mbele ya darasa ili wenzako **wakuulize** maswali ya ufahamu na wewe **uyajibu**.

## F. Kujizatiti na ufahamu wa habari

**Kazi ya 13:**

**Soma** kwa makini kifungu cha habari hiki **ili uweze** kuyajibu maswali ya ufahamu:

***Usafi wa mwili***

Usafi wa mwili ni miongoni mwa mambo ambayo binadamu analazimishwa kutilia mkazo sana. Msisitizo huu unatokana na kuwa usafi wa mwili una uhusiano wa karibu sana na uboreshaji wa afya yetu.

Usafi kama hali ya kutokuwa na uchafu, unaweza kuhusu:

a. Mazingira yetu (kama vile usafi wa nyumba);

b. Vitu tunavyotumia katika kazi mbalimbali (kama vile usafi wa vyombo vya jikoni);
c. Lugha tunayotumia (kama vile usafi wa lugha au maneno);
d. Roho zetu (kama vile usafi wa roho yaani kutakasa roho zetu kutokana na sala);
e. Mwili wetu (Mfano: Usafi wa meno) na kadhalika.

Ila, katika kifungu cha habari hiki, tutazungumzia usafi wa mwili tu.

Wazazi na walezi wana nafasi kuu na muhimu katika makuzi na usafi wa mwili wa mtoto. Kitendo cha kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili ni njia bora kabisa ya kumwepusha na maadhara mengi. Mtoto anavyokua ndivyo azoeavyo. Misingi sahihi ya usafi anayofundishwa na watu hao ndiyo inayomwezesha kutilia mkazo usafi wa mwili wake katika maisha yake ya baadaye. Misingi ya usafi wa mwili inapaswa kufundishwa na kuwa sehemu moja ya maisha ya kila siku ya binadamu. Usafi wa mwili unawahusu watu wote, awe:

- Mtoto wa shule za chekechea;
- Mtoto wa shule za msingi;
- Mtoto wa shule za sekondari;
- Mwanafunzi wa vyuo vikuu;
- Wafanyakazi wote;
- Watu wote wanaohitaji kuboresha afya yao.

Mambo ya kuzingatia katika usafi wa mwili ni mengi lakini yaliyo muhimu sana ni yale yanayohusu:

a. Usafi wa kinywa;
b. Usafi wa mikono;
c. Usafi wa nywele;
d. Usafi wa nguo.

Kuhusu usafi wa kinywa, madhara yanayoweza kusababishwa na uchafu wa sehemu hizo ni mengi. Meno machafu huweza kuoza na kuvunjika, fizi inaweza kuvimba, kuoza na kutoa harufu mbaya na kadhalika. Upigaji mswaki wa mara kwa mara unashauriwa kwa watu wote. Mtu huweza kupiga mswaki:

- Asubuhi anapoamka kabla ya kifunguakinywa;
- Kila mara baada ya chakula hasa vyakula vyenye sukari;
- Usiku kabla ya kulala.

Vyakula vyenye sukari husababisha ugonjwa wa kuoza kwa meno kwa kiwango cha juu.

Usafi wa mikono nao unapaswa kuzingatiwa sana. Uchafu wa mikono unaweza kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile kuharisha, kipindupindu, kuhara damu, nimonia, ebola na mengineyo ambayo kila mwaka husababisha vifo vya watu wengi sana. Njia moja bora ya kujikinga na magonjwa na kuepuka

kueneza magonjwa ni “kunawa au kuosha mikono kwa ukawaida”. Ni rahisi kupata homa na mafua kama utagusa pua au macho yako huku mikono yako ikiwa na viini.

Pindi unataka kulinda afya yako na ya wengine dhidi ya maambukizo ya magonjwa, unapaswa kunawa mikono:


a. Baada ya kutoka chooni;
b. Kabla ya kutayarisha, kuhudumia au kula chakula;
c. Baada ya kupiga chafya, kukohoa au kupenga kamasi;
d. Baada ya kutupa takataka;
e. Kabla na baada ya kumtembelea mgonjwa;
f. Baada ya kumgusa mnyama au kinyasi cha mnyama;
g. Baada ya kumbadilishia nepi mtoto au kumsaidia kutumia choo;
h. Kabla na baada ya kutibu jeraha au kidonda na kadhalika.Kunawa au kuosha mikono hufanyika namna gani? Hizi zifuatazo ni hatua za kufuatilia ili kitendo hicho kifanyike ipaswavyo:

- Lowesha mikono yako katika maji safi ya bomba na kisha utumie sabuni;
- Sugua mikono yako pamoja ili kupata povu. Usisahau kusafisha kucha, vidole, pande zote za mkono na katikati mwa vidole vyako;
- Endelea kusugua kwa sekunde ishirini (20) hivi;
- Safisha mikono yako katika maji safi yanayotiririka;
- Kausha mikono yako kwa kutumia kitambaa safi au karatsi ya kukaushia mikono.

Kuhusu kucha, hakikisha kuwa zimekatwa ili viini vya maradhi visije vikajificha chini ya kucha. Ni rahisi kufanya hivyo ili kuzuia magonjwa na kuokoa maisha yako.

Kuhusu usafi wa nywele, zinaweza kukatwa au kusukwa mara kwa mara na kusafishwa vizuri kwa kutumia maji na sabuni. Kitendo hiki kitasaidia katika kupunguza uyabisi na kuzuia chawa wa kichwani iwapo nywele zitakuwa chafu na kutooshwa vizuri.

Usafi wa mwili unahusiana sana na usafi wa nguo. Ni lazima wakati wowote nguo zetu ziwe safi yaani zifuliwe kwa sabuni na zibadilishwe mara kwa mara ili mtu asiwe na mwenendo wa kihuni.



Nguo zinazohusika ni:

a. Mavazi ya nje kama vile shati, mpira, blauzi, kofia, kanzu, viatu, suruali...;
b. Mavazi ya ndani kama vile chupi, soksi, sindiria,...;
c. Mashuka kitandani na taulo.

Soksi, taulo, mashuka au sindiria zikivaliwa kwa muda mrefu bila kubadilishwa hutoa harufu mbaya. Hivyo, chawa nao huweza kujitokeza na kuyahatarisha maisha yako.

Dumisha usafi wa mwili ili uweze kujilinda na maambukizi ya maradhi na kuepusha kuenea kwake. Kumbuka kuwa “Kinga ni bora kuliko tiba”.

**Kazi ya 14:**

**Jibu** maswali yafuatayo ambayo yanahusu **ufahamu** wa kifungu cha habari cha hapo juu:

1. Taja mambo manne yanayoweza kuhusika na usafi.
2. Eleza umuhimu wa kumfunza mtoto kuhusu usafi wa mwili.
3. “Baadhi ya watu hawana budi kutohusika na usafi wa mwili.” Eleza waziwazi.
4. Tofautisha “shule za chekechea” na “shule za msingi.”
5. Kwa nini usafi wa kinywa ni muhimu sana?
6. Ni wakati gani tunatakiwa kusugua meno?
7. Ni wakati gani tunalazimishwa kunawa mikono yetu?
8. Eleza jinsi ambavyo kitendo cha kuosha mikono kinafanyika?
9. Eleza umuhimu wa kusafisha nguo ndani za mtu?

**Kazi ya 15:**

**Nguo hizi** zinazoonekana kwenye picha huitwaje?



1. ..................................................



2. ................................................



3. ..................................................

## G. Kuandika

**Kazi ya 16:**

Andika sentensi mbili tofauti zinazofuata ***muundo*** huu na kutumia maneno ambayo yametajwa kwenye jedwali:

| Ufahamu | ni | neno | ambalo | linatokana | na | kitenzi | "kufahamu" |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| .............. | ni | neno | ......... | ............ | ..... | ............ | "kufungua" |
| ............. | ni | kitenzi | ......... | kinahusiana | .... | ............ | "ubatizo" |

**Kazi ya 17:**

Kwa njia ya mishale, **ambatanisha** tungo za kikundi cha A na zile za kikundi cha B ili kupata sentensi **sahihi**:

| Kikundi cha A | Kikundi cha B |
|---|---|
| 1. Uchafu wa mikono unaweza kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile kuharisha, | usafi wa mwili wake katika maisha yake ya baadaye |

| | |
|---|---|
| 2. Upigaji mswaki wa mara kwa mara | na kusafishwa vizuri kwa kutumia maji na sabuni |
| 3. Misingi sahihi ya usafi anayofundishwa na watu hao ndiyo inayomwezesha kutilia mkazo | kipindupindu, kuhara damu, nimonia, ebola na mengineyo. |
| 4. Kuhusu usafi wa nywele, zinaweza kukatwa au kusukwa mara kwa mara | unashauriwa kwa watu wote. |

**Kazi ya 18:**

Jiunge na wenzako wawili na **kuchagua** hadithi simulizi moja ya Kiswahili. Someni **kwa sauti** na ufasaha hadithi hiyo na **kutayarisha maswali** mbalimbali ya ufahamu. Kundi lenu **libadilishane** na kundi jingine na **kujibu** maswali ambayo yametayarishwa.

## SOMO LA 25: UFUPISHO WA HABARI

**Kazi ya 1:**

Shirikiana na mwenzako ili kujadili kuhusu yale yanayoendelea kwenye picha hii. Mnafikiri kuwa watu hawa wanazungumzia **nini**?




**Kazi ya 2:**

Someni kifungu cha habari kinachofuata na **kukihusisha** na picha hii.

*Mbinu zinazofuatiliwa katika ufupisho wa habari*

**1. Umuhimu wa somo la ufupisho wa habari**

**Katushabe:**

Mwalimu, katika kidato cha nne tulijifunza ufupisho au muhtasari wa habari. Kwa nini somo hili linarudiliwa?

**Mwalimu:**

Katushabe, kumbuka kuwa mwaka jana tulikubaliana kwamba muhtasari au ufupisho wa habari ni baadhi ya mazoezi mwanafunzi anayolazimishwa kufanya akiwa masomoni. Ndiyo sababu somo hili linarudia.

**Lieta:**

Ndiyo Mwalimu! Ingekuwa vizuri kutukumbusha kwani wengi kati yetu wameisha sahau mengi kuhusu ufupisho au muhtasari.**Mwalimu:**

Asante sana mwanangu! Kumbukeni nyote kuwa ufupisho wa habari ni ustadi wa kuiandika upya kwa ufupi habari uliyoisoma. Ufundi huo hulenga kuisoma habari, kuielewa vizuri (yaani kuifahamu) na kuweza kuieleza au kuiandika upya kwa maneno machache ukiyalinganisha na yale ya awali. Jambo ambalo ni muhimu katika zoezi hilo ni kutopotosha ujumbe wa habari asili. Zoezi hili huwawezesha wanafunzi na watu wengine kupima ufahamu wao na uwezo wao wa kujieleza kwa maneno machache.

**2. Sifa za ufupisho wa habari**

**Hamuduni:**

Asante sana Mwalimu! Sote tunakushukuru kwa kutukumbusha umuhimu wa ufupisho. Inaonekana kuwa ufupisho au muhtasari ni zoezi muhimu maishani mwetu. Walakini, ingekuwa vizuri kutukumbusha pia sifa za ufupisho wa habari.

**Mwalimu:**

Vizuri sana Hamuduni! Tuseme kuwa mimi nanyi tuko uwanjani. Tunashiriki katika mashindano ya ligi kuu ya Kombe la Kuendeleza Usawa wa Jinsia nchini Rwanda. Mwalimu hangeshirikiana na nyinyi ili timu ijinyakulie ushindi?

**Samanta:**

Mwalimu, sote tungesaidiana na kushikamana.

**Mwalimu:**

Asante sana! Hebu tushirikiane katika shindano hili yaani somo letu. Mutabazi, zitaje sifa za ufupisho wa habari.

**Mutabazi:**

Asante sana Mwalimu! Mniwie radhi nikisahau jambo fulani. Katika kidato cha nne tuliona kuwa ufupisho wa habari:

a. Huwa ni mfupi kuliko habari ya mwanzo. Kwa hiyo, ni lazima "ubahiri wa maneno" utumiwe;
b. Huwa na ujumbe ule ule uliokuwa katika habari ya mwanzo;
c. Hujumuisha mawazo makuu yaliyodondolewa kutoka habari ya mwanzo;
d. Mawazo haya makuu sharti yapangwe katika mtiririko wenye mantiki.

Hizo ndizo sifa za ufupisho wa habari.

**Mwalimu:**

Vizuri sana mwanangu! Mmpigie makofi mwenzenu. Haya ni matunda ya somo la ufahamu. Mnakumbuka? Kila mwanafunzi analazimishwa kutilia mkazo masomo mbalimbali anayojifunza. Siliviya, hebu tukumbushe hatua zinazofuatiliwa katika kuandika ufupisho.

**3. Hatua zinazofuatiliwa katika kuandika ufupisho**

**Siliviya:**

Mwalimu, hatua ninazokumbuka ni hizi zifuatazo:

- Kuisoma au kuisikiliza habari kwa makini na mara nyingi ili kuielewa vizuri. Hatua hii ndiyo iitwayo "ufahamu wa habari";
- Kutambua na kubaini mawazo makuu yanayojitokeza katika kila aya;
- Kuyaunganisha mawazo makuu na kuandika au kuelezea ufupisho wa habari hiyo kwa maneno yako mwenyewe bila kupotosha maana ya habari ya kwanza;
- Kuhesabu idadi ya maneno ya ufupisho ili kuyapunguza ikiwa yanazidi idadi iliyotakiwa;
- Kama muda unaruhusu, pitia tena habari ya mwanzo kisha upitie tena ufupisho ili kujiridhisha kuwa hujaacha taarifa yoyote ya muhimu.

Ikiwa kuna upungufu wowote ni lazima arekebishe au akamilishe taarifa pale inapohitajika. Ili kufanikisha shughuli hii, mfupishaji anatakiwa kujiepusha na matumizi ya lugha chafu, misimu, urudiaji, mzunguko wa kimaelezo au maelezo yasiyoleta upya wowote katika habari.

**Mwalimu:**

Asante sana mwanangu! Elimu isiyo na ubaguzi isifiwe! Sasa, someni kifungu cha habari kinachofuata na kutoa ufupisho wake kwenye ukurasa mmoja.

## A. Maswali ya ufahamu

**Kazi ya 3:**

Soma kifungu cha habari na **kujibu** maswali yafuatayo:

1. Eleza maana ya “ufupisho wa habari”
2. Eleza umuhimu wa somo la ufupisho wa habari kwa mwanafunzi.
3. Kwa nini ni lazima kutumia “ubahiri wa maneno” katika ufupisho.
4. Ni kigezo gani muhimu unachoweza kuchunguza ili kutambua ikiwa mfupishaji amefanikisha kazi yake?

## B. Kusikiliza

**Kazi ya 4:**

Sikiliza jinsi mwenzako au mwalimu anavyokisoma kifungu cha habari.

## C. Kusoma

**Kazi ya 5:**

**Soma** habari hii zaidi ya mara moja ili kuielewa vizuri.

## D. Msamiati

**Kazi ya 6:**

Eleza maana za maneno yafuatayo:

1. **Kulenga**
2. **Kufanikisha**
3. **Upungufu**
4. **Hatua**
5. **Aya**

**Kazi ya 7:**

Katika jozi, tungeni **sentensi moja** kwa kila neno kati ya hayo ya hapo juu.

**Kazi ya 8:**

Jaza jedwali lifuatalo ukizingatia yale ambayo umeyasoma katika habari ile. Jedwali linaitwa “**Ufupisho wa habari**”.

| 1<br>Sifa za ufupisho wa habari | 2<br>Hatua zinazofuatiliwa katika kufupisha habari |
|---|---|

**Kazi ya 9:**

**Kamilisha** sentensi zifuatazo kama **zilivyotumiwa** katika kifungu cha habari:

1. Haya ni ..................... ya somo la ufahamu.

| | |
|---|---|
| 2. Ingekuwa vizuri ......................... kwani wengi kati yetu wameisha sahau mengi kuhusu ufupisho au muhtasari | |
| 3. Kumbukeni nyote kuwa ufupisho wa habari ni ....................... kwa ufupi habari uliyoisoma. | |

## E. Kuzungumza

**Kazi ya 10:**

Kwa kushirikiana na mwenzako,elezeni sifa za ufupisho mzuri.

**Kazi ya 11:**

Kwa njia ya mazungumzo, fuata **muundo huu** wa sentensi hii na kuzitaja **sifa tatu** za ufupisho wa habari. (Mfano mmoja umetolewa):

| | |
|---|---|
| **Ufupisho wa habari** | **huwa mfupi kuliko habari ya mwanzo**<br>....................................................<br>..................................................... |

## F. Cheka kidogo

**Kazi ya 12:**

Mlevi aliingia katika duka la madawa na kusema, “Tafadhali, ninahitaji kondomu”. Bila kusita, Mhudumu akabwatuka, “Kaka, huna heshima! Si uagize kwa lugha nzuri...” Jamaa akaona isiwe tabu, akamwambia Mhudumu kwa upole huku akigusa kwa kidole, Tafadhali dada! Ninaomba unipatie nguo ya kiungo hiki cha siri”.

**Waambie** wenzako **kichekesho** kingine unachojua.

## G. Kuandika na kufupisha

**Kazi ya 13:**

“Ni lazima nguo nazo ziwe safi.” Tumia maneno ambayo yalitolewa badala ya neno “nguo” lakini usibadilishe **muundo** wake.

| Ni | lazima | nguo | nazo | ziwe | safi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | meno | | | |
| | | kinywa | | | |
| | | mikono | | | |

**Kazi ya 14:**

Katika jozi, someni kifungu cha habari kifuatacho na kufanya muhtasari wake. Ufupisho huo uwe 1/3 ya kifungu cha habari chote.

***Mazao ya biashara na fedha za kigeni***

Katika Afrika hivi leo kuna baadhi ya watu wa kawaida ambao hujiuliza jinsi gani mazao ya biashara kama mkonge, korosho, tumbaku, kahawa,... huwasaidia iwapo mazao hayo huuzwa katika nchi za ng'ambo.

Swali hili huzushwa na msisitizo wa viongozi wengi kwamba wananchi walime mazao hayo ili kuweza kupata fedha za kigeni. Kitu ambacho wananchi hawa hawakielewi ni vipi fedha za kigeni hufanya kazi kubwa ya kuinua maendeleo ya nchi. Wengi wao hawajui kwamba hata vitu ambavyo hutumiwa katika maisha ya kila siku huhitaji fedha za kigeni kununuliwa kutoka nchi za kigeni. (Hapa fedha za kigeni maana yake ni zile fedha ambazo kimataifa zinakubalika kufanyia biashara, mathalani dola, yen na kadhalika). Tuchukue mfano wa nyembe za kunyolea. Nchini Rwanda nyembe hizo huagizwa kutoka Ufaransa na nchi nyingine. Lakini kitu kama nyembe ni watu wachache wanaoweza kufikiria kwamba huhitaji dola au faranga za Ufaransa kuweza kununuliwa kutoka nchi za nje.

Hata bidhaa ambazo huzalishwa nchini Rwanda nazo zina uhusiano wa moja kwa moja na fedha za kigeni. Tuchukue mfano wa kiwanda cha bidhaa za plastiki kilichoko jijini Kigali. Ili kiwanda hiki kiweze kufanya kazi barabara, ni lazima baadhi ya malighafi iagizwe kutoka nchi za nje. Rwanda haina viwanda-mama vya kuzalisha mitambo. Hivyo, mitambo nayo huagizwa kutoka nchi za nje.

Hivi, ndiyo kusema kuwa msisitizo wa kuzalisha mazao ya biashara unaofanywa na viongozi wengi ni wa msingi. Ni jukumu la viongozi kuwaelimisha wananchi juu ya suala hili ili wanapofanya shughuli ya uzalishaji wa mazao ya biashara waelewe fika umuhimu wake kwa taifa. Ni kwa kufanya hivi tu: Wananchi watazalisha mali wakiwa na mwamko na hatimaye kuweza kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Kadiri bidhaa zitakavyoongezeka, ndivyo mapato ya fedha za kigeni yatakavyokua, na ndivyo nchi itakavyostawi kiuchumi. Matokeo yake ni maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

**Kazi ya 15:**

Kwa kushirikiana na mwenzako, kumbukeni hadithi moja mliyoisoma au kusikiliza, kisha toeni muhtasari wake mbele ya darasa.

**Kazi ya 16:**

Fuata habari kwenye redio au runinga kwa kuandika mawazo muhimu, kisha andika ufupisho wa habari hiyo na kuwasimulia wenzako kuhusu habari hiyo.

# SOMO LA 26: MUHTASARI WA MATUMIZI YA NYAKATI KUU ZA KISWAHILI

**Kazi ya 1:**

Tazama picha hii. Unaona **nini**?




**Kazi ya 2:**

Taja **nyakati kuu** zinazoweza kutumiwa katika sentensi ya Kiswahili.

**Kazi ya 3:**

Andika sentensi hizi katika hali yakinishi, wakati uliopita, ujao, uliotimilika na wa mazoea:

1. Kabanda **anarutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu **anasamehe** watu wote waliopora mali yake.

**Kazi ya 4:**

Andika sentensi hizi katika hali kanushi, wakati uliopita, ujao, uliotimilika na wa mazoea:

1. Kabanda **anarutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Mariamu **anasamehe** watu wote waliopora mali yake

**Kazi ya 5:**

"Maana ya sentensi hutegemea sana matumizi ya nyakati". Eleza kinagaubaga.

**Kazi ya 6:**

Katika jozi, **someni** na **kulinganisha** sentensi zifuatazo ukitegemea nyakati na hali mbalimbali:

1. Kabanda **anarutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
2. Kabanda **alirutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
3. Kabanda **amerutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
4. Kabanda **atarutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
5. Kabanda **harutubishi** shamba ili kupata mavuno mengi.
6. Kabanda **hakurutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
7. Kabanda **hajarutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.
8. Kabanda **hatarutubisha** shamba ili kupata mavuno mengi.

**Kazi ya 7:**

**Kamilisha** sentensi hizi zenye dhana ya masharti:

1. Wangejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake,..................................................
2. Barabara zote zingekuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda..........................................
3. ..............................................., kisingalipiga marufuku ubakaji wa watoto nchini mwetu.
4. Ukimwadhibu mtoto, ............................................................................................................

**Kazi ya 8:**

Andika sentensi nne za hapo juu katika **hali kanushi**.

| **Wakati** | **Hali yakinishi** | **Hali kanushi** |
|---|---|---|
| 1. Wakati uliopo | Kiambishi wakati: **-na-** | Kiambishi wakati: **-Ø-** |
| | Mfano: Kabanda a**na**chek**a**<br>Kabanda a**na**shukur**u** | Mfano: Kabanda **ha**chek**i**<br>Kabanda **ha**shukur**u** |

| | | |
|---|---|---|
| Wakati uliopo huonyesha jambo linalotendeka sasa hivi, wakati huu au muda huu unaoendelea.<br><br>Katika wakati uliopo hali kanushi, kitenzi chenye mwisho (-a) kinatumia (-i) badala ya (-a). Kila kitenzi chenye mwisho (-e), (-i) au (-u) kinabakia na mwisho wake wa awali yaani (-e), (-i) au (-u)<br>Mifano:-Mwalimu anawasamehe wanafunzi →Mwalimu hawasamehe wanafunzi<br>Kalisa anasali → Kalisa hasali.<br>Mama anakushukuru kwa matendo yako →Mama hakushuru kwa matendo yako | | |
| 2. Wakati uliopita | Kiambishi wakati: **-li-** | Kiambishi wakati: **-ku-** |
| | Mfano: Kabanda a**li**cheka<br>Kabanda a**na**shukuru | Mfano: Kabanda **haku**cheka<br>Kabanda **haku**shukuru |
| Wakati uliopita huonyesha kitendo kilichofanyika muda mrefu uliopita kama vile jana, juzi, wiki iliyopita, mwezi uliopita,... | | |
| 3. Wakati ujao | Kiambishi wakati: **-ta-** | Kiambishi wakati: **-ta-** |
| | Mfano: Kabanda a**ta**cheka<br>Kabanda a**ta**shukuru | Mfano: Kabanda **hata**cheka<br>Kabanda **hata**shukuru |
| Wakati ujao huonyesha kitendo ambacho kitatokea baadaye, kesho, juma lijalo na bado hakijafanyika lakini kinatarajiwa kufanyika. | | |
| 4. Wakati uliotimilika | Kiambishi wakati: **-me-** | Kiambishi wakati: **-ja-** |
| | Mfano: Kabanda a**me**cheka<br>Kabanda a**me**shukuru | Mfano: Kabanda **haja**cheka<br>Kabanda **haja**shukuru |
| Wakati uliotimilika huonyesha kitendo ambacho kimekamilika muda usio mrefu kama vile daika kumi ambazo zimepita,... | | |
| | | |
| 5. Wakati wa mazoea | Kiambishi wakati: **-hu-** | Kiambishi wakati: **-Ø-** |
| | Mfano: Kabanda **hu**cheka<br>Kabanda **hu**shukuru | Mfano: Kabanda **ha**chek**i**<br>Kabanda **ha**shukur**u** |
| Wakati wa mazoea huonyesha kitendo ambacho hufanyika mara kwa mara au kila siku na kadhalika.<br><br>Katika wakati wa mazoea hali kanushi, hutumia mtindo wa hali kanushi ulio sawa na ule wa wakati uliopo. | | |

**Matumizi ya nyakati katika hali mbalimbali**

Kuna nyakati nyingine ambazo zinatumiwa mara kwa mara. Nyakati hizo ni hizi zifuatazo:

| **Kiambishi cha hali** | **Mfano wa sentensi** |
|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| **-nge-**<br>Tungo kanushi | Tungo ya kinishi | U**nge**mwadhibu mtoto, a**nge**pata adabu njema. |
| | U**singe**mwadhibu mtoto, a**singe**pata adabu njema | |
| **-ngeli-**<br>Tungo kanushi | Tungo ya kinishi | U**ngeli**mwadhibu mtoto, a**ngeli**pata adabu njema. |
| | U**singeli**mwadhibu mtoto, a**singeli**pata adabu njema. | |
| **-ngali-**<br>Tungo kanushi | Tungo ya kinishi | U**ngali**mwadhibu mtoto, a**ngali**pata adabu njema. |
| | U**singali**mwadhibu mtoto, a**singali**pata adabu njema. | |

Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya **-nge-, -ngeli-** na **-ngali-.**

- **[-Nge- ]** huonyesha kuwa kitendo fulani lazima kifanyike ndipo tendo jingine nalo lifanyike. Kitendo hakijafanyika na kwa hiyo, jambo jingine halijatokea lakini kuna uwezekano wa kufanya kitendo hicho na jambo hilo jingine litokee.

- **[-ngali- au –ngeli-]** huonyesha kuwa kitendo fulani hakijafanyika na kwa hiyo, jambo fulani halijatokea wala hakuna uwezekano wa kufanyika kitendo hicho kwa sababu wakati umepita na hakuna uwezekano wa wakati huo kurudia. Wakati mwingine ku-towezekana huko kunaambatana na majuto.

- Viambishi hivi ni vimbishi vya masharti vinavyoweza kutumika katika wakati uliopo na uliopita**: Mfano: -**Nengeona mwalimu wetu sasa, ningeweza kumuuliza maswali haya yote (Wakati

uliopo).

-Kama wezi wale wangetoroka siku ile, polisi wangewakamata wote (Wakati uliopita).

| | |
|---|---|
| **Kiambishi -ki-** | • Kiambishi **-ki-** hutumiwa kuonyesha masharti.<br><br>**Mfano:**<br>-Mkishinda mtihani huu, mtapewa zawadi nzuri<br>- Ukimwadhibu mtoto, atapata adabu njema<br>• Lakini kiambishi hiki **-ki-** hutumika pia kuonyesha kitendo kimoja kilipokuwa kinatumika kitendo kingine kilikuwa kinatendeka pia (wakati uliopita).<br><br>**Mfano:** Wanafunzi walikuwa wakisikiliza vizuri, mwalimu wao alipokuwa akisimulia<br>hadithi ile.<br><br>• Kiambishi **-ki-** hutumika kuonyesha iwapo kitendo kitakuwa kikiendelea wakati kingine kitafanyika (wakati ujao).<br><br>**Mfano:** -Wageni wetu watakuwa wakitazama michezo ya kuwaburudisha, tutakapokuwa tukiwaandalia chakuka kizuri.<br>• Kiambishi **-ki-** hutumika pia kuelezea tendo lililokuwa likiendelea kwa muda mrefu.<br><br>**Mfano:** Wanafunzi wa kidato cha tano wamekuwa wakionyesha michezo ya kuigiza kila mwaka. |
| **Kiambishi -po-** | • Kiambishi kingine kinachotumiwa katika nyakati mbalimbali ni –**po-**Kiambishi **-po-** huweza kuonyesha tendo lililofanyika na kufuatwa na jingine (wakati uliopita).<br><br>**Mfano:** Mkurugenzi wa shule alipongeza wanafunzi wote, alipoona matokeo ya mitihani ya mwaka uliopita.<br>• Kiambishi **-po-** hutumika kuonyesha kuwa tendo litafanyika na kufuatwa na jingine (wakati ujao).<br><br>**Mfano:** Mwanafunzi huyu atakapojibu swali hili atapewa alama nzuri. |
| **Kiambishi -ka-** | • Kiambishi **–ka-** hutumika tunaposimulia au kutoa maelezo juu ya matukio ya matendo yanayofuatana.<br><br>**Mfano**: Mukandori alipofika shuleni, aliwakuta wanafunzi wenzake , wakazungumzia mambo mengi waliyokutana nayo katika likizo yao, wakafurahi kisha wakacheka sana.<br>• Kiambishi **-ka-** huweza kutumika pia katika wakati uliopo unaoendelea au wakati ujao; yaani tunapozungumzia matendo yatakayofanyika.<br><br>**Mfano:** -Nenda ukanunue kalamu na daftari.<br>- Twendeni tukaombe ruhusa ya kwenda kanisani.<br>-Tutakwenda mjini tukatazame mchezo wa timu ya shule yetu. |

| | |
|---|---|
| **Wakati usiodhihirika** | Katika mawasiliano, kuna uwezekano wa kutumia nyakati zisizodhihirika.<br><br>**[-a-] Mfano**: Kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza. (Hali yakinishi)<br>Sisi twasubiri nyumbani. (Hali kanushi)<br>**[-Ø-] Mfano**: Kizuri hakijiuzi, kibaya hakijitembezi. (Hali kanushi)<br>Sisi hatusubiri nyumbani. (Hali kanushi)<br><br>Wakati usiodhihirika hutumia kiambishi **-a-** kuonyesha kitendo kinachoendelea kutendeka katika wakati usiodhihirika.<br><br>**Wakati uliotimilika usiodhihirika**<br><br>**[-ka-] Mfano**: Mariamu a**ka**angalia juu a**ka**mwona nyoka. (Hali yakinishi)<br>Wakati uliotimilika usiodhihirika huonyesha kitendo ambacho kinakamilika katika wakati usiojulikana au kitendo kinachofanyika baada ya kingine. Hutumiwa katika masimulizi. |

## TATHMINI KUHUSU SURA YA NNE

Soma maswali yafuatayo na **kutoa** majibu:

1. Katika jozi, chagueni hadithi simulizi moja ya Kiswahili na kutayarisha maswali ya ufahamu juu yake,kisha badilisheni na kikundi kingine ili kila kundi lisome hadithi iliyochaguliwa na kujibu maswali ya ufahamu
2. Toeni ufupisho wa hadithi hiyo mliyoichagua na kuwasomea wenzenu muhtasari huo.

3. Tunga sentensi moja kwa kutumia nyakati na hali zilizotajwa hapo juu.

# FAHARASA AU ORODHA YA MSAMIATI ULIOTUMIWA

| | |
|---|---|
| **Anasa** | : Mambo au hali ya raha nyingi |
| **Aula** | : Bora zaidi |
| **Buibui** | : Mdudu anayetandaza utando wa kukamatia nzi na wadudu wengine |
| **Bwege** | : Mtu mjinga au mpumbavu |
| **Bwerere** | : Kitu cha bure au cha mahonyo |
| **Chane** | : Shada moja la mkungu wa ndizi (kundi dogo la ndizi zinazojifungia kwenye fundo moja) |
| **Dafrau** | : Mgongano wa nguvu baina ya vitu viwili au zaidi (Kupigwa dafrau=Kugongwa na) |
| **Darubini** | : Chombo chenye lensi kinachofanya vitu vilivyo mbali vionekane karibu na vidogo vionekane vikubwa |
| **Dema** | : Mtego wa samaki uliofumwa kwa matete au vijiti |
| **Dondoo** | : Tabia ya uzinifu; uzinzi |

| | |
|---|---|
| **Fahali** | : Ng'ombe dume |
| **Fanani** | : Mtaalamu wa kusimulia wengine hadithi |
| **Hadhi** | : Cheo cha mtu |
| **Hohehahe** | : Mtu ambaye hali yake ya maisha si nzuri; mtu asiye na mbele wala nyuma; maskini sana |
| **Itikadi** | : Imani katika jambo la kidini na jinsi ya mapokezi yake; mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa au za kiuchumi |
| **Jadi** | : Asili ya mtu anakotoka; ukoo au kizazi cha mtu |
| **Jakamoyo** | : Masumbufu ya rohoni; kero la moyo |
| **Janga** | : Balaa; hatari; tabu |
| **Jasiri** | : Shujaa; hodari (Mfano: Mtu jasiri) |
| **Kalima** | : Tamko; kauli |
| **Kasha** | : Aina ya sanduku kubwa hasa hutumiwa kuwekea nguo au vitu vya thamani |
| **Kedi** | : Mambo yasiyopendeza; mambo ya kinyumenyume; hila |
| **Kiada** | : Kwa utaratibu wake; vizuri; vema |
| **Kichaka** | : Mahali penye miti mifupimifupi na nyasi, miiba na kadhalika; kituka |
| **Kigezo** | : Mtu, kitu au jambo la kuigwa |
| **(Ki)holela** | : Ovyoovyo; bila ya mipango |
| **Kiitikio** | : Sehemu ya wimbo ambayo mwimbaji huitikiwa; kipokeo; mkarara |
| **Kina** | : Silabi zenye sauti za namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadha hususa katikati na mwisho wa kila mstari wa ubeti wa shairi |
| **Kitasa** | : Chombo mfano wa kisanduku kidogo chenye komeo ndani kitumiwacho kwa kufungia mlango, sanduku, kabati na kadhalika |
| **Kizibao** | : Vazi kama koti fupi lisilo na mikono |
| **Kochokocho** | : Kwa wingi; tele |
| **Kuadhimisha** | : Kusherehekea jambo au siku kwa kuitukuza au kuisifu |
| **Kuadhiri** | : Kuvunjia heshima; kuaibisha |
| **Kubaini** | : Kueleza waziwazi; kufafanua |
| **Kuboronga** | : Kuharibu; kuvuruga |
| **Kuchanganua** | : Kuchambua dhana, fikira au maandishi |
| **Kufeli** | : Kushindwa katika mtihani |

| | |
|---|---|
| **Kuganga** | : Kufanyia mgonjwa matibabu; kutengeneza kilichovunjika au kuharibika |
| **Kugwengwenya** | : Kubandua kwa meno kama vile nyama kwenye mfupa; kuguguna |
| **Kuhuluti (sha)** | : Kuweka vitu mahali pamoja; kuchanganya |
| **Kukonda** | : Kuwa na wembamba wa mwili; kudhoofu |
| **Kulenga** | : Kutuliza macho mahali kwa kusudi ya kupata shabaha |
| **Kuliwaza** | : Kubembeleza ili kutoa mtu majonzi; kupoza |
| **Kunata** | : Kushika mahali kwa nguvu kama vile inavyoshika gundi |
| **Kupambanua** | : Kuonyesha tofauti waziwazi; kufafanua |
| **Kupenya** | : Kupitia kwenye tundu ndogo, ufa au mwanya finyu na kuingia ndani |
| **Kupepesa** | : Kuchezesha kope kwa kuzipeleka juu na chini kwa haraka; kukopesa |
| **Kupotosha** | : Kitu kuharibika kwa kupoteza sifa kilichokuwa nayo |
| **Kurekodi** | : Kuhifadhi mambo kama vile kwa maandishi au kwa kuyanasa katika kinasasauti au sahani za santuri kwa ajili ya matumizi ya baadaye |
| **Kushamiri** | : Kuenea kwa jambo au habari; kuzagaa; kutapakaa |
| **Kustarehe** | : Kukaa au kuishi bila ya kuwa na shida au usumbufu; kuwa na raha |
| **Kutathmini** | : Kutia kitu thamani; kuthamini |
| **Kutoma** | : Kuingia ghafla au kwa nguvu |
| **Kuwanda** | : Kuwa nene; kunenepa |
| **Kuwekeza** | : Kutia kitu mahali fulani kwa ajili ya manufaa ya baadaye |
| **Kuzagaa** | : Kuwa kila mahali; kuenea kila mahali |
| **Kwenda shoti** | : Kwenda mbio |
| **Labeka** | : Tamko la kuitikia; abee; naam |
| **Libasi** | : Mavazi au nguo |
| **Ligi** | : Mkusanyiko wa timu za michezo kama vile klabu za mpira wa miguu zinazopambanishwa ili kupata mshindi au bingwa |
| **Maarufu** | : Kinachojulikana mahali kote |
| **Majungu** | : Vyungu vikubwa (Chungu ni chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kitumiwacho kwa kupikia) |
| **Maktaba** | : Mkusanyo wa vitabu vingi; nyumba ambamo watu huenda kujisomea au kuazima vitabu |
| **Malighafi** | : Mali ambayo haijasafishwa kama vile madini (dhahabu, lulu,...) |
| **Mapato** | : Kitu kinachopatikana hasa baada ya kazi au biashara |
| **Mkafuu** | : Aina ya mti |

| | |
|---|---|
| **Mkataba** | : Makubaliano yanayofikiwa kwa kuandikiana baina ya watu au vikundi viwili au zaidi ili kufanya jambo au kazi fulani |
| **Mkizi** | : Aina ya samaki wa baharini ambaye anaweza kuruka sana |
| **Mkungu wa ndizi** | : Tawi la mgomba lenye ndizi (sehemu yote yenye ndizi) |
| **Mkwe** | : Jina la heshima aitwalo baba, mama, au ndugu wa mzazi ambaye mtoto wake ameoa au kuolewa na mtu fulani wa mtoto huyo; mcheja |
| **Mrija** | : Chombo chenye uwazi ndani kinachotumika kufyonzea vitu viowevu au kutengenezea filimbi au kiko cha tumbaku; njia yoyote ya kujipatia faida ya binafsi kwa kuwanyonya wengine |
| **Mshororo** | : Mstari katika shairi |
| **Msimu** | : Majira; kipindi kirefu cha wakati ambapo jambo fulani (kama vile mvua, jua,...) hutokea |
| **Mtaji** | : Mali inayotumika kuanzishia biashara au kazi nyingine yoyote ya kuzalisha mali |
| **Mtema kuni** | : Mtu akataye kuni |
| **Mtemi** | : Mtawala wa kienyeji katika sehemu fulani za nchi mbalimbali |
| **Nadra** | : Hali ya kutopatikana mara kwa mara |
| **Nakala** | : Kitu chochote kilichonukuliwa kama vile maandishi, mchoro, picha,... |
| **Nana** | : Tamko litumikalo kumwitia mwanamke kabla au badala ya kutaja jina lake |
| **Ndwele ("uwele" katika umoja)** | : Maumivu mwilini; ugonjwa |
| **Niwie radhi** | : Ninakuomba msamaha |
| **Ovyo(ovyo)** | : Bila ya kufuata utaratibu; bila ya mpango |
| **Pembejeo** | : Vitu mbalimbali (kama vile mbolea, madawa,...) vinavyotiwa katika mashamba ili kuweza kupata mazao mengi tena mazuri |
| **Popoo** | : Tunda gumu lenye umbo la duara lililofunikwa na makumbi kama vile nazi, ambalo hukatwa vipande vyembamba na kutafunwa pamoja na tambuu |
| **Radhi** | : Hali ya nafsi kuridhika au kutosheka na matendo ya mtu |
| **Risala** | : Taarifa inayopelekwa kwa mtu au watu fulani aghalabu inayoeleza haja inayotakiwa |

| | |
|---|---|
| **Saini** | : Sahihi; maandishi ya jina la mtu ya kuthibitisha au kuidhinisha kutendeka au kupatikana kwa kitu au jambo fulani kwa kuandika jina lako |
| **Sime** | : Kisu kikubwa chenye makali pande zote mbili |
| **Stadi** | : Mbinu zinazotumiwa katika kutenda jambo fulani kiufundi |
| **Taadhima** | : Heshima; utukufu; unyenyekevu |
| **Taasisi** | : Sehemu au idara inayoshughulika na uchunguzi wa fani mbalimbali |
| **Tukio** | : Jambo lililofanyia au lililotokea |
| **Tumbuu** | : Chombo cha chuma kinachowekwa kwenye mhimili wa mlango na kutumiwa kwa kufungia |
| **Ubeti** | : Kifungu cha maneno katika shairi |
| **Uchumba** | : Makubaliano ya pande mbili baina ya mwanamke na mwanamume wanaotaka kuoana |
| **Udhaifu** | : Hali ya kudhoofika au kutokuwa na nguvu au kuwa mnyonge |
| **Ufaraguzi** | : Hali kutenda jambo bila kutarajiwa kufanywa |
| **Ufisadi** | : Maovu; uharibifu |
| **Ukinzani** | : Hali ya ukaidi; upinzani |
| **Ukongwe** | : Hali ya kuzeeka |
| **Umbu** | : Jina wanaloitana ndugu wazawa wa kike na wa kiume |
| **Umeme** | : Miali ya moto inayoonekana kabla ya radi; nguvu zinazotoa cheche |
| **Ushamba** | : Tabia za kijinga zinazofikiriwa kuwa ni za mtu anayeishi mbali na miji yaani katika vitongoji vya mbali |
| **Ustaarabu** | : Hali ya kustaarabika au kuwa na vitendo, tabia na mwenendo unaolingana na maadili ya jamii inayohusika |
| **Utandawazi** | : Upanuaji kwa kina kirefu wa mawasiliano miongoni mwa jamii mbalimbali |
| **Utengano** | : Hali ya kuweka mtu kando |
| **Wadhifa** | : Cheo ambacho mtu anakuwa nacho kazini; madaraka |
| **Waya** | : Uzi wa madini ya chuma unaotumiwa katika kusafirisha umeme, mawimbi ya sauti na kadhalika |
| **Wenzo (nyenzo)** | : Kitu kinachorahisisha kazi |
| **Wimbi** | : Mtutumko wa sauti au nuru zinazosafiri hewani au wa maji baharini au ziwani... |
| **Zeruzeru** | : Mtu mwenye ulemavu wa ngozi ambaye nywele na ngozi yake imekosa rangi yake kamili na badala yake kuwa nyeupe sana na ambaye macho yake hayawezi kuvumilia mwangaza mwingi |
| **Zizi** | : Aina ya boma au ua lililojengwa maalumu kwa kufugia mifugo kama vile ng’ombe, mbuzi, punda, na kadhalika |

# MAREJEO


1. ABDILAHI Nassir, *Tamrini za Kiswahili: Kitabu cha pili*, Nairobi, Oxford University Press, 1974
2. Co-Publishing Committee, *Hadithi za kwetu*, Nairobi, Co-Publishing Committee, 1987
3. INTANETI, *Tovuti mbalimbali*, Januari-Machi 2016
4. MBUNDA Msokile, *Misingi ya uhakiki wa fasihi*, East African Educational Publishers Ltd, Nairobi, 1993
5. MINEPRISEC, *Ikinyarwanda: Gusoma no gusesengura imyandiko*, Kigali, Nzeri 1982
6. Mohamed, M.A. & Saidi, A.M, *Kamusi ya Visawe*, Nairobi, East African Educational Publishers Ltd, 2002
7. Mohamed, A.M., *Sarufi Mpya*, Dar-es-salaam, Press and Publicity Centre, 1986
8. Mulokozi, M.M., *Fasihi ya Kiswahili*, Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, 1996
9. Mulokozi, M.M., *Tenzi Tatu za Kale*, Dar-es-Salaam, TUKI, 1999
10. NICKY STANTON, *Mastering Communication*, Hampshire, Macmillan Master Series, 1996
11. NKWERA, F.M., *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo*, Dar-es-salaam, TPH, 1978
12. OXFORD University Press, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi, Kenya, 2007
13. Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari, *Kitabu cha Kiswahili III B*, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Agosti 1987
14. Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari, *Kitabu cha Kiswahili IV-VA*, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Novemba 1987
15. Wamitila, K.W., *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*, Nairobi, Focus Publishers Ltd, 2003
16. Wamitila, K.W., *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*, Nairobi, Focus Publishers Ltd, 2008